سواحلي

https://www.path-2-happiness.com/sw

The Path to Happiness

MIJADALA KUHUSU FURAHA

Khalid Abul Futuh

Kituo cha Al-Futuh cha maarifa.
2015 - 1436

The Path to Happiness
MIJADALA KUHUSU FURAHA
Khalid Abul Futuh

Miongoni mwa machapisho ya:

Space Channels

Kituo cha Al-Futuh cha maarifa.

MIJADALA KUHUSU FURAHA

Khalid Abul Futuh

www.path-2-happiness.com

Utangulizi

Himidi zangu ni kwa Allah na swala na salamu zimwendee Mtume wa Allah jamaa na sahaba zake na wanaomfuata.

Hapana shaka kuwa zama zetu zimefunikwa na mawimbi ya fikra na mitazamo mingi, yote inaashiria kiu ya mwanadamu wa zama hizi juu ya majibu ya maswali makubwa katika maisha na kutoka katika hali ya mtanziko na upotevu ambao anaishi, ana kiu cha kumpata atakaye muongoza kwenye njia ya sawa, kama vile ambavyo dunia inashuhudia mambo ambayo hayajawahi kutokea katika ufunguzi wa maarifa na uharaka wa kuhama kwake, na kwa hali hii ni wajibu wa kisheria kwa Waislamu kufikisha neno la Allah kwa watu, na kufikisha kwa ndimi za wanaozungumza nao, yaani kwa mantiki yao na sio tu kwa lugha yao. Hii ndio iliyokuwa Da'wah ya Mitume wa Allah kwa watu wao.

Qur'an imehimiza mijadala kwa kutumia haki na elimu, na kupendezesha mijadala hiyo kuwa katika nafasi ya da'wah kwa yaliyo mazuri, Allah Ta'ala amesema:

"Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka. "(16:125),

Na kuhimizwa hilo mahususi kwa Ahlu kitaab; amesema Allah

"Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa, isipo kuwa wale walio dhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeyaamini yaliyo teremshwa kwetu na yaliyo teremshwa kwenu. Na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja. Na sisi ni wenye kusilimu kwake."(29:46)

Na wakalifanya hivyo manabii na Uulul 'Azm miongoni mwa Mitume, tunamuona nabii wa Allah Nuuh ('Alayhi salaam) akitajwa na watu wake:

"Wakasema: Ewe Nuhu! Umejadiliana, na umekithirisha kutujadili. Basi tuletee hayo unayo tuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli."(11:32),

www.path-2-happiness.com

Qur-an imetupigia mifano mingi katika mijadala yake pamoja na washirikina na makafiri, bali imetaja hoja zao ambazo kwa hoja hizo walipinga Qur-an na ujumbe wake bila hata kupotosha au kusitasita na majibu ya hoja zao isipokuwa ni kwamba Uislamu kama ambavyo ni da'wah ya imani vile vile ni da'wah ya kutengeneza ya kuleta mabadiliko, hili na lile haliwi ila kwa kubadilisha fikra mbali mbali na kuzipanga upya akili, na hilo haliwi ila kwa kukinaisha ambako mjadala unakuwa ni moja kwenye nyezo zake kubwa.

Katika hali hii ndugu yangu Dr. Abdullah bin Salim Bahamam alinipa fikra ya kutunga kitabu kinachojadili mambo muhimu ambayo huchafua sura ya Uislamu kwa wasio Waislamu, na hilo liwe kwa njia ya mjadala katika hali ambayo kitabu hiki kitafasiriwa katika lugha nyingi na kitoke katika hali tofauti za kifani na njia zinazolingana na nyakati. Nikaiona kuwa ni fikra nzuri ya kuzingatiwa na kufanyiwa kazi.

Nimeanza kazi hii nikiwa ni mwenye kukinaishwa na umuhimu wa kazi hii bila kupata ugumu wake; kwani mimi nimeweka wasifu wa wahusika ambayo imeweka vifungo juu yangu wakati wa kuendelea na kazi.

Nimepanua kundi la wanaozungumziwa pamoja na Waislamu ambao wanataka kuongeza maarifa kuhusu Uislamu kwa njia nyepesi iliyo wazi wakati huo huo, ambayo hufaa kukuza fikra zao na kujadiliana na maadui wa Uislamu.

Kama nilivyoainisha vigezo vya kuchagua maudhui kuwa yawe ni maudhui ya jumla ambayo yanaunda misingi ya dini ya Kiislamu, au yanayoelekeza kwenye Uislamu na yanatengeneza vidhibiti vya kuangalia ndani na kuutambulisha.

Na nimependelea yaliyomo yawe kwa sura ya vipengele vinavyojitegemea, (ambazo zimefikia thelathini (30), kila kipengele kinashughulikia maudhui inayojitegemea; kiasi cha kutoa fikra iliyo kamilika kuhusu maudhui husika, wala haihitaji kipengele kingine ili kukamilisha sura ya kiakili iliyojengwa kwa msomaji (au mtazamaji) kuhusu maudhui inayoshughulikiwa.

Na kwa kuwa maudhui ya vipengele hivi yanatarajiwa kutoka kwa njia ya tamthilia yenye kuonekana, nimejaribu kuyaweka katika hali ya usawa vipengele vyote, bali hata idadi zenye kulingana maneno ya vipengele vyote. Na ukubwa huu umfae msomaji wake katika sura ambayo ni kama vile kumeza kidonge (kapsuli) chenye fikra iliyoshiba, na bila shaka hii ni athari ya kutimia kwa vipengele vyote vya maudhui husika, nilikuwa ninachagua yaliyokuwa muhimu zaidi.

Nikaacha mtindo wa makala ya kuelezea tu na kuhamisha kwenye mtindo wa mjadala, nikijaribu kuongezea aina ya shauku na hamasa katika maudhui za fikra ambazo zina sifa za ugumu ndani yake lakini nyongeza hii haifikii kiwango cha kisa, riwaya au tamthilia.

Kama ambavyo mimi nimechunga yanayonasibiana na hoja mbali mbali na majibu ya mjadala kwa mantiki ya kundi linalozungumziwa, elimu na maarifa yake, vile vile yanayonasibiana na kiwango cha ujumbe wenyewe na kiwango cha elimu wanaozungumziwa.

Changamoto kubwa iliyokuwa inanikabili ni kumvisha mtu mwingine asiyekuwa Muislamu na kujaribu kuzungumza kwa mantiki yake na kutoa dalili kwa hoja yake, na chanzo cha changamoto hii ni kuwa mimi sijawahi kuishi na aina ya mtu huyu wa pili nikaishi nae maisha hai, kama ambavyo lengo la mjadala wa Da'wah ulikuwa na athari ambayo hatuwezi kuiacha kuilezea katika kuelekeza mjadala huu.

Nimejaribu sana kushikamana na vigezo hivi, wala siwezi kudai kuwa nimetekeleza vigezo vyote hivyo na namuomba msamaha msomaji kwa upungufu wowote utakaotokea.

Kama ambavyo sitakosa kutanabahisha kuwa mijadala yote hii haitoshi kutoa sura kamili kuhusu Uislamu au kutatua utata wote ambao maadui wa Uislamu wanaeneza, (wanakuza) hata hivyo nadhani zinatosheleza kuondosha kizuizi chenye kumzuia asiyekuwa Muislamu na kuufahamu Uislamu–madamu vizuizi vingine vitaondoka.

Ningependa kuashiria kuwa wakati wa kuandika (kwa takriban baada ya mjadala wa kumi na mbili) nilifahamu kupitia mmoja wa marafiki kuwa kuna mfano wa zoezi kama hili lililofanywa na Ustaadh Tawfiq Ar-Rifai, aliyoipa anuani: "Uamuzi ni wako." ni nikakitafuta katika maduka ya karibu ya vitabu na nilipokuwa nikikaa wakati huo; ili kuulinganisha na niliyokuwa naendelea nayo, nilifahamu kuwa kilikwisha madukani, na hakikuchapwa tena baada ya hapo, kadhalika nilikitafuta katika

www.path-2-happiness.com

mtandao wa intaneti lakini sikukipata, hata hivyo niliona onesho lake katika moja ya makongamano, nilifahamu kupitia hapo kuwa kuna maudhui yanayofanana baina yetu, pia kuna maudhui mengine tulizopanga katika kitabu chetu sikujua kama aliandika, pamoja na kuwa fikra ya kitabu chake na chetu zinakaribiana sana, katika onesho lile mada ilikuwa inavutia, na kitu kilichokuwa na mvuto mkubwa ndani yake ni kuwa ulikuwa ni mjadala wa kweli ambao ameufanya Ustaadh Tawfiq akiwa pamoja na mke wake kwa upande mmoja, na Wamagharibi kwa upande wa pili, na baada ya kushauriana na ndugu yangu Dr. Abdullah Bahammam tuliazimia kumaliza tulichokianza na hili ndilo lililokuwa.

Kama ambavyo ninapenda vile vile kuashiria kuwa nimefanya marejeo kwenye mamia ya kurasa katika intaneti na nimevichukua huko baadhi ya dondoo na zingine nikaacha, hata hivyo sijaonesha hilo katika footnote, kwa kutonasibiana hilo na kiini cha mjadala ambao nategemea kwa ajili ya mada hii, kwa sababu tanbihi za mwisho wa kurasa zitashughulisha umakini wa msomaji na ufuatiliaji wake, na hivyo kukata mtiririko wa fikra zake, badala yake marejeo yamewekwa mwisho wa kitabu pamoja na ufafanuzi kwa mwenye kutaka ziada ya kujisomea.

Mwishowe…. Wahusika wa mjadala huu ni watatu: wawili miongoni mwao ni wale ambao mjadala unaanza na kumalizika kwao nao ni: Rashidi ambae ni mwandishi na mwana habari wa Kiislamu ambaye huishi nchini Uingereza, na Maiko, Mwingereza mzawa ambaye anafanya kazi ya ualimu, walifahamiana kupitia mjadala katika moja ya mitandao ya kijamii, baada ya hapo walikubaliana kukutana katika moja ya migahawa ya London, ili waendelee na mijadala yao uso kwa uso, kisha aungane nao katika ziara yao ya Paris Bwana Rajev, mwanafunzi wa uhandisi kutoka India ambaye anasoma nchini Ujerumani.

Kwa sasa nawaacheni kwenye mjadala wa kwanza, Rashidi pamoja na Maiko; nikiwatakia mpate kwenye mijadala hii kitu kipya.

Khalid Abu Al-Fotoh.

khaled@alfotoh.com

www.path-2-happiness.com

Kikombe cha Usahaulifu

Kikombe cha Usahaulifu

Rashidi alikutana na rafiki yake Maiko mgahawani kulingana na ahadi yao, pindi tu walipokaa Maiko akamuwahi Rashidi kwa kusema:

Usiku huu napendekeza maudhui ambayo naamini utakubaliana na mtazamo wangu.

Rashidi: Subiri kidogo rafiki yangu, hebu tuagize kinywaji kwa heshima yako!!,

Maiko: Samahani kwa kuwa na pupa, una haki katika hilo.

Maiko alimuita mhudumu…nae mhudumu akaelekea kwao, akamuuliza Rashidi anachokitaka.

-**Rashidi:** Chai

Mhudumu (kwa mshangao): Chai?!

Rashidi: Pamoja na ndimu.

Mhudumu (kwa mshangao zaidi): Chai pamoja na ndimu?!

Maiko (huku akicheka): Ndio, ni Muislamu huyo hanywi pombe…nami hali kadhalika chai na ndimu nikitanguliza samahani kwa kujipendelea ili nifanane na rafiki yangu.

Mhudumu aliondoka ili awaletee mahitaji yao wakati ambapo Rashidi alikuwa akiguna huku akiuliza: Sijui kinachoshangaza ni nini katika hilo?!

Maiko: Ewe rafiki yangu, kwa hakika unywaji pombe nchini mwetu ni kama vile unywaji wa maji, kuna aina nyingi na ladha nyingi na njia nyingi za unywaji; ndio maana mhudumu akashangazwa na 'oda' yako ambayo haina pombe, hanywi hivyo isipokuwa mtoto…samahani…samahani…

Rashidi: Hilo kwa hakika ni jambo la kushangaza!

Maiko: Nini la kushangaza? Hili si jambo jipya kwetu, na halipo nchini kwetu peke yake, bali nchi zote za Magharibi.

Rashidi: Hili haswa ndilo jambo la kushangaza.

Maiko: Ki vipi?!

Rashidi: Kwa sababu wengi wenu ni Wakristo, na inakuwa ni wajibu kwenu kuamini kitabu kitakatifu, na taurati imebainisha kuwa katika kunywa pombe kuna madhara makubwa na imeeleza kwa kutahadharisha, "Usiwe miongoni mwao wanywao mvinyo…"(Mithali 23:20) na imekataza kulewa: "Ole wao waamkao asubuhi na mapema, wapate kufuata kileo; wakishinda sana hata usiku wa manane mpaka mvinyo imewaka kama moto ndani yao…." (Isaya 5:11).

Na katika maandiko ya injili imekuja katika Mambo ya Walawi (10:8). "Kisha BWANA akanena na Haruni, na kumwambia. Usinywe divai wala kileo chochote, wewe, wala wanao pamoja nawe…" na katika safari ya hukumu (13:14). "Asile kitu chochote kitokacho katika mzabibu, wala asinywe divai, wala mvinyo, wala asile kitu chochote kilicho najisi; hayo yote niliyomwamuru na ayatunze. Kisha Manoa akamwambia huyo Malaika wa BWANA…." Na mengineyo katika maandiko hayo mengi yenye kukataza unywaji pombe, na kukataza kukaa na walevi, bali huchukizwa hata kuwaangalia.

Maiko: Subiri ewe Rashid: Usidhani kuwa ni wewe peke yako tu ndie mwenye kujua vitabu vitakatifu, viongozi wengi wa dini huku kwetu wamehalalisha unywaji pombe, na wengine wamesema kuwa hata kwenye taurati kuna mtume mmoja amekunywa pombe hadi akalewa, nami nimewasikia baadhi yao wakisema kuwa kilicho haramishwa ni kulewa tu, na katika injili ni kuwa masihi alikunywa pombe, katika injili ya Luka tunasoma: (7:33) "Kwa kuwa Yohana mbatizaji alikuja, hali mkate wala hanywi divai, nanyi mwasema, ana pepo. Mwana wa Adamu amekuja, anakula na anakunywa; nanyi mwasema, tazama mlafi huyu,

www.path-2-happiness.com

na mnywaji wa divai, rafiki yao watoza ushuru na wenye dhambi.”

Rashidi: Unachokisema ewe rafiki yangu kinatupelekea katika matatizo mawili makubwa yenye athari kwa mtu wa Magharibi na jamii za Magharibi:

Ya kwanza: Nasikitika kukuambia:Ukweli wa kitabu chenu kitukufu hivi sasa inathibitisha kuwa ndani yake kuna upotoshaji mwingi na kuwa mikono inayomhudumia ibilisi imekipotosha; kiasi cha kukifanya kinapingana katika itikadi nyingi miongoni mwazo ni: Kuharamisha pombe na kuihalalisha, na kunasibisha kunywa kwake na masihi (amani juu yake) kuwa ameinywa na wakati huo huo ikamkosha na hilo, imekuja katika Luka vile vile (1:15) ikitoa wasifu wa Masihi (juu yake amani) kwa ndimi ya Jibril (amani juu yake), kwani tunasoma: “Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za BWANA; hatokunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye.” Angalia mgongano upo wazi.

Ya Pili: Watu wenu wa dini wamekihodhi kitabu kitakatifu, baadhi yao wanadai kuwa wanaongea kwa jina la bwana, lakini wengi wao wanaona wana mamlaka ya kuharamisha na kuhalalisha, na nyie mnawafuata wao kwa hilo.

Maiko: Kweli kabisa, na kwa hili ninakuambia ukweli kuwa: Wengi wetu hawaamini ukweli wa kitabu kitakatifu wala hawaamini watu wa dini, kuna mabadiliko makubwa sana yametokea katika jamii zetu tokea zama za kunyanyuka kwa Ulaya.

Kwa hiyo basi tunapotaka kufuata kwa ukweli imani yetu hutupeleka kwenye akili na elimu za maada tu,…achana na vitabu vitakatifu na mambo ya dini, tuzungumze kwa kutumia akili na elimu.

Rashidi: Niruhusu nianze kuzungumza: Hili ni tatizo lenu nyinyi na dini, na haya ni matokeo ya tabu mlizopata na udhalimu wa kanisa na kupiga kwake vita elimu na sayansi, haswa katika karne ya kati, na kwa masikitiko mtazamo wenu wa dini ni mtazamo ule mliouona kwa Kanisa, na mnaonyesha kuwa dini inagongana na elimu na nafasi ya dini ipo kwenye kuabudu tu. Ama Uislamu hatusumbuki na tatizo hili, bali dini yetu inahimiza elimu, na ndani ya dini yetu hakuna siri takatifu ambazo zinahodhiwa na watu wa dini pekee.

Kwa ujumla tuzungumze katika lugha ambayo utatosheka nayo, lakini hilo haliendi kinyume na dini yangu, na nitakuthibitishia hilo.

Maiko: Haya tafadhali nieleze.

Rashid: Umezungumza kuwa unachoamini hivi sasa ni akili na elimu, kwa kuanza nakuuliza: Ikiwa akili ipo katika umuhimu mkubwa kiasi hiki, je, Pombe inailinda akili hiyo au inaipoteza?

Maiko: Huu ni mtego, sio swali.

Rashidi: Mwenyezi Mungu amemkirimu mwanadamu na kumfadhilisha juu ya viumbe wengi aliowaumba–na akamneemesha kwa neema ya akili, katika Uislamu Mwenyezi Mungu amemfanya asiyekuwa na akili hawajibishwi kisheria, Mwenyezi Mungu ametuamrisha tuilinde neema hiyo tukufu na kutoiga kitu kinachoweza kuiathiri, bali kuilinda ni moja ya mambo matano ya msingi katika Uislamu, kwa ajili hiyo ndio maana Uislamu umeharamisha pombe au kutumia mihadarati au mfano wa hayo katika vitu ambavyo vinaweza kupoteza akili ya mtu.

Maiko: Ni yepi hayo mambo matano ya msingi ambayo umeyataja?

Rashidi: Tukizamia hayo yatatuondoa katika maudhui yetu, hata hivyo kwa ujumla mambo hayo ya msingi ni matano: Dini, nafsi, akili, heshima na mali.

Maiko: Vizuri, endelea

-Rashid: Kinachojulikana kielimu ni kuwa alkoholi (ambacho ndicho

www.path-2-happiness.com

kinacholewesha) kinamezwa mara moja na utumbo mkubwa na mdogo, na haraka huingia katika mishipa ya damu, kisha baada ya hapo husambaa katika kila kimeng'enya cha kiwiliwili kwa wepesi sana, ikiwemo katika seli za ubongo.

Alkoholi huathiri (hata kama ni kidogo kiasi gani (0.03) katika mfumo wa akili (ubongo) na husababisha kupunguza umakini na utulivu katika harakati na kutoweza kutoa hukumu sahihi ya vitu, na ndio maana Qur-an yetu ikaharamisha kwa nguvu kwa kusema:

"Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet'ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa." (5:90).

Maiko: Hata hivyo tunaona kuwa katika pombe kuna baadhi ya faida, mfano kuchangamsha, kupasha joto, haswa katika nchi zetu zenye baridi.

Rashidi: Qur'an haikanushi kuwa katika pombe kuna baadhi ya faida, Allah Ta'ala amesema:

"Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake. Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake mpate kufikiri"(2:219), kwa sababu faida hizi hazilingani na madhara yake ndio maana Qur-an ikaharamisha, njoo tuzungumzie elimu ambayo unaiamini.

Mbali na athari zake za kitabia na madhara ya kinafsi na ya kijamii na matumizi ambayo hayazingatii hisia ambazo zinaweza kupelekea kwenye kufanya jinai na kutumbukia kwenye hasara ya mali na kuwaudhi wengine, elimu imethibitisha kuwa unywaji pombe na haswa kufikia kiwango cha ulevi na uraibu wake unasababisha madhara mengi ya kiafya:-

1-Huathiri katika tezi za mwili na husababisha mapigo ya moyo.

2-Husababisha kubanana kwa mfumo wa mkojo.

3-Husababisha vidonda vya tumbo na matatizo katika mfumo wa chakula.

4-Huleta matatizo makubwa na maambukizo ya moja kwa moja katika mdomo, koo, utumbo na ubongo na tezi ya endocrine.

5-Kuharibika kwa maini, kiasi cha kuyafanya maini yavimbe kama vile yanatokota motoni kiwango ambacho mtu hawezi kupona na ambayo yanapelekea katika kansa ya ini.

6-Madhara ya pombe kwa mfumo wa pumzi ni vigumu kuyahesabu.

Ama ulisemalo kuhusu kujipa joto kwa kutumia pombe, hilo hutokea kutokana na athari ya damu ya mnywaji pombe juu ya ngozi yake, ambayo hutokea kwa kupanuka kwa mishipa midogo ya damu kwa njia zote mbili za mshipa mkubwa upelekao damu moyoni na mirija ya damu, na ndio tunaona juu ya ngozi kumejaa damu yenye uvuguvugu ambayo hutoka katika maeneo mbali mbali mwilini ikibeba harara na joto; na ndipo hapo mnywa pombe anapojihisi kuwa ni mwenye joto lakini joto lenyewe sio la kweli, na ndio maana tunamuona mnywa pombe ngozi yake imekuwa nyekundu na hudhani kuwa hasikii baridi, na damu huendelea kuzunguka katika kiwiliwili katika mzunguko wake wa kawaida; kiasi cha kiwiliwili kukosa harara ya ndani na joto lenye kuhitajika katika matendo ya Fisiolojia ya kila siku katika maisha ya mtu.

Kuna njia zingine za kupata joto tofauti ya unywaji pombe, kinachofahamika ni kuwa Waislamu ambao wanaishi katika sehemu za baridi hawaingii kwenye kupata joto kwa kunywa pombe.

Maiko: Lakini angalia Ustadh Rashid maneno yako yanahusika tu katika hali ya mtu kulewa, na juu ya hilo nadhani kuwa unywaji pombe kidogo haudhuru.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rashidi: Tatizo linajificha katika kuwa mtu anapoanza kunywa pombe huhisi uchangamfu kisha kiwiliwili kutaka nyongeza ya alkoholi; kinachofanya mnywa pombe kutaka ziada ya hilo, na kila anapozidisha kiwango cha alkoholi kiwiliwili kinahitaji nyongeza zaidi na hivyo hivyo kadhalika hali inaendelea.

Niache nikutajie ufupisho wa utafiti wa tiba huko New Zealand; imeashiria kuwa madhara yanayotokana na unywaji wa pombe (hata kwa kiwango cha chini au cha kati) kinazidi faida yoyote inayotarajiwa. Utafiti huu unapingana na ufahamu ulioenea katika nchi za Magharibi kuwa, kikombe kimoja tu cha pombe kila siku kinaweza kuzuia maradhi ya moyo, katika makala iliyotolewa na jarida la Lancet Medical. Profesa wa elimu ya magonjwa ambukizi wa Chuo Kikuu cha Auckland New Zealand, Dr. Rud Jackson anaona kuwa uwezekano wa kuzuia maambikizi yoyote ya ugonjwa wa moyo kwa ulevi mdogo au wa wastani wa pombe, ni mdogo sana kulinganisha na madhara yanayopatikana kutokana na unywaji pombe.

Hapa kunafichuka muujiza wa kisayansi na wa kisheria katika hadithi tukufu ya Mtume (Swala Llahu ‘alayhi Wasallam) inayosema: “Kila kinacholewesha ni haramu, kinacholewesha kingi chake basi kichache chake ni haramu.”

Maiko: Oouh, ulikuwa ni mjadala moto moto, nadhani mimi nina haja ya kupata glasi ya ndimu baridi (Juisi), ili tuhitimishe nayo kikao chetu.

Rashidi (Akicheka): Ndimu bila ya chai?! Isipokuwa hukutaja maudhui ambayo mimi nitaafikiana nawe.

Maiko: Basi na iwe ndio mjadala wetu ujao.

Rashidi: In sha Allah Ta’ala.

www.path-2-happiness.com

Je, Mke Mmoja Anatosha?!

Je, Mke Mmoja Anatosha?!

Pamoja na Rashidi kufika kwenye ahadi waliyokubaliana kwa wakati alimkuta Maiko akimsubiri mezani, huku akiwa ameshachukuwa kinywaji cha maamkizi….Rashidi alimsalimia na kukaa kwenye kiti chake.

Maiko: Nimekuletea kinywaji chako ukipendacho, chai kwa ndimu… hivi ndivyo nilivyodhania kuwa utakunywa ukipendacho daima.

Rashidi: Maamkizi yaliyokubaliwa, pamoja na kuwa ndicho kinywaji nikipendecho, ila napendezwa zaidi kubadilisha hata kama hicho kingine kitakuwa ubora wake ni mdogo…nadhani hii ni tabia ya wanadamu wote.

Maiko: Huenda nikaafikiana nawe, lakini hebu tuachane na hili, tuanze maudhui yetu….Samahani Je, nikuagizie kinywaji kingine?

Rashidi: Hapana, hapana asante, inaelekea una hamasa sana na mjadala!

Maiko: Sio katika sura hii, lakini ili muda usituache katika kuzungumzia maudhui mengine kama ilivyopita katika kikao chetu kilichotangulia.

Rashidi: Kama ni hivyo na tuanze basi.

Maiko: Kama niliyokuambia katika kikao chetu kilichopita, maudhui ambayo nataka mjadala wake kuuzungumzia, naamini utaafikiana nami katika mtazamo wangu, pamoja na elimu niliyonayo kuwa imesambaa katika jamii yenu itikadi ya kinyume na mtazamo wangu huu.

Rashidi: Vizuri sana, mimi sipendi kutofautiana, na mjadala wangu pamoja nawe ili kufikia kwenye kushirikiana kutosheka, au kwa uchache ufahamu ulio sahihi kwa mtazamo wa kila mmoja wetu. Kama ni hivyo maudhui ni ipi basi?

Maiko: Kwa ufupi ni kuwa mimi naamini kuwa mahusiano ya ndoa yanapaswa kuwa ni ya mmoja katika pande zote mbili, kwa njia iliyo wazi zaidi. Ninadhani kuwa mfumo wa wake wengi ambao Uislamu umeuhalalisha ndani yake, kuna aina ya dhulma kwa mwanamke …je, huwafikiani nami katika hilo?!

Rashidi: Mwanamke gani unayemkusudia?

Maiko: (akiwa ni mwenye kushangazwa): Mwanamke! Nakusudia mke wa ndoa!....Je, kuna mwanamke mwengine katika mahusiano haya?!

Rashidi: Kama tulivyokubaliana huko nyuma, utafiti sahihi wa mambo unapaswa kuwa katika duara zima lililokamilika ambapo mambo yote huangaliwa kwa upana wake.

Maiko: Vizuri, lakini ni nini athari ya hilo katika maudhui yetu?

Rashidi: Athari yake ni kuwa tunapoyatafiti mas-ala haya inatupasa tuangalie maslahi ya mwanamke kwa kuzingatia jinsia yake, yaani wanawake wote, na kuangalia maslahi ya jamii kwa ujumla wake, bali maslahi ya mwanamume vile vile na kuzingatia tofauti iliyopo kati ya mwanamke na mwanamme.

Maiko (Akimkata): Hapa haswa ndipo tulipofika katika chanzo chenyewe cha dhulma kilichoko kwa wanawake huko kwenu, tofauti kati ya mwanamme na mwanamke!....Hakika tofauti hizi mnazolingania ni thamani ilizojiwekea mfumo dume wa jamii za Mashariki, lengo lake ni kumtawala mwanamke na kustarehe nae….ni tofauti gani hizi?! Kwa nini basi mwanamke nae asipewe haki ya kuolewa na mume zaidi ya mmoja?! Je, hiyo sio dalili yenye kuthibitisha matamanio ya mwanamke katika jamii hii?!

Rashidi: Pole pole rafiki yangu, umenitupia mabomu ya maswali ambayo hatuwezi kuyakabili mara moja…tutayajadili yote hayo, hata hivyo acha tutegue mabomu haya, na tuanze na lile lililokuathiri. Je, huamini kuwa kuna tofauti kati ya mwanamme na mwanamke?

Maiko: Tofauti gani?

Rashidi: Kwanza kabisa….ni tofauti za kibailojia, kati ya maumbile ya kiwiliwili ya mwanamke na ya mwanamme!

Maiko: Bila ya shaka yoyote kuna tofauti za kibailojia, lakini kuna uhusiano gani wa tofauti hizi na maudhui yetu?!

Rashidi: Sitozungumza nawe kwa mtazamo wa kidini ambao ninaamini kuwa ni muhimu kwa mtu aliyejisalimisha nao na kuridhika nao, lakini nitazungumza nawe kwa mtazamo wa akili na elimu ulioutangaza mwanzo kuwa ndio unaoamini….nisikilize bwana:

Tafiti nyingi zilizofanyika hivi karibuni zimethibitisha kuwa kemia ya upendo kwa mwanamme inatofautiana na mwanamke; kiasi kilichopelekea taasisi nyingi za kielimu kufanya utafiti kwa kina kuhusu hisia za mapenzi kati ya mwanamme na mwanamke, wanazuoni wakapata matokeo ya kushangaza kuwa jeni za mwanamme humsukuma katika mahusiano ya

www.path-2-happiness.com

wanawake wengi, wakati ambapo jeni za kike zinamsukuma mwanamke katika utulivu katika uhusiano wa mtu mmoja, vivyo hivyo elimu leo hii imethibitisha kuwa mwanamme anaweza kumpenda zaidi ya mwanamke mmoja, bila ya mahusiano hayo kuathiri mapenzi kwa wengine.

Kadhalika mtandao wa CNN umemnasibisha Profesa wa Saikolojia katika Chuo Kikuu cha Utah State huko Marekani, Liza Diamond, kuwa kuna dalili za kibaolojia kuwa mahusiano ya mwanamme kwa wanawake wengi kijinsia ni jambo linalotokana na maumbile yao ya kiwiliwili.

Kundi la watafiti katika Chuo Kikuu cha Oxford huko Uingereza katika utafiti wao wa mwaka 2007 umethibitisha kuwa wanawake wako kinyume na wanaume; muda wao mwingi huelekezwa kwenye viwiliwili vyao na kwa watoto wao kwa sababu ya Homoni Oxytocin ambayo inazidisha wao kuwa karibu zaidi katika uhusiano wao na watoto wao.

Utafiti mwingine mpya umeashiria kuwa sehemu maalumu katika akili ya mwanamme ni kubwa zaidi ya mara mbili ya mwanamke, na huenda tofauti kubwa kati ya ubongo wa mwanamme na mwanamke ni kuwa wanaume wana sehemu maalumu inayoshughulika na hamu ya kijinsia kubwa zaidi mara mbili na nusu kulinganisha na ile ya mwanamke.

Je, hudhani kuwa tofauti hizi hazina athari?!

Maiko: Ikiwa taarifa hizi ni za kweli, basi bila ya shaka zitakuwa na athari.

Rashidi: Hivyo basi unachokielezea kuwa ni matamanio ya kinyama ya mwanamme, na mahusiano yake na wanawake wengi ni jambo lisilokuwa na uhusiano pekee na Uislamu na jamii ya Mashariki….Nami ninauliza swali naomba unijibu kwa ukweli na uwazi kama ulivyoahidi. Ni marafiki zako wangapi ambao hawana mahusiano na wanawake wengi? Sikusudii mahusiano yako peke yako.

Maiko: Hata kama unakusudia mahusiano yangu peke yangu, hili ni jambo linalojulikana huku kwetu na katika jamii zetu… lakini sio ndoa moja kwa moja.

Rashidi: Sawa, kinacholengwa katika jamii zetu kipo katika jamii yenu vile vile, pamoja na tofauti kubwa ambayo nitakutajia.

Hata hivyo nitakuzidishia juu ya hilo; Uislamu sio uliovumbua mfumo wa wake wengi, uhusiano na mfumo huu ulikuwepo tokea staarabu nyingi huko nyuma, na hakukuwa na kiwango maalum cha idadi kwa

mwanamme, kama ambavyo ilikuwa ni ruhusa katika dini zote za mbinguni hali hii iliendelea kuruhusiwa katika dini ya Uyahudi hadi karne ya kati pindi ilipotangazwa na mwanazuoni Giorshom Eshkanaz (960-1040) uharamu wa zaidi ya mke mmoja, ama kanisa halikukataza hilo isipokuwa katika karne ya kumi na saba, lakini katika baadhi ya makanisa ni jambo lililoruhusiwa hadi sasa, kama ilivyo kwa madhehebu ya Mormon.

Maiko: Kama ni hivyo, hayo yalikuwa ni mambo ya zamani, ama sasa hivi mwanadamu ameendelea na kustaarabika zaidi.

Rashidi: Maendeleo na ustaarabu hauwi katika kupambana na maumbile ya mwanadamu na kutoitikia haja zao na kuvuka juu ya maslahi yao, hailingii akilini kusemwa: Kuwa mwanadamu katika zama za kale alikuwa akila nyama za wanyama (ng'ombe, mbuzi na kondoo) na kuvaa sufi za kondoo na ngozi ya mbuzi, na kukabaki kuwa kula nyama na kuvaa sufi au ngozi ni matendo ya kukosa maendeleo na ya kinyama…. hata hivyo inaweza kusemwa: Kwa hakika maendeleo ya mwanadamu yanaweza kuyaendeleza matendo haya zaidi ili kuitikia zaidi haja zake na kudhamini zaidi maslahi yake na hili haswa ndilo lililoletwa na Uislamu.

Maiko: Kivipi?

Rashidi: Wewe unasema kuwa mahusiano ya mapenzi na kijinsia mengi yako nje ya duara la ndoa lililoenea katika jamii zenu za Magharibi, nayo ni dhulma yenyewe kwa mwanamke na ufisadi kwa jamii yenyewe, ni mahusiano ambayo hayapelekei katika utulivu wa nafsi wala hayathamini haki mbali mbali, wala kusimamisha jamii iliyosalimika, na ikiwa suala hili la wake wengi lipo katika staarabu za kale bila ya mipaka, Uislamu umekuja ukamfanyia uadilifu mwanamke pindi ulipoitikia haja zake na kumfanya mshirika wa kisheria katika ndoa, na ukaiwekea udhibiti na vifungo vya ndoa hii ili kudhamini kiasi kikubwa cha mafanikio ya taasisi hii ya familia.

Uislamu unachunga maslahi ya kila mwanamke, na umeweka mizani sawa sawa kati ya matamanio ya mwanamme na kuyaacha huru, na yote hayo kwa misingi ya taasisi ya kijamii ya kwanza ambayo imevunjika kwa kiasi kikubwa katika nchi zenu… familia.

Maiko: Lakini sensa ya kisomi inasema kuwa kiasi cha uzazi wa watoto wa kike ni sawa na wa kiume takriban, na ukitekeleza misingi ya wake wengi basi watabakia baadhi ya wanaume bila ya wake, na hili vile vile litakuwa ni jambo la hatari.

www.path-2-happiness.com

Rashidi: Ikiwa takwimu za kisomi zinathibitisha hilo, na huthibitisha kuwa wastani wa umri wa wanawake ni mkubwa kuliko wastani wa umri wa wanaume, katika ulimwengu wa Magharibi huishi wanaume kwa wastani wa umri wa miaka saba kwa upungufu wa wanawake, na tofauti hii inazidi kila mara kwa karne iliyopita, kwa mfano: Huko Ujerumani hufikia umri wa mwanamke miaka themanini, ama mwanamme hufikia wastani wa umri wa miaka sabini, wakati ambapo tofauti hii ilikuwa ni ya miaka miwili tu katika mwaka 1900.

Mwanazuoni Daniel Kroger kutoka chuo kikuu cha Michigan huko Marekani anasema: Katika nchi nyingi ulimwenguni mwanamme anaishi katika umri pungufu kwa mwanamke na anaongeza 'Kroger' moja katika sababu ya tofauti hii, ni tofauti ya homoni kati ya mwanamke na mwanamme; kwani homoni za mwanamme hurutubisha jeni ambazo husababisha maradhi ya moyo na mzunguko wa damu.

Naongezea hilo: Uwezekano wa vifo vya wanaume vinavyotokana na vita katika nchi zenye migogoro ni mkubwa, pia mara kwa mara wanaume hufariki kutokana na kazi ngumu na za hatari wazifanyazo, mbali na matukio mengine mbali mbali ambayo wahanga wake wengi ni wanaume.

Yaani, idadi ya wanawake katika jamii mbali mbali inazidi idadi ya wanaume, na hii ni hali halisi inayoshuhudiwa na takwimu za nchi nyingi ulimwenguni, kuongezea tatizo la wanaoachwa wajane.

Je, wanawake hawa ambao hawakuolewa wataachwa wakiendelea kupata matatizo haya ya kinafsi na ya kijamii na ya kitabia, au wasukumwe kuomba haki zao na kushibisha matamanio yao ya kimaumbile kwa kificho, jambo ambalo linawaathiri wao na kuiathiri jamii kwa ujumla, au waendelee kufuata mfumo wa kijamii ambao utaitikia haja za jamii katika mipaka ya udhibiti wa kisheria ambayo huchunga uwezo wa mazingira ya mwanadamu, na kudhamini hilo litimie kwa njia ya uadilifu, bila ya kuwepo dhuluma au msukumo kutoka upande wowote ule?.

Hilo lilijibiwa na mwanazuoni wa mambo ya jamii Mfaransa Dr. Gustav Lubon, aliposema: "Ama kwa hakika mfumo wa wake wengi wa Mashariki (akikusudia Uislamu) ni mfumo mzuri unaonyanyua kiwango cha tabia za mataifa, na familia huzidi kushikamana na humpa mwanamke heshima na furaha ambayo haipatikani Ulaya."

Tafadhali nipatie glasi ya juisi ya ndimu na kikombe cha chai.

Waridi Lenye Kuvuja

www.path-2-happiness.com

Waridi Lenye Kuvuja

Rashidi alipokaa tu kwenye meza alitoa ‘laptop’ yake na alipokuwa akishughulika kuiwasha Rashidi akamwambia **Maiko:**

Leo hii nitakuonesha kipande cha video nadra kuonekana, kipande cha nusu dakika tu, lakini si cha kawaida, kwani itatubeba na kutupeleka katika historia na zama zake, muda wa karne hivi.

Kwa kujali hayo kichwa cha **Maiko na Rashidi** vilikaribia ‘skrini’ ya laptop yake na macho yao yakalenga skrini.

Maiko: Oooh nzuri sana! Ni kiasi gani nilivyofurahi hali naangalia maisha yalivyo Uingereza, nchi yangu, maisha ya miaka mia moja iliyopita, angalia furaha katika nyuso za wapitao barabarani… mwangalie mtoto huyu na furaha aliyonayo! Yalikuwa ni maisha ya kawaida kabisa… ni maisha yaliyo karibu kabisa na nafsi ya mwanadamu.

Rashidi: Nitarejea kuonesha video hii ili uone jambo lingine muhimu.

Rashidi akiirejesha tena ‘klipu’ ile ya video huku akiendelea na mazungumzo yake na **Maiko:**

Angalia! Huyu mwanamke, na huyu wa pili, wanawake watano, angalia pamoja nami, wote hakionekani kwao isipokuwa kichwa kilichofunikwa kwa kofia na glovu, na mavazi yao ni mapana hayaonyeshi miili yao.

Maiko: Kweli kabisa.

Rashidi: Kama ni hivyo ni kitu gani kilichotokea?

Maiko: Kuhusu nini?

Rashidi: Katika jamii zenu.

Maiko: Unakusudia watu kwenda uchi na upungufu wa heshima?!

Rashidi: Haswa, lakini inaashiria vile vile kuwa hali hiyo inatokana na kuanguka kwa mfumo wa kimaadili kwa ujumla.

Maiko: Huu ni uhuru wa mtu binafsi, leo hii sisi ni jamii inayotukuza uhuru, na kila mmoja anayo haki katika kuchagua mfumo wa maisha autakao.

Rashidi: Bila ya shaka nafahamu hilo, jambo hili linahitaji mtu kufanya kikao au vikao vya mjadala kulizungumzia kwa umakini, hata hivyo kinachonivuta mimi ni kule kukubaliana kwenu kijamii kwa mabadiliko haya ya kimaadili na wote wakirejea katika rejea moja katika uchaguzi wenu.

Maiko-Haijifichi kwako kuwa kuna kinachoitwa ‘Utamaduni wa jamii’, na ndio ambayo watu hubadilika wakafanya matendo wanayofanya watu bila kurejea kwenye rejea, bila ya watu kushangazwa au kupingwa, na kupitia tamaduni hii huenda ikatokezea tofauti za aina kati ya chaguzi za mtu binafsi….

Rashidi: Ni nzuri sana, tukichukulia hali hii na tukitafiti kilicho cha sawa na makosa ndani yake, tutaona kuwa kitabu chenu kitakatifu kinalingania kwenye kujiheshimu na kutoonyesha mapambo; imekuja katika barua ya Paulo ya kwanza kwa Thimotheo (2:9-10)

“Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu.”

www.path-2-happiness.com

Maiko: Ewe bwana haya yanawafaa wale wanawake wenye kujinasibisha na Kanisa tu, ama sisi katika maisha yetu nje ya Kanisa nilishawahi kukuambia hapo kabla kuwa, sisi tumekataza dini isituingilie katika maisha yetu tokea zama za mwanga na mwamko.

Rashidi: Lakini ewe rafiki yangu klipu hii tuliyoiona kuhusu wanawake wenye kujiheshimu barabarani na sio kanisani, na hilo ni baada ya hizo zama unazozitaja za mwamko, tena baada ya kupita karne nyingi….na hata kama nikikubaliana nawe kuwa dini haina nafasi katika maadili yenu bado ninajiuliza: Nini kilichotokea?! Nini kilichowabadilisha wanawake wenu kwenda kwenye hali hii ya kwenda uchi?!

Maiko: Wewe unaona jambo ambalo hukulizoea kwa mtazamo wako, lakini mimi naliona ni jambo la kawaida tu, hebu nikuzindue jambo katika klipu ile, nayo ni picha katika msimu wa baridi kali au kwa ujumla ni wakati wa baridi, na hili linaonekana katika mavazi ya wanaume na watoto katika msimu huu wa nguo zenye kiza….Huenda hali hiyo mnayodhania inatokana na sababu ya hali ya hewa ya baridi, hata hivyo haikatazi ukweli wa mambo kuwa; wanawake katika zama hizo walikuwa katika hali ya heshima zaidi na hata baada ya muda huo kwa wakati mrefu, ama ni nini sababu ya kilichotokea? Ni kwa sababu maadili na mitazamo ya watu imebadilika kutokana na maendeleo ya jamii.

Rashidi: Hii ni kadhia nyingine ambayo itabidi tuipangie muda wa kikao chake, nayo ni masuala yanayohusu maadili, mimi pamoja na ufahamu wangu kuhusu sayansi na njia zake, naona kuwa maadili yanatofautiana na kufuata kwake maendeleo haya unayoyasema.

Maiko: Hamna neno tulipangie hilo muda wake wakati mwingine, lakini hebu nikuulize bwana Rashidi, kwa nini nyie siku zote mnajali kumuangalia mwanamke kama kiwiliwili tu? Kwa nini jambo hili linawashughulisheni sana?!

Rashidi: Uislamu unamuangalia mwanamke na mwanamume kuwa wao ni wanadamu, na mwanadamu ameumbwa kutokana na kiwiliwili, roho na akili, hatuwezi hata mara moja kupuuzia chochote katika hayo, sio tu kiwiliwili chake, bali hata ile hisia ya uhayawani ndani ya mwanadamu, mwanadamu huyu hawezi kuwa juu na kupaa ili afikie kwenye kiwango cha juu ila kupitia mfumo kamili uliokamilika, ambapo ndani yake kuna maadili na masuala yake ya kiroho pamoja na taratibu za kijamii na kisheria, na nyie mlipodhani kuwa mmepata mwanga wa maendeleo na kutenganisha Kanisa, au kwa lugha nyingine dini na maisha, na kuridhia kwenu Kanisa kujitenga na mambo yake ya kiroho ili akili ijitupe nje ya mipaka ya dini na kiwiliwili, kuwa huru na kufanya mkitakacho, na kwa ajili hii shetani amepata uhuru mkubwa katika ustarabu huu wa kustarehe, kama anavyostarehe hayawani nje ya mipaka ya kimaadili na kidini, ili kushibisha matamanio yao ya kinyama na kuhamasisha mwanamke kuonesha maumbile yake kwa njia nyingi.

Maiko: Hata hivyo tunawaona wanawake wakiwa katika hali hii ya kwenda uchi asubuhi na jioni, wala matamanio haya unayoyaita ya kinyama hayatushughulishi.

Rashidi: Je, unadhani kuwa hiyo ni fadhila au maadili mazuri? Kwa hakika adhabu ya mtu aliyezoea kuangalia hali zenye kuhamasisha kama hizo ni mtu kupatwa na hali ya ubaridi wa jinsia, na linafuatiwa na dhara jingine kubwa kuliko hilo, nalo ni kuendelea kutafuta kitu kingine chenye kuhamasisha zaidi sio kile alichokizoea, kitu ambacho kinapelekea katika hali isiyokuwa ya kawaida ya kimapenzi.

www.path-2-happiness.com

Maiko: Hizo athari au madhara unayosema yapo ya namna mbali mbali; kuna ya karibu na ya mbali.

Rashidi: Ndio kuna madhara yanayofuatia hali hii hadi mtu kufanya uhalifu; na kama mtu hakupatwa na ubaridi huu wa jinsia kwa sababu ya mazingira ya kiwiliwili chake au kwa sababu za kijamii au za kimalezi, basi mtu huyu atapatwa na mfazaiko wa jinsia na matokeo yake yatakuwa ni kuongezeka kwa ubakaji, na hili ndilo haswa linalosajiliwa katika takwimu za matukio ya ubakaji, acha nikutajie kidogo:

Takwimu za Wizara ya Ndani ya Ufaransa imeashiria kutokea kwa matukio 4,412 ya ubakaji katika kipindi cha mwaka mmoja, yaani takriban wastani wa tukio moja kwa kila masaa mawili.

Huko Uingereza Polisi walifanya operesheni kubwa katika jiji la London kwa ajili ya kuwahamasisha wanawake kujifunza fani za kujilinda mtu binafsi, badala ya kusalimu amri pindi anapovamiwa na wanaume, na hiyo ni baada ya tangazo la kuzidi kwa uhalifu wa kutumia nguvu na ubakaji katika jiji la London kuwa asilimia 11% (kumi na moja) kwa muda wa mwaka mmoja.

Ama Amerika: Kituo cha wahanga cha taifa kimetangaza kunusuru haki za wahanga wa matumizi ya nguvu: Na wastani wa ubakaji uliopo Marekani imefikia 1.3% (asilimia moja nukta tatu) ya mwanamke aliyebaleghe kwa dakika moja, na kituo kiliongeza: Mwanamke mmoja kati ya wanane waliobaleghe huko Marekani walikumbwa na ubakaji, na hiyo ni mwaka 1991.

Ama katika mwaka wa 2009 takwimu zinaashiria kuwa mmoja katika kila wasichana watatu wa umri wa miaka 14 (kumi na nne) hubakwa, na ndani ya Marekani kuna nusu milioni ya ubakaji kila mwaka, na ya kuwa asilimia sitini na moja (61%) ya wasichana wa Kimarekani wamepoteza bikira zao kabla ya umri wa miaka kumi na mbili (12).

Kuna aina zingine za uhalifu, huitwa uhalifu wa kunyamaziwa, nayo ni kushambuliwa kazini kwa wanawake walio chini ya wakubwa wao kazini, kwa kawaida matukio haya hayaripotiwi; kwa sababu ya hofu ya mwanamke kuhusu kazi yake au tamaa ya kupata fidia au ugumu wa kuthibitisha.

Bila shaka namba hizi haziwakilishi ukweli wote; kwani kituo cha kuhamasisha wanawake wanaobakwa kinakadiria kuwa asilimia 35 (thelathini na tano) hunyamaziwa na kutoripotiwa ukilinganisha na asilimia moja tu inayotolewa taarifa yake.

Maiko: Hata hivyo tatizo kama la ubakaji ni tatizo gumu, lina mambo mengi ndani yake, kama vile kinafsi, kimalezi na kijamii, bali hata kiuchumi vile vile.

Rashidi: Hili ni kweli, hata hivyo hatuwezi kukana kuwa moja ya matatizo makubwa: Ni ile hali ya watu kushawishiwa kijinsia walau kwa kuangalia tu, kinachovutia kuangalia ni kuwa utafiti wa Marekani umefikia kuwa: uhalifu wa ubakaji hupungua wakati wa baridi, na huenda upungufu huu unatokana na kupungua kiwango cha wanawake kuvaa mavazi ya uchi, au ni kwa sababu watu hawatoki sana nje muda huu; kinachofanya kuwepo kwa nafasi ndogo ya kukutana, na hali zote mbili hizi zinathibitisha sababu yenyewe.

Maiko: Lakini mwisho wa siku ni kuwa wanawake wenyewe ndio wanaotaka hayo kwa matakwa yao, huo ni uhuru wa mtu binafsi kama nilivyokuambia, wala hatuwezi kuwazuia hilo.

Rashidi: Hili ndilo linaloonekana kwa nje, lakini ukweli ni kuwa

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

viongozi wa jamii ya Magharibi wakiongozwa na wanaume, ndio ambao wamepelekea utamaduni huu wa kwenda uchi, na wakaupamba, na wakautayarishia mazingira saidizi, na wakavumbua njia rahisi za kuusambaza; ili wastarehe na mwanamke bila ya kuwepo kizuizi bali wao wameweka sheria zenye kudhulumu stara ya mwanamke, maisha yake na udhaifu wake; hivyo basi sheria iliyotungwa huko Magharibi huwa ni laini kwa hali ya mwanamume mbakaji zaidi kuliko inavyomuonea huruma mwanamke aliyebakwa; kitu ambacho kinasaidia kuhamasisha ubakaji, bali baadhi ya nchi za Magharibi zinahesabu ubakaji kuwa ni katika makosa ya maadili na sio miongoni mwa uhalifu wa kutumia nguvu.

Chukua mfano huu: Huko Finland, moja katika nchi inayohesabika kuwa iliyoendelea sana katika kumjali mwanamke, mtu mmoja alimlazimisha mwanamke kufanya nae mapenzi katika benchi la walemavu katika maegesho ya magari akimpigiza mwanamke yule kichwa chake ukutani na mikono yake nyuma ya mgongo wake, kulingana na mwendesha mashtaka jambo hili si ubakaji, kwani matumizi ya nguvu yaliyotumika yalikuwa madogo!!! Na yule mtu alilaumiwa kwa kumlazimisha muhanga wake kufanya tendo la ndoa na akahukumiwa jela kwa masharti (pamoja na kusimamisha utekelezaji wake) kwa muda wa miezi saba!!

Ewe rafiki yangu! Ni jamii ipi yenye amani kimaadili, ni jamii yetu ya leo hii, au ni ile jamii ya tokea karne iliyopita?! Je, ungependa kuangalia klipu mara nyingine?!

Maiko: Jambo lipo wazi bwana Rashidi, lakini kwa mtazamo wa Uislamu mnalionaje jambo hili?

Rashidi: Jambo hili linahitaji kikao, bali vikao vingine ili kulijadili.

Sitara ya Kimaadili

www.path-2-happiness.com

Sitara ya Kimaadili

Rashidi alikutana na Maiko kulingana na ahadi waliyowekeana kati yao pembeni ya stesheni ya treni inayosafiri Paris kupitia English Channel… walitafuta kiti wakakaa wakisubiri muda wa kuondoka treni.

Maiko: Nadhani wakati unatutosha kubadilishana mazungumzo kuhusu mtazamo wenu juu ya mavazi ya mwanamke… utanieleza kuhusu Hijabu …….au sivyo?I

Rashidi: Watu wengi wanaamini kuwa Hijabu ni vazi la kufunika kichwa tu, wala watu hawajui kuwa Hijabu ni fikra na mfumo wa kijamii… yatupasa kuangalia jambo hili kwa mtazamo huu.

Maiko: Nimekuona umeandaa maudhui haya na umeyapa uzito mkubwa zaidi usiostahiki!

Rashidi: Sisi tunaona watu wakitofautiana katika kuweka vigezo vya kuisitiri miili yao, na kila kundi linaona kuwa, vigezo vyake ndio maendeleo na ustarabu, wakati ambapo kundi moja linaliona kundi lingine kuwa halijaendelea, na hawa huwaangalia kundi lingine kwa mtazamo wake wa kimaadili na kifikra tu. Hivyo basi hapana budi kuwepo na maafikiano ya marejeo ya mipaka ya sifa za jumla kwa upande wa sitara yake ya mwili.

Jambo hili ni kama nilivyokuambia kwa upana wake, ukiniruhusu kwanza nikuoneshe baadhi ya misingi ambayo itaweka karibu mitazamo yetu.

Maiko: Haya karibu.

Rashidi: Nadhani kuwa sisi tunakubaliana kuwa haiwezekani kupata suluhisho katika masuala ya maisha ya msingi ya mwanadamu isipokuwa baada ya kufahamu undani wa mwanadamu na kufahamu ukweli wa maarifa yake kamili.

Maiko: Hii ni hali ya kawaida.

Rashidi: Nadhani maendeleo makubwa ya kielimu yaliyofikiwa na tunayoendelea kuyaona, ni dalili ya mipaka ya elimu ya mwanadamu, yale yaliyokuwa yamejificha kwake jana, leo hii yapo wazi, na yale ambayo ulikuwa ukiyaamini jana, husahihishwa leo hii, na hivi ndivyo vile vile mwanadamu anavyovumbua-kesho na ya kuwa leo hii alikuwa ni mjinga au kwa uchache wa elimu yake ilikuwa na mipaka. Jambo hili limetajwa katika Qur'an, "Na wanakuuliza khabari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo tu." (17:85).

Maiko: Naafikiana nawe, lakini kuna uhusiano gani wa yote hayo na maudhui yetu?!

Rashidi: Hebu nisubirie rafiki yangu sijakamilisha bado, kwani tutakapo kubaliana kuhusu hilo baadae tutajua kuwa kuna sehemu zilizojificha katika masuala haya ambazo hatuwezi kuziingia katika kina chake, na hii ni kutegemea na kujitenga na matamanio yetu binafsi na taathira za mazingira, na hili ni gumu kulikwepa. Na hata kama tutashughulikia masuala haya katika njia hii basi tutakutana na pingamizi, na mipango ambayo tutaichukua katika msingi huu itakuwa ni pungufu au potofu, si hivyo tu, bali inaweza kuwa ni njia iliyo kinyume na njia sahihi ya kutatua tatizo na kuleta suluhisho.

Maiko: Bila shaka haya ni matokeo ya kimantiki, lakini kwa upande mwingine hakuna mbele yetu isipokuwa kutumia akili zetu zenye

www.path-2-happiness.com

kutufikisha kwenye fikra na maarifa, na kuzama ndani ya utafiti, makosa na masahihisho ni bora kuliko kuacha mambo bila uvumbuzi na utatuzi na kusubiri mtu kufikia kwenye nukta ya kulingana ambapo mambo yake yatanyooka.

Rashidi: Kama ni hivyo wewe unakubaliana nami kuwa suluhisho ni lazima liwe na sifa ima ya kuzidisha au kupunguza, lakini wewe unaona kuwa tunalazimika katika hilo, na ya kuwa hakuna mbele yetu uchaguzi mwingine zaidi ya huo.

Maiko: Naam, ninaona hivyo.

Rashidi: Ama sisi tuna uchaguzi mwingine pembeni ya mambo haya.

Maiko: Unakusudia nini kusema: “Sisi!? Na lipi hilo suluhisho?

Rashidi: Ninachokusudia: Sisi Waislamu tuna uchaguzi ambao tunauona ni uokozi (ukombozi) wa ulimwengu na uchaguzi huu unahitimisha kuwa aliyeumba watu ndio anaowafahamu zaidi, kama alivyosema Allah: “Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?” (67:14), na yeye Allah peke yake ndie ajuaye wasifu wa mwanadamu na kile anachokihitaji na kinachomfaa na kile kisichomfaa, na wakati huo huo Allah ametakasika dhidi ya matamanio ya mwanadamu, hisia na mwelekeo wake, kwa hivyo basi Allah pekee ndie mwenye uwezo wa kuweka mfumo mzuri kwa mwanadamu kwa hekima na ulinganifu, na hili linaonekana wazi katika Qur’ani.

Maiko (Akimkatisha): Maneno yako yameshikamana vizuri bwana Rashidi, hata hivyo usisahau kuwa mimi siamini dini yako, hivyo usinilazimishe kwa jambo ambalo siliamini…..niambie lile ambalo tumeafikiana kama tulivyokuwa tukijadiliana.

Rashidi: Pamoja na kuwa kanuni hii ni msingi ambao kila Muislamu amejisalimisha nao, ninaamini inampasa kila mwanadamu, isipokuwa sioni tatizo kuwa tukamilishe mjadala wetu kama utakavyo, lakini bila shaka katika mwanga wa kujitosha mwenyewe, yaani: Katika mipaka ya mfumo wa kijamii ambao nimekutajia hapo kabla kuwa hijabu ni sehemu katika mfumo huo…

Maiko: Hakuna neno.

Rashidi: Nilikuambia katika kikao kilichopita: Sisi hatuwezi kusahau nafasi ya kiwiliwili kwa mwanadamu, bali hata ule uhayawani wake, mwanamume kwa tabia ya maumbile yake anavutika na mwanamke na cha mwanzo anachokitamani ni kiwiliwili chake; katika hilo basi mavazi ambayo yataonesha kiwiliwili chake yatamletea matamanio mwanamume na kumshawishi mwanamume kumshambulia au kumtongoza mwanamke.

Maiko: Mimi naona katika mtazamo huo kuna kumdhalilisha mwanamke na mwanamume pamoja, kumdhalilisha mwanamke ni kumuangalia kuwa mwanamke ni kiwiliwili tu na kupuuza akili yake, maarifa na maadili yake, na kumuangalia kama vile ni mtu mpungufu ambaye hawezi kujihifadhi mwenyewe, na kwa upande mwingine ni kumdhalilisha mwanamume kwa mtazamo kuwa mwanamme anaonekana kama mnyama mkali mwenye kushambulia muhanga wake (mwanamke).

Rashidi: Je, rafiki yangu unaona mwanamke anaposimama mbele ya kioo ili ajipambe na kuchagua nguo zake zenye kuvutia huwa anafanya hivyo ili aridhishe akili ya mwanamme au maadili yake? Au kwa uchache hufanya hivyo ili amvutie mwanamume, na kama sio kwa kumfanya avutike kwake na kumuwinda? Na je unaona kuwa mwanamume

www.path-2-happiness.com

anapomuangalia mwanamke mzuri aliyejipamba na kupendeza atavutika kwa upeo wa akili yake na hulainika kwa mapenzi katika upana wa utamaduni wake pindi anapomuangalia mara ya kwanza?

Sote tunajua kuwa mwanadamu yupo katika hatua tofauti katika silika, matamanio na matayarisho ya kuvuka vigingi, kama walivyo katika viwango tofauti vya fadhila na adabu, na mwanamke mwenye kuvaa hijabu huonekana kuwa ni mwenye heshima na hapendi kuwavutia wanaume ili wamtongoze, na hivyo hawi kivutio kwa watu wenye nafsi dhaifu na maadili mabaya. Qur'an imelitaja hilo kwa uwazi kuwa hijabu humkinga mwanamke dhidi ya ufasiki.

Maiko: Hata hivyo bwana Rashidi mimi ninaona kuwa tabia za baadhi ya wavaa hijabu hazilingani na maadili mema, na hili linathibitisha kuwa jambo hili linarejea kwenye dondoo zingine zisozokuwa uvaaji wa hijabu; kama vile malezi na kushikamana na maadili mema.

Rashidi: Maneno yako yana sehemu ya ukweli, mtu asidai kuwa kwa kuvaa kwake kipande cha kitambaa basi atabadilika kuwa mwanamke mwema, lakini hili halimaanishi kuwa asivae hijabu, hata kama mtu atasifika na tabia njema, au ya kuwa daktari aliyekosea au kutumia vibaya utaalamu wake hiyo haina maana kuwa kasoro ipo katika utaalamu huu, lakini humaanisha kuwa mtu huyu mwenye makosa anahitaji kunyooshwa, hivyo basi daktari huyu au mwanamke huyu aliyevaa hijabu au wengineo mfano wao, ni wanadamu, hutokewa na udhaifu wa kibinadamu.

Kwa upande mwingine Uislamu ulipoweka sheria ya hijabu kwa wasifu wake ukaiwekea kanuni ya kutoangukia kwenye machafu au katika hatua zake haujaishia kwake tu, bali umehusisha mfumo kamili kama vile maadili mbali mbali, na ukawekea mipango; ili kudhamini kufika katika viwango vya juu vya maadili mema katika maisha ya mwanadamu, na kwa ufupi: Mwanamke mwenye maadili mema huvaa hijabu, na sio lazima kuwa kila mwanamke mwenye kuvaa hijabu ndio mwanamke mwema.

Maiko: Lakini hilo halimaanishi mtazamo hasi kuwa kiwiliwili cha mwanamke kinafanana na ushetani? Je, yatupasa sisi kuchukizwa na kiwiliwili hiki?!

Rashidi: Uislamu ulipoweka wajibu wa hijabu haikuwa hivyo kuwa kiwiliwili cha mwanamke ni kiovu, inabidi kifunikwe, bali umewajibisha hilo ili hisia za mwanamme za kijinsia (za kimaumbile) zisihamasishwe, na haswa zaidi kwa wale wenye nyoyo dhaifu na tabia mbovu. Hivyo Uislamu ukaweka sheria ya hijabu kumlinda mwanamke na kuvamiwa na kubakwa na wanaume, na kadhalika kumlinda mwanamme na kutofanya zinaa–kama ambavyo sheria ya Kiislamu ilivyojali kubakisha hisia za mapenzi na hamasa za kijinsia katika mipaka ya mahusiano ya ndoa pekee, na hilo hupelekea kwenye mshikamano wa kijamii.

Maiko: Lakini ewe bwana Rashidi, ikiwa hijabu ni kinga dhidi ya mvuto wa mwanamume kwa mwanamke, kwanini basi wanaume nao wasivae hijabu vile vile ili iwe ni kinga dhidi ya wanawake kwa wanaume, kwani mwanamke hana matamanio kama alivyo mwanamume?

Rashidi (Huku akicheka): Swali zuri…Kwa hakika Uislamu umewajibisha nguo kwa mwanamume kwa uchache kuliko ilivyo kwa mwanamke, na huenda hekima katika hilo ikawa inaonekana kwa zaida ya maarifa ya wasifu wa kila mmoja. Utafiti uliofanywa na Dr. Benjamin Hayden huko Marekani hivi karibuni umethibiisha kuwa mwanamume hufurahishwa na kuona ladha kwa kumuangalia mwanamke, kwani katika akili yake kuna sehemu ambayo humsukuma mwanaume kufanya

www.path-2-happiness.com

jitihada ya kumtazama mwanamke mzuri kwa matamanio, wakati ambapo mwanamke hafanyi juhudi hizo kumuangalia mwanamume mwenye kuvutia. Dr. Benjamini Hayden ni mtaalamu wa vichwa na ubongo wa wanadamu katika chuo kikuu cha Duke. Maelezo haya yameandikwa katika jarida la “Berlin Morgon Post la Ujerumani.

Kupitia utafiti huo waliangalia na kutafuta sababu ambazo zinamsukuma mwanaume kutumia juhudi hizo ili kujistarehesha kwa kumtazama mwanamke mzuri mwenye kuvutia, na kinyume chake ni sahihi kulingana na mwanamke, na ikabainika kuwa tofauti iliyo wazi kati ya mwanamke na mwanamume, ipo kwenye ubongo ambapo katika ubongo wa mwanamume kuna sehemu ambazo zinakuwa na nishati zaidi, pindi anapomuona mwanamke mzuri, na hilo ndilo linalomfanya kuhisi raha na kustarehe, ama mwanamke hali yake ni tofauti, kwani yeye haathiriki kwa hali yoyote ile anapomuona mwanamume mwenye kuvutia.

Matokeo ambayo utafiti huo umeyatoa ni: jambo la kwanza lenye kuvuta mtazamo wa wanaume katika sura za wanawake wazuri ni uso, (wa mwanamke) wakati ambapo mwanamke huangalia sura haraka haraka bila kuangalia sehemu maalum.

Nukta nyingine: Ni kuwa, mwanamume ni jasiri zaidi na mwenye kuthubutu katika kushambulia kuliko mwanamke; ambapo utafiti umedhihirisha kuwa, ujambazi kwa mwanamume huzidi mara tano ya mwanamke, hivyo basi kama mwanamke ataamua kufunga mlango katika kuhamasisha na kutochukua hatua ya kwanza, basi atafunga milango ya mwanamume kuthubutu na kuvuka mipaka yake au kumshambulia.

Maiko (Akifanya haraka): Nadhani wakati umefika kupanda treni…. haya twende.!!

Mwanamke ni Malkia

www.path-2-happiness.com

Mwanamke ni Malkia

Baada ya treni kuanza kuondoka, marafiki wawili, Rashidi na Maiko walikuwa tayari kuanza mazungumzo yao wakati wa safari.

Maiko: Tumezungumzia mambo mawili yanayohusu haki za mwanamke: wake wengi na hijabu… Nini rai yako tukamilishe mambo yaliyobakia kuhusu maudhui haya?

Rashidi: Fikra nzuri, huenda katika hilo tukafunga faili letu.

Maiko: Jambo la kwanza linalonijia akilini mwangu katika maudhui haya ni kwa nini Waislamu wameshikilia mwanamke kutoshiriki kama mwanamume katika nyanja za maisha?

Rashidi: Sisi ewe rafiki yangu tunaposema kuwa mwanadamu ana sehemu ya maada au ya uhayawani, haina maana kuwa wasifu wa sehemu hii na malengo yake au matunda yake katika uhayawani; kuna tofauti kubwa; sisi tunakuta kuwa kuna muelekeo mkubwa zaidi wa kijinsia kwa mwanadamu kuliko kwa mnyama, wakati ambapo nguvu ya kujaamiana ni dhaifu zaidi mara nyingi kuliko muelekeo huu, kinyume cha mnyama.

Tukichukua kwa mazingatio kilichowekwa katika maumbile ya mwanamke (mbali na matamanio ya kijinsia) kama vile haya, heshima, kujizuia, na unyoofu, bila shaka tunatohoa kutokana na hilo na yaliyotangulia kuwa makusudio ya kuwepo kwa nguvu ya mvutano wa kijinsia kwa mwanadamu ni kufanikisha mawasiliano ya kudumu baina ya wanandoa na sio kuishia kwenye kila matamanio ya kijinsia katika utendaji wa kijinsia, na hilo ndilo lililoelezwa ndani ya Qur'ani mara nyingine kwa "utulivu" na mara nyingine, "upendo na rehema". Huu ni kwa upande wa nafsi… nataraji maneno yangu yako wazi.

Maiko: Takriban yapo wazi.

Rashidi: Kwa upande wa kibaolojia, utafiti umethibitisha kuwa mwanamke anatofautiana na mwanamume katika kila kitu. Katika umbile la nje, hadi maungo ya ndani, hadi katika seli za kiwiliwili chake; seli za mwanamke zimepigwa muhuri wa kike, na umbile lake linatofautiana na la mwanamume, mfumo wa kiwiliwili chake umewekwa na kuandaliwa kwa ajili ya kuzaa watoto na malezi yake, yaani ili uwiane na wadhifa wa mama, na pindi anapofikia baleghe humjia hedhi ambayo kwayo kila

kiungo cha kiwiliwili chake kinaathirika nayo, hata hali yake ya kinafsi na ya kiakili inaathirika, hapo bado hatujazungumzia kuhusu hali ya mimba, nifasi na kunyonyesha.

Bali Homoni na hali ya kinafsi ya mwanamke inatofautiana na ya mwanamume, hivyo kwa mkabala wa maisha ya ujasiri ya mwanamume na kuthubutu kwake tunakuta haya ya mwanamke na kudeka kwake.

Na kwa upande mwingine: Mtoto wa mwanadamu anahitaji (tofauti na wanyama wengine) uchungaji na malezi ya wazazi wake kwa miaka mingi, kwani mtoto wa kibinadamu huchelewa kukamilika nguvu na uwezo wa kujitegemea katika maisha, na hili ndilo linalotakiwa mahusiano ya mwanamume na mwanamke yasiishie kwenye mahusiano ya kijinsia tu, bali kuvumilia kwake ndio matunda ya mshikamano wao na kushirikiana kwao katika maisha, na kwa ajili hii vile vile mwanadamu ameumbwa kuwa na fikra ya kuwapenda watoto wake mapenzi makubwa ambayo wanyama wote hawana.

Maiko: Baada ya hayo ni nini?

Rashidi: Kwa kifupi ni kuwa hili linathibitisha kuwa familia ndilo umbo la kijamii la kawaida kabisa la mwanadamu, na tunaweza kuweka wazi nafasi ya kila mtu na wadhifa wake katika umbo hili au umoja huu, nayo ni nafasi inayolingana na malengo ya umoja huu wa mshikamano na tabia yake (makazi, mapenzi na huruma), na yanalingana vile vile na uwezo wa kila mtu.

Maiko: Nimefahamu unachokusudia, kwa maana hiyo duru ya familia ni kueneza roho ya mapenzi ili kuhakikisha utulivu wa nafsi ya familia na kuwachunga kwa kuwalea mume na watoto.

Rashidi: Sawa kabisa, na nafasi ya mwanamume ni kuhakikisha kuwa familia inapata mahitaji yake, na yote yanayohitajika katika kupambana na kukabiliana na hali ngumu na mashaka juu ya hayo.

Maiko: Lakini mtazamo huu unatufanya tupoteze nusu ya uwezo wa uzalishaji katika jamii.

Rashidi: Kinyume kabisa; mtazamo huu unatufanya tuipate jamii yote, lakini kila mmoja katika nyanja yake stahili; mwanamke anapopambana na maumbile yake na kutoka nje akisongamana na wanaume kazini kwa hilo anapata tabu kubwa kwa kazi yake mpya, na familia yake inapata shida na kutaabika; na hilo limepelekea jamii nzima kupata shida. Katika

www.path-2-happiness.com

hali hiyo mwanamke amejaribu mno kusawazisha baina ya kazi yake na shughuli zake za nyumbani na kuwalea watoto wake lakini hakufanikiwa; kwani hilo litamfanya awe mke mtulivu na mama mwenye huruma lakini wakati huo huo awe mwanamke mchapa kazi kazini, yote hayo kwa pamoja atayapata wapi? Hivyo matokeo yakawa kuingia katika ncha nyingine, ili kujaza faragha ile ambayo mwanamke ameiacha, na sehemu hizi zilizojaza nafasi ambayo aliiacha, na ncha hizi hazikuwa matarajio au stahili kwa ajili ya majukumu haya, na kuongezea hilo: Wanawake kusongamana na wanaume kazini nje ya nyumba zao kumemfanya mwanamke kukumbwa na matatizo ya kushambuliwa na wanaume na kinachofuatia baada ya hapo miongoni mwa yanayoambatana na hayo, kama vile kumtongoza, kumbaka na mengine dhidi yake, na kazi anazochagua wakati wa kazi zake katika aina nyingi za kazi anazozifanya nje ya nyumba yake.

Maiko: Tunapozungumzia nafasi ya mwanamke katika maisha kama ni nafasi ya familia, basi hilo linatusukuma katika mazungumzo ya jambo lingine, ambalo naliona kuwa linambagua mwanamke au lipo dhidi ya mwanamke, jambo hilo ni usimamizi wa mwanamume kwa mwanamke.

Rashidi: Usimamizi wa mwanamume hauna maana kumbagua mwanamke, bali ni mfumo wa kitaasisi katika jamii ambao unaitwa familia, taasisi yoyote lazima iwe na mipaka yake ya kazi na mgawanyo wa kazi na wadhifa wa kila mmoja, pamoja na kujali uwezo wake wa kiutendaji, na kwa maana hiyo mkurugenzi kazini utu wake sio mkubwa kuliko muhasibu au mfanyakazi mwingine au anafaa zaidi kuliko wengine.

Katika maisha yetu ya kitendaji ya kila siku tunashuhudia kuwa taasisi au jamii inaweka baadhi ya mipaka iwe kwa kulazimisha juu ya watu kwa ajili ya wengine au kwa baraza la wadhamini peke yao, kwa mfano: Shirika linaweza kuweka aina fulani ya mipango, au kuweka aina fulani ya ulinzi, au kupitia mafunzo fulani, au kuwakataza kuacha kazi na kutoka nje ya shirika bila ya ruhusa, au kutoshughulika na shughuli nyingine zaidi ya kazi alizopangiwa, bali wakati mwingine shirika likiingia mkataba na mfanyakazi wake na kumwekea mipaka fulani baada ya kuacha kazi kwenye shirika lake….Yote haya yanafanyika na kukubalika, wala hakuna mwenye kuangalia katika mikataba hii kuwa ni ubaguzi au kuwadhulumu wafanyakazi wake. Yote haya yapo chini ya mfumo maarufu ulio wazi kama ambavyo hakuna taasisi wala kituo kilichofanikiwa bila kuwepo kwa mkuu wake aliyepata nafasi kubwa yenye kulingana na majukumu aliyowekewa shingoni mwake na maswala yatakayoweza kumtokea.

-Vivyo hivyo, taasisi ya familia ili iweze kufanikiwa haina budi kuwa na mfumo wanaopitia wote, na mfumo huu unaweza kuwa na baadhi ya vifungo na makatazo au wajibu (kujilazimu) ….Hapana budi kuwepo kiongozi mwenye nafasi inayolingana na majukumu yake, na hivyo kuwa na uwezo wa kutatua jambo pindi tofauti au mtafaruku unapojitokeza. Hata hivyo hapana budi vile vile kutekelezwa mfumo huu vile vile na kutumia nafasi hii katika kivuli cha msingi wa maisha ya kifamilia tuliyoyazungumza, nayo ni mapenzi na huruma na maisha ya masikilizano yenye kuhakikisha lengo la kuishi.

Maiko: Ikiwa hali ndiyo ilivyo, kwanini usimamizi uwe kwa mwanamume? Kwa nini usiwe kwa mwanamke? Je huoni kuwa huo sio usawa?

Rashidi: Pamoja na kupendelea kwangu neno usawa, ambalo ni bora kuliko neno ‘uadilifu’ isipokuwa ninasema: Usawa au uadilifu unakuwa katika haki, ama haya tuliyomo ndani yake ni mgawanyo wa kazi na kuziba nyadhifa za kijamii zinayolingana na uwezo wa mtu na yaliyotayarishwa kwake.

Tulipokuwa tunazungumzia taasisi ya familia tumesema kuwa mwanamume na mwanamke kila mmoja ametayarishwa kwa umbile tofauti, na matayarisho haya yanalingana na nyadhifa mbali mbali za kijamii, wala usisahau kuwa katika mkabala wa usimamizi wa mwanamume kuna majukumu ambayo hakupewa mwanamke, na usimamizi wa mazingatio haya ni majukumu zaidi kuliko upendeleo, ni ubebaji wa majukumu na hili linahitajia uvumilivu zaidi na kutofanya haraka kuchukua maamuzi, na hii haina maana kumdharau mwanamke au utu wake.

Nyadhifa za kijamii hazimfai mwanamke vile vile; kwani wanawake ni kama vile alivyosema Mtume wetu Muhammad: “Wapungufu wa akili?

Maiko: “Wapungufu wa akili? Hakika mtazamo huu ni wa kumdunisha mwanamke, kama ambavyo mwanamke amethibitisha uwezo wake wa kielimu, na uwezo wake wa akili hautofautiani na wa mwanamume.

Rashidi: (Akicheka): Jambo la ajabu kabisa ewe rafiki yangu kuwa watu wengi niliozungumza nao kwa mazungumzo haya walifahamu ufahamu huu uliofahamu, jambo lililokusudiwa kuhusu akili sio akili hii ya maarifa bali ni uwezo wa kusimamia mambo kwa mizani ya sawa sawa,

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

na kudhibiti nafsi na hisia mbali mbali, kinachomsaidia katika kuchukua maamuzi sahihi wakati wa matatizo na mazingira tata, yaani kwa maana nyingine; kinakabiliana na upole na kuelekea kwenye matamanio, wala mtu hawezi kupinga kuwa tabia ya mwanamke huelekea kwenye huruma zaidi na huathirika zaidi kuliko mwanamme hii ndio tabia ya hisia zake, na nafasi yake ya kijamii inapaswa kulingana na tabia yake hii, na huenda hekima hii vile vile hufunga nafasi ya mwanamke ili ayaendee majukumu yake ya kifamilia kwani yeye ndio mhimili wa familia.

Maiko: Tunapozungumzia dhulma ya mwanamke na mtazamo wa kumdunisha, ni vizuri kutajwa haki zake katika mirathi, kwanini inakuwa mirathi ya mwanamke ni nusu ya mwanamume?!

Rashidi: Kwanza kabisa: Sio katika hali zote fungu la mwanamke katika mirathi huwa ni nusu ya mwanamume.

Pili: Utukufu wa mwanaadamu haututaki tuwape watu haki tunazowapa wengine; uadilifu hauna maana ya usawa katika hali zote, lakini usawa ni wajibu pindi hali na mazingira yanapokuwa sawa, yaani: hapana budi kuzingatia tabia ya mwanamke na nafasi yake katika maisha, na haki zake ziwe sawa na majukumu yake.

-Katika masuala ya mirathi kwa mfano: Anachokipata mwanamke kinakuwa ni chake peke yake, wakati ambapo mwanamme mirathi yake atagawana na mkewe, watoto wake na ndugu zake, kama watakuwa bado hawajaolewa na wazazi wake kama bado wapo hai na hawana wa kuwahudumia, hapo litakuwa ni jukumu lake, mbali ya kuwa mwanamume ndie atoaye mahari kwa mwanamke na yeye ndie mwenye jukumu la kutayarisha nyumba baada ya kuoa na samani zake, na mwanamume ndie mwenye jukumu la kutoa matumizi ya nyumba, mke na watoto, wala haipasi mwanamume kumlazimisha mwanamke kufanya kazi, nae hana haki katika mali ya mke wake, mbali yakuwa mwanamke anajitegemea kwa mali yake kwa ukamilifu, jambo ambalo wanawake wengi wa nchi za Magharibi bado hawajalifikia, ambapo inadaiwa kuwa ndio wenye usawa zaidi.

-Je, kuna lililobakia katika maudhui haya ambalo tunapaswa kulijadili?

Maiko: Naam, imebakia suala la talaka, lakini nashauri tupumzike kwanza.

Kuparaganyika Kwa Nyumba Yenye Matatizo

www.path-2-happiness.com

Kuparaganyika Kwa Nyumba Yenye Matatizo

Baada ya mapumziko ya usingizi mdogo wa mchana, marafiki wawili walibadilishana viti vyao ili kuimarisha nishati zao, kisha Maiko akaanza kuzungumza:

Kinachoonekana ni kuwa katika jamii nyingi za Waislamu talaka zimeenea, nami nadhani sababu yake ni Uislamu kuruhusu talaka.

Rashidi: Kwanza: Uislamu haukuwa wa kwanza kuleta sheria ya talaka, kabla ya Uislamu kulikuwepo na talaka takriban ulimwengu mzima, na wakati huo mwanamume akichukia tu humfukuza mwanamke awe na haki au makosa, bila hata mwanamke kuwa na haki au fidia kutoka kwa mwanamume, na pindi ustaarabu wa Kiyunani ulioposhamiri, talaka nayo ilishamiri bila kuwepo sharti au kifungo maalum, ama kwa Uyahudi ilikuwa ni dini inayoruhusu talaka na ilikuwa ni haki na matakwa pekee ya mwanamume, kama ambavyo alikuwa ana haki ya kumuacha mke wake bila hata ya udhuru, pamoja na kuwa waliona ni bora kuwepo na udhuru wa jambo hilo, na kilichoonekana katika talaka kwao ni kuwa: Mwanamke anapoolewa na mume mwingine hawezi tena kurudi kwa mume wake wa mwanzo.

Pili: Je, Talaka imeenea katika jamii ya Kiislamu hata tuseme kuwa Uislamu kuruhusu talaka ndio sababu ya hilo, hebu tuangalie takwimu mbali mbali ulimwenguni ili tulinganishe.

Huko Marekani wastani wa talaka kati ya mwaka 1992 hadi 1995 ilikuwa ni 502 (mia tano na mbili) Katika kila hali elfu za ndoa, na wastani huu unatarajiwa kuongezeka, na hii imepelekea serikali ya Marekani kuficha viwango hivi vya talaka pamoja na kuwa walikuwa wakitoa viwango hivyo hapo kabla, hivyo tokea mwaka 1999 hadi sasa imekuwa inafichwa. Huko Urusi wastani wa talaka kati ya mwaka 2001 hadi 2004 ilikuwa ni talaka 750 (mia saba na hamsini) kati ya ndoa elfu moja, huko Sweden katika miaka hiyo hiyo talaka 539 (mia tano thelathini na tisa) katika kila ndoa elfu moja. Uingereza kulikuwa na wastani wa talaka 538 (mia tano thelathini na nane) kati ya ndoa elfu moja baina ya mwaka 2000 hadi 2003.

Japan kulikuwa na wastani wa talaka 366 (mia tatu sitini na sita) kwa kila ndoa elfu moja kati ya mwaka 2000 – 2004.

Ama nchi zingine zilikuwa chini ya hapo, kwa mfano Jordan 184 katika ndoa elfu moja baina ya mwaka 2000 hadi 2004, ama Palestina ilifikia 142 katika mwaka huo huo katika ndoa elfu moja.

Huko Misri kati ya mwaka 2000-2003 kulikuwa na wastani wa talaka 134 (mia moja thelathini na nne) kati ya ndoa elfu moja, katika nchi ya Syria baina ya mwaka 2000 hadi 2002 kulikuwa na wastani wa talaka 84 (themanini na nne) katika ndoa elfu moja. Lybia ilifikia talaka 51 (Hamsini na moja) katika ndoa elfu moja kati ya mwaka 2000 hadi 2004, Iran ilifikia 97 (tisini na saba) katika ndoa elfu moja katika mwaka 2000 hadi 2003.

Je, baada ya hapo tutasema kuwa talaka imeenea katika jamii za Waislamu, na kuwa sababu yake ni Uislamu kuruhusu talaka?!

Maiko: Lakini inajulikana kuwa Uislamu ni maarufu kwa wepesi wa kutoa talaka ukilinganishwa na dini na mifumo mingine ya kijamii.

Rashidi: Wazo hili limebeba maudhui mengi, hebu niruhusu niyazungumzie kwa upana.

Maiko: Endelea.

Rashidi: Maudhui ya kwanza: Ni kuamini wepesi wa kutoka talaka moja kwa moja, bila ya shaka hakuna sharia au mfumo wowote wa kijamii ambao unahamasisha talaka…huenda nikakubaliana nawe kuwa huenda akapuuza jambo hili ambae hajilazimishi na mafundisho ya Kiislamu, na hutumia baadhi ya fursa vibaya, lakini wakati huo huo inabidi tujue kuwa mafundisho ya Uislamu yako mbali na tabia hizi, kwani ni mafundisho ambayo yapo wazi kiasi cha kuondoa athari mbaya, na kinachotokea katika baadhi ya jamii ni matokeo ya jamii hizi kuwa mbali na ukweli wa dini ya Kiislamu, sheria na mifumo yake.

Maiko: Je, unaweza kuifafanua nukta hiyo?

Rashidi: Asili ya ndoa katika Uislamu ni mkataba wa kudumu na ni haramu kuuwekea muda maalumu, kwa namna ambayo inawajibishwa maisha yao ya ndoa yaendelee na yadumu hadi mauti

www.path-2-happiness.com

yatakapowatenganisha, mkataba huu wa ndoa umeitwa mkataba mzito, na hilo ni kwa vile inaelekeza kinacholingana kuuheshimu na kutofikiria kuuvunja, hata hivyo talaka ni jambo linalochukiwa katika Uislamu isipokuwa katika hali ya wakati wa dharura, wakati ambao Uislamu umeelekeza kufanyika jitihada za kusuluhisha na kuheshimu pande zote mbili na kuhifadhi mambo ya familia yaliyobaki.

Uislamu umelingania kwenye kukaa na mke bila kumpa talaka atakapochukizwa na sifa asiyoipenda, na ukamkumbusha kuangalia sifa zingine ambazo anaweza kupata na kumfanya akamatane na ndoa yake, na kulinda utukufu wa ndoa. Pia Uislamu ukahadharisha utani katika kutumia au kutoa neno la talaka, kama ambavyo imemuamrisha mume kudhibiti hisia zake na kufanya pole pole katika kumnyoosha mke, na Uislamu ukaweka taratibu kama wana ndoa hawawezi kutatua tatizo lao basi pande zingine ambazo maslahi ya wana ndoa zinawagusa ziingilie kati na kutatua tatizo lenyewe, kisha mwishowe ndipo linapokuja suala la talaka tena katika hatua tofauti kama jaribio la kutoa fursa ya kurudiana wanandoa, Uislamu haujahukumu kubomoa maisha ya wanandoa mwanzo wa ugomvi wao, bali umeweka mara tatu mume anaweza kumrudia mkewe baada ya talaka ya kwanza na ya pili, na hata katika talaka ya tatu Uislamu, umemruhusu mume kumrejea mkewe lakini hilo hutokea baada ya utaratibu ambao utawaumiza wote wawili, nao ni kuolewa kwa mke huyu aliyeachika na mwanamume mwingine.

Maiko: Haya ni maudhui ya kwanza, ni yapi mengine?

Rashidi: Nukta nyingine muhimu ni ule mtazamo mbaya katika kuangalia hali halisi ya jamii zingine zisizokuwa za Kiislamu, ukweli ni kuwa talaka inaweza kutokea kwa sababu ndogo, bila shaka unalijua hilo, kwa mfano Marekani inatajwa kuwa inawezekana kimahakama mmoja wa wanandoa akaachika kwa sababu ya uraibu wake mkubwa wa kompyuta au kufuatilia vipindi vya televisheni, huko Canada inatosha kuthibitisha kuwa mmoja wa wanandoa anakoroma anapolala ili wakati huo apate haki ya kumpa talaka, ama Italia talaka inaweza kutuka ikiwa mmoja wa wanandoa anamlazimisha mwenzake kazi za nyumbani, na Uingereza kuzembea jambo la mwanandoa mwenzake kunapelekea kwenye talaka.

Mahakama za Japan zimekubaliana kutoa hukumu ya talaka ikiwa mmoja wa wanandoa atalala kwa namna ambayo haitomfurahisha mwenzie mtaka talaka.

Maiko: Ulichokitaja bwana Rashidi ni sahihi, lakini huu ni uhalisia katika mahakama za kisekula zilizojitenga na dini. Ama Ukristo msimamo wake mkali kuhusu talaka unafahamika isipokuwa kwa sababu chache tu ambazo ni vigumu kuthibitisha.

Rashidi: Mimi ninadhani kuwa huku kushupalia talaka hakuendani na maisha ya mwanadamu, na hilo linafafanuliwa kuwa baadhi ya Wakristo waishio katika nchi za Waislamu wanaona tofauti kati ya dini hizi mbili, wanaweza kuacha dini zao kwa kukimbia taabu hii wanapofikia katika nukta ya kuyatenganisha maisha yao ya kijamii na wala wasipate majibu kutoka kwenye dini yao kwa mazingira ya maisha na ugumu wake.

-Na hili ndilo lenye kuupambanua Uislamu, Uislamu unalazimisha maisha ya ndoa yawe ya milele, umewawekea sheria watu wanaoishi ardhini, wana mambo mahsusi na tabia zao za kibinadamu na mazingira yao ambayo yanaweza kubadilika, na huweka pembeni wakati huo huo makosa katika uchaguzi ambao hauwezi kuvumbuliwa isipokuwa ni kwa uzoefu tu, mabadiliko katika mazingira haya yanaweza kupelekea kuangukia katika kosa hili yanaweza kusababisha matatizo katika viwango tofauti, wakati mwingine yanaweza kutokea matatizo na yakawa makubwa yasiyoweza kuvumilika ila kwa hasara za kinafsi, kijamii na hata za kifedha au kiuchumi ikawa ni hasara kubwa, hivyo sharia ya Kiislamu imewawekea namna ya kushughulikia tatizo (matatizo haya) pindi maisha yanapokuwa magumu na njia zikawa za dhiki na njia za kusuluhisha kushindikana. Katika hili Uislamu ni dini inayokwenda na wakati, na ni dini yenye uadilifu kwa wote; mwanamume na mwanamke kwa pamoja na familia, hivyo kusahihisha muelekeo hadi kuachana na kuanza majaribio mapya ni bora kuliko kuungua kwa moto wa mifarakano na magomvi au kuendelea na hali hiyo pamoja na kukosekana kusudio la ndoa na lengo lake, ambapo malengo yake muhimu ni: Utulivu wa nafsi ndani ya mapenzi na huruma na kuasisi familia tulivu yenye mafanikio.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

“Talaka katika Uislamu ni suluhisho na kunyoosha njia, na fursa ya mabadiliko na kutoa nafasi ya maisha mapya yenye mafaniko zaidi.

Rashidi: Mimi naona sheria ya talaka iliyotajwa katika Uislamu ni katika ubora wa dini hii na kwenda pamoja na mazingira yake.

Maiko: Lakini kwa nini Uislamu umefanya haki hii ya kutoa talaka ni ya mwanamume peke yake, hivi hii sio dhuluma kwa mwanamke?.

Rashidi: Kwa mara nyingine, inapasa kuangalia mambo kwa upana wake na kuchunga maeneo yote, na ninakusudia kuangalia katika jambo hili kupitia mfumo kamili wa kijamii, kuanzia katika ndoa yenyewe na malengo yake na mtazamo wa familia na wadhifa wa kila pande na haki zake.

-Hapa tutataja kuwa imethibitika kisayansi kwamba mwanamke kwa tabia yake ni mwenye hisia na kubadilika na mhemko kuliko mwanamume, kitu ambacho kinamfanya mwanamume kuwa na udiriki zaidi na kukadiria matokeo (mazuri) ya jambo hili, na hivyo kuweza kudhibiti hisia na hasira zake anapokuwa ameghadhibika.

Kama ambavyo hasara za utoaji wa talaka zinakuwa ni za mwanamume pekee, nae ndie atakayebeba hasara za mali, na inamlazimu mwanamume gharama za mali baada ya talaka wala hapana shaka yoyote kuwa gharama hizi za mali ambazo zimetokana na maamuzi hayo ya talaka itakuwa ni sababu za ziada ambazo zinafanya wanandoa kudhibiti nafsi zao.

Pamoja na hayo: Uislamu pamoja na kufanya talaka kuwa ni haki ya mwanamume peke yake, isipokuwa haukupuuza kumpa mwanamke njia ya kujitenga na mume atakapoona sababu za msingi za kufanya hivyo, na hili kisheria linafahamika kwa jina la Khulu’u yaani kuvua, kwa kutumia vidhibiti na sheria ambazo zitahifadhi haki za pande zote.

Rashidi: Je, rafiki yangu ungependa tuzungumzie hali ya mwanamke katika nchi zenu?!

Maiko: Naona tule chakula cha mchana.

Mwanamke Baada ya Kuwa Huru

www.path-2-happiness.com

Mwanamke Baada ya Kuwa Huru

Rashidi na Maiko walimaliza kula chakula cha mchana. Rashidi aliangaza macho yake juu, kisha akamuwahi rafiki yake:

Rafiki yangu mpenzi Maiko, umeninyeshea kwa mishale ya kunikosoa na umeuweka ustaarabu wangu kizimbani.

Maiko: Sio mishale wala sio tuhuma ewe sahiba yangu, ni mjadala na ukosoaji wenye lengo la kufikia kwenye ukweli, na nadhani sisi tumepiga hatua kubwa katika mijadala hii na yote yenye kuhusiana nayo, kadhalika nashukuru uungwana wako na mtazamo mpana, lakini je, mazungumzo yangu yoyote yaliyotangulia yamekutia dhiki?!

Rashidi: Hapana, hapana, hukuniudhi, lakini nimekusudia ili picha yetu ikamilike hapana budi kuangalia maeneo yake yote, na pia tulinganishe hali ya mwanamke kwenu na kwetu vile vile, yaani ustaarabu wenu na wetu, na nadhani mazungumzo yetu yaliyopita kuhusu mwanamke yameweka wazi kiasi fulani cha taswira ya kadhia ya mwanamke katika ustaarabu wa Kiislamu, kilichobaki ni kuangalia katika kadhia hii kwa miwani ya ustaarabu wenu.

Maiko (Huku akicheka): Sawa nafungua kichwa changu kwa mishale na nafungua mlango wa kizimba.

Rashidi (Akitabasamu): Kwa nini tunajiweka katika eneo la kupigana? Mahusiano yetu haya yanaweza kuwa ni mahusiano ya mjadala na ushirikiano ili kufikia kwenye ukweli kama ulivyotaja.

Maiko: Nakubaliana nawe kabisa, ungependa tuanzie wapi?!

Rashidi: La kwanza ambalo linafaa kuliangalia ni nafasi ya mwanamke katika rejea mbali mbali za ustaarabu.

Maiko: Mtazamo kwa mwanamke na njia ya kuishi nae inatofautiana na mtazamo wa mtu binafsi na kumtathmini kulingana na makuzi yake, malezi na elimu yake, kadhia hapa sio kuangalia nafasi na hadhi ya mwanamke huyu katika kitabu hiki au rejea ile.

Rashidi: Hili ni sahihi, hata hivyo wakati huo huo hatuwezi kuacha rejea ambazo zinatengeneza utamaduni wa mtu yule na kutengeneza maadili ambayo yanaathiri mtazamo wake wa mambo, na ninaposema 'rejea' sikusudii vitabu au kutengeneza mwamko wa mtu na utamaduni wake, inaweza kuwa katika rejea hizi huenda kukawa na rejea za kielimu lakini vile vile kila chenye kuathiri katika kutengeneza mazingatio ya mtu na utamaduni wake, baadhi ya visa vya watu na makabila mbali mbali na visa vya kale vyenye kuchukua sura ya sanaa za jadi, hali kadhalika semi, methali na hekima ambazo huvutwa kutoka katika fikra za ndani za watu kwenda kwenye mtazamo wa mtu binafsi, kwa hiyo rejea kwa mtazamo huu kwa nafasi yake huathiri katika malezi na makuzi ya mtu.

Maiko: Mimi naamini kuwa hadhi ya mwanamke na mtazamo kuhusu mwanamke hautofautiani baina ya vitabu vitakatifu vya mbinguni; katika kitabu chetu kitakatifu kuna kufanana mno na Qur'an yenu, muhtasari wa mtazamo huu ni kuwa: Namna alivyoumbwa mwanamke ameumbwa kutokana na mwanamume, na mwanamke ndiye sababu ya dhambi ya kwanza na sababu ya kutolewa peponi, na nafasi yake kijamii na majukumu yake.

Rashidi: Maneno haya kuna pande ambazo nitatofautiana nawe; suala la dhambi ya kwanza na kutolewa kwa Adam na Hawa peponi katika Qur'an inatofautiana na kitabu chenu kitakatifu. Hawa sio sababu ya shetani kumshawishi na kumpoteza Adam, hivyo basi suala la kutolewa peponi sio la mwanamke.

Ukweli ni kuwa mtazamo kuhusu mwanamke na nafasi yake imekuja katika kitabu kitakatifu kuwa: Uzawa wa mwanamke unaongeza unajisi wa kina mama! Injili inasema: "…Mwanamke akipata mimba na kuzaa mtoto wa kiume, unajisi wake utakuwa siku saba kama kwenye hedhi, kisha baada ya hapo hukaa siku thelathini na tatu kutoharisha damu yake…., lakini akizaa mtoto wa kike najisi yake itakuwa kwa muda wa wiki mbili kama kwenye hedhi yake, kisha hukaa siku sitini na sita katika kutoharisha damu yake."

Rashidi: Ama matendo ya mwanamke katika jamii kwa mtazamo wa Ukristo ni kuwa wanawake wanakatazwa kufungua midomo yao kanisani, katika kitabu kitakatifu cha Wakhorinto ya kwanza 14:34-35 katika kitabu cha Agano Jipya imeandikwa: "Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena; bali watii kama vile inenavyo torati. Nao wakitaka kujifunza neno lolote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa." Haya yote hayana mfano wake kwenye Qur'an.

www.path-2-happiness.com

Maiko: Kwa ujumla ni kuwa yale maendeleo yaliyotokea katika jamii yetu hayawezi kufahamika bila kuunganisha na mizizi ya utamaduni wa Kigiriki na Kiroma ambayo yamechanganyika nayo, na kama hayatachukuliwa mazingatio taathira ya harakati za kidini na islahi za Protestanti ndani yake, pamoja na athari ya fikra za mwamko wa Ulaya na mapinduzi ya Ufaransa na mabadiliko ya jamii wakati wa mapinduzi ya viwanda katika jamii hii.

Rashidi: Ama kwa kuwa umetaja utamaduni wa Kigiriki na Kiroma, kuna mkanganyiko mkubwa kuhusu mtazamo wa mwanamke kulingana na wakati tunaouzungumzia au hata maendeleo na ustaarabu ambao tunaushuhudia hivi sasa, na tunapofungua ukurasa wa historia ya mwanamke wa Kigiriki tunaona jinsi alivyonyang'anywa uhuru wake na matakwa yake binafsi na nafasi yake katika jamii, walikuwa wanadharau nafasi yake na kumuona ni mnyama wa kuuzwa na kununuliwa, na kumnyang'anya uhuru wake wa matumizi, na kumuharamishia urithi kisheria, hivyo pindi ustaarabu wa Kigiriki ulipopata maendeleo hali ya mwanamke ilibadilika haraka sana, ikawa mwanamke anachanganyika na wanaume na kuingia katika vilabu, kilichopelekea kwenye uchafu na uzinifu, na malaya wakaonekana ni viburudisho vya watalii na wanayo nafasi katika ustaarabu wao na jamii yao, hivyo sanamu za wanawake walio uchi zikatengenezwa kwa jina la sanaa na fani.

Pamoja na tofauti zilizopo, msimamo wa ustaarabu wa Kiroma haujabadiliki sana, nao ni kumdharau, na kumchukulia kuwa yupo chini ya mwanamume ambae ana haki ya kumfanya anavyotaka, sheria ya Kirumi imemvua mwanamke na haki zote za kijamii katika hatua zote za maisha yake, kisha baada ya hapo sheria kuhusu mwanamke ikaanza kubadilika, mabadiliko haya yanatokea katika mfumo na sheria zao zinazohusu familia na ufungaji ndoa na utoaji talaka; mambo yakabadilika kichwa chini miguu juu, na hivyo ufungaji ndoa kwao ukawa hauna maana na mwanamke kupewa haki zote za kurithi na kumiliki, kisha mtazamo wao kuhusu mahusiano ya mwanamume na mwanamke yakabadilika kwa kutokuwepo mkataba wa kisheria kati yao.

Maiko: Na kuongezea: Kwa ujumla kumetokea maingiliano na kupelekea kuathiriana kati ya ustaarabu wa Kigiriki na Kiroma na ule wa Kanisa kuhusu mwanamke pindi Ulaya ilipoingia katika Ukristo, mtazamo na rai za watu wa dini kuhusu mwanamke zikaathirika na kubadilika kwa hali halisi waliyokuwa wakiishi nayo.

Rashidi: Naam, pindi viongozi wa Kanisa walipoona muelekeo wa hali hiyo katika jamii za Kiroma katika kuenea kwa uchafu na maovu na kilichopelekea katika tabia chafu katika jamii, walimchukulia mwanamke kuwa ndie aliyesababisha yote haya; na wakatangaza kuwa mwanamke ni mlango wa shetani na inampasa kuonea haya uzuri wake; kwani ni silaha ya ibilisi kwa fitna na ushawishi….Watu wa Magharibi wakaendelea kumdharau mwanamke na kuzuia haki zake zote katika karne za kati, hata katika zama ambazo ilidhaniwa kuwa mwanamke ameshapata nafasi yake katika jamii, bado haki za matumizi ya mali yake hakuwa nayo ila kwa idhini ya mume wake.

Maiko: Lakini, huoni rafiki yangu kuwa mjadala wetu umegeuka somo la historia?! Tunaweza kuruka kutoka katika hatua hii ili kufikia pale mabadiliko yalipoanza ambayo ndiyo yaliyotufikisha hapa, ninakusudia zama zile za mwamko, kisha mapinduzi ya Ufaransa na yaliyofuatia baada ya hapo.

Rashidi: Sio historia, lakini ni utafiti wa chanzo chenyewe, kwani mimi ninaona kuwepo kwa mahusiano kati ya hali hizi na rai ambazo zinaonwa kuwa ni historia na baina ya hali halisi ya mwanamke katika nchi za Magharibi leo hii pamoja na tofauti ya muonekano wake.

Je, huoni kufanana baina ya hakika hizi za kihistoria na haki za mwanamke katika nchi za Magharibi?!

Maiko: Unakusudia nini kwa mfano?

Rashidi: Mfano: Mwanamke kutumika kama chombo cha kustarehesha wanaume, ilipodhaniwa kuwa mwanamke wa Magharibi amepata haki zake kwa kuwekewa sheria za usawa kati yake na mwanamume katika sehemu zote, mara ikaonekana kuwa amegeuka kuwa ni chombo cha kuchezea katika mikono ya mwanamume, mfano jina la mwanamke kuwa chini ya kivuli cha mumewe na katika himaya mali yake vile vile; ambapo haiba ya mwanamke ilikuwa imefichwa na mumewe na hili halikuondoka ila ilipoanza karne ya ishirini.

Maiko: Lakini mwishowe, mwanamke alipata haki zake, na kwa hiyo akawa sawa na mwanamume katika nyanja zote, hata katika kupata kazi katika vitengo mbali mbali.

www.path-2-happiness.com

Rashidi: Lakini ukandamizaji wa mwanamke Magharibi na kunyimwa haki zake, pamoja na kuwa zingine zimenyanyuliwa kwa kuwekewa kanuni, mikataba na sheria mbali mbali, ila hali ipo kwa kiwango kile kile, hata kama jina la ukandamizaji wenyewe litabadilika na malengo yake kwa jina la harakati hizi, ambazo mwanamume alimtumia mwanamke kama mtego wa kukusanya mali na starehe kadhalika, na mwanamke akabadilika na kuwa bidhaa ya kiwiliwili kuwaridhisha wateja katika sehemu za starehe na michezo na njia ya kupata mali kwa watangazaji biashara, na hii ni kilele cha udhalilishaji wa utukufu wa mwanamke; kiasi cha kumfanya mwanamke aje juu katika baadhi ya nchi na kutaka kutotumika katika matangazo ya kibiashara.

Kadhi wa Sweden, Briggette Hoff Haher akizungumzia uhuru, usawa na ukombozi wa mwanamke anasema: Kwa hakika mwanamke wa Sweden ghafla amegundua kuwa amenunua hali ya kufikirika (anakusudia uhuru aliopewa) kwa thamani inayotisha nayo ni furaha yake ya kweli."

Ripoti ya Msemaji wa nchi za Ulaya akizungumzia hali ya mwanamke katika nchi za Ulaya na vipi yale madai ya uhuru na ukombozi wa mwanamke kupata haki zake zilikuwa ni kauli mbiu kavu zisizo na maana wala hazina ukweli wowote ule, imekuja ripoti kuwa mashirika ya Ulaya hayafanyi juhudi za kutosha ili kuvunja (kizuizi hiki) ambacho kinawafanya wanawake wasipate nafasi za juu za utawala.

Ane Demanto Pole, msemaji wa nchi za Ulaya katika mambo ya kijamii: "Ulimwengu wa kazi na biashara unaonesha tofauti kati ya jinsia mbili kwa sura iliyo wazi, wakati ambapo-mwanamke anatamaliki kati ya asilimia 20% -30% ya wadhifa wa juu ulio rasmi na utawala wa sekta za umma huko Ulaya, ama nafasi zake katika mashirika binafsi haizidi asilimia 25 huko Ufaransa, 6.3% Uingereza, na nafasi yake ya juu katika benki haizidi asilimia 5% tu.

Kadhalika msemaji huyo wa Ulaya alionesha tofauti nyingine ya mishahara iliyopo kati ya mshahara wa mwanamke na ule wa mwanamume, haswa katika nyadhifa za utawala; ambapo mwanamke anapata mshahara chini ya asilimia 16% ya mshahara wa mwanamume.

Maiko (Akimkatiza): Naona treni imefika kituo chake cha mwisho… tutayarishe mizigo na tukusanye.

Upambanuzi wa Ustaarabu

www.path-2-happiness.com

Upambanuzi wa Ustaarabu

Baada ya masaa mawili na robo ya safari, marafiki wawili walifika Paris, mji ambao Rashidi hajawahi kuutembelea hapo kabla. Marafiki hao wawili waliondoka kwenye kituo cha treni na ilielekea kuwa Maiko anaifahamu vizuri Paris na kuna uhusiano wa mapenzi kati ya Maiko na mji wa Paris.

Maiko: Rashidi! Hii ndio Paris mji mkuu wa Nuru…. hapo ndipo walimwengu walipojifunzia kauli mbiu ya (Uhuru, Udugu na Usawa), na misingi hii ya haki za mwanadamu zikaenea ulimwenguni kote.

Rashidi: Angalia Maiko…..mwanamke amekamatwa na polisi na sioni jambo lolote baya alilofanya!

Maiko: Ooh, amevaa nikabu, siku mbili zilizopita kanuni ya kukataza uvaaji nikabu imeanza kutekelezwa Ufaransa katika sehemu za umma, na huenda amekamatwa kwa ajili hiyo, huenda polisi huyu kamkamta ili amtoze faini kwa kwenda kinyume na sheria hii au anaweza kuwekwa hata ndani.

Rashidi: Katika sehemu za umma?! Yaani kanuni hii inamruhusu kuvaa nikabu nyumbani kwake….mashaAllah:…..uhuru wa hali ya juu kwa mwanamke kwa Kiislamu na kwa Waislamu! Nimekumbuka kanuni hii, na nimekumbuka kuwa kanuni hii haipo Ufaransa peke yake, ipo mfano wa kanuni hii huko Ubelgiji na pia kuna mji Kaskazini mwa Italia imepitisha kanuni hii vile vile, na kuna juhudi ya kupitisha mfano wa kanuni hii huko Holland na Uhispania, ama huko Australia serikali imewapa haki polisi ya kuangalia uso wa mvaaji nikabu ili kumfahamu.

Maiko: Ninaamini mwenyewe kuwa katazo hili linamkwaza mwanamke na uhuru wake binafsi kuvaa akipendacho, na kutolewa kwa kanuni hii huhesabiwa kuwa ni kurudi nyuma kwa uhuru wa Ufaransa, kwa hakika huku ni kugusa uhuru binafsi katika nchi ambayo kuna zaidi ya mada mia moja za kisheria zinazotaka kuheshimiwa kwa uhuru wa wengine.

-Hata hivyo wao wanaona kuwa hilo linaendana na misingi ya dola yao ya kisekula ambayo inakataza matumizi ya nembo za kidini, kama ambavyo watawala wa Ufaransa wanaielezea nikabu kuwa ni aina mpya ya utumwa ambayo Jamhuri ya Ufaransa haikubali katika ardhi yake.

Rashidi: Misingi ya usekula inahadharisha matumizi ya nembo za dini katika dola yenyewe na taasisi zake za umma, lakini hazihadharishi kwa watu binafsi, kisha kwa nini basi tahadhari hii iwe ni kwa Waislamu peke yao tu? Je, hilo linafanyika kwa wenye kuvaa misalaba vifuani mwao au wenye kuvaa mavazi ya masista watawa?! Jambo la kushangaza kuhusu ufahamu wa utumwa kwa watu hawa katika mantiki yao, Je, kumsukuma mwanamke kuwa uchi na wanaume kustarehe nae kila pembe sio utumwa, na mwanamke kujisitiri kiwiliwili chake chote kwa uchaguzi wake na kwa matakwa yake ndio utumwa?! Naam ewe bwana wangu kwa hakika ni utumwa, lakini ni utumwa kwa Allah (Mungu), Mola wa walimwengu.

Sasa nimefahamu maana ya uhuru katika kauli mbiu ya mapinduzi ya Ufaransa, ni uhuru wa kutojihusisha na Mungu (Allah) na utumwa kwake, na sio uhuru wa viumbe, uhuru huu uliotolewa na utawala wa kisekula ambao umechukua nafasi ya Mwenyezi Mungu na kulimbikiza madaraka yake na kuyagawa na kuruhusu kwa wamtakaye na namna watakavyo. Walikuwa wakisema kuhusu uhuru, “uhuru wako utaishia pindi pale uhuru wa mwingine utakapoanza.” Je, wanahesabu watu kuangalia viwiliwili vya wanawake ni uhuru na haki na wakati huo huo wakaufunga na kuubana uhuru wa mwanamke wa Kiislamu?! Hili silo suala la hijabu, ni khofu waliyonayo Ulaya kuhusu Uislamu.

Maiko: Usikuze mambo bwana Rashidi, Waislamu wengi wanaishi Ulaya na wana haki zote kama walivyo watu wengine, na mbali na hiyo wanapata fursa za kielimu na kufanya kazi kuliko hata katika nchi zao.

Rashidi: Mimi sikuzi mambo, lakini nazungumza kwa sababu kuna ushahidi mwingi wa hilo, ni khofu tu ya Uislamu.

Maiko: Mfano nini?

Rashidi: Mfano: Kukataza minara kujengwa Uswisi, nchi ambayo ndio inayolinda haki za binadamu, nchi isiyofungamana na upande wowote, nchi yenye makubaliano na mapatano ya Geneva. Ni matatizo gani ambayo minara itasababisha au madhara gani katika jamii katika nchi ambayo Waislamu hawazidi asilimia nne tu ya wakazi wote, na kuna minara minne tu?!! Bila shaka ni jambo lililo wazi kuwa marufuku hii imebeba ndani yake khofu ya maradhi na msimamo wa uadui dhidi ya Uislamu.

www.path-2-happiness.com

Maiko: Pamoja na kuwa mimi binafsi sikubaliani na marufuku hii, isipokuwa ninafahamu kuwa minara hii ya adhana hupingana na maadili ya nchi zao, ndio maana wanapinga ili utambulisho wao usiguswe.

Rashidi: Ninapofikiria kuwa ni jinsi gani marufuku hii haigusi wala haienei na kusambaa katika alama na nembo zote za sehemu za ibada kama vile minara ya makanisa na mahekalu ya Mayahudi, basi wakati huo nafahamu mipaka ya usekula ambayo wanalingania katika nchi zao na kudai wamesimamisha misingi yake, na ninafahamu ukweli wa usawa wanaoulingania, na ya kuwa jambo hili haliishi hapo, bali linavuka mipaka kwenda kwenye kila nembo na alama ya Uislamu na hata ikiwa alama hii ni Mtume Muhammad mwenyewe, Mtume wa Uislamu, kama tulivyoona katika tatizo la kumchafua Mtume wetu kwa katuni kama ilivyotokea nchini Denmark na nchi zingine zilizoshabikia uadui huu.

Maiko: Bwana wangu, huu ni uhuru wa kujieleza, katika nchi zetu hakuna kitu kitakatifu au kinachokatazwa katika uhuru wa kujieleza, ni mara nyingi Yesu mwenyewe na nembo za dini nyinginezo zilikumbwa na zahama na dharau hizi.

Rashidi: Bali kuna matakatifu kwenu ambayo hayaguswi, hakuna uhuru wa kujieleza wala uhuru wa utafiti wa kielimu; baada ya jarida la Denmark lililochora katuni za Mtume Muhammad, kisha uadui ule kuenea katika baadhi za nchi za Ulaya, na nchi nyingi za Magharibi kutetea hali hiyo pamoja na kukosolewa kwa alama kubwa ya dini ya zaidi ya watu bilioni mbili ulimwenguni, na kukataa kwao kuomba radhi kwa hoja ya uhuru wa kujieleza…Mahakama moja huko Holland imewahukumu kundi la Waislamu huko Holland faini ya Euro elfu mbili mia tano kwa kueneza Katuni inayoonesha kuwa maangamizi makubwa waliyopata Mayahudi ni kitu kilichotengenezwa na Mayahudi au wameyakuza zaidi kuliko yalivyotokea, serikali ya Holland imetetea uamuzi huo kuwa Mahakama ya Ulaya ya haki za binaadamu ambayo inatawalia umuhimu mkubwa wa uhuru wa kujieleza inatetea kwa nguvu suala hilo.

Moja katika mahakama za huko Ufaransa katika mwaka 1998 ili muhukumu mwanafikra wa Kifaransa Bwana Roger Garoudy kwa tuhuma ya kutia shaka katika maangamizi ya Mayahudi, nae alitia shaka idadi iliyotajwa ya kuuwawa Mayahudi katika mikono ya wanazi huko Ulaya.

Katika mwaka 2006 mahakama ya Austria ilimhukumu mwanahistoria wa Uingereza David Irving jela miaka mitatu kwa sababu alipinga maelezo ya kuunguzwa kwa Mayahudi.

Katika mwaka 2009 mahakama nchini Ujerumani ilimpiga faini ya Euro elfu kumi Askofu wa Kikatoliki wa Uingereza Richard Williamson kwa sababu tu alisema kuwa wahanga wa Kiyahudi waliokufa katika kambi za maangamizi ya Nazi ni kati ya watu laki mbili hadi tatu tu.

Na wengineo wengi, wote hao hawakupata uhuru ule wa kutafiti au uhuru wa kuzungumza na kimbilio katika matukufu haya.

Maiko: Kinachothibitika ni kuwa kuna historia ya uadui baina ya Ukristo na Uislamu, ukiongezea hali ya sasa hivi inayoendelea ya matumizi ya nguvu ya Waislamu wenye kasumba, jambo lililowafanya watu wengi kuuogopa Uislamu kuliko mfano wanavyoogopa Uhindu na Ubudha. Je, utapinga kuwa baadhi ya matendo ya Waislamu huwa ni sababu kubwa ya kuwepo khofu dhidi ya Uislamu?

Rashidi: Ehe, hii sasa tunakaribia kwenye ukweli, sipingi kuwa baadhi ya matendo na makundi ya Waislamu ni sehemu ya makundi yenye uadui, na maadui hutumia hali hiyo katika kuchochea hali ya uadui na khofu dhidi ya Uislamu na Waislamu. Hata hivyo wakati huo huo inatupasa tuweke mambo katika sehemu yake na katika uzito na ukubwa unaostahiki; sisi hatuwezi kupuuzia kuwa kuna mambo mengine ya operesheni na mikakati ya uadui dhidi ya Uislamu na Waislamu, kwa kutumia matukio haya ambayo umeyataja ambayo lengo lake ni kufikia malengo ya makundi ya kibaguzi au ya kiadui dhidi ya Uislamu na Waislamu…. Vinginevyo kama sisi tutafuatilia matukio kwa uwazi bila upendeleo basi tutakuta kuwa hakuna kundi la kidini au la kikabila ambalo litakosa kufanya uadui hata kwa wale wenye kunasibiana nao, lakini kuyaonesha matukio haya au kuyasambaza kuwa ni Waislamu wote ndio wanayoyafanya au hata kuyapuuzia ndiyo ambayo yanayopaswa kuangaliwa kwa makini na hili linaingia katika ukurasa wa usahaulifu.

Maiko: Unakusudia nini kusema mambo mengine?

Rashidi: Nitakutajia baadhi ya hayo mambo, na sio yote:

Ulaya ilifungua milango yake kwa wahamiaji wa Kiarabu–na Waislamu kwa malengo maalumu, miongoni mwa malengo hayo ni: Kuongeza idadi ya watu huko Ulaya ili kuziba pengo la upungufu wa watu unaotokana na

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

kuvunjika kwa familia huko Magharibi na hali ya kutotaka kuzaa kwa watu wake, na bila shaka ufunguzi huu wa kupokea wahamiaji wa Kiislamu haukuwa kwa kuwatumia watu wazima walioshiba adabu na desturi za Kiislamu, lakini ilikuwa ni tamaa ya kupata kizazi kipya kitakachozaliwa katika nchi za Magharibi ambacho inawezekana kukifinyanga katika ustaarabu mpya ambao utatengeneza jamii mpya na utamaduni mpya katika nchi za Magharibi baada ya miaka hamsini ya mwanzo…hivi ndivyo ulivyokuwa mpango wa 'wanastratejia' wa Magharibi.

Hata hivyo wana-stratejia hao wa Magharibi waliona ule mwamko wa kurejea katika Uislamu katika ulimwengu wa Kiislamu umehamia katika nchi za Magharbi, na ikawa ni kikuta cha njia katika njia ya kukamilisha kuwa changanya wahajiri wa Kiislamu na watoto wao katika ustaarabu mpya wa kimagharibi badala yake watoto na wasichana kuwa na hijabu au familia yenye kushikamana na Uislamu na misingi yao ya dini, hili sasa likawa ni kikwazo cha kufanikiwa kwa sera yao ya kuwachanganya kwa ukamilifu.

Kizazi hiki cha watoto wa kiislamu kikawa ni chanzo cha khofu katika kutekeleza 'programu' ile ya kuwaweka pamoja, na hivyo basi: Magharibi ilijikuta uso kwa uso na tatizo la kujitokeza kwa nguvu mpya ya watu inayobeba wasifu na utambulisho wa kiistaarabu tofauti na utambulisho wa watu wa Magharibi.

Hivyo basi, sababu kuu ya operesheni hii ya kibaguzi ni ile hisia chungu ya hatari ya kupoteza utambulisho wake, na hili ndilo lililopelekea katika kukerwa na kila alama ya nembo ya Uislamu; wao wanaogopa kuwa mandhari haya pamoja na kuwa ni madogo lau yakibakia yakiwa katika hali ya mpangilio wa Kiislamu bila shaka yataenea kwao… na hivyo kuamua kuyafuta yakiwa bado ni machanga; hivyo basi mgongano wa ustaarabu hivi sasa upo dhidi ya Uislamu baada ya kuondoka itikadi nyinginezo, na hili ndilo lililoelezwa na mwanafikra wa kimarekani bwana Samuel Hannington kuwa ni: "Migongano ya ustaraabu", akionesha kuwa kuna harakati ya kifikra na ya kisiasa huku magharibi.

Maiko: Tumefika mgahawani, maudhui mpya uliyoanzisha yanahitaji mijadala mingi.

Pamoja na Freud Ndani ya Mgahawa - Paris

www.path-2-happiness.com

Pamoja na Freud Ndani ya Mgahawa - Paris

Utafutaji wa hotel inayofaa ulimaliza siku yote iliyobakia baada ya marafiki wawili walipowasili Paris, mwishowe walifikia katika Hosteli ya Vijana wa Paris, dhahiri ilionekana kuwa wana haja ya mapumziko; walimalizia usiku uliobakia usingizini, siku iliyofuatia marafiki wale wawili, walitoka ili kuufahamu mji na alama zake, katikati ya kuzunguka kwao walipita katika mgahawa mmoja….

Maiko: Unaonaje Rashidi tuingie tupate kikombe cha chai na tupumzike kidogo kwenye mgahawa huu.

Rashidi: Hamna kizuizi, kweli nami ninahisi nahitaji kupumzika kidogo.

Maiko: Katika mgahawa huu alikuwa akikaa Sigmund Freud, yule tabibu nafsi mashuhuri, je, ulishawahi kumsikia?

Rashidi: Ndio, yule ambaye jina lake linahusishwa na skuli ya uchambuzi wa nafsi katika saikolojia, na kadhalika anahusishwa vile vile katika kulingania katika uhuru wa vidhibiti vya kimaadili na kuhalalisha mambo ya kijinsia.

Maiko: Kwetu sisi ni mwanazuoni mwenye hadhi yake bila ya kujali hayo uliyoyataja.

Rashidi: Ninadhani ni moja katika nguzo za fikra ambayo imeumba ustaarabu mpya katika jamii za nchi za Magharibi, akiwa pamoja na Darwin, Immanuel Kant, Karl Marx, Émile Durkheim na Sater, kila mmoja katika wao amesimama kwa nafasi yake katika kutingisha fikra za watu wa Magharibi na kurejesha mfumo wake katika hali inayotakiwa kulingana na matakatifu mapya ya Magharibi….na kila mmoja katika wao alifanya kazi ya kubomoa: dini, maadili na desturi za watu.

-Nadharia ya Darwin ya ukuzi na maendeleo ilikuwa ni cheche ambayo ilituma makombora mawili ya hatari ya kifikra, walioitumia waliokuja baada yao ili kupiga miundo mbinu ya kifikra wakati huo; Kombora la kwanza: Kueneza fikra ya ukuzi yenye kudumu ambayo inapuuza fikra ya kuthibiti (yaani mwanadamu habadiliki) baada ya hapo ni ukiasi wa kila msingi wa mambo ya maadili, fikra na taswira mbali mbali..

Kombora la Pili: Fikra ya uhayawani wa mwanadamu na umaada wake na umaada wa vipengele vyenye kuathiri ndani yake, pamoja na kupuuzia kukubwa nafasi ya roho, na kupinga kuwa mwanadamu kaumbwa na Mungu, kwa hiyo ukawa mwanzo wenye nguvu wa kubomoa ufahamu muhimu kuhusu maswali makubwa ya kifalsafa kuhusu Mungu, mwanadamu, ulimwengu na marejeo ya mwanadamu.

Ama nafasi ya Freud ilikuwa ni kumuweka mwanadamu katika fundo za kijinsia, na akapinga kuwa mwanadamu anaelekezwa na akili katika maadili yake, na akasema kuwa kitu cha msingi chenye kumsukuma mwanadamu katika maisha yake ya kila siku ni ladha, na kutokea hapo mifumo yote ya kimaadili imevunjika na kubomoka na hiyo kuonekana kuwa ni kukosa maendeleo na kurudi nyuma, na mtu wa namna hii kuonekana ni mtu asiyeishi katika hali halisi na kukosa kuwa mtendaji.

Maiko: Naamini kuwa kuna dondoo zenye kushirikiana baina ya ustaarabu wa wanadamu, kadhalika pia kuna dondoo ambazo kila ustaarabu unatofautiana na mwingine, kwa mfano mitazamo hii, 'Mungu, mwanadamu na ulimwengu' ni vitu ambavyo jamii zote hushirikiana, hata hivyo kila ustaarabu hutofautiana na mwingine katika mitazamo hii; moja katika staarabu hizi zimeshinda mtazamo mmoja kuliko mitazamo miwili iliyobakia na hivyo huonekana katika mtazamo wa kwanza.

Katika ustaarabu wa Ulaya leo hii, na baada ya zama za mwamko, mtazamo kuhusu ulimwengu ulitawala katika ustaarabu huu, na pindi fikra za kisomi na kisayansi zilipoenea katika jamii ya Kimagharibi zama zile, zilifuta fikra ya kuwa mwanadamu kaumbwa na Mungu na kuja kwa mtazamo wa kimaada, na hivyo basi kuua kabisa mtazamo wa kiroho kwa mwanadamu, kwa hakika Darwin alikuwa katika wanafikra wakubwa aliyeasisi muelekeo ule.

Rashidi: Nakubaliana nawe kabisa katika hilo, lakini nitakubainishia baadhi ya uliyosema:

Kwanza: Sababu ya msingi na kubadilika kwa fikra hizi hadi kuwa mapinduzi ya kweli kwa wakati ule ni uwepo wa hali fulani ya faragha ya kiroho na kielimu katika jamii ya kimagharibi wakati ule, ongeza na utawala wa Kanisa na kung'ang'ania kwake rai zake mbovu kuhusu maumbile na uhai pamoja na itikadi yake ya kuwalazimisha watu kuamini rai zile.

Pili: Ni kuwa katika makosa yaliyoenea ni kuitakidi kwamba sababu ya maendeleo ya nchi za Magharibi ni kutegemea kwao rai na nadharia ambazo zilienea mwanzoni mwa mwamko ule na katikati yake.

Tatu: kuwa rai na nadharia za wanafikra na wanafalsafa hao zilianza

www.path-2-happiness.com

kupungua na kuondoka moja baada ya nyingine baada ya mapinduzi ya kweli ya kisayansi, pamoja na hayo ni kuwa wenye uwezo mdogo wa utamaduni huko Magharibi na Mashariki bado wameangukia katika kuathirika na propaganda ambazo zinategemea rai zile.

Ama mazungumzo yako kuhusu kushirikiana kwa ufahamu baina ya mitazamo ya staarabu ni kuwa umenikumbusha ulinganisho (mzuri) wenye kuvutia kati ya nadharia ya Freud katika kufasiri mfumo wa mwanadamu na maneno ya mwanazuoni mmoja wa Kiislamu, yameandikwa inakaribia miaka mia saba.

Maiko: Nzuri sana kuwepo mfanano kati ya maneno ya Freud na mtazamo wa mwanazuoni wa Kiislamu zama zile.

Rashidi: Sio kufanana kwa mtazamo, bali kufanana kwa kile tunachoweza kukiita mfanano wa umbo, ili nikubainishie zaidi: Je, unafahamu mjengo wa mfumo wa nafsi kulingana na Freud?

Maiko: Ndio, naufahamu vizuri sana, kwa ufupi ni kuwa Freud alifikiria kuwa madamu mwanadamu ana mifumo mingine ya kibaiolojia inayoratibu uhai wa mwanadamu kama vile mfumo wa chakula au mfumo wa damu na mingineyo, hivyo basi mwanadamu nae ana mfumo wa nafsi ambao una sehemu zenye uhusiano baina yake.

Na mfumo huu una kile alichokiita: (Id), (Super Ego) na (Ego).

(Id), Ni sehemu inayohusika na silika na matamanio binafsi yenye kumsukuma mtu pamoja na uzoefu uliojificha na mielekeo ya awali ya kijima yenye msukumo wenye kuendelea katika sura ya upofu ili kujitokeza katika sehemu ya hisia, kwa lengo la kutekeleza na kufanikisha matamanio kulingana na msingi wa ladha, (Id) ni mfumo wa kale zaidi wa nafsi uliojengeka, (Id) ina yote ayabebayo mwanadamu pindi anapozaliwa na kila ambacho kitakachoainisha umbo lake maalum, hivyo basi (Id) inawakilisha alichokirithi mtu.

Ama (Super Ego) tunaweza kuuelezea kuwa ni mlolongo wa maadili ya jamii husika na misingi ya maadili mema, yaani: Yale ayapatayo mwanadamu kutoka kwa wengine; na inakusanya athari za malezi na tabia azipatazo mtoto kutoka kwa wazazi wake, shule na jamii, athari za desturi ya familia yake, kabila au ukoo wake, taifa na dini, pamoja na muktadha wa jamii inayomzunguka moja kwa moja, pia (Super Ego) inaathirika pindi mtoto anapokuwa na walezi wanaowawakilisha wazazi wao au mbadala wao, kama vile baadhi ya walezi na watu ambao wanawakilisha ruwaza njema za jamii…katika (Super Ego) inamili kuwa mbali kabisa na matendo yote ya matamanio na ya kisilika, ambapo hiyo (Super Ego) ni sehemu ya dhamira ya mtu, nayo ni sehemu au eneo linalohusika na maadili mema yaliyo mbali na uhalisia, matilaba yake siku zote ni kufikia ukamilifu na sio katika ladha kulingana na Freud.

Ama Ego unaweza kuuelezea kuwa ni matokeo ya mgongano au maafikiano kati ya (Id) na (Super Ego), kati ya matamanio yenye kusimama kwa msingi wa ladha na maadili yaliyosimama chini ya udhibiti na mipaka, hivyo basi (Ego) ni hisia zilizoamka ambazo zinafanya kazi ya kusuluhisha matatizo yenye kuibuka pamoja na hali halisi au kati ya matamanio baina yake ili kuhifadhi na kuweka sawa haiba ya mtu, nayo mwishowe ni matokeo ya haiba ya mtu inayoonekana katika tabia yake ya nje.

Kwa hiyo (Super Ego) ni ile sehemu iliyojitenga na (Ego) na kuidhibiti, na kwa ajili hiyo inasimama kama tahadhari kwa (Ego) kuwa chini ya utawala wa (Id) na kutekeleza matilaba ya matamanio yaliyojificha.

Rashidi: Ufafanuzi mzuri Maiko, unaelezea utafikiri Freud mwenyewe anazungumza kwenye mgahawa akiwa anakunywa kikombe cha chai.

Lakini nakamilisha maelezo haya mazuri, kuwa Freud anathibitisha ugumu wa kazi ambayo unaisimamia (Ego) katika mfumo wa Nafsi, na kazi hii ni ngumu (au haiwezekani kabisa) ni kusuluhisha matilaba kinzani, nayo ni juu ya (Ego) kuitika matilaba ya (Id) na ambayo kimsingi ni matamanio ya kijinsia, na wakati huo huo kuchunga matakwa ya nje yanayoizunguka (Super Ego) nayo ni mahitajio ya kimaadili na ya kijamii; na hivyo basi inaelekea suala la muwafaka baina yake kuwa ni gumu, na ndio maana (Ego) inajaribu kutengeneza mahusiano ya kufahamiana na muwafaka pamoja na (Id) na hujaribu kujibu na kushibisha hamu zake, na hivyo kugongana na (Super Ego) ambayo ni hali halisi ambayo inaratibu mahusiano ya kijinsia kulingana na vigezo husika ambavyo vinapelekea mara nyingi katika kuzuia matamanio ya kijinsia. Ikiwa (Ego) itaweza kuwafikisha mizani ya sawa kati ya (Id) na (Super Ego) pamoja na hali halisi, mtu ataishi maisha yenye muwafaka, ama ikiwa (Id) ikishinda au (Super Ego) ikitawala kwa mtu itapelekea hilo katika migongano; kushindwa kwa (Ego) kusuluhisha kati ya mahitaji na matakwa haya pinzani, hupelekea katika hali za maradhi.

Jambo lililo la hatari hapa: Tutakapo sema: Kuwa uzima wa Nafsi kwa mtazamo huu yaani (Ego) pamoja na (Id) kupata muwafaka; yaani:

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

matamanio na matilaba ya kihayawani pamoja na (Super Ego); yaani misingi ya maadili mema, na kuwa kushindwa kutoitikia matakwa haya ya (Id) hupelekea katika kuficha hisia na matamanio, na kwa kuzingatia kuwa kutoweza kwetu kuibadilisha (Id)….haitobaki mbele yetu kufikia muwafaka huu isipokuwa kubadilisha (Super Ego) na kuiangamiza ikilazimika jambo hilo, hivyo basi ikawa hapana budi kuiondoa dini pamoja na maadili katika maisha yetu, na kuzibadilisha kwa maslahi yenye kukubaliana na matamanio ya mwanadamu na mahitajio yake ya kijinsia na ya kibinafsi ambayo yanatekelezwa na (Id). -Hili ndilo haswa lililotokea katika nchi za Magharibi pindi walipoondosha na kung'oa dini na maadili mema, na hivyo wakayapa uhuru matamanio na mahusiano ya kijinsia yasiyokuwa na udhibiti katika vifungo vya maadili na tabia njema, na ustaarabu wake kusimama katika hilo, familia ziliparaganyika baada ya hapo, bali utu wa mwanadamu ulipotea; ilipokuwa sasa huwezi kutofautisha kati yake na jamii ya Kihayawani isiyokuwa na akili ambayo haijui vidhibiti vya kimaadili nje ya maumbile yake na silika….naona kuwa sisi tunarudi tena kwa Darwin baada ya kuwa tumeanza nae.

Maiko: Unakusudia kusema: Ikiwa matamanio yaliyojificha na kuzikwa yatatafuta njia ya kushibisha (iwe ni moja kwa moja au isiwe moja kwa moja) hilo litapelekea kulingana na ufahamu wako kwa Freud na madhehebu yake kuwa ustaarabu ambao unasimamia maadili mema ni ustaarabu unaosimama katika kufukia hisia na kuzuia matamanio ya mtu.

Rashidi: Ndio, ustaarabu wa kimagharibi pindi unapotoa maadili mema hufanya hivyo kwa kuondosha utukufu wa Mwenyezi Mungu katika hesabu zao, wakati ambapo Waislamu wanaona kuwa maadili mema katika jamii za mwanadamu ni jambo la msingi kabisa na kuwa chanzo chake kiwe ni cha kisheria kutoka mbinguni na sio kwenye akili za wanadamu, kwa sababu akili pekee yake mwishoni itapotea, ama akili hiyo hiyo ikiwa ipo katika mipaka ya kisheria basi maadili yatakayopatikana kutokea hapo yatakuwa ni maadili mema.

Lakini hukuniambia mimi ewe Rashidi alichokisema mwanazuoni huyu kuhusu dini yenu ambayo umeizungumzia. Je, alichokisema kinawafikiana na maneno haya au vinapingana?

Rashidi: Kwa hakika alichokisema kipo katika mfumo unaotokana na maadili na mitazamo, na kukionesha katika mfumo huu na kuweka maneno yake katika mtiririko wake yatakuwa marefu, ninaona kuwa tuakhirishe hadi kikao kijacho.

Nafsi ya Mwanadamu Baina ya Mifumo Miwili

www.path-2-happiness.com

Nafsi ya Mwanadamu Baina ya Mifumo Miwili

Sehemu waliyofikia Rashidi na Maiko ilikuwa sehemu nzuri kwao, nyongeza ya urahisi wa gharama ya makazi, ndani yake kuna kiwanja cha michezo na sehemu za kujisomea na kupumzika, na uwezekano wa mawasiliano, na muhimu zaidi ya hilo ni kuwepo wageni wenye umri unaolingana nao na viwango vyao vya elimu.

Maiko na Rashidi walipumzika katika moja ya meza katika ukumbi wa kijamii (mkutano) na kila mmoja akaagiza kinywaji akipendacho, kisha Maiko akaanza kuzungumza:

Katika mazungumzo yetu yaliyopita tuliishia kwenye yale aliyoyasema mwanazuoni huyu kuhusu dini yenu ambayo umezungumzia, na je, alichokisema kinaafikia na au kinapingana?

Rashidi: Sio masuala ya kuafikiana au kugongana, Uislamu ni mfumo kamili unaojitegemea kikamilifu, na umesimama katika misingi ya wazi, hata hivyo sitorefusha kuuelezea…Mwanazuoni huyu jina lake ni Ibnu Qayyim, amezungumza katika vitabu vyake kuhusu uhusiano kati ya moyo, nafsi na akili, lakini nitapenda kwanza kuashiria kuwa alichokisema kilikuwa ni kwa mujibu wa ufahamu ambao unaambatana pamoja na misingi ambayo ustaarabu wa Kiislamu umesimama, hivyo basi napenda kuunganisha mazungumzo yangu yaliyotangulia kwa kufafanua tofauti kati ya mfumo huu na madai ya nadharia ya Freud ambayo yametengeneza sehemu kubwa ya hali halisi ya jamii ya magharibi na maadili yake.

Maiko: Ili tuweze kutumia wakati wetu vizuri, niachie niweke bayana sehemu ya mwisho ya maneno yako, pamoja na kuwa yapo kinyume na unachoamini, natarajia utanisahihisha.

Rashidi: Karibu.

Maiko: Tunachokipata kutoka katika nadharia ya Freud ni aina nyingi za haiba ya mtu, zinawakilishwa na yafuatayo:

Pindi silika na matamanio ya kijima au ya kihayawani yakitawala (yaani: Id) kwa mtu, basi (Ego) ya mtu itaonekana kuwa ni mtu mbinafsi au muovu mwenye kufanyia uadui haki za wengine, yeye atakuwa anatafuta kushibisha matamanio yake na kuitikia haja zake za kihayawani, na kusaga saga maadili mema na desturi njema na yaliyo matukufu (Super Ego).

Na ikiwa maadili mema, desturi njema na matukufu yatatawala (Super Ego) juu ya (Ego), basi utadhihirika kwa mtu huyo upole na utawa lakini asiyeishi katika uhalisia wake na wakati huo akisaga saga katika njia yake hiyo silika na matamanio ya kijima.

Haiba itakuwa ni sahihi na tulivu atakapoweza kulinganisha na kuweka sawa baina ya matamanio na silika kwa upande mmoja, na maadili na vifungo vya nje kwa upande mwingine, na hilo hutokea kwa kuficha na kufukia baadhi ya silika hizi katika baadhi ya hali au kuondokana na vifungo na maadili katika baadhi ya nyakati zingine kwa kadri ya makadirio ya kila hali.

Rashidi: Vizuri sana, tumefikia kujua tofauti kati ya nadharia hii na ustaarabu wa Kimagharibi ambao tumeuangalia kijamii na kuulinganisha na mfumo wa Kiislamu… na tofauti hii huonekana katika kumaliza hali ya uadui na mgongano kati ya (Ego) na (Super Ego) bila ya kimojawapo kuacha haki zake na hilo ni kupitia ulingani makini na ukamilifu unaoenea sehemu zote za mipaka ya wanadamu katika nyanja za maisha yake, na siri katika hilo hujificha kwa ninachokiita tahadhari ya kupetuka haki.

Maiko: Kwa mara ya kwanza ndio nasikia hili la kupetuka haki, na utanieleza ni vipi haki zinapetukwa, hata hivyo niache kwanza nikuambie kuwa maneno yako yanathibitisha fikra ya uumbwaji wa mfumo wa nafsi.

Rashidi: Fikra ya uumbwaji wa mfumo wa nafsi ndiyo ambayo nimekutajia hapo mwanzo kuwa, mmoja wa wanazuoni wa Kiislamu bali baadhi yao wamesema yanayofanana nayo kabla ya mamia ya miaka, angalia alichokisema mwanazuoni huyu anayeitwa Ibnu Qayyim katika moja ya vitabu vyake, hapo Rashidi akatoa kitabu, kisha akasoma: “Hivyo basi mambo ni manne: Yanayochukiza yanapelekea katika kuchukiza, na yenye kuchukiza, yanapelekea katika yenye kupendwa, na yenye kupendwa yanayopelekea katika yenye kupendwa, na yenye kupendwa yanayopelekea katika yenye kuchukiza. Kwa hiyo yenye kupendwa yenye kufikisha katika yenye kupendwa hukusanyika ndani yake muitaji wa kutenda katika sura mbili, na yenye kuchukiza yenye kupelekea katika yenye kuchukiza hukusanyika ndani yake muitaji katika kuacha katika sura mbili.

Kumebakia sehemu mbili zinazovutana na waitaji wawili; Mwenye kuita katika kutenda na kuacha (vita katika balaa na mtihani). Katika hali hii nafsi huathiri kilicho karibu nae zaidi, na hilo ni lile lenye haraka zaidi, na akili na imani huathiri chenye kunufaisha na kubakia zaidi, ama

www.path-2-happiness.com

moyo upo katika miito miwili, wakati mwingine upo kwa huyu na wakati mwingine kwa huyu, wanazuoni wa Kiislamu wanataja huku wakidhukuru maandiko ya Qur'an na hadithi za Mtume Muhammad kuwa pindi akili inapoghafilika (Super ego) basi wakati huo matamanio yanakuwa katika nishati (Id) bila ya mlinzi au msimamizi.

Je, huoni mfanano katika wadhifa (kazi) za nafsi na (Id) kwa Freud, na kati ya akili na imani na (Super ego) na moyo na (Id).

Maiko: Kama ni hivyo basi kuna mfanano mkubwa.

Rashidi: Kuna tofauti ya msingi kati ya maneno haya na yale, tofauti inayopambanua mfumo huu na ule, tofauti hii inajificha katika kauli ya Ibnu Qayyim (nayo ni vita kati ya balaa na mitihani), wakati ambapo Freud anaona kuwa uzima wa mtu (Ego) ambayo ni moyo kwa Ibn Al-Qayyim) ipo katika kuitikia silika (Id/Nafsi) na matamanio yake. Ama katika mfumo wa Kiislamu unaona kuwa mwitikio wa silika hizi na matamanio ndani ya nafsi na msukumo wake katika uhalisia huchukuliwa kuwa ni mitihani kutoka kwa Allah, wala haifai kuitikia mwito moja kwa moja ili kuiridhisha (Id/Nafsi), vile vile haitakiwi kuiangamiza moja kwa moja na kuipeleka kwenye hesabu ya (Super Ego) au akili na imani kama ilivyo kwenye utawa.

Na huu ndio wastani na kulinganisha mizani ambayo hatuyapati katika isiyokuwa Uislamu; kudhibiti matamanio na silika, na kushibisha haja za silika za mwanadamu bila ya kugongana na akili na imani na bila ya kupetuka haki zingine.

Maiko: Sasa ni nini makusudio ya kupetuka haki?

Rashidi: Makusudio yake ni kuwa maadili na tabia njema zina haki zake, na kwa upande mwingine matamanio na silika zina haki zake vile vile, na Uislamu unahadharisha kutopituka moja wapo ya maadili na matukufu ya tabia au hata matamanio au hata silika kushambulia haki nyinginezo, kwa maana ya kwamba haya ni maadili matukufu na hizi ni haja chafu, na ili kuyaelezea vizuri nakutajia hadithi ya Mtume wa Uislamu, "Makundi matatu ya watu yalikwenda katika nyumba ya Mtume Muhammad na wakauliza ibada zake na walipoambiwa walizihesabu kama kwamba ni kidogo, wakadhania kuwa hilo ni kwa sababu Mtume Muhammad ana sifa tofauti nao, na wao kwa sababu wana madhambi mengi zaidi hivyo basi nao wanatakiwa wafanye ibada nyingi zaidi kiasi cha kukata hoja zao za kimaumbile, katika hilo mmoja wao akasema: Ama mimi nitaswali usiku umri wangu wote wala sitolala, mwingine akasema: Mimi nitafunga (sitokula asubuhi hadi jioni) kila siku na wa mwisho akasema: Mimi sitooa daima. Mtume Muhammad akawaendea na kuwaambia: "Nyie ndio mliosema hivi na vile, ama Wallahi mimi ndie mcha Mungu wenu zaidi, lakini ninafunga na nakula, na ninaswali usiku na kulala na ninaoa wanawake, mtu ambae ataacha sunnah (mwenendo) yangu si katika mimi." …watu wale waliongeza kitu katika dini (Super ego) ambayo kiuhalisia ni vitu vya ziada kufanya na vyenye kupendeza na kutakiwa, lakini yalikuwa yamevunja haki zingine hata kama haki hizi zitahusu nafsi ya mtu (Id), imekuja katika hadithi nyingine yenye kubainisha vizuri zaidi msingi huu: "Hakika Mola wako ana haki juu yako, na nafsi yako ina haki juu yako, na familia yako ina haki juu yako, hivyo kila mwenye haki mpe haki yake." Katika Qur'an Tukufu zipo aya nyingi zenye kuthibitisha hilo, miongoni mwa aya hizo ni:

"Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi." (28:77),

"Wala usiufanye mkono wako kama ulio fungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi."(17:29)

Na bila shaka rafiki yangu unafahamu kuwa Uislamu umekataza utawa..

Katika Uislamu mtu anairidhisha akili yake, dhamira yake, kutekeleza dini yake na kushibisha haja zake za kimaumbile…bila kupingana.

Wakati Rashidi na Maiko wamezama katika mjadala wao, alisogea karibu yao kijana aliyekuwa amekaa kwenye meza pembeni yao, alisimama mbele yao na kuanza kuzungumza:

Je mtaniruihusu nikae pamoja nanyi?

Maiko na Rashidi kwa furaha… karibu.

Kijana: Kwa hakika nimefurahishwa na kuvutiwa na mazungumzo yenu, nitafurahi kama tutafahamiana na kunishirikisha kwenye mjadala wenu.

Maiko: Mimi sina tatizo.

Rashidi: Karibu, karibu, nikutambulishe kwa rafiki yangu Maiko kutoka Uingereza, yeye ni mwalimu, na mimi ni Rashidi kutoka Misri, ni mwandishi wa habari na mtunzi wa vitabu.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kijana: Karibuni sana, na asanteni kunikaribisha kujiunga nanyi, nijitambulishe kwenu, mimi ni Rajev, kutoka India, nasoma uhandisi Ujerumani, nipo hapa Paris kuwatembelea baadhi ya rafiki zangu.

Maiko na Rashidi: Fursa nzuri kufahamiana nawe Rajev.

Rashidi: Kama tunaona kuwa wanazuoni wa nafsi wa Magharibi hawaangalii nafsi isipokuwa kupitia aibu, maradhi, na maafa ya nafsi.. ama katika Uislamu nafsi imebeba ndani yake kheri na shari, na kuna uwezekano wa kubadilisha hali ya nafsi na kuigeuza na kuitoa kwenye dhuluma ya uhayawani na kuifikisha nafsi ile kwenye kilele cha ukamilifu bila kugongana na umbile la mwanadamu au kutia kasoro haja zake.

Rajev: Najifunza kutoka katika mjadala wenu kuwa matamanio yaliyofichwa daima yanatafuta kushibishwa kwa haja zake kwa njia ya moja kwa moja au kwa kuzunguka, basi hilo litapelekea kuzingatia ustaarabu unaosimama katika misingi ya maadili mema kuwa ni ustaarabu uliozaliwa kwa kuficha mahitaji na matamanio ya mwanadamu kulingana na mtazamo wa Freud.

Rashidi: Kwa hakika ustaarabu wa Kimagharibi unapozalisha maadili mema huzalisha kupitia kushinda mtazamo wa ulimwengu juu yake, na humpa mwanadamu kipaumbele kwa kumzingatia kuwa ni bwana wa ulimwengu huu, yote hayo yamejitokeza kwa kuondoa fikra ya Mungu katika ustaraabu. Ama mtazamo wa ustaarabu katika Uislamu ni kuwa Mungu ndie yuko juu, hata hivyo mtazamo huu haufuti mwanadamu kutamalaki ulimwengu.

Rashidi: Huu ni ushahidi madhubuti kuwa maadili katika jamii za wanadamu ni lazima chanzo chake kiwe kutoka katika ufunuo (wahyi) na sio akili, kwani akili peke yake inapotea, ama akili ikiwa katika mipaka ya wahyi basi maadili yatakayozalishwa yatakuwa ndio yenye kutakiwa.

Maiko: Uwepo wako ewe Rajev utakuwa na athari njema katika mjadala wetu, naona tuweke ahadi ya kuonana kesho katika sehemu hii hii tuanze mjadala wetu mpya, mnaonaje?

Rajev: Ndio, sawa kwangu.

Rashidi: Nitafurahi kama mkikubali kupokea mwaliko wangu wa chakula cha mchana katika kikao chetu nayo ni kwa heshima ya rafiki yetu mpya Rajev.

Maiko na Rajev: Kwa furaha kabisa.

Haja Yetu ya Imani

www.path-2-happiness.com

Haja Yetu ya Imani

Marafiki wale walikutana kwa mujibu wa ahadi yao katika hoteli ya nyumba ya vijana, baada ya kuangalia 'menyu' **Maiko na Rashidi** wakaorodhesha oda yao, wakati ambapo Rajev alikuwa akiangalia menyu kwa umakini zaidi na akasema:

Hoteli nyingi hazijali kuweka vyakula vya mboga mboga, hata hivyo ninaweza kuagiza chakula chenye kunifaa.

Maiko: Kwa hiyo wewe ni miongoni mwa wala mboga mboga?

Rajev: Ndio inafikia asilimia arubaini (40%) ya wala mboga mboga nchini India.

Rashidi: Je, hilo ni kwa sababu ya dini au afya?

Rajev: Ukweli, katika dini ya Uhindu ambayo nilikuwa nikiamini, ulaji wa nyama ya ng'ombe ni haramu kabisa, India ulaji mboga mboga ni maarufu mno kwa wenye kufuata dini ya Uhindu, pamoja na kupungua idadi yao kwa sasa kutokana na ugumu wa kufuata mfumo huu na ukatili wake, ama mimi binafsi napendelea zaidi vyakula vya mboga mboga kwa ajili ya afya na mazingira..

Rashidi: (Akimuita mhudumu): kwa hisani oda yetu hii hapa.

Maiko: Lakini wewe Rajev umeacha dini yako kuelekea dini ipi?

Rajev: Si popote, masomo yangu nchini Ujerumani yamenipa fursa ya kusoma sana na kunifanya kuwa huru na kuangalia Uhindu kwa jicho la kukosoa na mashaka mengi, na hata hivyo sijakinaishwa na Ukristo, kwa ajili hiyo mimi niko karibu zaidi na upagani.

Maiko: Mimi nakukaribia wewe kwenye shaka hii, hata hivyo ninaamini kuwa mwanadamu ana haja ya kuwa na uhusiano na Mungu baadhi ya nyakati, lakini uhusiano huu usiwe kupetuka mpaka na kumtawala mwanadamu.

Rashidi: Mimi naamini kuwa maneno haya yanahitaji mjadala na umakini.

Maiko: Mazungumzo gani unayokusudia?

Rashidi: Hii fikra ya kumkana Mungu, na nafasi ya dini au Mungu katika maisha ya mwanadamu.

Rajev: Ninaamini ugunduzi wa mwanadamu katika elimu umemfungulia siri nyingi, umemfanya kutokuwa na haja ya tafsiri iliyojificha, tafsiri za kiroho, na naamini kuwa ulimwengu unaongozwa na kuhukumiwa na kanuni za kielimu (kisayansi) ambazo inaziongoza. Tunaweza kusema: Ulimwengu ni chombo cha kimakenika (kinachofanya kazi) ipo chini ya kanuni madhubuti na kila kinachotokea kina sababu ambayo hupelekea katika matokeo ya lazima yaliopangwa, na madamu kanuni hizi za kimakenika zinaendesha ulimwengu kulingana na sheria zake, basi hakuna haja ya kuwepo (fikra) ya Mungu ambaye atatawala ulimwengu.

Rashidi: Elimu (sayansi) ni chombo kizuri cha kufasiri yanayotuzunguka, lakini suala la (msingi) sio hili, hatuwezi kuzungumzia masuala makubwa kama haya, bali ni masuala makubwa yaliyowashughulisha wanadamu tokea mwanzo wa historia, huondoshwa kimoja hata ikiwa kuondoshwa huku hutuvutia au katika tunachokiamini, kuna mapana mengi katika maudhui, miongoni mwayo ni:

Je, elimu ina tafsiri ya yote yenye kutuzunguka? Bila shaka jibu ni hapana….Elimu haiwezi kufanya hilo, tukichukulia elimu ya nyota (astronomy) kwa mfano, tunaona nadharia za elimu hii kuwa yale yaliyovumbuliwa na elimu hii katika ulimwengu hadi leo hii huwakilisha asilimia tano tu (5%) na baki ya mambo mengi yako kwenye kiza, hatujui chochote kuhusiana nayo, na hii ni kulingana na uwezo wake wa sasa na walichokifikia, vinginevyo ingeweza kuwa yale wasioyafahamu ni makubwa zaidi.

Ikiwa hiyo ndio hali halisi ya ulimwengu wa (mambo yaliyo wazi) na kugusika, hali ikoje katika ulimwengu uliojificha?!

-Hilo linatufanya tujiulize: Je, elimu ina mipaka inayoishia mbele yake? Yatupasa tufahamu kuwa uwezo wa elimu vyovyote itakavyokuwa ina mipaka yake katika kufasiri kila kitu; Ulimwengu ulojificha sio katika yanayojulikana kwa njia za elimu, kwa sababu elimu haiwezi kufasiri baadhi ya matukio ya Kifizikia ambayo tunaishi nayo sasa, vipi kwa elimu ya ulimwengu uliojificha ambao hauwezi kuwa chini ya maabara ya majaribio na vyombo vyenye hisia vya kudiriki?!

Tukiongezea hapo; Elimu yetu ya jambo fulani haipasi kutupeleka kwenye kumkana aliyeiumba wala kupunguza uzuri wa mgunduzi wake, kwa hiyo ikiwa mtu mshamba alipoona televisheni alishtuka na kushangaa, kisha baada ya hapo akajua nadharia na njia inayofanya televisheni kufanya kazi, hilo halitomfanya kudharau thamani ya kazi hii

www.path-2-happiness.com

au kumkana aliyeitengeneza, vivyo hivyo mfano wake ikiwa tutaweza kupiga hatua katika elimu ya biolojia katika kufichua seli na kuvumbua DNA; na kuonekana maajabu yake, Je, ina maana kuwa katika hilo hakuna miujiza? Au kuwa maumbile yake hayana muumba wake? Kinyume kabisa, kwa hakika maajabu yote haya ambayo mwanadamu amesimama nyuma akiwa ameshindwa kufanya mfano wake kuanzisha kisichokuwepo au kutafsiri jinsi ya utendaji wake na hilo ni upeo mdogo linampelekea kwenye imani kuwa nyuma ya maumbile haya kuna muumba.

Chukua mfano mwingine: Anasema Profesor Syell Bays Hamkan nae ni mtaalamu wa Kimarekani katika biolojia:

-“Kwa hakika ni tendo la ajabu katika kubadilika chakula na kuwa sehemu ya kiwiliwili kabla ya kunasibishwa na Mwenyezi Mungu, leo hii kwa uthibitisho mpya, limekuwa ni tendo la kikemia, Je, hili limebatilisha uwepo wa Mungu? Ni nguvu gani iliyozifanya elementi hizi kuwa chini ya elementi za kemikali zenye faida? Chakula baada ya kuingia kwenye kiwiliwili cha mwanadamu hupitia awamu nyingi katika mfumo wake binafsi, na ni jambo lisilowezekana kufanikisha uwepo wa mfumo huu wa ajabu kwa maafikiano barabara; imekuwa ni lazima baada ya kushuhudia huku kuamini kuwa Mungu anafanya kwa kanuni zake nyingi ambazo ameumba nazo uhai.

Maiko: Lakini nadharia ya Darwin ya Evolution (nadharia ya mageuko) imethibitisha mtazamo huu huu; ulazima wa elimu kuachana na uwepo wa Mungu Muumba, na imethibitisha (vile vile) kuwa viumbe hai vimekulia chini ya kanuni ya uteuzi wa mazingira na ukuzi, na wala sio kuumbwa.

Rashidi: Jambo hili linatupelekea kujiuliza maswali muhimu kulingana na nadharia hii au nyinginezo; Je, tafsiri ya elimu ni kamili katika hali zote? Wengi katika watunduwaji wamesahau kuendelea kwa elimu kuwa katika sifa za elimu ni kulimbikiza na kuleta mapinduzi, nazo hutengeneza au kuumba chombo cha maendeleo ya maarifa na sayansi, ambapo elimu inalimbikizwa na ugunduzi hadi kufikia kwenye kiwango ambacho kitaleta sheria mpya halisi katika kurejesha mtazamo katika maarifa ya zamani, ambayo yatabadilisha mtazamo wa mwanadamu kuhusu elimu.

Katika nadharia ya Darwin ambayo kwa vyovyote vile ni tokeo la kielimu, haijafikia kwenye kiwango cha ukweli wa kisayansi wala hata kufikia kiwango cha kuwa ni nadharia, bali ni fikra kuhusu mageuzi na ukuzi, fikra hizi zimegongana na ugunduzi wa elimu mpya ya embryolojia

(elimu ya kiini tete) vile vile machimbo ambayo yamethibitisha kuibuka ghafla kwa makundi ya wanyama wakati mfupi ambayo yalijulikana kama zama za cambria (zama za mwanzo za jiolojia) na muda huu kujulikana kwa jina la Mlipuko wa Cambria hii ndiyo ilivyokuwa badala ya kukua mmoja, kuendelea na kukaa na kufuatana na mwingine, kama isemavyo nadhari ya ukuzi na mageuzi.

Rajev: Kama ni hivyo basi, Je, hakuna uwezekano wa kuwa mwanazuoni huyu aliibuka ghafla tu na bila ya kuwepo kwa muumba wake?

Rashidi: Niruhusu nikubainishie maana ya bahati nasibu kupitia matumizi ya misingi ya elimu ya hesabu na kanuni hizo za bahati nasibu; ili uweze kujua ni kiasi gani zinaweza kutokea.

Kama tukijaalia kuwa tuna sanduku kubwa lililojaa herufi za alfabeti, uwezekano “A” kuangukia jirani na “M” ili kutengeneza neno ‘AM’ huenda ikawa ni mkubwa kiasi fulani, ama uwezekano wa herufi hizi kujipanga (zenyewe) zikatengeneza nyimbo au shairi, bila shaka unakuwa finyu sana, iwapo itakuwa sio muhali (lisilowezekana).

Wanazuoni wamehesabu uwezekano wa kukutana atomi nyingi na uwezekano wa kutengeneza amino asidi (Amonium Acid) ambayo hutengeneza protein na nyama na wakakuta kuwa hilo linahitajia miaka bilioni nyingi na kuwepo na mada ambayo haitoshelezi kuwa nao, hii ilikutengeneza sehemu moja tu kwa udogo wake, sasa iweje kwa kutengeneza maumbo ya viumbe hai wote, miongoni mwa mimea na wanyama, sembuse kutengeneza maisha yenyewe na ulimwengu wenyewe… ni jambo ambalo haliingii akilini kuwa hili limetokea kwa bahati mbaya tu.

Hakika matawi yote ya elimu huthibitisha kuwa pana mfumo makini wa ajabu wenye kudhibiti na kuratibu uliotapakaa katika ulimwengu huu, msingi wake ni kanuni na nyendo za kilimwengu ambao haugeuki wala haubadiliki, ambao wanazuoni wanakesha kuufanyia kazi katika kuugundua na (kuujua) kuuzunguka, gunduzi nyingi za kisayansi zimefikia daraja la juu kabisa na umakini mkubwa kutuwezesha kutarajia kupatwa jua na mwezi na mengineyo katika mazingira yaliyo dhahiri kabla ya kutokea kwake kwa mamia ya miaka.

Basi ni nani aliyeweka kanuni hizi na kuwekea kila atom katika atom zilizopo, bali hata katika iliyo chini zaidi ya wizani wa atom kwenye ukuaji wake wa mwanzo?! Ni nani aliyeumba mfumo wote huu na maafikiano yale? Ni nani aliyesanifu akapendezesha usanifu ule na akakadiria na

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

kufanya uzuri makadirio yale?! Je, vyote vimeumbwa bila ya uwepo wa muumba, au watu wenyewe ndio waumbaji? Hivi ndivyo Qur'an kitabu cha Waislamu kinavyosema:

"Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?" (52:35)

Kwa kweli kanuni na mfumo ambao unaendesha ulimwengu huu, na uzuri ule ambao tunauona popote pale macho yetu yatakapoelekea yanaonyesha kuwa kuna muumba muweza, mtambuzi ameanzisha huu ulimwengu.

Maiko: Lakini hapa linajitokeza swali pamoja na kutilia kwangu nguvu malengo yake nayo ni: Ni ipi haja yetu kwenye dini na kumuamini Mungu? Watu wengi wanaishi maisha yao bila ya kuamini kwao Mungu na bila ya wao kuwa na dini wanayoifuata.

Rashidi: Masomo ya Anthropolojia (elimu kuhusu mwanadamu) na elimu kuhusu dini yameunga mkono kuwa haja ya dini ipo kwa watu wote na zama zote na katika jamii zote, mwanadamu tokea hapo zama za kale alikuwa akitafuta Mungu anayeweza kumuabudu na kujikurubisha kwake, akiamini kuwa ni mwenye nguvu na mwenye kutawala ulimwengu, muumba wa kila kitu yu hai wala hafi.

Hakika maumbile ya mwanadamu yanashuhudia kuwa kila mwanadamu anapopata dhiki yoyote au anapotishwa na hatari au matarajio yake yakakaribia kupotea wakati huo mwanadamu huyo ana haja ya kibaolojia inayomsukuma kwenye kumuamini Mungu.

Kama ambavyo bila imani hii mwanadamu aghalabu anakuwa mnyama anayetawaliwa na matamanio wala hayarejeshwi na dhamira yake.

Rajev: Niruhusu ustaadh Rashidi, nimeishi katika nchi yenye dini nyingi mno, na nikahamia Ulaya na kufahamu dini zingine na wenye dini hizo, nimekuta kuwa, kila mwenye dini anatofautiana na mwingine katika taswira yao kuhusu Mungu, vipi tunaweza kutafsiri tofauti hii? Na vipi nitajua sifa anazosifika nazo mungu wa haki? Vivyo hivyo: Vipi nitajua dini ya haki dhidi ya nyinginezo?

Rashidi: Namuona mhudumu akija na chakula, na ninawaahidi kuyajadili masuala haya katika mijadala ijayo, lakini kwanza hebu tuafikiane katika kauli ya mwanafizikia Albert Einstein;

"Elimu bila dini ni kiguru, na dini bila ya elimu ni upofu."

www.path-2-happiness.com

Minara ya Njia

Minara ya Njia

Katika moja ya meza hapo Social Lounge, walikutana marafiki watatu; Rashidi, Maiko na Rajev, na kila mmoja kuagiza kinywaji akipendacho, kisha Rajev akaanza kuzungumza:

Katika kikao chetu kilichopita tulifikia kwenye mazungumzo kuhusu sifa ambazo anasifika nazo Mungu wa kweli, na jinsi ya kufahamu dini ya haki kwenye zingine.

Maiko: Niache nithibitishe uhakika na kuuliza swali: Bila shaka elimu katika matawi yote imepita hatua kubwa sana, kwa mfano elimu ya tiba leo hii imeitangulia iliyokuwepo kabla ya karne mbili, teknohama (Teknolojia ya habari na mawasiliano) imepaa mno, na kadhalika hakika nyingi zilizopo kwenye elimu ya Kemia…., na mara kwa mara mitaalaa huendelezwa kufundisha elimu hizo kwa haraka mno, kiasi cha kufikia vumbuzi mpya, hatupati katika elimu hizi za maada atakayesema leo hii miongoni mwa wanazuoni wa maada kuwa ardhi inafanana na mpira kwa mfano, wakati ambapo katika elimu za fikra bado ipo katika kujadili kadhia zile zile za miaka elfu iliyopita juu ya: Kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, dini ipi ni ya kweli, ni mfumo upi unamfaa mwanadamu katika maisha yake, na maana ya uadilifu…..na nyinginezo katika mitazamo na taswira mbali mbali, ukisema kuwa elimu inaendelea na kukua, kwa nini basi tusiseme vile vile kuwa nayo dini inakua na kuendelea?

Rashidi: Tokea maelfu ya miaka imani inagongana na taswira na fikra mbali mbali, na mgongano huo unaendelea hadi leo hii, kwa njia ya moja kwa moja au isiwe ya moja kwa moja, na hii Ina maana kuwa akili ya mwanadamu haijafikia katika elimu ya fikra kwenye maendeleo kama elimu za maada zilivyofikia maendeleo makubwa, na hii ni kwa sababu msingi wa uwepo wa mwanadamu haukubadiika, vivyo hivyo kadhia kubwa za msingi wa mwanadamu zinazoshughulisha fikra zake hazijabadilika vile vile.

Mwanadamu siku zote anatafuta tafsiri pana ya uwepo inayokusanya kila kitu, na huamiliana kwa msingi huu na uwepo huu..hutafuta tafsiri inayosogeza udiriki wake kwenye tabia ya hakika kubwa ambazo anaamiliana nazo, tabia ya mahusiano na hakika hizi, zinazotufanya kuwa ni watu tulioumbwa, yaani viumbe ambavyo vinaainisha mahusiano yao na Mungu pamoja na wengine, kwa hivyo basi tunaweza kufaidika na waliotutangulia katika kadhia hizi kama ambavyo tunaweza kufaidika na waliomo, hivyo basi maudhui ambayo imeshajadiliwa ndio maudhui hayo hayo yaliyoibuliwa, nayo ni maudhui yanayohusiana na ulimwengu, maisha na mwanadamu, ikiwa watu wameafikiana katika hakika nyingi za kielimu za kimaada wao hawakuafikiana katika hakika nyingi zinazohusiana na maudhui nyingi, taswira na mitazamo ya kifikra mbali mbali, na hali hii haitoisha ila kwa kuisha mwanadamu.

Maiko: Hivyo basi tunaweza kusema: Sisi hatuwezi kufikia kwenye hakika katika mfano wa maudhui haya.

Rashidi: Nani amesema hivyo? Vinginevyo nini faida ya mjadala?! Ninaamini kuwa tunaweza kupitia mjadala wetu wa kifikra pamoja na umuhimu wa kujitenga ili kufikia kwenye haki na kuacha matamanio na kasumba, kwa mwenye kutaka kufikia kwenye ukweli kwa nia safi na kufuata njia inayopelekea huko basi Mwenyezi Mungu atamuongoza kwenye njia hiyo, na dalili ya hilo ni kuwa pamoja na kuwepo kwa mgongano huu maendeleo yalishafikiwa chini ya Manabii na waja wema au watu wenye fikra, bali wakati mwingine kupitia dola mbali mbali, hata hivyo makusudio ni kuwa babaiko na migongano ni sifa inayosuhubiana na kadhia za kifikira au za kibinadamu nayo ni tatizo la zama zote za kale na za sasa.

Lakini niache nikutanabahishe katika nukta mbili muhimu katika suala hilo, nazo ni:

Kwanza: Kutangulia katika elimu ya maada haina maana kuwa yatakuwepo maendeleo ya kifikra, taswira na ufahamu, kwani hakuna mafungamano baina ya maudhui mbili na dalili ya hilo kwa mfano ni ukaribu wa kimaada wa Marekani na Japan pamoja na tofauti zilizopo za taswira na ufahamu na fikra ya mwanadamu na ya kidini, na hii ina maana kuwa kuendelea kwa baadhi ya jamii katika baadhi ya elimu za kimaada haina maana kuwa ni lazima ziendelee katika elimu na fikra.

Pili: Ni kuwa, hakika haipati usahihi wake na kutiwa nguvu na kundi la watu au kupinga kwao kwa sababu jamii ya mwanadamu mara nyingi huangukia kwenye batili, bali historia ya mwanadamu imesajili mjumuiko wa watu wengi wapo katika taswira zenye makosa au matendo yasiyokuwa ya kimaadili au hata ujambazi wenye kutisha.

www.path-2-happiness.com

Rajev: Naafikiana nawe katika hilo, lakini naona kuwa sisi tupo katika vyanzo tofauti vya staarabu, na kadhalika sote tunabeba itikadi na taswira mbali mbali, hivyo hapana budi tuafikiane kwanza katika misingi au hoja ambazo tunathibitishia ukweli wa jambo au kutosihi kwake.

Maiko: Naona kuwa hakuna njia ya hilo isipokuwa kupitia njia mbili: Akili, au elimu.. hili ndilo tunaafikiana wote.

Kimsingi nakubaliana nawe, lakini ni akili gani unayoikusudia? Kwani akili yangu sio akili yako, kadhalika elimu gani?, Je, unakusudia elimu ya majaribio peke yake?

Nakusudia matumizi ya akili ya kuzaliwa ambayo watu wawili wowote hawatofautiani au hoja za kiakili ambazo tunakubaliana nazo, na nadhani sisi hatutofautiani juu ya hakika za kisayansi zilizothibitishwa kisayansi, na bila shaka hii ni tofauti na zile fikra za kielimu au nadharia au majaribio ambayo hayajafikia kwenye kiwango cha ukweli, je, huafikiana nami katika hilo.

Rashidi: Nakubaliana nawe katika hilo, lakini naashiria katika hoja nyingine ambayo umuhimu wake haupo mbali na hoja hizi: Nayo ni hoja ya mazingira katika maumbile. Ambapo nataka kuleta hoja nyingine inayohusu mamlaka ya matumizi ya akili na sayansi. Kwamba kuna tofauti kati ya kinachothibitishwa ana akili kuwa ni kosa au hakiwezekani au kile ambacho akili inakiona kuwa ni kigumu kukifahamu.

Rajev: Unakusudia nini kwa hoja ya maumbile?

Rashidi: Nakusudia: Hisia au muelekeo wa mwanzo wa ndani ya mwanadamu ambao wanashirikiana watu wote, kuna tabia na sifa ambazo zimewekwa kwenye vitu vilivyopo, iwe ni kwa vitu, mimea, au mwanadamu na mnyama, kwa mfano: Tunasema kuwa katika maji kuna sifa ya kuchemka itakapofikia daraja mia moja, au mwili wa mwanadamu unahitajia uwe na joto kati ya asilimia 34-42 ili mtu abakie kuwa hai, mambo haya yapo katika vitu hivi ila vimekuwa bila ya mwenyewe au chenyewe kutokuwa na matakwa yake katika hilo.

Maiko: Unakusudia silika iliyopo kwa mwanadamu na mnyama?

Rashidi: Silika zilizopo kwa mwanadamu na mnyama, nayo ni maelezo kuhusu sifa mahususi za ndani inazozitoa katika maisha yake, kama vile silika ya kushambulia na kuwinda kwa wanyama wakali, hakuna mtu ambaye anaingiza uelekeo kwa wanyama, au kuelekea na kurudi katika nchi zao za asili kwa ndege, na kuhamahama kwa samaki, na silika ya umama kwa wanawake, na mwenye silika ile anaweza kulifahamu hilo lakini asitanabahi siri ya silika yake.

Ama maumbile na mambo ya kimaumbile, hayo yanapatikana kwa mwanadamu tu, nayo vile vile ni mambo ya kiasili kwake na sio anayoyapata kutoka nje, naye anayajua na kuyadiriki, lakini tofauti kati ya maumbile na silika, ni kuwa silika huwa katika mambo ya kimaada, wakati ambapo maumbile ya asili (Fitrah) huhusiana na mambo ya kibinadamu, kwa mfano: Kupenda elimu na maarifa, kutafuta ukweli, hamu ya uvumbuzi, kuelekea kupenda kheri na fadhila, kuelekea kupenda uzuri…. Mwanadamu hupenda vitu hivi na kuvitafuta na kuvutika navyo bila kuingilia mazingira yenye kumzunguka wala bila ya kuyapata kutoka kwenye malezi anayolelewa au makuzi yake ya kijamii, kwa hivyo mambo ya fitra yamepandwa kwa mwanadamu na huota katika dhati yake, mfano wake ni mfano wa silika za kihayawani, lakini ni mambo maalumu kwa mwanadamu, na fitra hii kwa mwanadamu ndio ambayo humfanya mwanadamu kukubali mazuri na kuchukia mabaya, hivyo huwezi kumpata mwanadamu mwenye maumbile sahihi anayechukia mafuta mazuri na mandhari nzuri na kuvutika na harufu mbaya na mandhari mbaya.

Rajev: Tutawezaje kuainisha mambo haya ya kimaumbile, ili tuweze kuhukumu kuwa jambo hili ni la kimaumbile au sio?

Rashidi: Mambo ya kimaumbile kwa mwanadamu yanajulikana kwa sifa nyingi miongoni mwazo ni:

Pana, yanayokusanya mengi, na yanayoenea kwa watu wote.

Ni ya zama zote, hayawezi kukidhi jambo katika zama moja na yasikidhi jambo jingine katika zama zingine.

Yanayotokea ndani ya mwanadamu mwenyewe na dhati yake, wala hayapatikani kwa mtu kusoma au kwenye mazingira, pamoja na kuwa elimu ndio itakayoyakuza na kuyaendeleza.

Hayawi chini ya utawala wa mazingira yenye kumzunguka, hata hivyo yanaweza kuathirika na baadhi ya hali, mambo ya maumbile yanaweza kubadilika usafi wake na kuharibika kwa tabia yake, hali hiyo ni kama

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

hali ya milango ya fahamu ya mwanadamu kama vile kusikia, kuona, kuonja akipata maradhi, hata hivyo kwa ujumla hayafutiki, bali yanaweza kudhoofika au kufifia bila kuondoshwa kwenye misingi yake.

Maiko: Naona kuwa sisi tumeafikiana juu ya yaliyoelezwa, lakini kwa sababu ya nukta hii ya mwisho nina mashaka katika baadhi ya mambo, kuwa maumbile ni moja ya nyenzo za kuthibitisha katika maudhui yetu.

Rajev: Tunaweza kujadili masuala yanayohusiana na maumbile wakati wake, tukikubaliana sote basi tutaafikiana juu yake, na na tusipokubaliana tutatafuta hoja nyingine.

Rashidi: Kwa mnasaba huu napenda kutanabahisha baada ya kuafikiana nyenzo hizi kuwa huenda baadhi ambao hawafahamu wakadhania kuwa kuwafikiana kwetu katika nyenzo hizi hakuafikiani na dini ya Uislamu, na hili ni kosa.

Maiko: Ninachokijua ni kuwa dini iliyosimama katika imani kwa maandiko matakatifu na kujisalimisha kwa ukweli wa kadhia zake haikubali mjadala au kusitasita, kwa ajili hii kumetokea vita vingi katika historia ya Ulaya baada ya uvumbuzi wa kielimu, ambapo Kanisa ilikuwa likipiga vita uvumbuzi na fikra ya akili inayojitenga na kitabu kitakatifu.

Rashidi: Maneno yako ni sahihi pamoja na kuzuia baadhi za rai zangu, hata hivyo hilo halihusu Uislamu, ni kweli dini inasimamia imani kwa maandiko matakatifu, na kukubaliana na usahihi wa kadhia zake ni usahihi kabisa, lakini Uislamu umeifanya akili, kufikiri, elimu inayotokana na mazingatio, kuangalia kwa kina, uzoefu katika nafsi na katika matarajio ni njia ya kumuamini Mwenyezi Mungu na Qur'an, kitabu kitakatifu cha Waislamu na Mtume wake… Historia ya Uislamu haijashuhudia mgongano huu na mgogoro unaozungumzia kati ya dini, elimu na akili.

Rajev: Jambo la kushangaza kabisa, kitabu chenu kuhimiza na kuheshimu akili, tafakuri na elimu!

Maiko: Namuona muhusika wa ukumbi anatuashiria kuwa muda wa kufunga umekaribia, tusimame katika nukta hii na tukamilishe kesho.

Rajev: Mimi nitakuwa mwenye shughuli kesho, nitafurahia kama mtakubali mualiko wangu kesho kutwa katika safari ya pembezoni mwa mto Seine.

Maiko na Rashidi: vizuri sana, bila shaka tutafurahi.

Mjue Mungu Wako

www.path-2-happiness.com

Mjue Mungu Wako

Katika Alasiri ya siku ya jua safi, walikutana marafiki watatu kulingana na ahadi yao waliyowekeana pembeni ya Mto Seine, Rajev aliwaita rafiki zake wawili wachukue boti lililoonekana la kifahari…. Marafiki hao watatu walisimama wakifurahia mandhari nzuri ya mto na kijani chake kinachoizunguka pande zake….Rashidi aliangalia katika upeo wa macho yake na akawaambia rafiki zake:

Mito, bahari, mimea, wanyama, milima na wanadamu na kila tunachokishuhudia katika ulimwengu huu, bali hata ambayo hatuyashuhudii wala hatuyaoni…. Yote hayo ni dalili ya wazi juu ya hekima yenye miujiza ambayo imefanya vitu hivi viishi, na inaonyesha kuwa ulimwengu huu una Muumba na Mola, Je, hamuafikiani nami katika hilo?

Rajev: Tuliafikiana katika kikao chetu kilichopita kuwa katika umuhimu wa ulimwengu kuwa na Muumba, hata hivyo kuna baadhi ya kadhia zinazohusiana na ukinaishaji huku ambazo zinafaa kujadiliwa na kuzichunguza.

Maiko: Ninaona jambo la muhimu kuanza nalo ni yaliotangulia kutajwa na Mhandisi Rajev kuhusu sifa ambazo anasifika nazo Mungu wa kweli.

Rashidi: Hakika kile tunachokiishi na kukishuhudia katika uzuri wa umbile la ulimwengu kimeshikamana na unachokitafuta, kwani asili ya imani na yakini ni kuwa Allah ndie wa haki na wewe uwe na 'mtazamo sahihi' kwa ulimwengu huu, ikiwa pamoja na nafsi yako uliyonayo, na hilo ni kwa kujua vipengele vyake na mpangilio wake na malengo ya kuumbwa kwa kila kiumbe ndani yake.

Maiko: Tumekubaliana kuhusu uwepo wa Mola Muumba wa ulimwengu, lakini taswira hii ya Mungu inatofautiana kwa kila dini, lakini kati ya taswira hizi nyingi kuna tofauti kubwa, hali inayopelekea baadhi ya watu kutoroka utafiti katika maudhui haya na kuishi maisha yanayokaribiana na kukana uwepo wa Mungu, hata kama hawatokiri hilo waziwazi.

Rashidi: Mna haki enyi swahiba zangu, lakini na kuongezea kuwa kukimbia huko hakuwakatazi na hisia ya haja ya kuwa na Mungu, bali kwa hakika baadhi yao wanapokana uwepo wa Mungu wanajitengenezea Mungu wao wenyewe na kufanya matamanio ya nafsi zao kuwa ni Miungu yao, hivyo basi kiburi cha wenye kukana uwepo wa Mungu muumba kimewafanya wakimbie kukiri uwepo wa Mungu na kuamini mambo mengine, sifa na uwezo ule wa Mungu ambavyo haifai kuipa isipokuwa kwa Mungu wa kweli bila hata ya haki yoyote isipokuwa kutoroka katika taswira potofu ya Uungu waliyoushuhudia au kuuishi.

Rajev: Tukiingia katika maudhui yetu tunaweza kusema: Kwa hakika Mungu ni lazima awe ni mwenye kuogopewa na mwenye kupendwa kwa wakati huo huo, mwanadamu huhisi haja ya kumuelekea yeye, huu ni kwa upande wa mwanadamu, lakini sifa hizi katika hakika yake huwakilisha hali ya mwanadamu inavyokuwa kwa zaidi ya mtu mmoja kuelekea kwa zaidi ya Mungu, hivyo basi: tuoneshe sifa ya Mungu wa haki ambaye watu wanapaswa kuafikiana.

Rashidi: Maneno yako ni mazuri na sahihi…na jambo linalounganisha tulilpoanzia ndani ya kukiri kwetu ulazima wa uwepo wa Mungu, na kuafikiana kwetu kuwa ulimwengu huu mzuri ulioshikana vizuri una Muumba mkadiria ulimwengu huu na kuupata wakati haukuwepo, Muumba huyu ndie ambaye tunamsifu kuwa ndie Mola, na Mola huyu ambaye ndie Muumba wetu na Muumba wa kila kitu. Ukweli ni kuwa Muumba huyu anastahiki kufanywa Mungu na kuabudiwa na hapaswi kuabudiwa asiyekuwa yeye; yaani: Kama ulivyosema wewe yapasa asielekewe yeyote asiyekuwa yeye kwa kumuogopa kabisa, mapenzi, hofu, na kutarajia kabisa...na kuanzia hapa tunaweza kugusa sifa za Muumba huyu wa haki.

Rajev: Tukikubaliana na maneno yako, ninaweza kusema: Sifa za mwanzo ni kuwa Mungu huyu yupo na awe HAI, kama ambavyo Mungu huyu hana budi kuwa ndie Muumba.

Rashidi: Hili ni kweli kimsingi (linahitajia akili ya kuzaliwa) vile vile Mungu huyu asiwe kwa dhati yake na sifa zake ameumbwa; kwani Muumba hawezekani kuwa ameumbwa; kwani kama atakuwa ameumbwa basi atakuwa mfano wetu, atakuwa na Muumba, hivyo hawezi kuwa Mungu wala hapasi kuabudiwa,; na katika hilo vilevile viumbe vyote haviwezi kuwa Miungu.

Maiko: Kama ni hivyo, yatupasa tufahamu nini maana ya Muumba?

Rashidi: Kwa ufupi, naweza kusema: Kuwa hakika Muumba ni mwanzilishi wa vitu, bila mfano au mtindo kabla yake, yaani: aliyevipata

www.path-2-happiness.com

vitu vyote baada ya kutokuwepo, nae pia ni muweza wa kuvipata kutoka kwenye kutokuwepo nae anakadiria vitu hivi na kuvijenga, katika makadirio yanayowajibishwa na hekima, yaani si mchezo wala kubahatisha.

Ama sifa za lazima kwa aliyeumbwa; Ni kutokuwepo kabla ya kuumbwa kwake; yaani mwenye kuzushwa, hapana budi wao kufa; yaani wawe na mwisho, vile vile wawe na uwezo wenye ukomo, na siku zote wanawahitajia wenzao.

Rajev: Ikiwa Mungu huyu ndie Mola Muumba, basi ni kawaida awe Mmiliki wa alichokiumba.

Na tunaposema vilivyomo mbinguni na ardhini ni vya Allah, vimeumbwa, ni lazima vyote vifahamike kwake; kwani kama vitajificha kwake basi mja huyo hatokuwa anafahamika na Mola wake, na atakuwa amejitenga na Muumba wake, kama ambavyo inathibitisha elimu yake; ustadi na umadhubuti ambao tunauona kwa viumbe, hili haliwi isipokuwa kwa ukamilifu wa elimu.

Rashidi:Yanayoambatana na umiliki; Kufanya atakayo katika Mbingu na Ardhi na vilivyomo baina yake, na juu ya elimu yake: Awe na haki katika kuyaendesha na kuweka miundo ya mambo, kanuni zake.

Maiko: Lakini na mimi vile vile nina miliki vitu, na mimi vile vile ninajua mambo mengi sana, Je, hayo yana maana na mimi ninazo sifa za Uungu? Hapana sidhani hilo kuwa ni sahihi!

Rashidi: Ugunduzi wako ni muhimu sana ewe rafiki yangu, nami naona kufafanua katika kutaja sifa hizi kwa njia hii kutarefusha pamoja na umuhimu wake, na tunaweza kufikia katika msingi wa jumla (kanuni kuu) ambayo tunaweza kuifanya kuwa ni kigezo cha sifa hizi, na tunaweza kwa kiasi kikubwa kutoa sifa kupitia kwayo; niruhusuni nioneshe sifa na alama za msingi huu; nayo kwa ukweli kulingana na taswira yangu iliyosimama juu ya utamaduni wangu wa Kiislamu.

Maiko na Rajev: Haya tafadhali tuelezee.

Rashidi: Tunaweza kufupisha msingi huu kwa yafuatayo:-

Kwanza: Tunaweza kugawa sifa katika makundi mawili:- Sifa pungufu na sifa kamilifu.

Ukamilifu ni: Kusifika na sifa nzuri pamoja na kuzuilika na kinyume chake cha sifa nzuri.

Na upungufu ni: Kusifika na sifa hasi pamoja na kuzuilika na kinyume cha sifa nzuri.

Hivyo basi: Ni juu yake kuzuia kusifika na sifa hii hasi yenye kuzuia kutakasika kwake, inatupasa kusifika na kinyume cha sifa hii, yaani; kusifika miongoni mwa sifa za ukamilifu; la sivyo kukana kutakuwa kukana upungufu; kwa sababu kutosifika kwenyewe ni upungufu na kushindwa.

Pili: Kitu ambacho kiumbe anajiona nacho, haiwezekani kukithibitisha kwa Muumba, kwa hiyo kila ambacho kiumbe anatakasika na anasifiwa nacho katika mambo yasiyopendeza ya aibu, hivyo Mungu Mtakasifu ndie mwenye haki zaidi ya kutakasika nayo na kutukuzwa wala haifai kuingia sifa mbaya na za aibu katika sifa zake kwa njia yoyote ile, kwani Mungu ni mkamilifu kwa njia zote.

Tatu: Kipambanuzi kilichokamilika kati ya Muumba na kiumbe, Muumba hana mfano wake na yoyote, ama yaliyokuja katika sifa ambazo anaweza kupewa Muumba na kiumbe; kama vile mfalme, elimu, huruma na mapenzi, hakuna mfanano wake katika maana ya kweli, kwa sababu sifa za Muumba aliyetakasika ni kinyume na sifa za kiumbe, kwani sifa za viumbe haziepukiki na upungufu.

Maiko: Laiti ungebainisha uyasemayo kwa mifano:

Rajev: Laiti ungelielezea nukta ambazo umezitaja na mifano halisi.

Rashidi: Vizuri, Nukta ya kwanza: Watu wote wenye akili wanakubaliana kuwa udhaifu ni sifa ya upungufu, vivyo hivyo kuhitaji wengine au vitu ni sifa ya upungufu, hivyo basi haifai kuwa Mungu wa kweli ni mwenye kusifika na moja ya sifa mbili hizi, bali hapana budi kuwa mwenye kutakaswa na sifa mbili hizi na (kuwa) mwenye kusifiwa kwa wakati huo huo na kinyume chake miongoni mwa sifa za ukamilifu ambazo ni: Nguvu, kutosheka, au kutowahitajia wengine, ndio maana Qur'an yetu imepinga Uungu wa masihi na mama yake (Juu yake amani ya Allah) kwa maneno matatu yaliyogusa kiini cha maswala haya, nayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu:

"Masihi mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume. Wamekwisha pita Mitume kabla yake. Na mama yake ni mwanamke mkweli. Wote wawili walikuwa wakila chakula. Angalia jinsi tunavyo wabainishia Aya, kisha

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

angalia vipi wanavyo geuzwa.” (5:75)

Ambaye atahitaji kula chakula kwa hakika anakula kwa sababu ya hisia yake ya njaa na yanayoambatana nayo kama vile udhaifu na unyonge, na mwenye kuhitajia chakula, na hivyo basi haifai wawe au mmoja wapo kuwa Mungu: kwani sifa za Mungu wa kweli hazithibitiki.

Vivyo hivyo: Kuwa na mtoto: Mungu wa kweli ametakasika na upungufu unaofanana na viumbe wenye kuhitajia, kwani mwenye kutaka mtoto anamtaka kwa kuendeleza utajo, msaada, urithi na mfano wake, nazo zote hizo ni sifa za upungufu, na uhitaji haumfai Mungu wa kweli.

Ama nukta ya pili: Watu wote wenye akili wanakataa kusifika na sifa ya kushindwa, kwa hiyo aula ni kutosifika mola wa haki na sifa hizi, bali hapana budi kusifika na sifa ya ukamilifu na sifa zinazokubaliana nae, ikiwemo sifa ya uwezo. Na hivyo basi ikiwa masihi hawezi kuzuilia nafsi yake na maudhi ya adui zake, au masanamu, wanyama wenye kuchukuliwa kuwa ni miungu kwa baadhi ya watu, hivyo hawezi kujilinda…basi hao watakuwa wanashindwa kuwalinda wenye kuwaabudu na wapenzi wao (hili ni suala la akili ya kuzaliwa) na hivyo basi ambae atashindwa hafai kuwa Mungu wa Haki Anayeabudiwa.

Wenye akili hawataki kusifika kwa sifa ya kudhulumu na hivyo basi: Mungu wa kweli hadhulumu, kwani yeye ni muadilifu….vivyo hivyo kila chenye kukana upungufu huwa na mkabala wa kuthibitisha kinyume chake.

Mwisho: Nukta ya tatu: Tuchukulie kwa mfano: Sifa ya elimu, nayo ni sifa nzuri na kinyume chake ni sifa hasi ya ujinga…ukamilifu ni kusifika na elimu na kuepushwa na ujinga, na upungufu ni kusifika na ujinga na kuepushwa na elimu. Mwenyezi Mungu Ndie Mwenye ukamilifu wote katika sifa ya elimu, kwani husifika kwa elimu timilifu na ujinga kwake unazuilika kabisa.

Ama mwanadamu ana ukamilifu wa kiwango fulani katika sifa ya elimu, kwani husifika na elimu katika baadhi ya mambo na husifika na ujinga kwa baadhi ya mambo mengine, hivyo basi ukamilifu wake ni mnasaba tu. Na mfano kama huo katika sifa nyinginezo.

Maiko: Nahisi baridi na haswa usiku unapoingia, nadhani haya yanatosha kwa usiku huu.

Nuru ya Mbinguni

(Haja ya Watu na Utume)

www.path-2-happiness.com

Nuru ya Mbinguni

(Haja ya Watu na Utume)

Rashidi alipoingia Social Lounge katika nyumba ya vijana waliyokuwa wakikaa, alikuta Maiko amekaa katika moja ya meza akiwa anaangalia sakafuni kama vile anachunguza taa zilizoning'inizwa humo. Rashidi alimuelekea na kumsalimu… Maiko hakutanabahi kufika kwa Rashidi… alivuta kiti na akamuelekea, na akamsemesha:

Inaelekea umeshughulishwa na kitu muhimu….. naweza kushirikiana nawe kwenye jambo lako?

Maiko: Ooh….samahani, sikugundua kufika kwako.

Rajev hajafika bado?

Rashidi: Imebakia dakika tano kwa ahadi yetu….

Huyo anatujia…

Rajev: Salamu njema rafiki zangu.. Nimefurahi kukutana nanyi.

Rashidi: Na sisi hali kadhalika.

Maiko: Kwa hakika mimi ni mwenye furaha kwa kuingilia nukta hii, hivyo basi: Ni nini lengo ambalo Mungu ameumba ulimwengu na binadamu na akampa neema zake?

Rajev: Nilikuwa nafikiria nukta hii hii kabla sijafika hapa.

Rashidi: Maswali yenu ni mazuri sana, na katika sehemu yake.. Hakika Mwenyezi Mungu aliyeumba wanadamu katika umbo bora, na akawadhalilishia yaliyomo ardhini na kuwateremshia kheri nyingi kutoka mbinguni, akili haiwezi kufikiri kuwa yote haya yameumbwa kwa mchezo tu na bila ya kuwepo kwa malengo.

Maiko: Vizuri sana kuzungumzia nukta hii, kama ni hivyo basi: Ni lipi ambalo Mwenyezi Mungu ameumba ulimwengu pamoja na watu na kuwapa neema?

Rajev: Nataraji hilo linaambatana na sifa za Mungu wa kweli ambazo imetangulia kutajwa katika mjadala uliopita, kwani Mungu alikuwepo kabla ya kuwepo viumbe hawa… hata hivyo siwezi kufupisha hilo kwa ukamilifu.

Rashidi: Sahihi kabisa ulichokitaja Rajev, nami najaribu kuainisha na kuleta karibu kwa mfano huu ambao naukusudia katika kulinganisha na sio kufananisha: Wewe unapopenda kitu basi utapenda uhakika wake halisi …. Au sivyo?

Rajev: Ndio, bila shaka.

Rashidi: Kama ni hivyo basi, nini kinachoweza kukuzuia kukitekeleza kiuhalisia?

Rajev: Sababu ambayo inaingia kichwani mwangu sasa hivi: Ni kutoweza kulitekeleza.

Rashidi: Utakapofanikisha uwezo huo basi utaupata….na hili ndilo jambo lenyewe.

Maiko: Mfano wako huo umezidi kunifumba na sio kunifumbulia.

Rashidi: Katika hilo una haki, lakini nitakamilisha, tulikubaliana katika mjadala wetu uliopita kuwa Mungu ana sifa nzuri, na miongoni mwa sifa hizi ni sifa zenye kupendwa; Mungu mtukufu na viumbe wake wanazipenda, na katika sifa hizi ni kuwa yeye Mungu mtukuka: Muumba ni Muweza, Mfalme na mwenye kupenda sifa hizi anahitaji kuzitekeleza.

www.path-2-happiness.com

Na kwa sababu Allah Ta'ala ni muweza, hakimzuii chochote katika kutekeleza matakwa yake, hivyo basi Mungu ameumba viumbe ili wawe ni athari katika athari za sifa zake zenye kupendwa; na kwa sababu yeye ni Muumba basi hupenda kuumba, na kwa sababu ananeemesha hupenda kuneemesha, na kwa sababu yeye ni Rahimu hupenda kurehemu, na kwa kuwa yeye ni Muweza basi hakuna kitu kinachoweza kumzuia katika kutekeleza kila ayatakayo.

Maiko: Kama ni hivyo: Ni nini sehemu yetu katika fomula hii?!

Rashidi: Nafasi yetu ni kuwa Mungu ametuumba ili tumtambue na tumtakase na mapungufu na aibu, na akatupa neema, sio tustarehe nazo tu, bali vile vile tumshukuru yeye juu ya hizo wala tusizipoteze, kwani yeye ni Mtukufu, anapenda kushukuriwa na kuhimidiwa, na hili linapelekea kumnyenyekea (ibada yake) peke yake, kwani yeye pekee ni mwenye kuneemesha na Muumba anayestahiki kufanyiwa ibada.

Rajev: Maneno yako yanaelea katika nukta mbili; Ya Kwanza: Je, maana yake abaki mmoja wetu hekaluni ili afanikishe unachokisema kuhusu maana ya uja kwa Mungu?

Rashidi: Hapana, hapana, sijakusudia ulichokitaja katika uchunguzi wako, maana hii ya uja kwa Mungu ni maana finyu haikubaliwi na Uislamu ambayo ndio dini yangu, uja na Ibada kwa Mungu kwa maana yake pana inahusisha maisha yote ya mwanadamu, pamoja na kuendeleza dunia yake na kusimamisha ustaarabu wa mwanadamu na utu wake.

Maiko: Lakini sisi tunaimarisha (tunaendeleza) ardhi na tunasimamisha ustaarabu wetu bila kurejea kwenye dini.

Rashidi: Ndio maana tunaona mashaka makubwa ya wazi ayapatayo mwanadamu ni matokeo ya ustaarabu huu. Kama vile kuenea babaiko, hofu, woga na wasiwasi. Watu kujiua, mparaganyiko wa kijamii, mwanadamu kumdhulumu mwanadamu mwenzake, haswa anapojua hakuna wa kumchunga… na hilo linakuwa ikiwa watu wameelekea zaidi katika u-mamboleo (usasa), yaani mifumo ambayo inajali vitu na uvumbuzi na kuviendeleza, wakati ambapo ubinadamu unapotea; ikiwa tutazingatia suala hili la utu basi hapana budi kuchunguza yanayojenga ubinadamu na kilicho muhimu zaidi ni ile roho yake, na tunapounganisha ustaarabu na kuhusisha na nishati za mwanadamu kwa Muumba wa mwanadamu basi pande zake zote zitashikamana na utu wake, bali pamoja na ubinadamu wote, pamoja na ulimwengu wote, kwa uchache ni kuwa ambaye amemuumba mwanadamu huyu na ulimwengu huu ni mjuzi zaidi kwa yanayomfaa na yasiyomfaa.

Maiko: Je, ina maana kuwa Mhandisi Rajev kwa mfano ili awe mfanisi wa kazi yake ni vizuri arejee kwenye vitabu vya dini? Hilo litawezaje kuwa? Kisha tukikubaliana na maneno yako vipi tutaweza kufikia yale ayatakayo Mungu ili maisha yetu yanyooke?

Rashidi: Maneno yangu hayana maana kuwa dini isiingilie masuala ya kitaalamu katika sayansi, lakini inaweka kanuni na misingi ya kimaadili ya matendo na ni sharti zetu katika maisha yetu, na mfumo au utaratibu ambao tutaufuata katika maisha yetu, kama vile utaratibu wa mahusiano yetu na wengine katika wanadamu, pamoja na jamii yake, kati ya jamii zingine, ongezea kumfahamisha mwanadamu huyu nafasi yake hapa duniani, na uhusiano wake na Mola wake.

Nitawapigieni mifano miwili ili kuwawekea wazi: Mungu Mtukufu ametuumba na ameumba ardhi na yaliyo juu yake, na akatuoteshea chakula katika ardhi kutokana na maji aliyoyateremsha kutoka mbinguni, kisha akatuoteshea dawa na sumu zenye kuuwa na akatuzawadia uwezo

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

katika akili zetu kuvitumia ili tujue yenye kudhuru na yenye kulisha, na akatupa uwezo kutumia uzoefu wetu katika kugundua mimea hii na kunufaika nayo na kutoa madawa ndani yake, kisha akatuwekea kanuni katika dini yake: “Kila chenye kutudhuru na kuwadhuru wengine ni haramu kwetu kufanya.’

Na mfano mwingine: Watu wote wanakubaliana na uzuri wa uadilifu na ubaya wa udhalimu, lakini tunapoingia kwa kina na kuangalia uadilifu huu, tunaona tofauti kubwa; kuwa akili zimetofautiana kwa malengo yake na makusudio yake, ongezea kugongana kwa maslahi katika kila kundi, hivyo basi: Sisi tuna haja ya kuwa chanzo cha uadilifu huu iwe ni kwa anayemiliki utawala wa juu kwa wanadamu wote, ambapo watu wote watakuwa sawa mbele yake, na upendeleo wa kundi au kuelemea au kunufaisha sehemu fulani utaondoka.

Ama namna ya kufikia katika maarifa ambayo Mungu anatutaka tuwe nayo; hilo limeunganishwa vile vile na sifa za Mungu Mtukuka, kwani Mungu Mtukuka ni mfalme na mwenye hekima… hili linaunganishwa na yale tuliyoyataja hapo kabla kwenye mjadala wetu kuwa Mungu ameumba ulimwengu huu kwa hekima na wala hakuumba kwa mchezo…Je, inafaa kuwa ni katika hekima kuwa na shirika ukaasisi na kujenga majengo yake na wafanyakazi wake kufanya kazi na kuzalisha na kutangaza bidhaa zake bila ya kuwepo utaratibu wa kazi na uongozi, na kanuni zinazowaongoza!!!

Maiko: Bila shaka hapana.

Rashidi: Basi unafikiriaje kuhusu ulimwengu huu na viumbe hawa … ndio maana Mungu akateremsha vitabu vyake ambavyo ni mikataba, ili iwe ni muongozo wa watu na kiongozi chao katika manufaa yao ya kidini na dunia, na hilo ni kupitia mabalozi baina yake na waja wake, ambao

ni Mitume yake walio miongoni mwa waja wa Mola. Akawabainishia maamrisho yake na makatazo yake ili wawafundishe watu kuhusu Mungu wao na kuwaelekeza kwenye alama za uadilifu na madhara ya dhuluma na udhalimu, kadhalika wawabainishie watu kinacho wanufaisha na kinacho wadhuru katika dunia na akhera yao.

Kwa hiyo mwanadamu ni mwenye haja kubwa ya ujumbe kwani yupo baina ya harakati mbili: Harakati moja inamvuta katika yanayomnufaisha, na harakati nyingine inamkinga na yenye kumdhuru, na Ujumbe huu ni kama mwangaza ambao utambainishia yenye kumnufaisha na yenye kumdhuru, nayo ni nuru ya Mungu katika ardhi yake na uadilifu wake baina ya waja wake.

Lengo la ujumbe sio kutofautisha kwa hisia kati ya chenye kunufaisha na chenye kudhuru, kwani hilo hutokea kwa wanyama wasio na akili; punda kwa mfano hutofautisha kati ya shairi na udongo. Kinachokusudiwa ni kutofautisha kati ya matendo ambayo humdhuru mtendaji katika dunia yake na akhera yake, na matendo ambayo yatamfaa hapa duniani na kesho akhera na kama sio ujumbe basi akili isingeongoka katika kujua yatakayomfaa na kumdhuru katika maisha yake.

Rajev: Ama nukta ya pili ni: Tunawaona watu wanatofautiana katika mtazamo wao kuhusu Mungu na namna ya kumnyenyekea na kumuabudu, sasa iweje wawe sawa sawa katika kustarehe kwa neema zake?!

Rashidi: Hii inatokana na hekima ya mitihani na uchaguzi ili kudhihirisha mtazamo wao kuhusu Mola wao, lakini kamwe hawawezi kuwa sawa katika malipo na marejeo yao, na malipo haya yatakuwa ndio msingi wa ujumbe wa Mitume ambao upo kwa sura ya sheria na mkataba ambao mtu anatakiwa kuurejea.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Maiko: Naongezea nukta ya tatu, nayo ni: Vipi watu wote wanaweza kufaidika na neema ya Mungu, wakati katika watu hao yupo muongo, tapeli na dhalimu, na wengineo wanaweza kukwepa adhabu zilizowekwa na jamii na sheria haiwezi kumfanya kitu?!

Rashidi: Hili pia ni katika hekima ya mtihani na majaribio, lakini watu hao wakikwepa adhabu na jamii kutekeleza adhabu juu yao, basi bila ya shaka hawataweza kukwepa uadilifu wa Mungu juu yao, na hili ni katika hukumu ya ufufuo na hesabu baada ya kifo katika Siku ya Kiama na malipo, yaani malipo kwa matendo mazuri na mabaya kwa Mungu, kwake binafsi na kwa watu wengine, katika siku hii yatakuwa malipo na hukumu ya haki kwa watesi.

Hata hivyo, hapana budi kuwepo kwa rejea watu wakihukumiana juu ya msingi huo na wawe wanalifahamu hilo na wanaweza kurejea…. hapa vile vile inakuja zamu ya ujumbe wa Mitume wa Mungu ambao watawaeleza watu msingi ambao watahesabiwa nao na ambao watawafahamisha ni nini kitakachotokea kwao kwa kwenda kinyume na msingi huu, na ambao watawajulisha watu maisha yajayo ya akhera yatakayo kuwa katika neema na adhabu chungu iumizayo, na nini kitakachotokea siku hiyo.

Rajev: Bwana Rashidi, je, unakumbuka kuwa tulizungumzia umuhimu wa mjadala kuhusu sifa au vigezo vya dini ya haki?

Rashidi: Sawa nakumbuka hilo.

Rajev: Nadhani umeshafikia muda wa kufungua faili hili.

Maiko: Ni kweli Rajev, nadhani tutenge mjadala wetu ujao kuhusu maudhui hayo.

Sifa ya Dini ya Haki



www.path-2-happiness.com

Sifa ya Dini ya Haki

Rashidi aliwapokea marafiki zake mbele ya mlango wa makumbusho ya Louvre kulingana na ahadi yao, aliwakaribisha wafanye ziara katika makumbusho yale na kusema:

Niliainisha sehemu hii na kuwaalika ili tufanye ziara katika makumbusho haya ili turejee na tukumbuke sehemu ya historia ya wanadamu kabla ya mazungumzo yetu ya mada ya leo hii…mnaonaje fikra hii?! Tunaweza kuachana nayo kama haifai.

Maiko: Mambo yako ya ajabu ewe Rashidi….unachukua rai yetu baada ya kutufikisha hapa, ilikuwa vizuri utushauri kabla hatujafika hapa… hata hivyo mimi sina neno…. Unaonaje Rajev?

Rajev: Nami sina kizuizi vile vile, lakini ni bora ziara yenyewe iwe ya harakaharaka kama tutataka tuzungumze maudhui yetu kama tulivyoafikiana na makumbusho ya Louvre ni kubwa na kuimaliza itachukua muda wetu mwingi na nguvu zetu.

Rashidi: Mimi naomba samahani kwa kosa langu hili, nilitaka kufanya jambo la kushtukiza kwenu, hata hivyo nilikosea.

Maiko**:** Usijali, basi na tufanye haraka kwani urefu wa kumbi zote ni kiasi cha 60,600 mita mraba na kuna zaidi ya vipande milioni moja.

Rashidi: Sikukusudia katika ziara yetu kuvumbua kumbukumbu za louvre, bali nilikuwa nataka watupe baadhi ya taarifa kuhusu maudhui ambayo tutaijadili… nadhani umuhimu wetu utahusika kwenye teknolojia ya athari ya staarabu za kale, na zote zipo katika mezanini na ghorofa ya kwanza.

Baada ya masaa mawili marafiki wale watatu waliondoka katika makumbusho yale, walionekana dhahiri kuwa na uchovu kutokana na matembezi yao.

Rashidi: Tunaweza kupumzika na kula chakula cha mchana katika hoteli iliyo karibu na hapa ambayo nimeijua kupitia intaneti.

Walipokuwa wakienda, Rashidi alianza mazungumzo yake.

Je; hamkuona kuwa mengi tuliyoona katika teknolojia ya staarabu mbali mbali yana mahusiano kwa njia moja au nyingine na dini, je, hiyo sio uthibitisho kuhusu nafasi ya dini katika maisha ya mwanadamu bila kujali ni wakati gani au sehemu gani aliyoishi?!

Rajev: Unachosema kinakubalika takriban na wanazuoni wa anthropolojia, wao wanasema kuhusu utafiti wao katika historia ya mwanadamu na athari zake walihitimisha ya kuwa kunaweza kuwepo ustaarabu bila ya kuwepo viwanda au kuwepo majumba na ustaarabu bila ya kuwepo sayansi wala falsafa, lakini wao hawakupata ustaarabu bila ya nyumba za ibada.

Maiko: Ukweli ni kuwa mwenye akili yoyote anasema kuwa dini si shari, bali hayo ni mambo ya msingi yanayounda ustaarabu kwa uwepo wa mwanadamu, lakini tatizo lililopo hapa ni kuwa kila mfuasi wa dini anaamini kuwa haki ipo kwenye dini yake na si nyingine, na huwalingania watu kwa hilo, na kila mwenye itikadi anawalingania wengine wafuate itikadi yao, na kumtukuza kiongozi wao, kila mwenye mila anaamini kuwa mila yake ni sahihi zaidi, hapo mtu anakuwa kwenye mtanziko; Je, dini ya kweli ni Uyahudi, au Ukristo au Ubudha au Uislamu? Ni njia ipi ya kujua dini ipi ni kweli au tuseme kuwa zote zipo katika haki maadamu kila mmoja katika dini yake anashibisha haja yake ya kufuata dini?! Hili ni babaiko, au sivyo?!

Rashidi: Ndio, ni mwenye babaiko lakini inawezekana kwa kiasi cha mazingatio na busara kuondoka katika babaiko lile…..Sasa hivi na sisi tukiwa na njaa hatutoshelezwi wala haturidhishwi kula chakula chochote kiwe chakula hicho kinafaa kuliwa na mwanadamu au mnyama, sisi haturidhiki kujaza matumbo yetu kwa chakula chochote kwa ajili ya kushibisha njaa yetu, sembuse kushibisha silika zetu za kiroho?…bila shaka hapana budi kuchagua chakula kinachofaa na kilicho sahihi.

Haiyumkiniki wakawa wote wapo katika haki, kwani haki ni moja wala haiwi zaidi ya moja, na haiyumkiniki dini zote hizi na mila zote hizi za wanadamu zikawa zinatoka kwa Mungu, na zote zikawa za haki na zikiwa nyingi (wakati ambapo haki ni moja) swali litakalobakia na kujitokeza; ni ipi ya haki? Hivyo basi hapana budi kuwepo na vidhibiti na vigezo ambazo kwazo tutaweza kujua dini ya haki, na dini ya batili. Tukipata vigezo hivi vinalandana na dini basi tutajua kuwa ni ya haki, na zikichanganyika vigezo hivi au kimoja wapo katika dini, tutajua kuwa ni vya batili.

Rajev: Katika mazungumzo yako sasa hivi umeweka kigezo cha

www.path-2-happiness.com

kwanza, nacho ni kuwa dini hii itoke kwa Mungu. Je, hapana budi dini iwe ni kutoka mbinguni? Ardhini kuna dini mbali mbali na si za mbinguni ambazo hufuatwa na mamilioni ya watu, kama vile ubudha, Uhindu, Ukonfusia na nyinginezo.

Rashidi: Hili ni la kawaida kabisa, kwani msingi wa dini yoyote ni kumuabudu Mungu au Miungu!! Ikiwa kweli tunakiri kuwa Mola peke yake ndiye aliyeumba ulimwengu na watu, na ndie ambae amewadhalilishia yaliyomo ardhini na akawaruzuku neema; hivyo hapana budi tukiri kuwa yeye peke yake ndie mwenye kustahiki kuabudiwa na kuwa yeye pekee ndie anayeabudiwa wala hakuna mshirika pamoja nae; Basi vipi aumbe na kuruzuku peke yake, na kushukuriwa na kuabudiwa asiyekuwa yeye?! Nyongeza ya hayo: Hapana budi dini sahihi ilinganie ibada ya Mungu mmoja, na ithibitishe sifa ya Uungu wa haki, na kutukuza Mitume yake na kuiheshimu.

Tuliafikiana katika kikao chetu kilichopita kuwa sifa za Mungu wa haki na haja ya wanadamu inapelekea kuwepo kwa dalili na uthibitisho ambao utamungoza mtu na kuratibu maisha yao na kuwafikisha kwenye furaha, na huu sio uthibitisho isipokuwa ni dini ambayo anairidhia mwenye kujua aliyeumba.

Kadhalika tulikubaliana pia; ni jambo la msingi kuwepo kwa siku ya mwisho ambayo binadamu watahesabiwa kwa matendo yao, na ndani yake dhulma zitarudishwa. Kwa hiyo Allah aliyetakasika pekee ndie ambae atawahesabu viumbe wake Siku ya Kiama, hivyo hapana budi hesabu zao kulingana na dini aliowateremshia, kwa kujengea juu ya hilo: Dini yoyote ambayo atakuja nayo mtu na kujinasibisha kwenye nafsi yake basi dini hiyo ni batili.

Napenda kuashiria hapa kuwa wafuasi wengi wa dini pindi unapowauliza uthibitisho wa itikadi zao, hutoa hoja kuwa waliwakuta babu zao katika dini na njia hii, kisha baada ya hao wanataja hekaya mbali mbali na habari zisizo sahihi, na wanategemea vitabu vilivyorithiwa, haijulikani aliyesoma wala aliyeandika na wala haijulikani ni lugha gani iliyoandikwa kwa mara ya kwanza, wala katika nchi yoyote vilipokuwepo; ni mchanganyiko uliokusanywa ikawa vikubwa kurithiwa na vizazi bila ya kuhakikishwa kitaaluma; na hili ndilo juu yetu kulikwepa, tokea hapa itakuwa wazi kuwa sifa muhimu ya dini ya kweli: ni kuthibitika kwa kunasibishwa na

chanzo chake, na usahihi hoja za Mtume anayewasilisha na kufikisha dini kutoka kwa Allah.

Rajev: Si neno, hivyo basi yatupasa tuondoke katika jumla ya misingi ambayo tumeafikiana, sawa katika hoja za kuthibitisha dalili: akili, elimu, maumbile, au katika hakika ambazo tumeafikiana, hapo kabla, kama vile kuwepo na Mungu na sifa za Mungu wa kweli, na haja ya watu na ujumbe wa kitume.

Maiko: Tukiafikiana katika hilo, itakuwa sifa ifuatayo: baada ya dini kuwa ya Allah, na aabudiwe Yeye Peke Yake: dini iwe pamoja na elimu wala isipingane nayo, na hivyo kuafikiana na akili sahihi. Hivyo tunaposema kuwa dini sahihi ni dini ya Allah, na akili sahihi ni umbile la Allah, hivyo basi ni muhali dini ya Allah kupingana na maumbile yake.

Rashidi: Naafikiana katika hilo, pamoja na kukuhakikishia mambo mawili:

Kwanza: Imetangulia kuwa tulichokikubali kuwa kuna tofauti kati ya kinacholazimishwa na akili kwa kutotokea au kuthibitishwa kwake, na kinachokuwa kigumu akili kusawirisha, kuna mambo katika dini na ni magumu akili kusawirisha au kujikinaisha kwa namna zake, hiyo ni duara la ghaibu… Mathalani: Kuwepo kwa Malaika na Mashetani, na namna ya Wahyi kwa Mtume mwanadamu, na maelezo ya Siku ya Kiama, lakini mambo haya yanatofautiana wakati ambapo akili hukataa kutokea kwake.

Kwa mfano: Kabla ya miaka mia moja ilikuwa ni vigumu mtu kuamini kama mtu anaweza kupanda au kutuma chombo angani (mwezini), au anaweza kumsikia na kumuona mtu mwingine aliye umbali wa maelfu ya Kilometa, lakini ndani ya akili hakukuwa na kinachosema haiyumkiniki hilo lenye ugumu kukubaliwa, hata hivyo tukisema kuwa mwanadamu mwenyewe ndani ya nafsi yake ana sehemu mbili tofauti wakati huo huo, au ya kuwa 1 + 1 + 1 = 1, hiyo basi akili itahukumu kwa kutowezekana hilo.

Pili: Kulingana na nukta iliyotangulia, baadhi ya vipengele vya dini haviwezi kudhihiri kwetu sababu zake kiakili (hekima zake) pamoja na kuwa havipingani na akili zetu, na hapa hapana budi tukubali madamu imani yetu imesimama juu ya msingi uliosalimika kwa hoja, kwani wewe lau kwa akili yako ukadiriki mtu mwenye kuaminika kwa asilimia mia

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

moja, wala hamna shaka yoyote katika uaminifu wako kwake, na mtu yule akataka kupima uaminifu wake kwako kwa kukuambia: “Nitilie sahihi yako kwenye karatasi hii nyeupe…..” Bila shaka utasaini bila ya kuuliza kwanini, ama ikiwa uaminifu wenyewe sio ukamilifu, utamuuliza lengo la karatasi hii, na mfano huo huo; imani au akida ni kuijenga uaminifu kwa Mungu kwa njia ya akili na fikra na vipengele vya dini, ni dalili ambayo utaitanguliza katika uaminifu wako kwa Mungu.

Maiko: Hivyo basi, miongoni mwa sifa ya dini ya haki, isigongane yenyewe kwa yenyewe, isiamrishe jambo kisha ikatengua kwa amri nyingine, wala isiharamishe jambo kisha ikahalalisha mfano wake bila ya sababu, wala isiharamishe jambo kisha inahalalisha kwa kundi maalumu na kuliharamisha kwa kundi lingine.

Rajev: Na tukisema kuwa dini hii ni dalili kwa mwanadamu kwa anachokitaka Mungu wao kutoka kwao, basi hapana budi dini hii iwe na yafuatayo: uongofu katika njia ya kumuabudu Mungu na dalili ya mwanadamu, kwa anayoyataka Mungu kutoka kwake, na utaratibu au mfumo ambao hapana budi mwanadamu kuufuata, na iweze kujibu maswali yote makubwa ya maisha, imjulishe alipotokea na anaelekea wapi? Na impe utulivu na amani na iwe inakwenda pamoja na maumbile ya asili aliyoumbiwa nayo mwanadamu.

Maiko: Ninaona kuwa ni muhimu dini ilinganie tabia na matendo mema, na ikataze maovu, na iwe rehema kwa waja kutokana na kujidhulumu wenyewe na kudhulumiana wao kwa wao, iwe dhuluma hiyo ni kunyang’anya haki au kuharibu kheri au wakubwa kuwadhalilisha wadogo.

Rashidi: Kuna sharti muhimu ambalo tumelisahau, nalo ni kuwa dini hiyo ikusanye sifa zote hizi, wala isikosekane sifa yoyote miongoni mwa hizo.

Maiko: Ninakutaka ewe Rashidi utuhadithie kuhusu dini yako kwa urefu, nimeona kuwa ninachokijua kuhusu dini yako ni kidogo, na mengine yamepotoshwa.

Rashidi: Nina kuahidi hilo katika kikao kijacho.

Mwanadamu Mtukufu Zaidi

www.path-2-happiness.com

Mwanadamu Mtukufu Zaidi

Akiwa katika hali ya uchangamfu Rashidi aliwakabili rafiki zake na kitabu huku akiwa amebeba laptop yake…. Alipowakaribia aliwasalimu haraka haraka wala hakusubiri majibu yao kisha akawaanza kwa kusema:

Leo hii nitaanza kwa kuitikia wito na hamu ya rafiki yangu Maiko…nipo tayari kuwaelezea misingi muhimu ya Uislamu, hawatofautiani wawili kwa misingi hii nayo ni: Imani kwa Mtume wa Uislamu….Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) nimewaletea kitabu cha mwana fikra wa Kimagharibi ambaye anamzungumzia Muhammad..sikilizeni anachosema …

Maiko: Pole pole rafiki yangu Rashidi…Nilikuwa nadhani kuwa kitu muhimu zaidi hususan katika Uislamu ni taswira yake kuhusu Mungu.

Rashidi: Hili ni kweli katika ujumla wake…hata hivyo umepetuka mpaka kwa sababu kadhaa, muhimu zaidi katika sababu hizo ni:

Uislamu kwa sifa yake ni Ujumbe wa Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) mtu asidai wala asidhanie kuwa taswira ya Uungu ni taswira iliyozuliwa na Mtume wa Uislamu, bali ni dini ya manabii na mitume tokea Adam hadi Masihi hadi kufika kwa Mtume Muhammad (amani kwao wote), bali ni asili ya dini ya wanadamu wote…na kilichotokea ni kuwa wanadamu walipotoka dhidi ya dini hii na wakapotosha taswira hii, ukaja Uislamu na kurejesha usahihi wa imani kwa Mwenyezi Mungu na kuwalingania watu wote kurejea katika upekee (tawhidi) wa Allah Mtukufu na kutomshirikisha kwenye ibada yake…Hivyo basi kumuamini Mwenyezi Mungu na kumpwekesha katika Uislamu ni mfumo wa mnyororo uliyoendelea kupitia historia tokea alipoumbwa mwanadamu wala haiishii kwa kuondoka dunia…ni dini iliyopatikana kabla ya kuzaliwa kwa Mtume wa Uislamu.

Jambo la pili: Nilidhani kuwa tumeafikiana kwa hilo katika vikao vyetu vilivyopita, kwamba inatosheleza kuvuka nukta hii.

Rajev: Je unakusudia kuwa katika Uislamu sifa ya mungu wa kweli ipo?

Rashidi: Naam, hii ni sahihi kabisa!

Rajev: Hivyo basi, ni vizuri ututajie kwa ufupi taswira ya Uislamu kuhusu Uungu kabla ya kuhamia kwenye yale uliokuwa unataka kutuelezea.

Rashidi: Vizuri…katika Uislamu mungu ni mmoja aliyemuumba mwanadamu na aliyeumba ulimwengu, hafanani na chochote katika ulimwengu, yeye ndie aliyeweka kanuni za kimaumbile na akaweka kila kitu kwa kipimo chake na kanuni zake, yeye ni mtukufu wa kila kitu na mkubwa wa kila kitu, na yuko juu ya kila kitu.

Hafanani na yeyote katika dhati yake, sifa zake na matendo yake, ana ukamilifu wote wala hazukiwi na upungufu katika sura yeyote ile, yeye ni mtukufu hakuzaa wala hakuzaliwa, wala hafanani na yeyote na hana mshirika na ni pekee ambaye anahuisha na anafisha.

Huyu ni Mola ni Mungu Peke Yake ambae hapaswi kuabudiwa asiyekuwa yeye, hana mshirika katika ufalme wake wala hana msaidizi, wala waziri, wala mshauri anayeabudiwa pamoja nae, wala hana wa kati aliye karibu nae zaidi, na anayeweza kufanya maombezi bila ya idhini yake, ibada ni halisi kwake peke yake tu kwa mambo yake yote.

Maiko: Kitabu ulichokuja nacho kinazungumzia nini?

Rashidi: Kinazungumzia Watukufu katika historia ya mwanadamu, cha mwandishi Dr. Michael Hart, nae ni mwanazuoni wa nyota, sayari na mahesabu ambaye anafanya kazi katika taasisi ya anga ya Marekani.

Maiko: Anahusika vipi katika masomo ya historia?!

Rashidi: Masomo na tafiti za historia huchukuliwa kuwa ni starehe na hamu za watu leo hii duniani, nae ameona kuwa miongoni mwa makumi ya maelfu ya mamilioni ya watu, vitabu vya historia havikumtaja isipokuwa watu ishirini elfu tu, hivyo akaweka vigezo na misingi kadhaa kwa kumchagua mbora wao zaidi katika watu wote hao, misingi hiyo muhimu ilikuwa:- Awe ni mtu wa kweli aliyeishi na isiwe ni ngano tu za kusimuliwa au mtu asiyefahamika, awe na athari kubwa, ni sawa sawa iwe athari hii ni nzuri au mbaya, na athari hii iwe ni ya kilimwengu na ienee katika historia ya wanadamu…nazo ni misingi mizuri kwa maudhui yetu.

Rajev: Ni mtu gani huyo mtukufu wa maoni ya mwandishi huyu?!

Rashidi: Mwandishi huyu amemchagua Muhammad, Mtume wa

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Waislamu kuwa juu kileleni kati ya watu mia moja aliowachagua, na uchaguzi wake huu sababu zake alizobainisha ni:-

Kisha Rashid akafungua kitabu na kuanza kusoma:-

“Nimemchagua Muhammad katika orodha hii na watu wengi watashangazwa na chaguo hili, na wana haki katika hilo, hata hivyo Muhammad ndie mwanadamu pekee katika historia aliyefanikiwa mafanikio makubwa zaidi kwa viwango vyote katika dini na katika dunia.

Yeye aliita watu katika Uislamu na akausambaza kama dini kubwa zaidi, na akawa ndio kiongozi wa kisiasa, kijeshi na kidini…na baada ya karne kumi na ya kifo chake, hiyo athari ya Muhammad ilibaki kuwa yenye nguvu mpya.”

“……na inaelekea ni kitu kigeni Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) kuwa kileleni pamoja na kuwa katika orodha ile idadi ya Wakristo likuwa kubwa sana kulinganisha na idadi ya Waislamu na huenda ilionekana kuwa ni jambo geni kuwa Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) kuwa namba moja katika orodha hii wakati ambapo Issa (‘Alayhi salaam) ni namba tatu na Musa ni wa kumi na sita.

Hata hivyo hilo lina sababu zake: Miongoni mwazo ni: Dini ya Muhammad ilikuwa ni kubwa na ya hatari zaidi katika kueneza Uislamu na kusimamisha misingi ya sheria yake kuliko ilivyo kwa Issa katika Ukristo. Pamoja na kuwa Issa ndie muhusika wa misingi ya maadili katika Ukristo, isipokuwa Paulo ndie ambae amesimamisha misingi ya sheria ya Ukristo, nae vile vile ndie muhusika wa maandishi mengi yaliyokuja katika Agano Jipya.

Ama Mtume Muhammad yeye ni muhusika namba moja na ni pekee aliyeweka misingi ya Uislamu, sheria na tabia za kijamii na kimaadili na misingi ya muamala kati ya watu katika maisha yao ya kidini na ya kidunia. Kama ambavyo Qur’an imeteremka kwake peke yake, na katika Qur’an Waislamu wanapata wanachohitaji katika dunia yao na akhera yao. Je, mnashangaa maneno haya?!

Rajev: Maneno yanayostahiki kutulia ndani yake, lakini niruhusu niseme: Mwandishi huyu hahusiki na tafiti za wanadamu.

Rashidi: Hata kama hahusiki katika tafiti za maisha ya watu lakini maneno yake yanakinaisha na yamejengwa katika misingi ya uwazi, wala hamna utata wowote katika kuegemea na kumpendelea Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam), Yeye ni Myahudi, na kama utahitaji ushahidi wa watu wengine niache nikuelezee baadhi yake…

Kisha Rashidi akatoa laptop yake akaanza kusoma baadhi ya faili alizo nazo na kusema:

Angalia bwana:

Anasema mshairi wa Kifaransa La Martine: “Ni mtu gani aliyediriki utukufu wa mwanadamu kama alivyodiriki Muhammad? ni mwanadamu yupi ambae amefikia ukamilifu kama alivyofikia Muhammad? Mtume Muhammad alivunja itikadi potofu ambazo zilifanywa watu kiunganishi baina ya Muumba na Muumbwa.”

Na mshairi wa Ujerumani wa kwanza, Goethe, anasema: “Nimechunguza katika historia kuhusu vigezo vya juu vya mwanadamu, nikavipata kwa Nabii Muarabu, Muhammad.

Mwanafasihi na mwanafalsa wa Kirusi na ulimwenguni, Testow: “Mimi ni mmoja katika waliofurahishwa na Muhammad aliyechaguliwa na Mungu mmoja ili awe mwisho wa ujumbe kutoka kwake, na yeye vile vile awe ni nabii wa mwisho.”

Ama mwandishi na mwanafikra wa Ki-Ireland, mashuhuri aliyekataa zawadi ya Nobel katika fasihi, George Bernard Shaw anasema: “Nimesoma maisha ya Mtume wa Uislamu vizuri mara nyingi, na sikupata ndani yake isipokuwa maadili kama yanavyofaa kuwa ni kwa kiasi gani nimetamani Uislamu kuwa ndio njia ya ulimwengu. Nimemsoma Muhammad nikamzingatia kuwa ni mtu wa ajabu, nikamuona kuwa, yuko mbali na ugomvi wa Masihi (‘Alayhi salaam), bali alipasa kuitwa muokozi wa wanadamu.

Maiko: Mazungumzo haya yanazunguka katika utukufu wa Muhammad, lakini kitu gani kinachothibitisha kuwa Muhammad ni Mtume wa Mungu?

Rashidi: Sikiliza ewe rafiki yangu anachosema mwanazuoni wa dini wa uswisi, Dr. Hanz Kin: “Muhammad ni nabii wa kweli kwa maana ya neno, wala hatuwezi kukanusha kuwa Muhammad ndie kiongozi na mshauri katika njia ya uokozi.”

Kuna dalili nyingi zenye kuthibitisha kuwa Muhammad ni Mtume wa kweli wa Allah.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Maiko: Ikiwa umeshatayarisha basi tuelezee, au kwa uchache wake.

Rashidi akiendelea kufungua baadhi ya mafaili kwenye kompyuta yake, kisha akasema:-

Katika uthibitisho wa ukweli wa Mtume: Ni vitabu vya mbinguni kunatabiri; katika kumbukumbu la Torati, Mungu anamwambia Musa: 18:15-30: “BWANA, Mungu wako, atakuondoshea nabii miongoni mwa ndugu zake kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye. Na kilicho maarufu ni kwamba ndugu wa Bani Israil ni Bani Ismail (yaani Waarabu), kama ambavyo mfanano kati ya Musa na Muhammad ni mwingi kuliko Mtume mwingine yeyote, na ibara “Nitamuwekea maneno yangu mdomoni mwake.” Ni ishara ya kutojua kusoma yaliyoandikwa kwa Mtume wa Uislamu.

Katika Injili ya Yohana Mtakatifu 14:15 “Masihi anawaambia wanafunzi wake: “Mimi naondoka, atakuja PERIQLYTOS, roho ya kweli; hazungumzi ya kwake mwenyewe, lakini yeye kama isemavyo, naye ananishuhudia mimi na nyie mnashuhudia; kwani mlikuwa nami.” asili ya neno PERIQLYTOS ni la kiyunani lenye maana himidi lenye maana la Ahmad au Al-Hamid au mwenye kushukuru sana nalo ni jina la kiarabu la Mtume Muhammad”

Katika dalili zingine vile vile: kumjulisha yasiyoonekana (Ghaibu), bali hata vipengele vyake vya ndani, na kumjulisha kuhusu mwisho katika mwanzo, na muujiza wa kisayansi wa ujumbe wake, na hukumu za kisheria.

Maiko: wapi? Yako wapi yote hayo?! Tupe mifano.

Rashidi: Yapo mengi kwenye Qur’an, kitabu alichoteremshiwa Muhammad, na ndio muujiza wake mkubwa.

Rajev: Kama ni hivyo, ni muhimu kuijua Qur’an hii kutokana nayo tutajua ukweli wa Mtume wenu, na tutaweza kujua misingi ya dini hii.

Rashidi: Ni kweli, na hili ndilo ambalo nataka kulipendekeza kwenu kuwa tuakhirishe hili hadi kikao kijacho.

Maiko: Kabla ya kuondoka nataka kujua: Kitabu hicho nitakipata wapi?

Rashidi: Kitabu ninacho kwa muda mrefu, lakini nimeona chapa mpya iliyotolewa hivi karibuni katika duka la vitabu karibu na tulipofikia, tunaweza kutembelea duka hilo kabla ya kikao chetu kijacho….

Ujumbe wa Mwisho

www.path-2-happiness.com

Ujumbe wa Mwisho

Marafiki watatu walikutana mbele ya lango kuu la mafikio yao kama walivyokubaliana baina yao, Rashidi aliwaongoza katika lile duka alipoona kitabu, “watukufu mia moja….mbora wao ni Muhammad”, pembeni ya nguzo za magazeti alisimama Maiko alikuwa anaangalia orodha: Ghafla alimuita Rashidi.

Rashidi…..Aliangalia maudhui iliyomvutia….ni maudhui kuhusu mjadala wetu leo hii: “Tangazo la kupatikana muswada wa kale wa Qur’an katika moja ya maduka ya vitabu Israil.”

Rashidi: Unakusudia kuniuliza ni vipi muswada huu umefika katika duka la vitabu Israel? Habari hii nimeisoma jana katika moja ya mtandao (website) baadhi ya wachambuzi wanaonyesha na kuashiria kuwa muswada huu uliibiwa Iraq katika vita vya washirika.

Maiko: Hapana, hapana sikusudii hivyo, nakusudia uhusiano na Qur’an ya asili mliyonayo, na uhusiano wa usahihi wa kuthibitisha Qur’an, kwani habari yenyewe inasema kuwa muswada wenyewe umeandikwa yapata kabla ya miaka 1200, yaani miaka 200 tu baada ya kuandikwa nakala ya kwanza ya Qur-an, hiyo ni habari ya kustaajabisha.

Rashidi: Kwanza: Hii sio nakala ya kale zaidi iliyovumbuliwa hadi sasa; Warusi wanasema kuwa nakala ya zamani ya Qur’an ipo katika mikono yao, hilo limethibitishwa na mtafiti wa kirusi, Yufim Ridhwan ya kuwa, X-ray ya carbon aliyofanya Holland imethibitisha kuwa muswada wa Qur’an ambayo ipo kwenye mikono yao inarejea katika karne mbili; karne ya nane na ya tisa.

Wakati ambapo Wamisri wanasema kuwa, nakala ya kale zaidi ya Qur’an imehifadhiwa katika Mash-had Hussein, Cairo, na inakaribia umri wake tangu miaka1400, na ni moja ya misahafu sita ambayo ilitolewa kopi na Khalifa wa tatu ‘Uthman bin Affan (Radhi ya Allah iwe juu yake) ili kuhifadhi Qur’an isipotee.

Huko Yemen nao wanasema kuwa, wamepata nakala ya Qur’an ilihifadhiwa wakati wa kukarabati msikiti mkuu wa Sana’a mwaka 1972, inarejea katika zama za ukhalifa wa kwanza wa Abu Bakr As-Swidiq.

Yote yanaweza kuwa sahihi; kwani nakala ile iliandikwa na kutumwa katika miji mingi.

Pili: Kauli ya kuwa Qur’an kuwepo mikononi mwa Waislamu katika zama za Mtume hii ni kauli iliyotulia kwa wanazuoni wa dini, na inaungwa mkono na wastashirikina, hata hivyo hawakubali kuwa imeteremshwa na Mwenyezi Mungu, wakati ambapo kitabu kitakatifu kwa agano zote mbili hakijathibitishwa asili yake.

Anasema Mustashriki mfafanuzi wa elimu ya Sosiolojia, Ernest Renan: “Qur’an haijapitiwa na upotofu au kubadilishwa.”

Anasema Mmarekani, Dr. Mike Hart, mwandishi wa kitabu ambacho tumekuja kukinunua sasa hivi: “Hakuna katika historia nzima ya ujumbe wa Mitume kitabu kilichobakia kwa herufi zake kamili bila ya kubadilishwa isipokuwa Qur’an ambayo imenukuliwa na Muhammad.” Ama mshairi wa Kijerumani Goethe yeye amefikia kusema: “Qur’an ni kitabu cha vitabu, nami naamini haya kama vile wanavyoamini Waislamu.” Bali alitangaza hadharani alipofikia umri wa miaka sabini, kuwa anaazimia kusherehekea kwa unyenyekevu usiku ule mtukufu ambao Qur’an ilianza kushuka kwa Nabii Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam).

Rajev: Na hii ndio maudhui yetu ya leo; ni kitu gani kinachothibitisha kweli kuwa Qur’an ni Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na ya kuwa Uislamu ni dini ya Mwenyezi Mungu iliyoteremka kutoka mbinguni?

Rashidi: Sio kuwa tu ni dini ya Mwenyezi Mungu iliyoshuka, bali dini pekee iliyo sahihi hivi sasa.

Maiko: Hebu tusogee pembeni; ili tusiwakere wenye kuja kutembelea maktaba hii kwa sauti zetu.

Rajev: (Akimwambia Rashidi wakiwa wanaelekea pembeni wakazungumze): Iwe kama usemavyo, lakini kipi kinachothibitisha maneno yako?!

Rashidi: Nitawathibitishia, kwa kadiri muda utakavyoruhusu, kwa hakika Qur’an ni maneno ya Mwenyezi Mungu na sio maneno ya Muhammad, na nitakubainishieni baadhi ya miujiza yake ambayo inadhihirisha elimu pana iliyokusanya inayovuka mipaka ya mwanadamu.

Maiko: Tuambie yenye kutukinaisha na tulichoafikiana, tuambie kuhusu elimu na akili.

Rashidi: Wenye kufuata Kanisa wanakuta kitabu cha dini yao kuwa ni kitabu kitakatifu, na utakatifu unapinga kosa na migongano, kwa mgongano huo na sifa za Mungu wa kweli ambaye anatakiwa kuwa

www.path-2-happiness.com

mkamilifu aliyetakasika dhidi ya upungufu; ili astahiki uungu huu.. sitozungumzia msimamo wa kanisa kuhusu elimu na vita ambavyo imepigana kati yake na wanasayansi kwa sababu ya maandiko ya kitabu kitakatifu kugongana na elimu, hata hivyo tuangalie katika Qur'an na changamoto yake katika uwanja huu:

Mmoja wa wanazuoni wa Kiislamu katika zama hizi, Sheikh 'Abdu Majid Az-Zindani pamoja na Profesa Guly Simpson mtaalamu katika magonjwa ya wanawake na mambo ya uzazi katika chuo kikuu cha Northwestern University huko Marekani, kuhusu maandiko ya Qur'an ambayo yanazungumzia hatua za mwanzo za maumbile ya kichanga anapokuwa manii, na namma ambavyo Qur'an inaonesha kuwa mwanadamu huumbwa baada ya kukusanywa kwa manii haya na baada ya hapo ndipo maumbile yanapokuwa, na baada ya hapo ndipo vipengele vya mwanadamu ambaye atazaliwa huanza kujengeka; rangi ya macho mawili, rangi yake ya ngozi, rangi ya nywele…., ambapo maelezo ya sayansi leo hii yamethibitisha kuwa urithi wa mwanadamu unakadiriwa katika hatua ya manii, na hili linaloafikiana na alichosema Mwenyezi Mungu:

"Ameangamia mwanaadamu! Nini kinacho mkufurisha? Kwa kitu gani amemuumba? Kwa tone la manii, akamuumba na akamkadiria." (Abbasa, 80:17-19). Na baada ya kusikia haya huyu Profesa alisimama katika moja ya mikutano akitoa rai yake kuhusu maudhui haya kwa kusema: "Qur'an imekuja kabla ya karne nyingi ikiunga mkono yale tunayoyaendea; kinachothibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Mungu…."

Niache nifungue laptop ili nisome baadhi ya ushahidi kwa kina…. Na tunamuona Profesa Keth Moore mwandishi wa kitabu The Human Developing. Hatua za maumbile ya mwanadamu, nayo nirejea ya kisayansi ulimwenguni iliyofasiriwa katika lugha nane alisimama katika moja ya mikutano na kusema: "Wasifu wa kichanga cha mwanadamu katika Qur'an Tukufu haiyumkiniki kujengwa kwake juu ya maarifa ya elimu ya karne ya saba."

Matokeo yenye kuingia akilini ni kuwa wasifu huu ulimteremkia Muhammad kama Wahyi; Hayumkiniki yeye kufahamu vipengele hivi; kwani alikuwa hajui kusoma yaliyoandikwa na kwa hiyo hakuwa amepata mafunzo ya kisayansi." Dr. Keith Moore hakuishia hapo bali aliweka aya za Qur'an na Hadithi za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) zinazozungumzia elimu ya kichanga (Embryology) katika kila kurasa ya kitabu chake.

Mwingine ni Profesa Yoshidi Kozani–Mkuu wa Anga-Tokyo, anasema: "Sipati ugumu wa kukubali kuwa Qur'an ni maneno ya Mungu; kwa hakika wasifu wa kichanga katika Qur'an haiyumkiniki kuujenga kwa maarifa ya kisayansi ya karne ya saba, tunachoweza kukitoa hapa ni kuwa wasifu huu ni Wahy kwa Muhammad kutoka kwa Mungu…." Je, mnataka nyongeza tena?!

Rajev: Je, ndani ya Qur'an kuna maelezo katika nyanja nyingine?!

Rashidi: Kuna ayah nyingi katika nyanja nyingi–Kwa mfano kuna ayah zinazozungumzia kuhusu hakika za kihistoria ambazo zimethibitishwa na elimu hivi sasa, kwa mfano kisa cha Musa na Firauni, Qur'an imezungumzia kifo cha Firauni na kuzama kwake, na kuokolewa kwa kiwiliwili (maiti) chake ili kiwe mazingatio ya vizazi kuangalia kisa hiki na kukumbuka mazingatio haya, na hilo ni kwa kauli yake Mungu: "Leo, basi, tutakuokoa kwa mwili wako, ili uwe Ishara kwa ajili ya walio nyuma yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na Ishara zetu."(Yunus, 10:92) na hapa kuna ishara tatu:

1-Namna alivyokufa Firaun, kwa gharika.

2. Kukiokoa kiwiliwili chake kutoka kwenye maji.

3. Kuhifadhiwa kiwiliwili chake katika sura ambayo inaweza kuonekana na watu (kutiwa dawa maiti).

Na hili haswa ndilo lililothibitishwa na elimu ya zama zetu, lakini kuhusu kiwiliwili (kilichotiwa dawa) hakijavumbuliwa isipokuwa mwaka 1898 C.E. yaani baada ya kifo cha Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa miaka elfu moja na mia mbili (1,200), na wakati huo bado haikujulikana sababu ya kifo chake ambacho kilikuwa ni kwa gharika, isipokuwa ni katika mwaka 1981 kupitia vyombo vya utaalamu wa hali ya juu na majaribio magumu yaliyofanywa na kundi la wana sayansi wa Kifaransa wakiongozwa na Profesa Maurice Buccaile ambaye hakujua kabla ya hapo kuwa Qur'an ya Waislamu imethibitisha hivyo, kitu kilichompelekea kutangaza Uislamu wake kisha baada ya hapo akaandika kitabu chake muhimu. "Qur'an, Taurati, Biblia na Sayansi… aliitia vitabu vitakatifu na kuvilinganisha katika elimu za sasa.

Katika Qur'an kuna ayah zenye miujiza mingi katika zaidi ya nyanja moja katika wakati huo huo; katika Surat Ruum Mwenyezi Mungu anasema: "Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa, Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda" (Ruum 30:1-3). Hapa kuna

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

sehemu mbili za muujiza wake; Kwanza: Qur'an inazungumzia kuhusu ushindi wa Warumi kwa Wafursi baada ya kushindwa kwao, yaani baada ya miaka michache: yaani katika muda wa miaka tisa na hili lilitokea kilichoahidiwa na Qur'an Tukufu baada ya miaka saba, ambapo kulitokea vita vingine kati ya Wafursi na Warumi mwaka 627 C.E. ambapo Warumi walishinda.

- Sehemu ya pili ya muujiza wa ayah: Imeelezea hali ya kijiografia ambayo haikuwa ikifahamika kwa wakati ule, nayo ni kuwa vita vilipiganwa sehemu ya chini (adna) ya ardhi, na neno chini kwa Kiarabu una maana mbili: sehemu ya karibu zaidi, msemo wa sehemu ya chini, kwa maana hiyo upande mmoja inakusudia sehemu ya karibu zaidi na Bara Arabu na kwa upande wa pili ni sehemu ya chini ya ardhi, yaani ipo chini zaidi ya kina cha bahari kwa futi 1312 yaani mita mia nne, yaani ni sehemu ya chini zaidi ambayo Satellite imesajili katika ardhi kavu, kama ilivyotajwa na encyclopaedia ya Uingireza, ukweli wa kihistoria kuwa vita vimepiganwa sehemu nyingi ardhini zilizo chini katika hodhi ya bahari maiti (Dead Sea) ambayo haikuwezekana kupimwa kwa kukosekana teknolojia ya zama zetu.

Maiko: Nadhani haya yanatosha Rashidi.

Rajev: Ni muhimu mimi kujua, je, Qur'an imezungumzia nyanja zingine kama vile elimu za nyota (astronomy), elimu kuhusu mambo ya ardhi, bahari na mengineyo?

Rashidi: Ndio, katika Qur'an kuna ishara za miujiza katika nyanja hizi na nyinginezo, kama vile mwanzo wa ulimwengu, mwanzo wa mwanadamu, elimu za tiba, elimu za mimea, elimu za wanyama, fizikia, historia na mambo ya hesabu..nyongeza ya miujiza ya Qur'an yenyewe na sheria zake na mengine mengi.

Maiko: Maudhui ambayo yatupasa kuzungumzia ni mengi, lakini kwa bahati mbaya tutamkosa rafiki yetu Rajev; kwani safari yetu ni kesho.

Rajev: Hili linanihuzunisha sana, nimefurahi kufahamiana nanyi na nimefaidika sana na mjadala wenu, tunaweza kuendelea kuwasiliana kupitia njia mbali mbali katika intaneti.

Rashidi: Fikra nzuri, nina fikra nyingine, mnaonaje tukasherehekea mnasaba huu ili tuuhitimishe kwa kumbukumbu nzuri?

Maiko na Rajev: Fikra nzuri.

Bara la Amani

www.path-2-happiness.com

Bara la Amani

Maiko na Rashidi walipanda treni wakirudi London, na baada ya treni kuondoka Maiko alianza kumwambia Rashidi:

Katika mazungumzo yako umekuwa unakumbusha mara kwa mara pointi muhimu sana ambayo naona hukuipa haki yake, mara nyingi ulikuwa ukisema: “Lengo la kuumbwa mwanadamu” na nakumbuka kuwa ulitaja mara moja kuwa lengo hilo ni kumuabudu Mungu, suala hili linanishughulisha sana na linawashughulisha na wale ninaowafahamu, mara nyingi mtu anakutana na matukio anajiuliza. Kwa nini mimi nipo katika dunia hii? Kwa nini tabu na mashaka yote? Kwa nini mgongano huu baina ya wanadamu, bali baina ya mwanadamu na ulimwengu? Je haya sio maswali muhimu?

Rashidi: Ndio, bila shaka ni muhimu, nami nadhani hilo linarejea katika mfumo wa maadili ya mtu wa Magharibi na utamaduni wake, hatima ya mgongano huo ni moja ya misingi muhimu ambayo juu yake unasimama utamaduni wa maada wa Ki-Magharibi, nayo imetoka katika staarabu mbili za zamani za Kiyunani na Kiroma ambao leo hii ustaarabu wa Kimagharibi umesimama katika nguzo zake ambayo hatima ya mgongano ni moja katika fikra za msingi katika staarabu mbili hizi: mgongano kati ya miungu, na mgongano kati ya wanadamu na Mungu na mgongano kati ya mwanadamu na mazingira, na mgongano kati ya nguvu ya shari na nguvu ya kheri, nyongeza ya faragha ya kiroho inayotokana na muelekeo wa kimaada ambao ustaarabu wa Ki-Magharibi leo hii umejitambulisha nao.

Maiko: Wewe unazungumza kama kwamba unamiliki sifa ya ufasaha ya kumvutia mtu unachotaka kumpa.

Rashidi: Jambo hili kwa Muislamu mwenye imani sahihi haliwezi kumkanganya; Muislamu anafahamu kwa Uislamu wake: Ametokea wapi, anakwenda wapi, nini thamani yake na ni kazi gani aliyo nayo mwanadamu?

Maiko: Bado swali langu lipo, bali umeniongezea maswali mengine mengi, ni ipi taswira ya Uislamu kujibu maswali haya?

Rashidi: Muislamu siku zote yupo katika muafaka na ulimwengu huu na vipengele vyake na kuwa vitu hivi vinashirikiana na mja mwema katika kumnyenyekea Mwenyezi Mungu na kumtukuza, kwa hakika katika sura ya uchaguzi na jinsi ilivyo ipo wazi kama ilivyo katika ulimwengu wetu wa wanadamu, au kwa sura halisi ya kimaumbile ama namna gani hilo halijulikani kwetu….Mara nyingi Qur’an imerejea utajo kuwa “Aliyemo duniani anamtukuza Mwenyezi Mungu.” Maneno haya yamekuja zaidi ya mara thelathini kwa tamshi “Kutukuza” na maana hii imerejea kinyume cha tamshi “Kusabihi” mara nyingi vile vile. Hivyo basi Muislamu mwenye utambuzi hufahamu ya kuwa yeye ni (kiungo) mwanachama katika timu ya nyimbo ya ulimwengu huu ambayo inamtukuza Mwenyezi Mungu Mtukuka, yeye yupo katika hali ya kuafikiana na ulimwengu huu na vipengele vyake na sio katika hali ya kupambana na kuchukizana.

Kama ambavyo huhisi mazoea ya kitabia na liwazo, na huona urafiki na sio uadui; kwani Qur’an imesema kuwa yaliyomo ulimwenguni yote yamedhalilishwa kwa mwanadamu, na kwa tamshi hili limekuja zaidi ya mara ishirini na kwa matamko mengine zaidi ya hivyo.

Maiko: Kuna nini nyuma yake! Nini kinachopelekea hilo?

Rashidi: Tukiangalia: anachokihitaji mwanadamu ili moyo wake utulie na hivyo kumpelekea katika furaha na kuishi katika utu wake……yote tunaona yanawakilishwa katika nukta tano: Kujisalimisha, kunyenyekea, kutii, Ikhlas (kuwa mkweli), na utulivu na hilo ndilo linalomhakikishia kiutendaji mwanadamu anapokuwa chini ya mwavuli wa uja ambao unakusanya ulimwengu wote, na tunaona kuwa haya maneno matano ndio maana ya Uislamu.

Maiko: Tafadhali nibainishie uliyoyasema:

Rashidi: Katika matunda muhimu ya taswira hiyo ni uhusiano wa mwanadamu na ulimwengu wake. Na kinachoakisi kwa yule aliyefuata Uislamu hisia za ndani za usalama na amani kwa nafsi yake pamoja na wanaomzunguka na kuishi kwake kwa msingi wa umoja, nalo linamrahisishia yeye kuhama kutoka kwenye hisia za umoja kuelekea kwenye umoja wa kihisia hadi kwenye umoja wa kutengeneza mfumo na kupatikana hali ya ulinganisho katika maisha yake, ulinganisho unaochunga pande zote za ubinadamu; kiroho, kiakili na kimwili.

Kama ambavyo Muislamu anaefahamu kuwa Mwenyezi Mungu ndie aliyetujulisha kuwa ametuumba na kutuumbia vyote vilivyomo ardhini:

“Yeye ndiye aliye kuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi…”(2:29) na akasema: “Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa

www.path-2-happiness.com

watu wanao fikiri."(45:13), anajua kuwa Mwenyezi Mungu hakutuumba na kutudhalilishia kisha tusiwe na uhusiano wowote! Ni lazima mahusiano ya mtu yawe wazi pamoja na yale yaliyodhalilishwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili yake, ikiwa hali ndivyo ilivyo hapana budi basi Mwenyezi Mungu kuteremsha elimu inayohukumu mahusiano haya kati ya mwanadamu na vitu hivi kwani Mwenyezi Mungu amesema: "Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Kiti cha Enzi…."(7:54), na akasema vilevile: "Ati binaadamu anadhani kuwa ataachwa bure? "(75:36), Yaani anafanya katika ulimwengu huu bila ya vidhibiti vya maamrisho na makatazo, na ikiwa ni hivyo, basi hapana budi Muislamu kujifunza na kufanya utafiti kuhusu dini yake ambayo yatamhakikishia uadilifu wa kilimwengu na wa kisheria ardhini.

Uislamu unaondoka kwenye msingi huu ili ulete mfumo kamili wa maisha, hivyo basi unaratibu uhusiano wa Muislamu na Mola wake, kama vile ibada zake na hali zake za kiroho, kama unavyoratibu maisha yake katika miamala yake; kama vile kuoa kwake na kuacha kwake, kuuza na kununua … desturi zake kama vile adabu za kula, kunywa, kulala. kuvaa, kuingia nyumbani na kutoka, hata usafi wake mwenyewe…vile vile unaratibu uhusiano wake na jamii yake, nchi yake, na jamii nyinginezo ili ihusishe nyanja zote za maisha katika sheria, uchumi, siasa, utamaduni na jamii….Hivyo Uislamu unaondoka hapo ili ujenge mfumo kamili unaohusisha nyanja zote za maisha na kuziratibu.

Dini kama ambavyo inaelekeza kwa muislamu hisia zake, hivyo hivyo imemwekea kanuni na kumsimamishia mizani za uadilifu na haki. Humuamrisha kujenga ardhi na daima kutafuta, kuvumbua kingo za ulimwengu na nafsi…yote hayo yanatokea kwenye wigo wa mahusiano na Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kumnyenyekea katika uja wake, majukumu haya ya kimaisha yakizoeleka na yakiwa yameunganishwa na mfumo wa Mwenyezi Mungu; basi wakati huo yatabadilika na kuwa ibada kwa Mwenyezi Mungu.

Maiko: Ulichokitaja ni athari ya khofu yangu katika kupetuka mipaka na kukakamaa, au sema wazi: Dini kutawala maisha.

Rashidi: Hapana budi tufahamu kuwa kila kitu kina nidhamu na utaratibu wake wa kuyaendesha mambo yake, na hivyo kila kipengele kinakuwa katika sehemu yake husika na faida zake, na kwa kuunganisha vipengele hivi kwa njia ya ukamilifu ndipo manufaa na faida ya nidhamu

au mfumo huu unapopatikana na malengo yake kufikiwa, na hili ndilo alilolitaka Mwenyezi Mungu mizani katika kauli yake: "Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani, Ili msidhulumu katika mizani. Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani. " (55:7-9).

Mizani ni uadilifu, na mizani hii ambayo ni uadilifu inakuwa katika kila kitu, na kama ambavyo ulimwengu huu umesimama katika vipimo na makadirio na juu yake kumesimama mfumo wote na sehemu zake, hivyo basi dini hii iliyoteremshwa na Muumba imesimama vile vile katika mizani na uadilifu.

Hivyo basi, mizani na kutodhulumu haki za wengine ni sifa ya jumla katika Uislamu, hili linatafsiriwa kwa uadilifu, linganifu na usawa katika mfumo wa mwanadamu ndani ya nafsi yake na katika maingiliano ya miamala yake na wengine.

Na ulinganifu wa mwanadamu na unyoofu katika taswira yake kuhusu nafsi yake na hukumu yake mara nyingi ndio inayohukumu taswira yake kuhusu wengine na hukumu juu yake, na katika maana ya ulinganifu huu na unyoofu ni kile kilichoelezwa na Allah kuhusu waja wake wema katika dua zao: "Na katika wao wapo wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto!"(2:201)

Na katika maana hii, aya tukufu zifuatazo ziliteremka:

"Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi."(28:77),

"Na wale ambao wanapo tumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo."(25:67)

Na,

"Wala usiufanye mkono wako kama ulio fungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi."(17:29).

Maiko: Inanisikitisha vile vile kuwa mwanadamu amekuwa sasa ananyonya damu ya nduguye mwanadamu, na maadili ya watu yameharibika kiasi cha fedheha na kupelekea nguvu aliyonayo mwanadamu aliyopewa na Mwenyezi Mungu atumie kumletea tabu na kumuangamiza badala ya kuitumia katika yenye kumpelekea kwenye furaha, amani na raha …Uislamu unaangaliaje tatizo hili?

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rashidi: Hii ni nyumba ya mateso ambayo mwanadamu amejitayarishia mwenyewe kwa ajili ya nafasi yake katika dunia hii, hakuna sababu isipokuwa ni kuwa mwanadamu kwa mchezo anajaribu kutawala chombo asicho kijua muundo wake, chombo hiki cha kibinadamu hajui siri zake ila ambae amekitengeneza, na anajua tabia zake, Yeye ndie mwenye kujua kinaendeshwa vipi.

Ama hivi sasa kama mwanadamu huyu akiweza kuzuia nafsi yake katika kutekeleza wazimu huu na kuamua kufuata kanuni alizowekewa na yule aliyetengeneza chombo kile, huenda akatengeneza upya kile ambacho hadi hivi sasa ameshakiharibu, vinginevyo hakuna tiba mbadala katika aliyonayo hivi sasa kama vile misiba, maangamivu, tabu, hasara n.k.

Maiko: Wewe unakusudia kuwa hakuna uokovu isipokuwa kwa kufuata mfumo wa Kiislamu, vinginevyo wanadamu wataishi katika tabu na mashaka?!

Rashidi: Kimantiki hii ni dalili katika kiwango cha mtu binafsi na katika viwango vya kijamii, duniani na akhera; hakuna kinachowezekana katika kuweka mipaka ya ukaidi na shari za mwanadamu katika dunia hii, isipokuwa hisia zake kwa aliyokuwa nayo kama vile anayoambatana nayo na majukumu, hivyo mtu akiwa na yakini katika dunia hii kufanya atakayo na hakuna atakayemuuliza anachofanya wala kuwepo nguvu juu yake inayomfuatilia ayafanyayo, hivyo basi hakutakuwa na mpaka wa ukaidi wake na ukorofi wake, kama ambavyo hili ni sahihi yanapohusiana na mtu, vivyo hivyo ni sahihi yanapohusu familia yake au umma au wakazi wote wa ardhini, huu ni uchaguzi wetu sote, ni uchaguzi wa kukiri uja wetu, kunyenyekea kwetu kwa Mola wetu na Mfalme wetu.

Mimi na wewe na wale wote ambao Allah amewamakinisha ardhini tunapambana na uchaguzi huu, na tulikuwa tumetahiniwa akili zetu na muruwa wetu na hisia zetu kwa wajibu na ahadi yetu, ni juu ya kila mmoja kuamua; Je, ni kweli yeye ametekeleza ahadi au ni haini wa ufalme wake wa kweli?

Ama mimi nimeamua ndani ya nafsi yangu kufuata njia ya utiifu na kutii ahadi, na mimi nimetoka kwenye utiifu wowote, basi, bila shaka kila mmoja atakuwa ametoka katika utiifu wa Mwenyezi Mungu. … Kwa hakika hili ndilo bara la amani.

• **Maiko:** Treni imefika katika kituo chake cha mwisho… haya twende.

Sheria ya Mwenyezi Mungu

www.path-2-happiness.com

Sheria ya Mwenyezi Mungu

Baada ya kukutana kulingana na ahadi waliyowekeana Maiko alianza kuzungumza na kusema:

Leo hii nimesoma kitabu kilichonivutia cha mmoja wa wahusika wa masomo ya Mashariki, ametaja ndani yake mambo mengi kuhusu sheria za Kiislamu, ningependa kujadiliana pamoja nanyi.

Rajev: Ni maudhui yenye umuhimu mkubwa.

Rashidi: Kama utaweza kutaja masuala haya mara moja ili tuweze kuyajadili.

Maiko: Vizuri, nitataja mengi yaliyovutia akili yangu, na si vibaya lau swali litajitokeza kutoka kwa Rajev bila ya kufungwa na yaliyokuja kwenye kitabu.

Rashidi: Karibu.

Maiko: Kitabu kile kimetaja kuwa sharia ya Kiislamu imechukua sheria za Kirumi, na baadhi ya vipengele vinafanana.

Rashidi: Niruhusu nikuambieni kuwa maneno haya ni ya zamani hata leo hii mustashrikina wengi wakubwa hawasemi maneno haya, binafsi nimekutana na mmoja wa mustashriki wa Kirusi amesomea tahasusi ya kanuni na sheria ya Kiislamu, jina lake Leornard Sukanan, na akasema maneno haya: “Kwa sasa hivi hakuna katika watafiti wa Kimagharibi mwenye kushikilia fikra kuwa sheria ya Kiislamu imechukua sheria za Kirumi, hili lilikuwa katika karne ya kumi na tisa, fikra iliyokuwepo kwa baadhi ya watafiti wa Kimagharibi. Ama leo hii fikra ya kanuni ya Magharibi inakiri bila kizuizi vifungo vyovyote-wala sharti lolote ya kuwa uwekaji wa sheria au utungaji wa sheria ya Kiislamu ni mfumo wa kisheria unaojitegemea, hauathiriki na sheria za Kirumi.”

Hili ni mosi, ama la pili: Kwa hakika chanzo cha utungaji sheria ya Kiislamu kinatofautiana kwa ukamilifu na sheria nyinginezo, kama nilivyowatajia mara nyingi ni kuwa Uislamu ni mfumo ulio kamili, kulingana na utungaji wa sheria hilo lina mhusu Muumba kwa aliowaumba kuwapa jukumu ambalo litafanikisha lengo la kuumbwa kwao, na haki yake ni kuwa asitoke katika utiifu kwa kuwazingatia wao kwamba ni watumwa wa mamlaka yake, hivyo basi chanzo cha asili cha sheria katika Uislamu ni Wahyi unaowakilishwa na Qur’an na Sunna ya Mtume, na sote sisi tunafahamu kuwa Mtume wa Uislamu alikuwa hasomi wala haandiki, ni hali ya kawaida kutopata fursa ya kusoma kwa mtu wa namna hii (mbali na kuchukua) kutoka vyanzo vingine vikiwa ni vya kigeni nae.

Haya ndio wanayosema mustashrikina David Santillan: “Tunajaribu kupata chanzo kimoja kinachobeba sheria mbili, mashariki na magharibi (Uislamu na Uroma) kama ilivyothibitika rai juu ya hilo, kuwa sheria ya Kiislamu ina mipaka rasmi na msingi thabiti haiyumkiniki kuirejesha au kuinasibisha na sheria na kanuni zetu kwa kuwa ni sheria za dini zinabadilisha fikra zetu za asilia.”

Ama yanayoweza kutokezea katika kufanana kwa mifumo ya kisheria hii inatokana na kufanana kwa matatizo ya mwanadamu, kisha kufanana kwa mapana ya suluhisho lake ambalo linaweza kutokea kwa maafikiano ambayo msingi wake ni kukadiria maslahi na ufisadi katika mazingira yenye kufanana au katika maumbile ya mwanadamu, mfano kauli ya Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) “Ushahidi ni kwa mlalamikaji na kiapo ni kwa anayekataa.”

Maiko: Lakini inabakia uwezekano wa kuchukua sheria za Kiislamu kutoka sheria za Kiyahudi na kanuni za Kanisa, kwa mazingatio kuwa ni dini mbili za mbinguni zilizoutangulia Uislamu.

Rashidi: Nitakujibu kwa jibu alilolitoa mmoja katika wanafikra wa Kimagharibi aliyehusika na jambo hili, anasema–mustrashrik wa Kijerumani Josef Shakhet: “Sharia ya Kiislamu inazingatiwa kuwa mfano wa maana yake haswa na ya kipekee katika kile kinachoitwa kanuni za dini, bali nikuwa sheria nyingine tukufu ambazo ni mfano wa kanuni za kidini zilizo karibu na sheria za Kiislamu kwa upande wa historia na jiografia (nazo ni sheria za Uyahudi na kanuni za Kikristo) zinatofautiana mno na sheria za Kiislamu na hilo ni kwa sababu sheria ya Kiislamu: ni pana mno na imebeba sura nyingi tofauti na sheria hizo zingine mbili, kwani zimekuja zikiwa natija za kuangalia na umakini zaidi kwa upande wa kidini katika maudhui za kanuni ambazo zimekuwa mbali kuliko kuchukua sura moja.”

Bali ni kuwa yeye anasema kinyume cha uwezekano unaomsukuma, anasema: “Upande mwingine wa bahari ya Mediteranian tunakuta sheria ya Kiislamu imeathiri sana matawi mengine yote ya kisheria…kuna athari

www.path-2-happiness.com

ya sheria ya Kiislamu katika kanuni za dini nyingine zote kama Uyahudi na Ukristo ambazo “Rehema ya Uislamu ulizikumbatia na wakaishi katika dola ya Kiislamu…na hapana shaka kuwa matawi mawili makubwa ya Kanisa la Mashariki ambayo ni Wanestori na Wayakobo hawakusita katika kuchukua uhuru wa sheria za Kiislamu na kuzitumia, na uchukuaji huu ulikuwa katika maudhui yote ambayo mtu anaweza kusawiri kuwa yanaingia katika mtazamo wa kadhi Muislamu.

Rajev: Kama ni hivyo basi ni bora ukatuelezea kuhusu tofauti liyopo kati ya sheria za Kiislamu na sheria zingine.

Rashidi: Ni vigumu kukuelezea tofauti zilizopo, na haswa kwa sababu hukunibainishia sheria yoyote ya kulinganisha nayo, hata hivyo ninaweza kukutajia sifa ya sheria za Kiislamu, na wewe mwenyewe unaweza kulinganisha baina ya sifa hizi na nyingine. Sawa vizuri hamna neno.

Rajev: Hakuna neno

Rashidi: Sheria za Kiislamu husifika kwa:

1-Chanzo chake ni kutoka kwa Mungu – kama nilivyowatajia ni kuwa sheria hii hupokea mada zake kutoka vyanzo viwili vya msingi; Qur’an Tukufu na Sunnah za Nabii Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam). Ama nafasi ya mwanadamu ni kuchimbua kwenye sheria hiyo na kuzilinda na kuziweka katika matukio ya maisha ya kila siku, na kwa sababu chanzo chake ni kutoka kwa Mungu: Ni kuwa hukumu zake zinalenga kuunganisha watu na muumba wao.

2-Kukusanya baina ya tuli (thabiti) na zenye kubadilika, uthabiti wake upo katika: Asili yake, ujumla wake na sehemu zake, ambazo hazibadiliki wala hazibadilishwi, ambazo zinahifadhiwa na kupotea, tofauti na sheria nyinginezo, ama ulegevu wake (uwezekano wa kubadilika) upo katika matawi yake, na sehemu zake, kinachoipa uwezo wa kuzalisha sheria nyingi nazo kulinganisha na matukio na kuyafanya yafikie kila kinachojitokeza (mapya) katika zama husika.

3-Uenevu: (wakati, mahala, mwanadamu na hukumu). Zama kwa maana ya kuwa ni sheria ya karne na zama zote, mahala kwa maana inatekelezwa bila kujali mipaka ya Kijiografia, na mwanadamu kwa maana: Inazungumza na watu wote kwa hukumu zake na kwa maana ya kuwa: Imeenea sehemu zote za maisha ya mtu, kwani inamuhusu mwanadamu katika hatua za maisha yake na katika mambo yake yote, na kuishi nayo katika hatua zake zote: kichanga, mtoto, kijana na mtu mzima na kumheshimu akiwa amekufa na kuhukumu mahusiano yote ya mwanadamu na Mola wake, nafsi yake na wengineo.

4-Iko katika uhalisia, na hili linaonekana wazi pale inapochunga na kujali uhalisia wa waliokalifishwa pale sheria ilipowekwa kwao na kutangamana, kama ilivyochunga pande zote za mwili wa mwanadamu, kiroho, kiakili, mtu binafsi au kundi la watu, wala hakupuuzia nguvu ya mtu binafsi au kundi la watu katika utekelezaji wake.

5-Usawa na Unyoofu, na hili linatimia katika kulazimiana na hukumu kwa ajili ya utaratibu wa kusawazisha kati ya matangamano yote (nayo ipo kati yao), hili ndilo linaipa nguvu na kudumu; kwa mfano: Sheria ya Kiislamu imeweka andiko la mtu binafsi kutamalaki chini ya udhibiti, na kupuuza kama vile ilivyo katika mfumo wa kijamaa, na kuuwacha wazi mno kama ilivyo katika mfumo wa kibepari, na ukahamasisha katika ushujaa nao upo katikati ya ujasiri na uoga, na ukaamrisha kutoa ambalo ni jambo lililo kati ya ubakhili na ubadhirifu kama hivi.

6-Kukusanya baina ya malipo ya kidunia na ya kiakhera, sheria hii inayoafikiana na sheria na mifumo mingine ya kisheria katika kuweka malipo ya mwenye kwenda kinyume na hukumu zake hapa duniani, na wakati ambao mkono wa kanuni iliyowekwa na mwanadamu haifiki katika kumuadhibu mwanadamu katika akhera yake, wakati ambapo sheria ya Kiislamu humkamia anayekwenda kinyume kwa kumuadhibu huko akhera, hilo linakusanya baina ya malipo mawili pamoja.

7-Kujali maslahi na kutogongana na elimu katika mambo ambayo yana uhusiano nayo.

Maiko: Wewe Rashidi daima unapenda kupamba dini yako kwa uzuri na umahiri.

Rashidi: Rafiki yangu sio suala la kasumba ya dini yangu, vinginevyo nini kauli yako katika maneno ya mshairi wa Kijerumani Goethe: “Sheria katika nchi za Magharibi ni pungufu ukilinganisha na mafundisho ya Uislamu, na sisi watu wa Ulaya kwa mitazamo yetu yote hatujafikia bado pale alipofikia Muhammad, hakuna atakayemtangulia.” Hili nalo alilizungumza Goethe kwa sababu nae alikuwa Muislamu?!

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rajev: Nukta ya mwisho katika sifa za sheria ya Kiislamu inataka ufafanuzi zaidi.

Rashidi: Nitakuletea mfano wa sheria kutogongana au kupingana na elimu: Katika mambo ambayo sheria ya Kiislamu inasifika nayo ni kusisitiza aina fulani ya uchinjaji wa wanyama ambao wanaliwa, mbali na idadi ya namna nyingi za wanyama hawa na kuongezea masharti mengine, hili tu ndilo nitakalojadili, yaani njia ya uchinjaji.

Njia ya Kiislamu inataka mnyama achinjwe akiwa hai kwenye mshipa wa shingo na kutong'oa au kutoa kabisa shingo yake, hili linahifadhi harakati za misuli baada ya kuchinjwa na humpa mnyama uhuru wa kutapatapa, kinachosaidia katika kuondosha kiasi kikubwa cha damu, ama katika njia zisizo za Kiislamu za uchinjaji mnyama huchinjwa bila kutajwa jina la Mwenyezi Mungu, na katika njia zenye makosa kama kunyonga kwa gesi au kwa umeme au kwa kupigwa risasi, njia zote hizi humkosesha mnyama uhuru wa kutapatapa na misuli yake kuwa huru; kiasi cha kusababisha mwili kubanwa na damu na hivyo damu kubaki katika kiwiliwili cha mnyama na unapelekea kusababisha bakteria wengi kuwepo na pindi damu hii inapotumbukia (mwilini) inazalisha sumu ndani ya mwili wa mwanadamu, na nyongeza ya hilo njia hizi zina mfanya mnyama kuumia kwa maumivu.

Lakini niachie nikuongezee nyongeza nyingine, sharti la kumtaja Mungu wakati wa kuchinja, pamoja haja ya hilo kwa mtazamo wa kimaada ambao haujali isipokuwa kumuua tu mnyama kwa ajili ya kumla, ama katika Uislamu kila kitu kimeunganishwa na kumpwekesha Mwenyezi Mungu Mtukufu na sheria imeunganishwa na mfumo kamili wa Dini kulingana na majibu ya maswali makubwa (Mungu, ulimwengu, mwanadamu na mwisho wake), Na katika hali hii mwanadamu kwa wasifu wake kuwa ni kiumbe katika viumbe vya Mwenyezi Mungu hana haja ya kuwafanyia uadui viumbe wengine na kutoa roho zao, isipokuwa kwa idhini ya Muumba wa kiumbe hiki, kwa lengo la kusimamisha maisha yake tu, hivyo basi kumtaja Mungu na jina lake ni kuomba ruhusa ya kutangaza mamlaka ya Mungu Mtukufu na kuwa tendo hili linalofanywa na Muislamu ni kwa ruhusa ya Mola wake aliyemhalalishia tendo hili, na ya kuwa Muislamu yupo katika unyenyekevu mkubwa kwake.

Maiko: Nikiri kwako kuwa ili kuweza kufahamu kwa kina sheria za Kiislamu na siri zake unahitaji ufanye utafiti wa kutosha.

Hakika za Kistaarabu:

www.path-2-happiness.com

Hakika za Kistaarabu:

Rajev: Alianza mazungumzo baada ya kukutana na rafiki zake kwa lengo la kuwaonesha picha alizozichukua hivi karibuni, akiweka wazi:

Picha hii nimepiga nikiwa Uturuki kwa mwaliko kutoka kwa mmoja wa rafiki zangu, nilishangazwa na niliyoyaona kutokana na athari za kistarabu katika nchi ile kongwe, rafiki yangu alinishtukiza kwa maarifa ya ustaarabu wa Kiislamu katika nchi yake, na kunifanya nirejee nilichokiona katika nchi yangu ya India.

Maiko: lakini mimi nina maarifa mengine kuhusu ustaarabu wa Kiislamu ambao unawakilisha upande mwingine wa ustaarabu wa Kiislamu.

Rashidi: Nadhani ni vizuri kwanza tuainishe mtazamo wa ustaarabu, kisha baada ya hapo tuangalie ustaarabu wa Kiislamu.

Maiko: Nadhani sisi tunaafikiana na mtazamo huu.

Rashidi: Hakuna neno, tuuainishe kwanza, na ikiwa kweli tumeafikiana basi tutaondokea hapo.

Maiko: Ustaarabu ni matokeo ya nishati ya mwanadamu iwe ni ya kimaada au ya kifikra ambayo jamii husika inaielezea kutokana na ubunifu wake na maendeleo yake kwa wakati maalumu.

Rajev: Nitaongezea maelezo machache katika maneno ya Maiko, nayo ni kuwa; ustaarabu ni mfumo wa kijamii ambao humsaidia mwanadamu katika nyongeza ya uzalishaji wake wa kitamaduni na kielimu na ustaarabu una vipengele vinne: Vyanzo vya kiuchumi, mfumo wa kisiasa, desturi za kimaadili na ufuatiliaji wa sayansi na fani nyinginezo.

Ustaarabu umejikita juu ya utafiti wa kielimu, na katika taswira ya fani kwa daraja la kwanza, upande wa kielimu unahusika na uvumbuzi wa kiteknolojia na elimu jamii, ama upande wa taswira ya kifani unahusika na fani mbali mbali za ujenzi, uchongaji na baadhi ya fani nyinginezo ambazo humpelekea mwanadamu katika maendeleo, hivyo basi fani na elimu ni vipengele viwili vinavyokamilisha (vinavyoongoza) ustaarabu wowote ule.

Rashidi: Ningependa kwanza kuchangia maneno ya rafiki yangu Maiko; tukitegemea ufahamu huu ulioutaja basi hapana budi kuangalia ustaarabu kuwa ni nishati ya mwanadamu katika daraja la kwanza, na matokeo ya mtazamo huu ni kuwa, hapana budi kuangalia katika maana zingine zote za mwanadamu bila kughafilika na chochote, vinginevyo ustaarabu huo utakuwa na mapungufu, au usipewe wasifu wa ustaarabu…hili ni moja.

Pili: Mandhari ya ustaarabu yanaweza kutofuatia baina ya jamii moja ya mwanadamu na nyingine, kwa wasifu wake kuwa yanaakisi msingi ambao juu yake jamii hii imeasisiwa na kuanzia hapo: inakuwa kuangalia usahihi wa maadili haya au makosa yake na kuafikiana kwake na utu wa mwanadamu na kiasi cha kulandana na mazingira yake anayoishi mwanadamu, ikiwa ni kipimo cha uzuri wa ustaarabu wowote, au uharibifu wake ….na hili ndilo ambalo litadhihiri kwetu masafa marefu baina ya staarabu mbali mbali na maafa anayoishi mwanadamu katika kivuli cha ustaarabu huu wa kileo wa Kimagharibi.

Maiko: Namuona bwana Rashidi akikimbia kujadili upande wa kiza katika ustaarabu wa Kiislamu, ambao tulikuwa tuuzungumzie.

Rajev: Huenda jambo hili likatutaka tumuombe Rashidi kututajia sifa za ustaarabu wa Kiislamu, na tofauti yake na staarabu zingine.

Rashidi: Vizuri, Ustaarabu wa Kiislamu umesimama katika taswira ya Uislamu kwa mwanadamu, ulimwengu na maisha, nitakutajieni sifa zake muhimu, lakini naomba niongezee vile vile mkabala na sifa hizi na sifa pambanuzi za ustaarabu wa Kimagharibi wa leo.

Sifa za msingi za ustaarabu wa Kiislamu ni:

Mwanadamu katika taswira ya Kiislamu: ambayo juu yake unasimamia ustaarabu huu, ni kiumbe kinacholelewa na Mwenyezi Mungu, amefanywa kuwa kiongozi katika ardhi hii, ameaminiwa juu ya mfumo wa Mwenyezi Mungu aliyetukuka, yu huru mwenye kuhiari, na ni juu yake yafuatayo: Kuwa mwenye kuamuriwa kufanya matendo mema yaliyojengewa juu ya mfumo huu, ni mwenye kuulizwa juu ya matendo ya utashi wake katika maisha haya duniani na huko akhera.

Ama mtazamo wa kiistaarabu wa Kimagharibi leo hii kwa mwanadamu ni kuwa yeye ni bwana wa ulimwengu huu, ni mtu huru hakuna kinachomzuia isipokuwa kile anachokitaka mwenyewe chini ya ubwana wake hapa ulimwenguni, mambo yake ya msingi huzunguka kwenye matamanio na ladha zake, nao ni umuhimu ambao anashirikiana ndani yake na wanyama wengine pamoja nae. Ustaarabu wa kimagharibi unamwona mwanadamu kuwa ni kiumbe asiye na malengo wala hesabu isipokuwa kwa kile alichokiainisha mwenyewe, kama ambayo malengo yake mwanadamu ya kidunia ni duni.

www.path-2-happiness.com

Ulimwengu katika taswira ya Uislamu ni kiumbe aliyelelewa na Mungu kama alivyo mwanadamu isipokuwa amedhalilishwa kumuhudumia mwanadamu, hivyo basi mwanadamu anafurahia kufuata mfumo wa Mwenyezi Mungu pamoja na ulimwengu huu na anakamilika pamoja nao na anahisi amani pamoja nao.

Ama mtazamo wa kimagharibi kuhusu ulimwengu ni kuwa huzunguka baina ya kuwa kuna mgongano kati ya mwanadamu na ulimwengu, na sio furaha, kwa hivyo basi, vita ni vikali kati yao.

Maisha katika taswira ya Kiislamu ni miliki ya muumba wa mwanadamu na ulimwengu, nao ni kituo katika safari ndefu kuliko tuonavyo; kuna maisha ya dunia ambayo huisha kwa vifo vya watu, na kuna maisha yajayo husubiri baada ya vifo vyao. Mwanadamu ameamriwa kuimarisha ardhi katika anayoridhia Allah Mtukuka, Muumba wa wanadamu na ulimwengu. Na maisha ni shamba la akhera, na kuna hesabu na malipo katika matendo yake ya kila siku duniani.

Ama ustaarabu wa Magharibi unayaona maisha kuwa ni ya kidunia tu, hauamini akhera wala hesabu na malipo, hivyo basi: Nafasi aliyonayo mwanadamu ni ya maisha haya ya dunia pekee.

Yote hayo tunapata matokeo kuwa ni muhali ustaarabu wa Kimagharibi kukutana na ustaarabu wa Kiislamu katika taswira, ni staarabu mbili kinzani.

Maiko: Bwana Rashidi niruhusu nikuambie nilichokifahamu kutokana na maneno yako:

Kwanza: Umesahau kitu muhimu katika nukta za ustaarabu wa Kimagharibi nazo ni dini za Ukristo na Uyahudi vile vile, kwa mfano wewe unasema kuwa mtazamo wa ustaarabu wa Kimagharibi hauamini akhera, hesabu wala malipo, na hili si sahihi, dini hizo mbili zinaamini akhera pamoja na kuwa vipengele vya imani hii inatofautiana kutoka dini moja kwenda dini nyingine.

Pili: Maneno yako hayo yanafaa kuwa ndio msingi uliosimamia ustaarabu wa Kiislamu ukiulinganisha na wa Kimagharibi, lakini sifa ambazo zinasimamia ustaarabu wa kiislamu hukuzizungumzia kama alivyokuomba rafiki yetu Rajev.

Rashidi: Rai yako ya mwanzo au uchunguzi wako wa mwanzo ninatofuatiana nawe; kuna tofauti kati ya misingi inayosimamia ustaarabu na yaliyomo katika jamii ile ambayo ustaarabu ule umeanzia, hapana shaka kuwa kuna taathira ya Ukristo na Uyahudi katika ustaarabu wa Kimagharibi, lakini hauwezi kudai kuwa ustaarabu wa Kimagharibi umesimama katika misingi ya dini hizi mbili, bali tunaweza kuthibitisha kinyume chake kabisa, nayo ni kuwa umesimama katika kupinga dini kwa ujumla na utawala mahususi wa Kanisa, yaani kwa matumizi ya akili tupu na mambo matupu ya kidunia tu, na hilo ndilo ambalo lipo kwa uwazi katika usekula, ambalo maana yake ni kutenganisha dini na maisha, nadhani mnakubaliana nami katika hilo.

Ama ugunduzi wako wa pili naafikiana nawe kabisa, lakini naongezea kuwa misingi hii ambayo inafupisha sifa za ustaarabu wa Kiislamu ni hii ifuatayo:

Ama (sanaa nzito) katika ustaarabu wa Kiislamu ni kumjenga mwanadamu kwenye: Kuchunga yaliyomo ndani yake, kushibisha utu wake, kufanikisha uhusiano wake na ulimwengu wake, na kufikia lengo la kuumbwa kwake.

Kufungamanisha na kuchanganya baina ya dini na dunia kwa upande mmoja na kati ya dini, akili na elimu kwa upande mwingine, na ukuzi wa mfumo na nishati ya ustaarabu juu ya msingi huu.

Ulinganisho na kuoanisha kati ya vyanzo ya maarifa ya ubinadamu, kwa hiyo; kweli yote, yenye kuhusiana na maada na zaidi ya hapo, ziko katika matumizi ya mwanadamu; anaweza kuyafikia kwa njia zake nyingi zilizopangwa kwa hatua, zenye kutegemeana, kwa hiyo vyenye kuweza kupatikana kisilika nyuma yake vinapatikana kihisia, kisha kufahamika kiakili na hizo za kiakili hupelekea kwenye vitangulizi vya kuweza kupokea mambo ya ghaibu kwa njia ya WAHYI na kujisalimisha kwake.

Kufunguka kwa staarabu na tamaduni zingine, yaani ustaarabu wa Kiislamu ni wenye kuathiri na kuathiriwa, ikiwa na maana ya kupokea na kutumia yanayowafikiana na ustaarabu wa Kiislamu kutoka katika yaliyozalishwa na umma zingine, na kufungua milango ili umma zingine ziweze kufaidika na uzalishaji na matukufu ya ustaarabu wa Kiislamu.

Rajev: Samahani bwana Rashidi, Maiko amesema ana maelezo kuhusu eneo ambalo ustaarabu wa Kiislamu umeboronga, naomba umpe fursa azungumzie ili picha yetu ikamilike.

Maiko: Jambo muhimu hapa ni kuwa dola iliyooanisha ustaarabu huu imesimama kwa ncha ya upanga, na imehusishwa na matumizi ya nguvu na ukatili.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rashidi: Rafiki yangu upanga hausimamishi ustaarabu, kwani moja katika shuruti muhimu ya ustaarabu ni utulivu na amani, nayo ni kinyume na hali ya vita, kama ambavyo ushindi wa kiaskari hauna maana kuwa ushindi katika uwanja wa fikra, utamaduni na ustaarabu ni juu yako kutafakari historia ya watatari, wamangoli na umma zingine zilizo kuwa na nguvu kubwa ya kiaskari lakini kwa nguvu zao hizo hawakutengeneza ustaarabu.

Lakini ikiwa unakusudia madai ya Uislamu kuenea kwa jihadi, mimi naashiria kwamba Uislamu ulienea na kusimamisha ustaarabu eneo kubwa ulimwenguni ambalo halijafikiwa na jeshi la Kiislamu, na maudhui haya yana fafanuzi nyingi, lakini nitakupelekea katika ushahidi na uthibitisho wa Wanafikra wengi wa Kimagharibi, katika hili, anasema mwandishi wa Kimarekani T. Lothrop Stoddard katika kitabu The New World of Islam "Ulimwengu mpya wa Kiislamu" Waarabu kamwe hawakuwa ummah uliopenda kumwaga damu na kupenda kunyang'anya na kuangamiza, bali walikuwa, kinyume na hayo, umma uliozawadiwa tabia njema, wakipenda kusoma, wenye kutumia vizuri neema, neema zile zilizomaliza staarabu zilizopita, pamoja na kuenea kuoana baina ya washindi na wenye kushindwa na kubadilishana fikra, maingiliano haya yalizaa ustaarabu mpya: ustaarabu wa Kiarabu."

Anasema Luteni wa jeshi la Kifaransa Conte Henry De Castry; "Sisi tunaamini kuwa kuangalia dini hii katika karne hii sasa hakubakisha athari yoyote kwa walicho dai kuwa imeenea kwa ncha ya upanga, lau dini ya Muhammad ingeenea kwa matumizi ya nguvu na kulazimisha basi isingekoma kuendelea kwake baada tu ya kuisha kombozi za Waislamu, wakati ambapo sisi tunaona kuwa Qur'an inakunjua mbawa zake kwenye sehemu zote zilizokaliwa."

Sipati neno lenye kuweza kuelezea athari za ustaarabu wa Kiislamu katika historia ya mwanadamu yenye ukweli kuliko maneno ya mwanahistoria wa Kifaransa Gustav Lubon:

"Hatuoni katika historia Umma wenye athari iliyo wazi kama Waarabu; Umma zingine zote zilizokuwa na uhusiano na Waarabu walichukua ustaarabu wao hata kama ulikuwa ni muda mdogo tu…."

Mwishowe: Ni juu yenu kuangalia maisha yanaonekana vipi yakitishiwa kuwaangamiza wanadamu kwa njia ya kuangamiza sifa zake za utu wa mwanadamu, katika kivuli cha ustaarabu uliopo hivi sasa, jambo ambalo kusimama kwa jamii ya Kiislamu ni la lazima kwa kulinda utu wa mwanadamu na ni hatima ya maumbile yake.

Jua la Waislamu Linaangaza Kwa Wanadamu

www.path-2-happiness.com

Jua la Waislamu Linaangaza Kwa Wanadamu

Baada ya kusalimiana, Rajev na Rashidi waliona pupa ya Maiko ya kutaka kuanza kuzungumza, Rashidi akamtania kwa kumuambia:

Haya Maiko je, umeandaa mshale wenye kutoboa katika kikao hiki, nitajaribu kuwa mbali na skrini kwa kukwepa mshale wako!!!

Maiko: Hapana, hapana, tulia….mara hii unaweza kukodolea skirini yako bila wasiwasi…ukweli ni kwamba mjadala uliopita umenihamasisha kuchimba ndani zaidi na kujaribu kufahamu mchango wa Waislamu katika maendeleo ya wanadamu, nikaona filamu hii yenye anuani “Gunduzi elfu moja na moja za Maktaba za siri.” (1001 inventions and the Library of Secrets) Muda wa filamu hii ni mdogo sana inachukua dakika (13) kumi na tatu tu, lakini ni yenye kuvutia na nzuri katika maudhui haya…inaelezea jinsi gani ustaarabu wa Kiislamu ulivyochangia katika maendeleo ya leo hii ya mwanadamu, filamu hii imepata zaidi ya tuzo ishirini ulimwenguni.

Filamu imechukua staili ya kisa kifupi, ambapo mkutubi wa maktaba ile anawaelekeza baadhi ya wageni wa maktaba wakati wa ziara yao ya moja ya maktaba ya shule, na katika ziara hii wanagundua nyakati zilizokuwa zikiitwa zama za kiza (dark ages), mwandishi wa hekaya hizo ambaye anaonekana katika skrini ni ‘Sir Ben Kingsley ambaye amechukua nafasi ya Mkutubi, ambaye baadae alichukua haiba ya mwanazuoni wa Kiislamu Al-Jazary, ambaye huwatambulisha vijana na baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu ambao wameishi katika zama hizo, huwatambulisha na hazina kubwa ya uvumbuzi ulioshuhudiwa na ulimwengu wa Kiislamu katika zama kati ya karne ya saba na karne ya kumi na saba, ambayo imepitia historia yenye msisimko ambao haujapewa heshima yake stahiki.

Rashidi: Ni nini muhtasari wa filamu yenyewe na inalenga nini?

Maiko: Filamu inalenga kuthibitisha kuwa kipengele cha msingi na msukumo mkubwa wa kuzaliwa karne ya mwamko huko Ulaya ni lile lililoshuhudiwa na ulimwengu wa Kiislamu katika mafanikio ya kielimu na ya kitamaduni ambayo yamefungua mtazamo mpya, mpana katika mikono ya wanazuoni na wavumbuzi ambao ni viongozi waanzilishi kutoka dini mbali mbali, na filamu inaonesha kuwa mtazamo huu ni hakika za Kihistoria imesahaulika kwa kiasi kikubwa.

Rajev: Maiko umeniongezea shauku ya kufahamu zaidi ya ulioyasema.

Maiko: Pana maelezo mengi katika jambo hili, miongoni mwa hayo ni: Kuwa Al-Jazry, mmoja wa wahandisi, mkemia na mvumbuzi katika historia, alivumbua saa ya tembo, ambayo utajo wake umekuwa kama vile simulizi tu, kama ambavyo alivumbua vifaa vingi ambavyo hutumika kama vyombo au mashine ambazo tunazitumia katika maisha yetu ya kila siku, kila sehemu katika mgongo wa ardhi, vyombo vya kimekaniki vimetengenezwa kulingana na wasifu wa kizamani ambao unabainisha jinsi nguvu ya upepo inavyoweza kutumika na maji ili kuleta mapinduzi katika kilimo….vile vile: Daktari wa ki-Andalus, Az-Zahrawy ambae amevumbua mamia ya vifaa vya operesheni kabla ya miaka elfu moja, hadi leo hii uvumbuzi wa vifaa vyake unaokoa maisha ya wagonjwa katika hospitali za kisasa, pamoja na kuzingatiwa kuchunga taratibu za operesheni miongoni mwao ni: Al-Hasan bin Al-Haythami wa mwanzo aliyefafanua wadhifa wa jicho, na kupitia filamu hiyo tunaona mfano wa vyombo na vifaa vya uchukuaji picha kwa undani na umakini zaidi, ili tuweze kujua jinsi Ibn Al-Haythami alivyoweka msingi wa uchukuaji picha na utengenezaji wa filamu.

Rajev: Nimeongeza taarifa muhimu bwana Maiko, lakini sio wewe peke yako ambaye umeyapa umuhimu na kufuatilia haya na kuyagundua, nami pia nimetafiti haya, na nimeangukia juu ya kitabu chenye kusisimua cha mwandishi mwanamke wa Kijerumani jina lake Sigrid Honka, chenye anuani. “Jua la Mwenyezi Mungu linaangaza kutokea Magharibi” Sun rising from west.

Maiko: Nini kipya ulichopata?

Rajev: Nimeangazia vitu vingi ambavyo sikuvitarajia, unajua kuwa maneno mengi yaliyopo katika lugha nyingi za Ulaya ni maneno ya Kiarabu?

Maiko: Jambo la ajabu kabisa! una hakika na unachosema?

Rajev: Kweli sifanyi utani, mathalani: Neno (Coffee) katika lugha ya Kiingereza na mfano wake katika lugha zingine za Ulaya, imechukuliwa kutoka neno la Kiarabu’ kahawa’ na ndani yake kumetoholewa neno ambalo linaashiria sehemu ambayo ndani yake kunanywewa kinywaji hiki…..Neno Rice limechukuliwa kutoka neno la Kiarabu ’Uruz’ na neno (sofa) kwa Kiarabu ni (sufa), ambayo ina maana ya kiti (kikalio) chenye

www.path-2-happiness.com

mwavuli jirani na msikiti, bali kuna maneno mengine mengi yenye maana ya kisayansi moja kwa moja nimeyapata vile vile, yenye kulandana na neno la kiarabu; kama vile neno (Alcohol).

(Kitabu) kimenijuza hakika nyingi nilizokuwa sizijui, mwandishi alizifupisha kwa kauli yake: “Hakika Ulaya inadaiwa na waarabu na ustaarabu wa kiarabu, na deni lililo katika shingo za watu wa Ulaya na mabara mengine kwa Waarabu ni kubwa sana, na ilikuwa ni wajibu kwa watu wa Ulaya kukiri hili tokea muda mrefu, lakini kasumba na tofauti ya itikadi zilipofua macho yetu, na kuacha kiza juu yake (pazia)”.

Rashidi: Rajev amenitia shauku kufahamu zaidi kilichokuvutia katika hakika hizi ambazo hukuwa unazifahamu hapo kabla.

Rajev: Mathalani: “Mimi sikuwa nafahamu kuwa wa mwanzo kujua makosa ya Galinous na kumkosoa, kisha akaja na nadharia ya mzunguko wa damu hakuwa Sarvitous wa Hispania wala hakuwa Harvie wa Uingereza, bali alikuwa ni mwarabu katika karne ya kumi na tatu C.E. naye alikuwa ni Ibn Nafiis, ambae alifikia uvumbuzi huu mkubwa katika historia ya binadamu na historia ya tiba kabla ya Harvie kwa miaka mia nne na kabla Sarvitous kwa miaka mia tatu…Sikuwa nafahamu kuwa mwanazuoni wa Kiarabu Muislamu Ibn Al-Haytham ndie wa kwanza kusahihisha kosa la Iqlidis na Batlimous, walipodai kuwa macho matupu ndio yenye kupeleka mwanga kwenye vitu ambavyo yanataka kuviangalia, alipokuja Ibn Haytham alitangaza kuwa kudai hayo ni makosa; kwani hakuna mwanga unaotoka machoni ili mtu apate kuona, bali ni kuwa vitu vyenye kuonekana ndivyo ambavyo vinaakisi mwanga machoni na hivyo mtu kupata wasaa kuviona kupitia miale yake, Kama ambavyo nilikuwa sifahamu kuwa Muislamu Muarabu Al-Bayruni ndie aliyevumbua dunia kuzunguka jua na katika mhimili wake na sio Nicolaus Copernicus au mwingine kama inavyosambazwa.. kama ambavyo mustashrikina huyu maarufu alivyotaja kuwa daktari wa Kiislamu Ar-Raziy ambaye anazingatiwa na wanahistoria kuwa mmoja wa madaktari wakubwa wa zama zote, ambae makala yake kuhusu ugonjwa wa majeraha mwilini na kujaa maji, na mapele yenye kujitokeza usoni na mwilini kuwa ni kazi ya mwanzo iliyofanikiwa sana kuhusu maradhi ya tumbo, ikielezea nguvu kubwa katika uchunguzi wa kimaradhi, hili lilikuwa maarufu huko Ulaya kiasi cha kuchapwa zaidi ya mara arubaini kwa lugha ya Kiingereza tokea mwaka 1489 hadi 1866. Kama ilivyotajwa kuwa waarabu katika zama hizi ambazo huko Ulaya ziliitwa zama za kiza walikuwa wakifahamu nusu kaputi (anaesthesia) katika tiba ambayo walidhania ni uvumbuzi wa hivi karibuni, wakati ambapo ukweli unasema, na historia inashuhudia kutumia sponji ya nusu kaputi ni fani ya waarabu pekee, haikuwa inajulikana hapo kabla….na kuna ufafanuzi mwingi ambao ni vigumu kuuelezea katika mjadala huu.

Rashidi: Kwa hakika hili linajibu madai ya baadhi ya watu ambao hawajui hakika za kihistoria au wanakana kuwa Waarabu na Waislamu hawakuchangia kitu kipya katika ustaarabu, haswa katika sayansi/elimu za majaribio ‘Experimental Science’ ambapo mwanadamu hakujua mfumo huu wa majaribio isipokuwa chini ya mikono ya Waislamu na Waarabu, niruhusuni ninukuu baadhi ya maneno ya wanazuoni wa Kimagharibi katika eneo hili.

Mustashrik wa Kifaransa Claude Cahen anasema: ikiwa wanazuoni wa Kiislamu (bila kujali muelekeo wao wa Kifikra) wana uwezo mdogo kuliko Wayunani katika kuzingatia na fikra tupu, lakini walifidia hayo kwa muelekeo wao katika elimu za majaribio, maendeleo ya elimu yaliyofuata yalibainisha umuhimu wa muelekeo huu hivyo basi elimu waliyoacha Waarabu ni elimu waliyoishi nayo na kuitumia katika kubaki, na Ar-Razy (mmoja katika wanazuoni wakubwa) alielezea na kufafanua vizuri kwa uwazi, uwezekano wa kuendelea kwa maendeleo ya kisayansi, nayo ni msingi wa ajabu kwa wanafikra wa zama za kati. Mtafiti mwanamke mtaliano Lora Fiche anajiuliza;

“Je, Waarabu hawakuwa ndio wa mwanzo ambao waliotutengenezea njia ya majaribio kabla ya Roger Becon kutangaza umuhimu wa jambo hilo kwa muda mrefu?! Na Kemia ikaendelea pamoja na elimu ya nujumi (astronomy) na kusambaa kwa elimu ya kigiriki, na kukua kwa elimu ya tiba na kuvumbuliwa kwa kanuni mbali mbali za fizikia, je, haya hayakuwa katika athari za Waarabu?!” Mwanafalsafa na mwanahistoria wa Kimarekani Will Durant anasema: “…Sayansi ya Kiarabu imekulia katika elimu ya kemia na njia za majaribio ya kisayansi, nazo ni nyenzo muhimu za kisasa za akili ndio fahari yake kubwa, na Roger Becon alipotangaza umuhimu wa kutumia njia hii huko Ulaya hilo lilikuja baada ya Jabir (Ibn Hayyan) kulitangaza kwa miaka mia tano, jambo ambalo lilimuongoza kwenye hilo ni nuru ambayo imeangaza njia kutokana na Waarabu wa Andalus na haukuwa mwanga huu wenyewe tu, isipokuwa

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

ni mwanga wa nuru ya Waislamu wa Mashariki.”

Na hili ni sehemu ndogo inayoweza kusemwa kuhusu nyanja za uvumbuzi wa ustarabu wa uarabu wa Kiislamu ambao umeutoa kwa watu.

Maiko: Kwa hakika mtu hawezi kukana mafanikio haya, hata hivyo hatuwezi kusahau vile vile kuwa ustaarabu huu umefaidika vilevile na staarabu nyinginezo kama vile ustaarabu wa Kiyunani.

Rashidi: Rafiki yangu hii ndio hali na tabia ya maendeleo ya kisayansi: Ni mnyororo ulioungana katika mafanikio ya mwanadamu, na ndilo linalofahamika kwa jina ‘mnyororo wa mizunguko ya ustaarabu’ na ndilo analolihimiza mustashriki wa Kifaransa Aldo Mail; “…..Elimu hii ya Waarabu inaeneza mnyororo wa mawasiliano na kuendelea baina ya staarabu za kale na ulimwengu mpya wa leo hii, na kama sisi hatutapambana na elimu ile ya Waarabu wala kuifahamu tutajikuta tukiwa watupu tu, inashindwa kufasiri kati ya staarabu za kale na staarabu zetu leo hii.”

Dr. Toby E. Huff wa kitengo cha Historia ya elimu wa Chuo Kikuu cha Harvard mwenye kitabu: The Rise of Early Modern Science: Islam, China and the West.” kuwa kuhamisha maarifa ya kisayansi na ya kifalsafa ambayo yamepandana na kuhifadhika katika ustaarabu wa kiarabu na Kiislamu kwenda Magharibi kupitia juhudi kubwa ya tarjama ambayo imesimamiwa na watu wa Ulaya katika zama za kati, ilikuwa na athari kubwa katika maendeleo ya fikra za Magharibi.

Lakini niache niseme: Kwa hakika mafanikio ya ustaarabu wa Kiarabu wa Kiislamu ambao unasifika na sifa ambayo haijawahi kusifika nao ustaarabu mwingine, kama vile:

Elimu ya Kiislamu sio tu haijatengana na dini, bali dini ilikuwa nguzo na nguvu yenye msukumo mkubwa.

Kwa hakika elimu ya Waislamu haikuwa siri, bali walipupia kuueneza kwa watu kwa mafungamano yao tofauti, kwa hiyo vyuo vyao vikuu vilikuwa wazi kwa wanafunzi wa Ulaya ambao walihamia kutoka kwenye nchi zao kutafuta elimu.

Hakika mimi ni mwenye kujifakharisha na ustaarabu ule.

Mwanadamu Anapotengwa

www.path-2-happiness.com

Mwanadamu Anapotengwa

Rajev na Rashidi walimtangulia Maiko kungia katika chumba cha mjadala, mazungumzo kati yao yakaanza kwa Rajev kumwambia Rashidi,

Kuna jambo nataka kulizungumzia na ningependa kujua taswira ya Uislamu; kwa kuwepo uhusiano wa jambo hili na taswira hii.

Rashidi: Tafadhali, zungumza.

Rajev: Katika nchi yetu (India) kuna tabaka linaloitwa Untouchables

na leo hii wanaitwa Harijans au (watoto wa Mungu), na jina hili liliitwa na kiongozi mashuhuri wa India Mahatma Ghandi..pamoja na kuwa serikali ya India ilitoa tahadhari ya matumizi ya neno untouchables mwaka 1949 isipokuwa hilo liliendelea vijijini na miji midogo huko India.

Rashidi: Lakini nini tatizo la kutengwa huku?

Rajev: Sio tatizo, ni balaa kubwa…..balaa la wanadamu liko wazi katika kumwaga haki za binadamu katika sura mbaya za dhulma.

Maiko nae anaingia na kuwasalimia wenzake.

Rashidi: Karibu Maiko, Rajev ameanza mazungumzo muda si mrefu, utaweza kufahamu maudhui yenyewe pindi Rajev atakapokamilisha mazungumzo yake – Rajev karibu endelea.

Rajev: Hili linatokana na mgawanyo wa kitabaka kulingana na dini ya Uhindu, tabaka la juu zaidi ni: Brahmins, na kulingana na itikadi yao ni wale walioumbwa na mdomo wa Mungu: Katika tabaka hili kuna mwalimu, kuhani, kadhi/hakimu, kisha linafuatiwa na tabaka la Kshatriyas, hawa wameumbwa na mkono wa Mungu, wanasoma na hutoa dhabihu na hubeba silaha kujinda, na wakifuatiwa na tabaka la Vaishyas, hawa ni wale walioumbwa na Mungu kwa mapaja yake hawa ni wakulima, wafanya biashara na hukusanya mali na ndio wenye kutoa kwa kuendesha vyuo vya kidini, mwisho wa matabaka haya ni Shudras, nao ni wale walioumbwa na Mungu kwa miguu yake, nao ni wenye asili ya weusi, ambao ndio tabaka la waliotengwa (untouchables), na kazi zao zipo katika kuhudumia tabaka zingine tukufu, na kazi zao ni zile za kudharauliwa.

Rashidi: Nimekufahamu ulichokusudia.

Rajev: Samahani, bado hujafahamu.

Maiko: Je kuna yaliyo mabaya zaidi ya hayo? na je, mgawanyo huu bado upo?

Rajev: Ndio, nimemueleza Rashidi kuwa muamala wa waliotengwa kwa mgawanyo huu bado upo katika maeneo ya vijijini, na kuna matendo ambayo huwezi kudhania yanayofanywa dhidi ya tabaka hili; kanuni za Kihindu za Manu ambazo ziliwekwa katika karne ya tatu C.E. zimejengwa juu ya kudharau tabaka la Shudra na waliotengwa; miongoni mwao ni: Kuwa mtu ambae atamfundisha Shudra mambo ya dini basi mtu huyo ataingia Jahanamu pamoja na Shudra.

Na ya kuwa waliotengwa waishi mbali na vijiji, wala wasitumie vyombo visivyovunjika, wala hawana haki ya kumiliki chochote zaidi ya mbwa na punda, na asivae isipokuwa nguo za wafu, na watembee peku peku, mapambo ya wanawake wao yawe ya chuma, na mahusiano yao yote yawe kati yao tu, na waoane wao kwa wao, na kanuni ambazo bado zinatawala jamii ya Wahindu zinasema kuwa, Shudra yeyote anapozungumzia mambo ya dini basi na amwagiwe mafuta ya moto mdomoni mwake!! Bali zaidi ya hilo ni kuwa, huko vijijini bado walitengwa na wamekatazwa kutoka majumbani mwao kabla ya saa tatu asubuhi na baada ya tisa mchana; kwani kivuli chao kinakuwa kirefu muda huo, na Brahma wanaogopa kivuli cha waliotengwa kisije kuwa najisi na Brahma hawawezi kula chakula hadi wajisafishe na najisi ya waliotengwa!!

Maiko: Haiwezekani! Hili linatokea katika zama zetu?! Ni asilimia ngapi ya watu hawa katika jamii ya India?

Rajev: Waliotengwa ni asilimia 45 ya wakazi wa India, yaani asilimia 80 ya Wahindu, wakati ambapo matabaka mengine matatu yote ni asilimia 11 tu ya Wahindu.

Rashidi: Lakini umesema kuwa serikali ya India imepiga marufuku tokea mwishoni mwa miaka ya arobaini, karne iliyopita kutumia wasifu

www.path-2-happiness.com

huu wa waliotengwa, hapana budi hilo kuwa la kisheria.

Rajev: Hili ni kweli, lakini tatizo linajificha katika fundo la nasaba safi na nasaba isiyokuwa safi, na tofauti ya watu ipo katika msingi huu, na huu ni msingi muhimu katika dini ya Uhindu; ambapo wanamuona asiyekuwa Mhindu na asiyekuwa katika tabaka tatu za juu kuwa ni mwanadamu mchafu.

Rashidi: Ni mfumo uliosimama juu ya dhuluma na kudhalilisha ubinadamu wa mtu, kubagua katika misingi ambayo mwanadamu mwenyewe hana mkono na mamlaka, hata hivyo ni uhusiano gani uliopo kwa uliyoyataja na taswira ya Uislamu?

Rajev: Uhusiano wake ni kuwa, wengi katika waliotengwa wanabadilika kuwa Waislamu na haswa kabla ya marufuku ile haijatolewa. Pamoja na kuwa waliishi wakati wa ukoloni wa Mwingereza ambapo jitihada za kuutangaza ukiristo kutoka kwao zilikuwa kubwa.

Rashidi: Huenda hilo linarejea kwa jinsi walivyouona Uislamu unavyoheshimu watu, kwani mwenye kuutambua ukweli wa Uislamu na haki za binadamu zilizo ndani yake, na usawa wake kati ya mkubwa na mdogo, na tajiri na masikini, na uhuru aliopewa mwanadamu, hapana budi aelekee kwenye dini hii na aingie…..nadhani waliliona hilo ndani ya kuishi kwao na Waislamu.

Maiko: Unataka kutuambia kuwa Uislamu unaheshimu uhuru wa watu na haki zao?....Uhuru na haki za binaadamu hazikufahamika kupitia dini bali zimewekwa na wanafalsafa na wanafikra wa Kimagharibi, wakapokwa na mataifa mengine katika mapigano mengi waliopigana dhidi ya dhuluma na kuvunjiwa haki zao na kupokwa uhuru wao…haki hizi hazipatikani kwenye Uislamu, uko wapi uhuru wa itikadi na haki ya kutoka katika dini ndani ya Uislamu? Uko wapi uhuru wa kujieleza na kusema? Wapi haki za wanawake?...isije ikawa imani yako kali kwa dini yako inakupelekea kuficha ukweli.

Rashidi: Umefungua mlango mpana katika masjala ya kifikra ewe rafiki yangu…nakuona unazungumza kwa lugha ya ushindi, kama kwamba Magharibi imekuwa ni kinara wa haki za binadamu… ikiwa Magharibi imefikia hali hii, unafasiri vipi hukumu nyingi zilizowaangukia wanafikra, waandishi na wanahistoria, kwa sababu tu walieleza rai zao.' Kwa kutia shaka Holocust (Mayahudi kuunguzwa na manazi) wakikataa kutokea kwake au wakipunguza idadi ya wahanga wake. Je! huku hakukuwa kuvunja haki na kuwazuia watu kupata habari, matokeo ya utafiti, na uhuru wa fikra na kujieleza?! Je, kuna anayeweza kutekeleza haki yake katika kuasisi chama cha Republic katika Uingereza ya Malkia, au chama cha Nazi Ujerumani?.....bali, je mtu kama mimi Muislamu ninaweza kuoa mke wa pili rasmi huku Uingereza? Pamoja na kuwa dini yangu inanipa haki hiyo, je, tawala hazitoingilia kuzuia haki hizi na kuninyima uhuru huu.

Maiko: Uhuru huu na haki hizi zinapingana kabisa na haki za wanadamu, haki hizi zimeshafinyangwa na kuwekwa katika sura za kanuni na sheria na hivi sasa yapasa watu wote kuziheshimu, shaka ya kuunguzwa (holocust) ni uadui dhidi ya Usemitiki nao ni ubaguzi kwa lengo la kueneza chuki, kama ni kinyume cha udugu na usawa nazo ni 'tuli' na 'matukufu' hatuwezi kwenda kinyume nayo hata kama uhuru mwingine wowote utazuiwa na kufungwa, na ndio hili hili la kukataza kuanzisha vyama ulivyotaja katika nchi hizo, kama ambavyo ndoa yako ya mwingine haingii chini ya haki katika (uhuru wa kuitakidi); kwa kuwa imetoka katika mipaka (mapenzi na dhamira ya mtu), na kwa sababu katika hilo ni kuvunja sheria na mkataba wa jamii wanayoishi, na ndani yake kuna uadui wa haki za wengine (mwanamke, hata kama atakuwa ameridhia), lakini wakati huo huo: imehalalishwa kwako kuishi na wanawake wengine nje ya mipaka ya kuwa ni mke, madamu hilo litakuwa ni kwa ridhaa yao.

Rashidi: Vizuri sana… Hivyo basi ninayoyaona mimi kuwa ni dhuluma na kunyimwa haki na uhuru wangu, wewe unaona kuwa ni udhibiti, na mfumo hakuna dhuluma ndani yake, na hilo ndilo haswa wafanyalo watu wa dini ya Uhindu ambao rafiki yetu Rajev ametuelezea, matendo ambayo yametuchafua sote, Je nao wanaona kuwa wanavunja haki za wengine? Bila shaka hulioni hilo.

Rajev: Ni Kana kwamba maneno yako yanaonyesha kuwa wao wana haki katika matendo yao na ubaguzi wao wa kitabaka unao chukiza.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rashidi: Hapana kabisa… lakini kusudio langu ni kubainisha kuwa hatuwezi kutenga haki na uhuru kutoka katika mfumo uliotungwa wala katika mipaka ya kisheria ya jumla ambayo inaidhibiti na kuijenga, ikiwa kweli tutataka kurejea haki hizi na uhuru huu hebu na tuchunguze maadili na misingi iliyosimamishwa na sio utekelezaji tu wa wafuasi wake, ikiwa tutakubaliana katika hilo, tutaona tofauti ya msingi kati ya nadharia za Kiislamu na zile za Magharibi na hilo ni lazima liakisi katika nyanja za haki za binaadamu na uhuru wake….na tofauti hii kimsingi inarejea katika tofauti ya mtazamo wa undani wa (utu) na hakika ya (haki) na maana ya (uhuru), chini ya mtazamo wa ujumla wa mwanadamu na mwanadamu, na maisha, na hili ndilo lililotokea kwa rafiki yangu pindi alipotupa mtazamo wa (dini), na (udugu) na (usawa) kulingana na mfumo wa kifikra wa Magharibi kuhusu haki na uhuru, na kuufanya kuwa ni tuli usioweza kubadilika pamoja na matukufu, wakati ambapo ufahamu huu ni tofauti katika Uislamu.

Ama tukizungumzia msingi wa haki za binadamu katika Uislamu, tunaona kuwa imepanda hadi kuwa ni wajibu unaolazimishwa na jamii yote kwa mtazamo wa kidini, Uislamu umeweka wigo wa haki nyingi na taratibu za wote na huruma na maadili mema, ongezea mfumo wake wa kikanuni, bali ni kuwa haki katika Uislamu haishii kwa mwanadamu bali hata kwa mnyama.

Maiko: Sikudhania kuwa mnyama ana haki katika dini yenu.

Rashidi: Uislamu umekataza kuudhiwa kwa mnyama, na imekatazwa kuuwawa kwa ajili ya burudani kama inavyotokea katika kulenga shabaha au katika mieleka, na achinjwe kwa kuliwa tu, na pindi Muislamu anapofanya hivyo, basi anatakiwa afanye hivyo kwa ruhusa ya Muumba wake, kwa jina lake, na kwa sheria aliyo wawekea, kama ambavyo hilo lina adabu zinachungwa kwa ajili ya mnyama achinjwae, ambalo hatulioni wakati wa mtu kumchinja mtu mwenzake pindi wanapopetuka mfumo wa Mwenyezi Mungu, kisu hakinolewi mbele yake, wala mwingine hachinjwi mbele yake…Je unadhani dini yenye kumpa mnyama haki hiyo itamnyima mwanadamu?!

Rajev: Nadhani jambo hili linahitaji ufafanuzi zaidi kupitia vikao vingine.

Haki za Mwanadamu Katika Uislamu

www.path-2-happiness.com

Haki za Mwanadamu Katika Uislamu

Rashidi: Rashidi alipofungua laptop yake na kuingia katika chumba cha mazungumzo alipata barua kutoka kwa Maiko ikisema: “Jitayarishe kwa kikao kijacho kuna masuala muhimu tuyajadili: Muamala na watu wengine, uzimaji wa mfadhaiko, uhuru wa fikra…kwa heri.”

Rashidi: Aliwakuta rafiki zake chumbani, aliwasalimu kisha akaanza kuzungumza:

Masuala yanayohusiana na haki za binadamu ni mengi wala hayaishi: katika uliyoyataja peke yake rafiki yangu Maiko–na hili linanipelekea kuweka mipaka ya jumla ambayo kwayo tunaweza kufahamu masuala haya, vyovyote itakavyotofautiana au kuwa mbali.

Maiko: Si vibaya kupiga baadhi ya mifano; kama yale niliyokutajia katika barua yangu kwako; ili mazungumzo yetu yawe ya vitendo zaidi ambayo yanaweza kutekelezeka.

Rashidi: Sawa kabisa, hamna neno.

Rajev: Umetutajia katika kikao chetu kilichopita kanuni ambayo tunaweza kuanza nayo, nayo ni kuwa ikiwa kweli tutataka kurejea haki hizi na uhuru basi na tuchunguze maadili ambayo yamesimamishwa juu yake na sio utekelezaji na matendo ya wafuasi wake.

Rashidi: Sahihi….ufahamu wa maadili ya ’uhuru’ haki za binadamu zimepakwa uzoefu (background) na mawazo na fikra ambazo haki hizi zimetolewa, na kuwa chini ya mfumo wa kimaadii wa jumla wa kijamii ambao umekuwa kutokana nayo..na hapa namuuliza rafiki yangu Maiko Je, anaweza kutuwekea wazi uzoefu wa kifikra na mfumo wa kimaadili wa Ki-Magharibi ambao haki za kibinadamu hizi zimesimama juu yake?

Maiko: Tunaweza kusema: Wasifu na mipaka ya kifikra na kimaadili ambazo uhuru na haki za kibinadamu katika mangaribi zinatokana na;

1-Akili, ambayo ndio marejeo ya haki hizi na uhuru huu, hata kama akili hii itachukuwa baadhi ya maadili ya kidini–(kama vile walivyoathiriwa Waliberali (wenye kupenda mabadiliko) na Waprotestant) lakini akili ndio inayobaki kuwa hakimu wa maadili haya kwa kukubali au kukataa.

2-Usekula (kutenganisha dini na maisha na dola); huu ni mfumo ambao ndani yake kunapangika haki hizi na uhuru.

3-‘Uhuru’ na ’Usawa’; ndio maadili ya juu kabisa ya jamii ambayo maadili mengine yoyote ya jamii yapo chini yake, nayo ni ‘tuli’ na ‘matukufu’ambayo hayawezi kuguswa.

4-Hadhi ya mtu na maslahi yake kuwa juu, pamoja na kutopuuza nafasi ya jamii na maslahi yake, yanayopelekea furaha na kuyapendezesha maisha ya mtu.

Rashidi: Maelezo mazuri kabisa, nakushukuru kwa hilo; kama ni hivyo: Ni wazi kuwa Rejea za Magharibi- (baada ya kutengana na Kanisa katika nyanja za maisha) ilielekea kwenye akili achilia mbali hisia za kimajaribio, na kutokana na rejea hizi kumechimbuka haki na uhuru, na ni wazi kuwa mfumo ambao ulianzisha haki hizi na uhuru huu ni Usekula.

Tunaweza kusema vile vile: Kuwa ‘uhuru’ na ‘usawa’ umekamata kileleni katika rejea hizi za Magharibi: Hivyo basi kufanikisha maadili haya (kulingana na mtazamo uliotulia wa Magharibi) yana kipaumbele halisi ambayo yanafaa kuwa chini yake, au kujifunga nayo, au unapangika juu yake maadili mengineyo ya jamii, kutokea hapa: ‘Uhuru’ na ‘usawa’ umekuwa ndio tuli na matukufu yaliyo kileleni kabisa ambayo hayawezi kuguswa kabisa, ambayo yanawezekana (vile vile) kutoa mhanga maadili mengine na haki zingine kwa ajili ya kuzihifadhi.

Na hii ndio tofauti ya msingi na ule uzoefu wa Uislamu na mfumo wake ambao umebeba maneno au istilahi kama hizo.

Rajev: Ili tuweze kulinganisha, tuwekee mipaka ya kifikra na maadili ambayo anga yake istilahi hizi zinaogelea (Haki za binadamu) katika Uislamu.

Rashidi: Katika Uislamu na (Jamii ya Kiislamu) kuna mfumo tofauti kabisa.

Kwanza: mkabala na (akili) na (hisia za majaribio) tunakuta katika Uislamu kuwa (wahyi) ni marejeo ya kwanza ya misingi na maadili ambayo huchimbuka kutoka humo ‘tuli’ na ‘matukufu’ yake, pamoja na kutopuuza umuhimu wa marejeo ya maarifa ya akili na hisia katika nyanja zake….

Pili: na mkabala wa (usekula) tunapata katika Uislamu (sheria) na kupangika dunia na dini pamoja nao kuna mifumo ambayo jamii hii inasimama.

www.path-2-happiness.com

Tatu: na mkabala wa 'Uhuru' na 'Usawa' tunakuta katika Uislamu kuwa kuna 'Uja' wa Mwenyezi Mungu na 'uadilifu' kati ya wanadamu (na uadilifu hauna maana ya usawa kama wanavyofahamu baadhi ya watu). Na zinastawi juu ya kilele cha maadili ya jamii ya Kiislamu, na kuhakiki maadili haya na kutoyachezea ndio kipaumbele ambacho mtu anapaswa akinyenyekee au kujifunga nacho au kupangika maadili mengine ya jamii pamoja nacho pamoja na haki za uhuru ulionao.

Nne: na mkabala na 'Ubinafsi' tunapata katika Uislamu kupokezana majukumu kati ya mtu na jamii, na maingiliano baina yao bila ya dhuluma au mmoja kupetuka na kumdhulumu mwingine.

Rajev: Huenda tukaachana na taswira hizi mbili juu ya baadhi ya haki ambazo watu wanatofautiana ili sura hii iwe wazi zaidi.

Maiko: Tunaweza kuainisha maudhui ya uhuru wa kuabudu ili kulinganisha kati ya taswira mbili hizi, yaani ya Uislamu na ya Umagharibi, kulingana na uzoefu wa kimaadili wa kila mfumo, ambao ndani yake kunatoka haki za binadamu za kila mfumo katika mifumo hii miwili.

Rashidi: Uhuru wa kuabudu au (uhuru wa kushika dini) ni eneo pana kivitendo na kuoanisha, na hii ni maudhui yanayorejea kwenye kutofautiana na ufahamu wa chini na mafungamano yake na utukufu wa maadili katika mifumo miwili hii.

(Mathalani) katika nchi za Magharibi ni haki ya kila mtu kufuata dini au kuwa mpagani au kubadilisha dini yake; kwani hilo linaingia katika mipaka ya haki ya 'Uhuru wa kuabudu', nayo ni haki 'binafsi ya mtu mmoja mmoja' haipasi kumuingilia.

Lakini wakati huo huo tunamuona Muislamu katika nchi za Magharibi, (Kinadharia) kuwa anaweza 'kuamini na kuabudu' anachokitaka…. isipokuwa hana haki ya kutumia uhuru wake kutekeleza anayoyaamini; yaani haruhusiwi na si haki ya Muislamu kutekeleza dini yake katika maisha yake; kwa mfano hukatazwa kuchinja kisheria (zaidi ya nchi moja amri hiyo ipo), kadhalika anakatazwa kuoa zaidi ya mke mmoja katika baadhi za nchi mwanamke hukatazwa kuvaa Hijab–nguo aliyoamrishwa kuvaa na dini yake, na matendo haya ni sehemu ya dini ya Muislamu…. Je,unaweza kufasiri hilo?

Maiko: Kwa sababu matendo hayo yameondoka katika mipaka (mapenzi na dhamira ya mtu), ikiwa imetoka kwenye haki yake katika (uhuru wa kuabudu); na kwa hivyo hilo ni kuvunja sheria na mkataba wa jamii na mfumo ambao umeridhiwa na watu wengi, ambao umehukumu kutenganisha dini na mambo ya maisha.

Lakini kwa wakati huo huo ninakutuliza ya kuwa inaruhusiwa kwa Muislamu huyu kisheria kuishi na wanawake wengine nje ya mipaka ya taasisi ya ndoa, madamu hilo litatimia kwa ridhaa yao na sio katika kitanda cha wanandoa.

Rashidi: Lakini matendo haya yamehalalishwa kisheria kinyume na dini yake ambayo anaamini na kujinasibisha nayo!

Bila shaka ninafahamu kuwa nyie hamuhesabu vifungo hivi kuwa ni kuvunja haki na uhuru, kwa sababu hampati uhusiano kati ya matendo haya na dini, bali mnazingatia kuzuia na kubana himaya ya mapato yenu ya kimaendeleo ambayo yamekuwa ni tuli tukufu zinazodhibitiwa.

Na muradi wa hilo ni taswira ya (Itikadi au dini) imekuja ikiwa imelandana pamoja na mtazamo wa Kimagharibi (Kisekula) wa dini, ambao unajitenga na maisha; hivyo basi dini kulingana na mfumo huu haina uhusiano na utaratibu wa jamii, lakini mapenzi au dhamira anayoihifadhi ndani ya nafsi yake, naye kwa hilo atengane moja kwa moja na matendo ya maisha, kama ulivyotangulia kuelezea.

Rajev: Sasa nimeanza kufahamu mtazamo wa Kiislamu.

Rashidi: Katika taswira ya Kiislamu 'uhuru wa kuabudu' umedhaminiwa 'katika mipaka' ya kuchunga 'tuli' za juu za jamii hii (uja na dunia ni kwa ajili ya Mungu Mtukuka), na kwa hilo: Jamii ya Kiislamu inakubali kumuingiza chini ya mwavuli wake kila mwenye kutangaza kukubali kwake utawala wa Mungu juu yake kwa ujumla, na kutengwa kila mwenye kutangaza uasi na kutoka katika utawala huu, na hapa ndipo jamii ya Kiislamu ilipopanuka kwa kuingiza matangamano na wafuasi wa dini nyingi ndani yake, pale ulipokubali kuishi pamoja na wenye kufuata Uyahudi, Ukristo na kuwaachia uhuru wa kuratibu mambo yao binafsi, wakati ambapo hilo halikutokea kwenye dini zingine za kipagani na hilo ni kwa sababu Uyahudi na Ukristo ni dini mbili zenye asili ya mbinguni na wao wanatangaza kuwa chini ya mwavuli ule wa uja ule kwa ujumla.

Lakini upotofu uliojitokeza kwa dini zile mbili kulingana na Uislamu (ni mgongano wa ukweli wa na uja wa Allah) ambao unafanya mzunguko 'uhuru wa kujieleza' kuwa mdogo zaidi kuliko unafanya mzunguko 'uhuru

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

wa kujieleza' kuwa mdogo zaidi kuliko mzunguko wa 'uhuru wa itikadi', hivyo basi si halali kwao kulingania dini zao, wala kudhihirisha alama za dini zao (zinazoelezea upotofu wao) nje ya mzunguko wa wafuasi wao; hivyo 'uhuru wa kuabudu' kutoka katika mzunguko huu huvunja utaratibu wa jamii na huvunja tuli za msingi na matukufu ya mwanzo katika kilele cha maadili ya kijamii.

Maiko: Na vipi kuhusu Uislamu kuwakataza watu kubadilisha dini?

Rashidi: Hili nalo linahusiana vile vile na nililolitaja; suala la murtadi (aliyeacha Uislamu) linahusiana na taswira kuhusu 'uhuru wa kuabudu' kulingana na taswira ya Uislamu; wakati ambapo Uislamu haumuadhibu ambaye hajaingia kabisa, wala haumlazimishi yeyote kuingia ndani ya imani yake: "Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua." (2:265), "Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae…."(18:29), "Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu. " (109:6) tunaona kuwa wakati huo huo unamkataza na kumuadhibu mwenye kuhama kwenda kwenye dini nyingine.

Tunaweza kufahamu msimamo wa Uislamu kwa murtadi, katika mazingira ambayo kuhama kule huzingatiwa kuwa ni kukosoa maadili ya juu zaidi ya msingi ambayo jamii imesimamishwa juu yake, au kwa lugha nyingine: Hilo huchukuliwa kuukosoa ukweli wa dini hii, au mwanadamu kutokuwa na haja nayo, na hilo halikubaliwi katika jamiii ambayo inategemea sheria yake na marejeo yake katika kuamini ukweli wa dini hii na haja ya mwanadamu kwa dini hii.

Mfano huu ni kutokea mtu katika nchi za Magharibi akataka kubomoa tuli za uhuru na matukufu na kuyaangusha, kidogo kidogo majibu yake atayapata mara moja kwa wafuasi wa uhuru huu, nao ni kunyanyua kauli mbiu: Hakuna uhuru kwa uadui wa uhuru; na hiyo ni kwa sababu matakwa haya yatatumia uhuru kuwa uhuru, yaani kuangamiza maadili ya juu na ya msingi ambayo jamii hiyo imesimamishwa.

Maiko: Nakushukuru Rashidi kwa ufafanuzi huu...nimefurahishwa na mijadala hii, ninatamani iendelee.

Samahani Kidogo

www.path-2-happiness.com

Samahani Kidogo

Maiko: Tuna dakika kumi hadi hivi sasa hajafika Rashidi…jambo la ajabu.

Rajev: Sahihi, hili litatuathiri katika ahadi zingine.

Baada ya muda si mrefu Rashidi anaingia chumba cha mjadala, na kuanza kuwasalimu rafiki zake wawili, kisha akaanza kusema:

-Samahani kwa kuchelewa kufika, kuna baadhi ya majukumu ambayo nilikuwa nayakamilisha, na ilikuwa vigumu kuyaacha au kuyaakhirisha.

Maiko: Bwana Rashidi niruhusu niseme: Hii ni tabia iliyokuwa mashuhuri kwa Waarabu na Waislamu kwa ujumla, wakati hauna hadhi kwenu, samahani kama ukweli huu utakukera.

Rashidi: Mengi uliyoyasema ni sahihi, ukweli ni kuwa tumezikosea nafsi zetu na tumetoa hisia mbaya kwa wengine dhidi yetu… hata hivyo nasahihisha kosa la tabia hizi mbaya mtu kuzinasibisha na Uislamu.

Maiko: Kama sio kutokana na Uislamu basi zitakuwa kutokana na nini? Mimi naona wengi wenye tabia hizi ni watu kutoka katika nchi zenu.

Rashidi: Kuna tofauti mbili muhimu kati ya watu wenu na watu wetu: Utamaduni na mazingira…ukweli ni kuwa ni mazingira na sio Uislamu ndio wenye kuwajibika na tabia kama hizi.

Rajev: Ni vipi hilo, jambo la lazima ni kuwa dini ndio ambayo inatengeneza muongozo muhimu wa utamaduni wenu?!

Rashidi: Hili ni kweli kabisa, lakini ukweli ni kuwa Waislamu wengi leo hii hawafuati mafundisho ya dini yao, ama ni kutokana na ujinga wao kwa mafundisho ya dini yao au ni kwa kupuuzia, na pindi athari ya dini na akida inapopungua kwa mwanadamu basi wakati huo huwa chini ya taathira ya mazingira yanayo mzunguka.

Maiko: Ni nini athari ya mazingira tunayozungumzia?

Rashidi: Nitakubainishia: Kwa mfano katika nchi zenu tokea zamani mlikuwa mkiishi katika hali ya hewa ya baridi sana, na kanuni ya kubaki na kupambana na mazingira imewafanya nyinyi kufanyia mahesabu athari ya hali hii ya hewa, na hivyo mkahifadhi chakula chenu kwa ajili ya nyakati za baridi, na mkakusanya kuni au mafuta ili mjitayarishe kukabiliana na wakati wa baridi….Vivyo hivyo mazingira yamewataka hata kabla ya kufikiria na kupanga kufuata aina fulani za tabia zinazokwenda pamoja na wakati wenyewe.

Ama katika nchi zetu zipo katika nchi zenye hali ya hewa ya wastani au joto la wastani, sifa zake ni kuwa na wastani wa hali ya hewa kwa mwaka mzima, vivyo hivyo kupatikana kwa mavuno yake na utajiri wake, hivyo juhudi za watu wake zikawa ni ndogo na hesabu za watu wake ni chache na mipango yake inatosheleza kuendelea kwa maisha; ikaathiri tabia za watu wa maeneo hayo wakamili katika kudeka (au kwa uchache sema ni: uvivu na uzembe (ambao husaidiwa na hali ya hewa ya joto) na hawakuhisi kuwa kutokuwa makini na kutoweza kusoma alama za nyakati ambazo zinaathiri kubaki kwao na kupambana kwao na mazingira.

Rajev: Hapana shaka kuwa mazingira yana athari kubwa kwa mwanadamu, na kupambana na athari zake huhitajia athari kubwa zaidi yake, Je, Uislamu haukuweza kubadilisha athari hii hasi ya kimazingira kwa kutojali mambo haya, au kwa kutoweza?

Rashidi: Ama kutoweza, hili lina sababu nyingi na hii si sehemu yake ya kulijadili, hata hivyo kwa ujumla tunaweza kusema kuwa Uislamu umeweza kutengeneza jamii zilizorejea kwake, kama ilivyoweza kupanga maisha ya wafuasi wake muda wowote ule, kuna mifano mingi katika eneo hili.

www.path-2-happiness.com

Maiko: Je unaweza kututajia baadhi tu ya mifano hii?

Rashidi: Kuna mifano mingi, miongoni mwayo ni:

Imehadithiwa kuwa ‘Ammarah bin Khuzaimat bin Thabit kuwa alimsikia Khalifa Umar bin Al-Khattwab akimwambia baba yake Khuzaymah: “Nini kinachokuzuia kulima ardhi yako?” Baba yangu akamwambia: “Mimi ni mtu mzima nitakaye kufa kesho.” ‘Umar akamwambia: “Nakulazimisha wewe kuwa utailima.” ‘Ammarah akasema: “Nilimuona ‘Umar akilima kwa mikono yake pamoja na baba yangu.” Sahaba ‘Abdullah bin Mas’ud amesema: “Mimi namchukia mtu ninayemuona ana faragha, hana chochote katika amali za dunia na amali za akhera.” na ‘Abdur-Rahman Ibn Al-Imam Abi Hatim Ar-Razi amesema; (akielezea hali ya baba yake): “Huenda alikuwa akila na ninamsomea, na akitembea na mimi ninamsomea na akiingia maliwatoni na mimi ninamsomea na akiingia nyumbani kutaka kitu na mimi ninamsomea.”

Rajev: Lakini, je, Uislamu umelipa umuhimu suala la matumizi ya wakati katika mafundisho yake, ili tupate maelekezo yake yaliyofuatwa katika zama zozote?

Rashidi: Ndio, Uislamu umetukuza sana suala la wakati na umuhimu wake umo katika kitabu (Qur’an) na Sunnah (mafundisho ya Mtume). Mwenye kupitia Qur’an na uongofu kutoka kwa Nabii wa Uislamu na katika sira ya masahaba (wafuasi wake) na Tabiuun (wafuasi wa wafuasi wa Mtume Muhammad)……Ataona hadhi ya juu iliyopewa matumizi ya wakati na kuheshimu ahadi katika hali zote, na mifano ya miongozo hiyo; ni Kuwa Allah aliyetukuka ameapa ndani ya kitabu chake zaidi ya mara moja kwa nyakati maalumu, amesema: “Naapa kwa alfajiri, Na kwa masiku kumi, Na kwa viwili viwili na kimoja kimoja, Na kwa usiku unapo pita,”(891-4)

“Naapa kwa usiku unapo funika! Na mchana unapo dhihiri! ” (92:1-2)

“Naapa kwa Zama! Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara, Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri. ”(103:1-3)

Na akaashiria kuwa katika ayah zake ni kuumba jua, mwezi, ili tuweze kujua idadi ya miaka na hesabu.

-Na hayo yote yamefanyiwa kazi katika ibada nyingi za Kiislamu; ibada zote zimehusishwa na wakati, mwanzo na mwisho, bali wakati ulioainishwa kwa kila ibada zina shuruti katika masharti ya kukubaliwa kwake na kusihi kwake, ndio maana sheria ya Uislamu ikalipa umuhimu sana jambo hili, nao ni kuuheshimu na kujipamba nao kama sharti ya kukubaliwa kwa ibada ile, mathalan Allah Tabaaraka anasema:

“Mkisha sali basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu mkisimama, na mkikaa, na mnapo jinyoosha kwa kulala. Na mtapo tulia basi shikeni Sala kama dasturi. Kwani hakika Sala kwa Waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalumu.”(4:103); kwa hivyo swala ambayo ndio nguzo ya dini huugawa mchana na usiku katika mafungu yenye miadi thabiti na alama zilizo wazi, vivyo hivyo nguzo zingine za Kiislamu zilizobakia: Funga ina muda maalumu katika mwaka, na kwa wakati wake Waislamu wanafuata utaratibu maalumu kila siku, vivyo hivyo Zaka ambayo ni mfumo na utaratibu wa kiuchumi na wa kijamii–ambao upo chini ya muda maalumu na makadirio maalumu, na vivyo hivyo tunaona kwenye ibada ya Hijja.

Wakati katika sunnah ya Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) una ushahidi mwingi ambapo sunnah imetilia umuhimu kama ilivyo Qur’an. Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) ametukuza heshima ya kutekeleza ahadi, nayo inangia katika jumla ya kauli yake: “na Waislamu wapo katika shuruti zao.” Hivyo kuainisha muda maalumu wa mkutano au kikao kunashurutishwa kila mtu mwenyewe kujilazimisha na ahadi

www.path-2-happiness.com

hiyo, akihalifu basi atakuwa amekwenda kinyume na alichojishurutisha katika nafsi yake, na Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) amefanya kwenda kinyume na ahadi ni sifa ya unafiki, Mtume amesema: “Alama za mnafiki ni tatu: Anapozungumza husema uongo, anapotoa ahadi huenda kinyume, na akiaminiwa hufanya khiana.” Hivyo mtu huyu aliyechelewa na kwenda kinyume na ahadi basi atakuwa amekwenda kinyume na ahadi ile.

Maiko: Lakini umuhimu wa wakati ni jambo lenye ushirika baina ya jamii, tamaduni na staarabu nyingi, kama ni hivyo Uislamu umeongeza nini?

Rashidi: Uislamu umeongeza thamani ya matumizi ya wakati na kuupangilia katika mapana matatu ya msingi: Kwanza: Huo ni ukomo, kwa hiyo wakati ni kitu kizuri na chenye thamani zaidi anacho miliki mwanadamu, hayo ni maisha yake, wala haiwezekani kuutanguliza au kuuchelewesha au kuuzidisha, na akiupoteza hautarajiwi kurudi kwake, na ndio maana Uislamu ukahimiza kuutumia wakati wake vizuri hadi ukomo wa mwisho, nao ni mwisho wa maisha ya mwanadamu, bali umemhusisha baada ya kifo chake na baada ya kufufuka na kuhesabiwa siku ya kiama, kama ambavyo Uislamu umemhimiza Muislamu kufaidika sana na wakati hata katika mazingira magumu kabisa; Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: “Ikisimama kiama na katika mkono wa mmoja wenu kuna mche na akaweza kuupanda kabla ya kusimama basi na afanye hivyo.”

Pili, nao ni: Kulazimika, Uislamu umefanya thamani ya kuwekeza wakati na kuupangilia ni kufuata na kuzingatia kuwa mpango huu na kuwekeza huku si hiari kwa Muislamu, bali ni lazima kwake, na hii inatokana na kuwa umri wake (ambao ndio kiasi cha muda wa kazi yake) pengine sio miliki yake halisi, bali ni hiba toka kwa Mungu wake ili auwekeze katika lile ambalo Mola wake analiridhia katika njia bora zaidi; na hapa Uislamu umeufanya muda kuwa Rasilimali ambayo mwanadamu atahesabiwa na kuulizwa namna alivyoutumia pale Mtume wa Allah aliposema: “Hauondoki mguu wa mja Siku ya Kiama hadi aulizwe mambo matano; Umri wake namna alivyoutumia….” Na akasema tena Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam): “Neema mbili zimepunjwa ndani yake kuna watu wengi; siha na faragha.” Na akasema: “Wahi matano kabla ya matano: Uhai wako kabla ya mauti yako, afya yako kabla ya maradhi yako na fursa yako kabla ya kushughulika kwako, na ujana wako kabla ya uzee wako, na utajiri wako kabla ya kufukarika kwako.”

Hapana shaka kuwa mtu ataulizwa zaidi pindi rasilimali yake inapozidi; Allah Ta’ala amesema: “Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale tuliyo kuwa tukiyafanya. Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani walio dhulumu hawana wa kuwanusuru.” (Fatir, 35:37) na Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: “Mwenyezi Mungu atachelewesha ajali (kifo) ya mja hadi atakapofikia umri wa miaka sitini.” Na imepokewa kutoka kwa Hassan Al-Basry (Allah Amrehemu) kuwa amesema: “Ewe Mwanadamu, wewe ni masiku, kila siku itakapoondoka basi na baadhi yako huondoka.” Na hii “Baadhi” hufanyika katika masaa, dakika na sekunde…kila dakika au sekunde huondoka na baadhi yako, hivyo basi wakati ni uhai.

Mapana ya tatu: Ni Ufufuo na malipo ya thamani hii, hivyo basi wakati ni katika mabadiliko ya nje, ambayo ni vigumu kwa mtu mwenyewe kuwa na utawala wake, au uwezo wa kuutawala, na kwa ajili hiyo Uislamu umeweka vichocheo vya ndani ya Muislamu ambavyo vitakuwa juu ya vichocheo hivi na misukumo ya kimaada, na hapa unakuja umuhimu wa kuchunguza dhamira kwa mazingatio kuwa ni kipengele cha msingi cha kudhibiti mpaka wa chini kabisa unaokubaliwa katika utoaji. Hivyo

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

basi uchunguzi/ulinzi wa dhati ya mtu katika Uislamu huwa ni khofu ya kuhesabiwa na Muumba, na kutamani thawabu zake na hili ndilo linalomfanya Muislamu kutumia wakati wake katika yenye kumfaa yeye pamoja na ummah wake.

Maiko: Dini hii ni ya ajabu sana, inaingilia kila kitu katika maisha ya mwanadamu, wala haimuachii mwanadamu uchaguzi hata katika maisha yake binafsi.

Rashidi: Hapana, yeye hutoa wasaa kwa mambo anuwai na khiari za kibinadamu, na hauachi nafasi kusongwa na mifumo mingine isipokuwa kwa mfumo wake tu, na hili linawiana na mtazamo wa Uislamu kuhusu mwanadamu, ulimwengu na maisha ambayo mifano yake imetolewa huko nyuma.

Hivyo basi Uislamu unaangalia thamani (wakati) sio tu kwa kuwekeza kwa upande wa kimaada, ambapo unaingia katika upande wa utawala au wa kiuchumi, bali mtazamo wake unakwenda zaidi ya hapo. Mwanadamu kwa mtazamo wa Uislamu kabla ya kuwa mwanazuoni au mzalishaji katika makonde ya kidunia au ya kimaada anakuwa Muislamu anayeongozwa, anayeogopa adhabu ya Allah na kutaraji malipo yake, na humchunga Allah katika matendo na maneno yake yote; hivyo basi matumizi ya wakati wake na kuupangilia katika Uislamu haina maana kuwa ni fikra tupu tu, lengo lake si kutumia wakati kwa lengo la kutumia wakati tu kwa kuzidisha faida yake ya kimaada na uzalishaji pekee, bali ni zaidi ya hapo! Kwa kuwa hilo ni lengo la kiroho ambalo linatokana na khofu ya siku ya kiama, siku ya hesabu na adhabu.

Rajev: Nina maneno mengine yenye kuhusiana na tabia za Waislamu, lakini ni bora niakhirishe hadi kwenye kikao kijacho.

Tafadhali Niruhusu

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Tafadhali Niruhusu

Kabla ya muda wa kikao chao baina ya marafiki watatu Rashidi alikuwa tayari na kompyuta yake akimsubiri Rajev na Maiko, baada ya muda mdogo walikuja hali ya kuwa wanafuatana, baada ya kusalimiana tu, Rashidi akaanza kuzungumza:

-Katika kikao chetu kilichopita Rajev ulisema kuwa kuna maneno unataka kusema yanayohusiana na baadhi ya tabia za Waislamu kinyume na maudhui ya kutimiza miadi.

Rajev: Naam, kinachoonekana ni kuwa kukosekana kuchunga kwenu misingi ya kuamiliana na wengine haiishi tu katika kutimiza ahadi, bali linaendelea katika nyanja zingine katika fani ya kuishi na watu.

Rashidi: Vipi hilo? Je, umeona kwangu kukosa adabu au kupetuka katika muamala nanyi?

Rajev: Hapana, hapana, samahani, sikukukusudia wewe mwenyewe, lakini hii ni hali halisi inayoonekana kwa sifa ya jumla; kulingana na matembezi yangu katika moja ya hoteli nimeona bango limeandikwa juu yake; “Marufuku kuingia mbwa na Mwarabu!” “Nilipochukizwa na bango lile nilimuuliza mwenye hoteli sababu ya kuandika vile, akaniambia kuwa hoteli yake ni ya kifahari, ni ya hadhi ya juu ambayo wanaingia ndani yake mawaziri na watu wakubwa, na ilitokea wakawapokea vijana wa Kiarabu siku za nyuma, lakini matendo waliyofanya hayakuwa mazuri na yanayowachukiza wateja wa hoteli ile.

Mara moja kundi la vijana wa kiarabu likapangua meza kwa utashi wao na kuwalazimisha wafanyakazi; kilichosababisha fujo na usumbufu hotelini.

Wakati mwingine ugomvi ukazuka miongoni mwao na wakawa wanagombana kwa sauti ya juu kabisa.

Na baadhi yao wakawa wanaosha vidole vyao kwenye sahani katika namna yenye kuchukiza kitendo kilichowaingizia kinyaa watu wengine.

-Bali wengine walikuwa wakijikuna migongo yao kwa umma na kisu.

Na yule mwenye mgahawa akasema kuwa, amepoteza wateja wengi wakubwa kwa sababu ya tabia zao mbaya; akaamua kuweka mpaka wa jambo hili nalo ni kuwakataza Waarabu kuingia katika mgahawa wake.

Rashidi: Mengi uliyoyasema ni sahihi, lakini kama nilivyokuambieni hapo kabla: sisi tumezikosea nafsi zetu kwa matendo yetu na tumewapa wengine fikra mbaya kutuhusu…lakini kwa mara nyingine ninasahihisha kosa hili lisinasibishwe na Uislamu.

Maiko: Huenda kosa hili nalo ukalirejesha katika taathira ya mazingira?!

Rashidi: Bila shaka, siwezi kuacha fikra ya nafasi ya mazingira na malezi mabaya waliyokulia vijana hao.

Maiko: Mimi najua athari za malezi, lakini sifahamu athari za mazingira katika mambo kama haya!

Rashidi: Nitakupatia mfano upate kujua athari yake; Nyie mnaishi katika nchi zenye kufahamika kuwa ni sehemu zenye baridi kali ambapo mvua nyingi hunyesha na barafu kudondoka na kuvuma kwa upepo mkali wenye baridi, na katika hali ya namna hii ya hewa mtu hawezi kuishi bila ya kufanya mahesabu vizuri ya mazingira haya na kuyawekea mbadala wa kukabiliana nayo. Hivyo basi, hapana budi kupanga makazi vizuri, na miundo mbinu katika njia inayochunga mazingira haya, na wakati wa kutekeleza kwake unatakiwa uwe makini, mathalani ni lazima kutengeneza paa na madirisha kwa umakini mno ili maji yasipite na kuingia, hata upepo wa baridi vile vile, hapana budi kuchunga mazingira haya katika kutengeneza na kuweka mfumo wa kupasha joto nyumba unaofaa, na matayarisho ya kuweka mahitaji yote na vifaa ya kupasha joto nyumba… yote yanatengeneza tabia ya kuwa makini na kupangilia vizuri mambo.

Wakati katika nchi zetu hakuna mazingira haya magumu ya hali ya hewa, hivyo mwanadamu hahisi hoja ya tabia hizi ili abakie kuwa hai, na akiacha hivyo aathirike na mazingira yake basi fujo itaenea na itakuwa ndio sifa ya maisha ya watu wake, na usisahau kuwa mazingira yetu ambayo kwa ukubwa wake ni tabia za majangwani na kubeba tabia ya ukavu ambayo huenda ikahamia katika ukavu wa hisia za watu.

Rajev: Kama ni hivyo. Je, tutamuachia mtu huyu awe chini ya utawala wa mazingira yake, bila kurekebisha tabia yake wala kupangilia maisha yake, na aendelee kuishi maisha ya fujo na asiweze kuishi vizuri na watu?

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rashidi: Sivyo hivyo kabisa, nilitaka kuwaambia jambo hili na uchambuzi huu ili kujaribu kuwafahamisha sababu ya kweli ya hayo tuyaonayo.

Rajev: Tukipata tofauti kati ya mataifa ya Ki-magharibi na yale ya Mashariki au ya Kiislamu katika mazingira ya hali ya hewa, tutaona vile vile tofauti katika dini ambayo inatawala; kwa nini basi Uislamu vile vile usiwe ni sababu ya hali hii tunayoiona?!

Rashidi: Uislamu umepanga maisha ya Muislamu na wakati wake; ili ufanye amali yake yote kuwa ibada kwa Allah Mtukuka kwa mtazamo mpana wa ibada ambao nimeshawaelezea hapo kabla; na wengine wanaweza wasifahamu kuwa zile nadharia za kutangamana na watu wengine (Etiquette) nyingi zinathibitisha kuwa fani hii inarejea kwenye dini hii ya Uislamu ambapo zimefika katika nchi za Uhispania kupitia Waislamu, na baada ya kuanguka kwake elimu hii ilichukuliwa na nchi nyingi, miongoni mwazo ni Ufaransa, Hispania, Uingereza na wakaiendeleza na kuongezea vipengele vingine na wakavipanga, hadi ikatufikia sisi kwa sura yake ya sasa.

Maiko: (Huku akicheka) nyie Waislamu mna kasumba sana na dini yenu na mnapenda kunasibisha kila kitu kizuri na dini yenu… sitokuambia unithibitishie hili, kwa kuwa nina jua hilo linahitajia utafiti mwingi mrefu, hata hivyo nitataka unithibitishie kuwa misingi hiyo ipo kwenye Uislamu.

Rashidi: Uislamu umerekebisha tabia ya mtu na maadili yake katika nyanja zote za maisha, na kuna misingi mingi kwenye Qur'an na Sunnah Tukufu ambayo tunaweza kuipanga katika nyanja za fani ya matangamano na watu (Etiquette).

Maiko: Haya ni maneno ya jumla sana rafiki yangu nitolee mfano uthibitishe ukisemacho.

Rashidi: Nitakupigia mfano ili nibainishe maneno yangu; tuangalie muamala wa Mtume (Swala llahu 'alayhi wasallam) pamoja na mke na watoto:

Tunapomuona mtu akimfungulia mtu mlango wa gari mke wake tunasema kuwa mtu yule amestaarabika, lakini Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) alikuwa anakaa ardhini na anaweka mikono yake na kumtaka mkewe asimame kwa miguu yake na apande ngamia.

Na muamala wa Mtume pamoja na wake zake, watoto wake na wafanyakazi wake ulikuwa wa huruma, uvumilivu na kumsamehe mnyonge. Wakati fulani Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) alikuwa amesujudu katika ardhi, na wakati huo akiwaongoza watu katika swala, akaja mmoja wa wajukuu zake wadogo na kumpandia mgongoni, Mtume hakutingishika hadi alipoteremka mgongoni mwake kwa kumchunga huyu mtoto.

Uislamu umelingania tabia ya kunyenyekea viumbe na upole, na Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) amesifika kwa hilo pamoja na kuwa Muhammad alikuwa ni Mtume mwenye kutukuzwa na wafuasi wake na alikuwa kiongozi wa dola, isipokuwa alikuwa mwenye sifa ya unyenyekevu mno, na miongoni mwa unyenyekevu wake alikuwa akiwasaidia wafanyakazi wake kufua nguo zake mwenyewe, na alikuwa hawabebeshi wafanyakazi wake yale wasiyoyaweza, na anawasaidia wakitaka chochote, pia alikuwa na tabia kama hiyo hata kwa wasio Waislamu, wakati fulani jeneza la Myahudi lilipita na yeye akasimama, waliposhangazwa waliokuwa pembezoni mwake aliwabainishia kuwa heshima ya maiti haitofuatishi kati ya watu.

Bali Uislamu umefungamanisha baina ya mwendo wa mtu na tabia zake, Qur'an imeweka misingi ya tabia njema hata katika kutembea, nayo ni kuwa mtu asinyanyue kichwa chake sana wakati anapotembea na kujikweza mbele za watu, wala asiiname chini kiasi cha kuonekana dhalili Mwenyezi Mungu amesema: "Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha. Na ushike mwendo wa katikati,..."(31: 18-19).

Rajev: Je, ukionana na yule bwana mwenye mgahawa unaweza kumpa sura hii kuliko ile aliyoiona kwa vijana wale?

Rashidi: Nitakutajia baadhi ya adabu za Kiislamu ambazo zinahusiana na niliyoyataja katika matendo mabaya ya vijana wale na wengineo katika sehemu hii au nyigineyo.

Miongoni mwa maadili haya: Uislamu umeamrisha kutoa salamu kwa wengine, na umetaka hilo lifanyike sana katika jamii, na ukaonesha kuwa ni sababu ya watu kupendana, na kujibu salamu ni jambo la wajibu kidini na sio tu jamii, kama ambavyo Uislamu umekataza kwa mwenye

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

kula ikiwa chakula kipo kinywani kutoa au kujibu salamu, vivyo hivyo kumsalimu aliyeanza kulala na kupunguza sauti kama watu wamelala.

Uislamu umechukizwa na mtu kupaza sauti bila ulazima: "…na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya kuliko zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda" (31:19), umemuita yule mtu anayemuita mwenzie kwa sauti kubwa nje ya nyumba yake kuwa hana akili;"Hakika hao wanao kuita nawe uko nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili. "(49:4)Na Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) hakuwahi kumfokea mtu wala kupaza sauti yake.

Uislamu umelingania usafi wa kudumu na kila sehemu: kwenye kikao, kwenye chakula, nyumbani, nje, na kuweka adabu ya kula na kunywa; na wakati huo watu walikuwa bado hawafahamu vifaa vya kulia kama vile vijiko na uma wala hakukuwa na sahani nyingi. Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) amekataza kula kwa kutumia vidole zaidi ya vitatu na amekataza kuzungusha mkono wa mlaji katika sahani, na kumuelekeza mtu kula kilichokuwa karibu nae, na asinywe maji kwa mkupuo mmoja bali mara tatu na kupumua baina yake wala asijaze tumbo lake kwa chakula na kunywa kupita kiasi….na ukachunga mipaka ya kijamii na ya kihisia ambayo yanaweza kutokea wakati wa kula, na hivyo ukafanya suala la kula kuwa ni mlango wa watu kuingiiana na kupendana kati yao, na ukapendelea mazungumzo wakati wa kula pamoja na mgeni wake ili asijihisi mpweke au kuona haya wakati wa kula. Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) alikuwa akimlisha mkewe kwa mikono yake mweyewe, na alikuwa akisema: "Sadaka bora ni tonge analoliweka mtu kwenye mdomo wa mke wake." Na Mtume alikuwa akinywa sehemu ile aliyoweka mdomo mke wake Aisha (Radhiya Llahu 'anha) na Uislamu umefungamanisha kati ya kula na ibada kwa Allah, na ukaamrisha kutajwa Allah wakati wa kula na kushukuru baada yake.

Maiko: Niache nikuambie Rashidi, kuna tofauti kubwa kati ya dini yenu na matendo yenu, na sisi tupo karibu ya mafunzo ya dini yenu katika nyanja hii kuliko nyie wenyewe.

Rashidi: Kwa masikitiko makubwa, maneno yako ni sahihi.

Tabia ya Qur'an

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Tabia ya Qur'an

Rajev: Alianza kuzungumza akielekeza maneno yake kwa Maiko na Rashidi akisema:

Mazungumzo yetu yaliyotangulia kuhusu baadhi ya tabia za Waislamu zinatusukuma kuzungumzia maadili katika Uislamu, je, hamuoni kuwa maudhui haya ni muhimu kuzungumzia?

Maiko: Ndio, mimi ninashangazwa na baadhi ya Waislamu, kwa upande nawaona wakiwa katika kiwango cha juu cha maadili mema, na kwa upande mwingine watu hao hao nawaona wakiwa na maadili ambayo hayalingani na sura ya kwanza.

Rashidi: Hili linarejea katika vipengele viwili: Kwanza: Mtazamo wako kuhusu maadili. Pili, Namna wanaofuata utaratibu na kutekeleza maadili fulani, tabia ya mtu fulani hudhihiri, vile vile athari ya mazingira na malezi kwa uwazi, achilia mbali kipengele cha kurithi kwa dhati ya mtu mwenyewe…hili ndilo aliloashiria mwenyewe Mtume wa Uislamu na kuthibitishwa na majaribio na utafiti wa kielimu na kisayansi.

Rajev: Laiti ukalielezea zaidi

Rashidi: Ishara hii tunaipata kwenye hadithi mbili za Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam): Ya kwanza: Mtume anamwambia mmoja wa sahaba zake kwa kauli yake: "Hakika ndani yako kuna tabia mbili azipendazo Mwenyezi Mungu na Mtume wake "uvumilivu na upole." Yule mfuasi wake akauliza, "ewe Mtume wa Mungu. Je, tabia hizo nimezitengeneza mimi au nimeumbwa nazo?" Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: "Bali Mwenyezi Mungu kakuumbia nazo?" Katika hadithi hii kuna uthibitisho kuwa uvumilivu na upole, anaweza kusifika nazo mtu kama tu ni vitu alivyoweza kuvirithi, yaani vipo katika jeni yake. Na katika Hadithi nyingine Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) anasema: "Hakika elimu ni kwa kujifunza na uvumilivu ni kwa kuvumilia, mwenye kuchagua kheri atapewa na mwenye kukwepa shari ataiepuka." Ndani yake kunathibitisha, kuwa yale maumbile ya uvumilivu (kwa yule mfuasi wa Mtume (Swala LLahu 'alayhi wasallam) ni ya kurithi inaweza kupatikana katika mazingira anayoishi mtu na hii inatokana kupitia malezi ambayo huchangia katika makuzi ya jamii.

Maiko: Hili linatupelekea katika upambanuzi wa kina wa kifalsafa na maelezo mengi, lakini bila kujali matatizo hayo ya kifalsafa, ningependa kwanza kutoa ripoti kuwa hisia za kitabia kwa mwanadamu ni hisia za kimaumbile, anabeba katika kupenda baadhi ya sifa na kuchukizwa na nyingine katika kila zama, kwani ukweli, amana uadilifu na kutekeleza ahadi yote hayo ndio aliyoyahesabu kuwa ndio ubinadamu katika sifa za kimaadili sahihi kwa kusifiwa katika zama zote (nyanja zote), utu haupendelei hadi hivi sasa, uongo, dhuluma, hiana na hadaa, vivyo hivyo hali ya kuliwazana, kuhurumiana, upaji (ukarimu) ukunjufu wa moyo na kusameheana.

Je, tunaweza kusema kuwa Uislamu unatofuatiana katika hilo na watu wote, Je, anaweza yoyote kudai kuwa Uislamu unamiliki mfumo wa kimaadili unaojitegemea uliopambanukana na mifumo mingine?

Rashidi: Pamoja na kuhifadhi mawazo yangu katika kukiri ukweli uliotaja, na madhumuni ya tabia njema na mapungufu ya kimaadili uliyoyataja, na naongeza katika maneno yako: Pamoja na hayo ikaibuka mifumo mingine ya kimaadili, si katika Uislamu tu, bali katika dini zote na mifumo mingine ya kijamii iliyotungwa na mwanadamu; kwani imetofuatiana kuainisha viwango vya uzuri na ubaya katika maadili na njia za kielimu katika kujua kheri na shari, na kwa sababu hazijaafikiana katika nguvu inayofanyakazi nyuma ya kanuni na kudumu juu yake, na sababu ya tofuati hii ni tofauti katika taswira ya ulimwengu huu na nafasi yake katika mfumo wake mpana na lengo la maisha juu yake.

Mathalani: Ubinafsi huchukuliwa ndio msingi wa nadharia nyingi za kimaadili huchukuliwa; katika karne ya mwamko (Renaissance) wa Ulaya Hobes na Spinoza walizungumza kwa nyakati tofauti kuwa hifadhi ya ya kubaki kwa dhati ndipo kheri inapolalia, kama ambavyo Freud kutokana na

maandishi yake ya mwanzo alitoa nadharia ambayo ndio inatengeneza tabia ya Wamagharibi wengi ambayo inatawaliw na mtazamo wa kuiridhia nafsi (self gratification). Mtazamo huu ambao umechukuliwa kuwa ni mtazamo wa msingi ukilinganisha na mitazamo mingine ya nafsi, ambapo uungwana na matendo mema huzingatiwa kuwa ni hali mbili zisizo za msingi zinapata taathira yake kwa kufungamanishwa na picha mbali mbali za kuiridhisha nafsi.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kwa mkabala wa tabia hizi za mtu mmoja mmoja maadili ambayo yanachukuliwa kutokana na jamii kuwa ni msingi wake, na ndipo zinapojengeka aina za maadili ambayo yanaonesha umuhimu wa kundi kuliko ule wa mtu binafsi.

Maiko: Tukisema kuwa Uislamu una miliki mfumo wa kimaadili uliopambanuka na mwingine, Je ni kwa misingi gani mfumo ule unasimama? Ni nini tabia na sifa zake?

Rashidi: Kama nilivyotaja kwenye mijadala iliyotangulia: Uislamu ni mfumo wa maisha, maisha ya mwanadamu ni ya uhalisia kwa kila nguzo yake; kama ulivyo ni mfumo ambao unajumuisha taswira ile ya kiitikadi na kuipa sura halisi yenye kujiweka kwenye maisha ya mwanadamu; kama vile taratibu za kimaadili na chemchem zitokazo hapo, na msingi ambao zinatokea juu yake, na utawala unaotegemea, na mfumo wa kisiasa, umbo lake na sifa zake, na mfumo wa kijamii na misingi yake ya uchumi, na falsafa yake na maumbo yake na mfumo wa kimataifa na mahusiano yake na mafungamano yake.

Na hili ndilo ambalo Dr. M. H. Durrani aliyekuwa kasisi wa Kanisa la England amelielezea kutokana na uzoefu wa maisha yake, kwa kauli yake:

Uislamu una mfumo wote wa kimaadili, ibada mbali mbali zimefaradhishwa kwa watu wenye malengo ya kimaadili… ina lengo la kumwongoza mtu kimaadili na kiroho kwa njia inayokubalika, kama ambavyo ina lenga kuisafisha akili yake na kuing'arisha, hivyo kuipa nguvu ili iweze kutekeleza majukumu yake kuelekea kwa wengine ambao wanaishi pamoja nawe, kwani Uislamu ni dini pekee kwa kuwa kwake ni nadharia na utekelezaji, mtu hatakiwi kuamini misingi na siri zilizojificha kama ilivyo hali ya dini ya Ukristo, kwani Uislamu unakubali nyanja za maisha ya kiroho na ya kimaada kwa wakati huo huo, na huweka yote katika sehemu yake inayohusika nayo, na husimamisha falsafa yake kwa misingi ya kushughulikia pande zote za tabia za mwanadamu.

Rajev: Tukihesabu kuwa huu ndio msingi ambao msingi wa mfumo wa Kiislamu unausimamia, ni muhimu kutaja sifa za mfumo huu na kitu muhimu kinacho upambanua na mwingine.

Rashidi: Tunaweza kukusanya sifa hizi za mfumo wa kimaadli wa Kiislamu kwa:-

Msingi wa kiakida (Kiitikadi): ambao ni kwamba, mwanadamu ni kiumbe mwenye kulelewa, na ya kuwa Muumba wake hujua zaidi yanayomfaa, na ya kuwa hakumuacha hivi hivi tu, bali amemtumia Mtume wake kufikisha mafundisho yake na wakimfahamisha mfumo wake, na ya kuwa mwanadamu huyu atafufuliwa baada ya mauti katika maisha yajayo ambapo atahesabiwa kwayo kwa aliyotanguliza miongoni mwa mambo ya kheri au ya shari katika maisha yake hapo duniani, na hili ni tofauti na maadili ya kisasa ya kimagharibi ambayo yametengana na dini pamoja na utengano wa elimu na maisha kutoka kwenye kanisa.

Tuli: Maadili ya Kiislamu yanaelezwa na misingi ya maadili thabiti na yanatokana na misingi na taswira thabiti ya mwanadamu na maisha na ulimwengu, nayo inaelekezwa kwa mwanadamu ambae ukweli wake haubadiliki, wala kiini chake kwa miaka mingi, hata kama itabadilika mazingira yanayoizunguka ya maisha na matukio,hivyo ukweli, uaminifu, uvumilivu utabakia kuwa ni matendo mema milele, na uongo, kusengenya, kuteta itabakia kuwa vitendo vibaya dahari yote, na matendo machafu yatabakia vivyo hivyo hayabadiliki hata kama yataenea kwa watu au yakaruhusiwa na baadhi ya mifumo, hata kama tabia na maisha ya watu yatabadilika.

Vya kupigiwa mfano pamoja na hali halisi: Ikiwa baadhi ya watu wanaona kuwa maadili ya Kiislamu ni ya kufikirika, isipokuwa ukweli wake wa kufikirika ni vya uhalisia ambao yanachunga hali halisi ya mwanadamu na nguvu zake, na hivyo kila mtu ana uwezo wa kuitekeleza na kwenda nao pamoja, haya ni maadili ambayo yanahifadhi maisha ya mtu kwa kuzingatia kuwa ni kiumbe kitukufu, na kufanya maisha yake yaendelee bila ya kupambana na vikwazo. Maadili hayagongani na tabia ya mwanadamu wala hayapingani, bali yatakamilika na kuishi pamoja; hivyo basi taswira ya Kiislamu ambayo ndani yake kuna sehemu ya uwekaji sheria ya maisha ambao Uyahudi umeujali sana na kuna upande wa kiroho ambao Ukristo umeuhimiza na hili ameliashiria mwandishi wa Kihindi Peggy Raderik kwa kauli yake:

"Kwa hakika mafundisho ya Uislamu ya kitabia yana hakikisha mchanganyiko timulifu baina ya kufikirika na uhalisia, na hivyo mwanadamu kuweza kwa maadili yake kumjua Mungu, na kuwa mtu wa

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Mungu wakati ambapo atakuwa ameshughulishwa na mambo ya maisha yake ya kila siku.”

Kujilazimisha (na kudumu katika hili): maana yake, mwanadamu kulinda na kushikamana na maadili haya katika kupambana na wanadamu wote, na hii ni kwa kuwa mwanadamu ni mwenye kuwajibishwa na maisha haya ya dunia, ana ujumbe, na anabeba majukumu, ana utashi ambao unahukumu matendo yake na ndio sababu ya malipo yake, hivyo basi suala la kushikamana na maadili ni alama kubwa ya majukumu ya mtu binafsi.

Majukumu: Haiwezekani mtu mwenye tabia njema bila kuwa na hisia za uwajibikaji, na hapa uwajibikaji una maana ya: mtu kukiri matendo yake, na yupo tayari kuwajibika kwa matokeo yanayotokana na kushikamana kwake na maamuzi yake; yawe ni hasi au chanya, mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya dhamira yake na jamii yake.

Na inahusiana na uwajibikaji (mipaka ya uwajibikaji), nayo katika Uislamu ni majukumu ya mtu binafsi yanayohusika na vyanzo vya maamuzi au matendo, nayo ni majukumu ya kijamii atakaposhiriki katika matendo au maamuzi zaidi ya mtu mmoja kama ambavyo kuna uwajibikaji wa kubadilishana kati ya mtu na jamii yake, lakini kuna kanuni isemayo “Mtu hawajibiki kwa matendo na maamuzi ya mtu mwingine.”

Kukuza uzindushi wa ndani wa nafsi (kilinzi cha ndani ya mtu) pamoja na kufungamanisha maadili mema na mfumo mzima wa kijamii: Mwanadamu ndie anayeupamba ulimwengu wake wa ndani, katika ulimwengu huu huzalika mawaidha ya kweli ya kujilazimisha na maadili, Uislamu umejihusisha na kujenga mawaidha haya kupitia mkazo katika kila hali ndani yake juu ya kile chenye kufahamika kama ni kuleta nia nayo ni kuhudhurisha makusudio ya ndani yaliyoainishwa na matendo mema ambayo mwanadamu anafanya, lakini Uislamu unajua kuwa mwanadamu sio mkamilifu wala aliyehifadhiwa na makosa, na kuwa mwanadamu huyo wakati mwingine anapatwa na muda wa kudhoofika na kuwaathiri walio mzunguka, hivyo basi: Mwanadamu hakuacha dhamira yake ndani yake, bali imemsaidia mtu kufuata misingi ya kimaadili aliyoainisha kupitia maamuzi yake kwa mkusanyiko wa makosa, na adhabu za kijamii na za kisheria, na za akhera kwa atakayetoka katika misingi hii.

Rajev: Kwa kweli, ni mfumo unaostahiki kuutafakari na kuuheshimu.

Dola ya Kiislamu

www.path-2-happiness.com

Dola ya Kiislamu

Marafiki watatu walipoanza kikao chao Maiko na Rajev walisikia sauti zenye kuingilia sauti ya Rashidi, walipouliza Rashidi aliwajulisha kuwa sauti hiyo ilikuwa ni taarifa ya habari, na wakasubiri hadi dakika kadhaa ilipokwisha….baada ya muda mfupi Rashidi alianza kuzungumza."

Samahani, nadhani mtanisamehe, najua mnajua umuhimu wa mtu kusikiliza taarifa ya habari siku hizi, kwa uchache kwangu…Je mnafuatilia kinachotokea kwenye nchi yangu siku hizi?

Rajev: Ndio, ni habari za kusisimua, matukio ya haraka haraka yenye kufuatana.

Maiko: Huenda kitu kikubwa kilichonivutia mimi ni kujitokeza kwa wanaoitwa Islamiyuun (Waislamu sana) na jaribio lao la kubadilisha mfumo wa nchi ili uwe wa Kiislamu….ni jambo lenye kutisha.

Rashidi: Kinachosumbua ni nini katika hilo.

Maiko: Dola za watu za kidini, zime jaribu nchi za kidini na imethibitika kufeli kwake, yalikuwa ni majaribio machungu; dola za kidini zimekoma zama zake tokea karne za kati.

Rashidi: Lakini unakusudia nini kusema dola ya kidini?

Maiko: Ni dola ambayo tabaka lenye kuhukumu linakuwa chini ya watu wa dini ambao wanadai kuwa wanazungumza kwa jina la Mungu. Miongoni mwa mambo muhimu katika dola ya kidini ni kuwa zinatoa haki kwa jina la Mungu na hili linarejea kwa kuwa wao wanazungumza kwa jina la Mungu; hivyo hujiweka katika nafsi zao katika muktadha wa sifa ya kuepushwa na madhambi na utukufu; na hupelekea hilo kudai kuwa wanaopinga utawala wao wanapingana na Mungu, na wao hawahesabiwi wala kuulizwa na yeyote.

Rashidi: Kwa bahati mbaya kuna tatizo la taswira tofauti dhidi ya dola ya Kiislamu, mimi naafikiana nawe kukataa sura hii uliyoitaja, na huitwa 'Theocratic', Lakini theocratic ni mfumo wa kutawala ambao unachukua nguvu yake (na sio tu kwenye mfumo wa sheria zake) kutoka katika dini;……ikiwa Ulaya imepata shida ya utawala huu chini ya mikono ya kanisa katika zama za kati, basi Uislamu haukujua sura hii na haujakubaliana na hali kama hii, katika Uislamu hakuna utawala wa watu wa dini, lakini kuna utawala wa dini chini ya watu wenye kufanya makosa na wenye kupatia, na wenye kuhesabiwa na kuadhibiwa, na wanauzuliwa ikibidi kufanya hivyo, kiini cha tofauti hapa ni kuwa dola ya Kiislamu rejea yake ni Uislamu na utekelezaji wake ni watu wenyewe, watu ambao hawamiliki utakatifu, hakuna katika Uislamu mtawala ambae anadai kuwa anapokea sheria zake na utawala wake kutoka kwa Mungu (baada ya kuzungumza nae) bali hapana budi umma wenyewe ushiriki.

Kama ambavyo uzoefu wa ulimwengu wa Kiislamu kuhusu dola ya Kiislamu ni uzoefu uliofanikiwa, uliopata maendeleo kwa wakati wake, kinyume kabisa na uzoefu wa dola za kidini Ulaya.

Rajev: Tumejua tofauti kati ya dola ya Kiislamu na dola ya kidini; sasa ni ipi tofauti iliyopo baina ya dola ya Kiislamu na dola isiyokuwa ya kidini?

Rashidi: Tofauti ni kubwa na za kimsingi kabisa, ninachokijali zaidi ni msingi wa tofauti yenyewe, ambayo inajificha katika tofauti kati ya taswira ya Uislamu na taswira ya kisekula ya ulimwengu, maisha na mwanadamu, mfumo wa dola katika Uislamu unatoka katika taswira ya Uislamu ambayo dini na maisha yanashikana, na hupamba mfumo uliokamilika anaoishi Muislamu, na kukamilika ndani yake nafasi ya mtu, umma na dola.

Ili tudiriki hayo ni juu yetu kudiriki kuwa: Ni ipi nafasi yetu ya kweli katika mamlaka ya Allah? Ikiwa tutakiri kuwa Mwenyezi Mungu ndie aliyetuumba basi kwa kawaida sisi hatuna hadhi yoyote isipokuwa kufuata radhi zake tu, na ikiwa tutakiri kuwa ardhi hii na mbingu hizi ni miliki yake pekee, inapasa tukiri kuwa haifai atakayepita katika miliki yake isipokuwa kwa utashi wake tu, na ikiwa tutakiri kuwa Mwenyezi Mungu pekee ndie anayetulea, na yeye pekee ndie ambaye anaturuzuku, hatuna nafasi sisi isipokuwa ni kuwa watumwa wake…..na ikiwa Allah ndie mwenye kutuhukumu na mwenye kuhukumu kila aliye katika ulimwengu huu, hatuna nafasi ya kweli hapa ulimwenguni isipokuwa ni kuwa katika ukamilifu wa utukufu wake na unyenyekevu kwake.

Maiko: Lakini, nini kinachotuita katika kurejea uzoefu ule kama sio

www.path-2-happiness.com

hadhari na maneno, mwanadamu anaweza kuamua mwenyewe vipi ataishi, na kipi ambacho kitampelekea kwenye furaha yake, na ni umbo lipi litafaa kupanga maisha yake, kisha baada ya hapo hakuna ubaya kufahamu ndani ya nafsi yake na kuendeleza uzoefu wake.

Rashidi: Ukweli wa mas-ala haya ni: Je, inafaa kwa mwanadamu kuwa mtu sahihi kwa utawala au uwekaji sheria au chanzo cha hukumu? Sisi tunajua kuwa chombo chochote ikiwa mtu mjinga atatawala kukiendesha basi bila shaka atakiharibu….Mathalani ikiwa mtu asiyejua kuendesha gari na yeye hafahamu hilo, tunajua hatima ya mpumbavu huyu, hebu tufikirie: Ikiwa hii ndio hali ya hiki chombo kidogo cha chuma inashindikana kukiendesha bila ya maarifa sahihi, iweje iwezekane kwa mwanadamu ambaye hajijui sembuse kuwajua wengine atawezaje kusimamia uendeshaji wa chombo cha mwanadamu, kilichochangamana ndani?!

Maswala mengine: Ni kuwa hakuna njia ya kufikia uadilifu isipokuwa kwa kutotawaliwa uwekaji wa mfumo wa maisha ya mwanadamu isipokuwa watu ambao utu wao unalingana katika mtazamo wake, wala asiamue haki kwa wote isipokuwa yule asiyekuwa na tamaa za mali za watu, familia, tabaka au umma kwa sifa maalumu, uadilifu hauwezi kusimama ardhini isipokuwa kwa njia hii tu.

Na mwanadamu hawezi kuwa mtupu kwa mahitaji yake mwenyewe; huu ni udhaifu wa mwanadamu unaolazimiana na kila mwanadamu, tuwaangalie viongozi wa kisiasa na viongozi wa kidini katika Brahma na wa Kipapa na Masheikh wa twarika na watu wenye nafasi zao za fedha, tunawaona wote hao wakijipangia na kujiwekea nafasi nzuri zaidi na kujipendelea, hivyo basi kila kanuni iliyowekwa kwenye dunia hii na sheria chini ya utawala wao huwapa wao haki zaidi na kuwapendelea ambayo hawakupewa watu wengine, na huyafanyia mapambo na kuyafanyia sheria kwa njia nyingi, na kwa bendera zao huwadanganya watu kuwa hayo ni katika hali ya kawaida, Je inawezekana ikawekwa misingi ya dola adilifu na jamii iliyokuwa sawa katika jamii ambayo hutawaliwa na watu kama hawa?!

Tuangalie dola kubwa ambazo zimetumikisha umma zingine ambazo zinategemea nguvu zake; ni kanuni ipi miongoni mwa kanuni, au mfumo gani miongoni mwa mifumo ambayo athari yake haisambai kwenye mishipa yake. Je, hutarajiwa kwa watu hawa wawawekee wanadamu mfumo au sheria ambazo zitasimamia misingi ya haki na uadilifu?!

Rajev: Lakini bwana Rashidi mnafanya nini katika dola ambayo kuna wana dini wengine ambao ni wachache ambao sio Waislamu…. kwa mfano sisi India, kuna dini zenye watu wengi lakini ni wachache (kulinganisha na Wahindi). Nyie mnapofanya rejea ya dola kuwa ni Uislamu mnalazimika kukubali dini ambayo si yenu.

Rashidi: Vizuri umenikumbusha jambo hili, pana nukta tatu ningependa kuweka bayana katika suala hili:

Ya Kwanza: Nawashangaa mnakataa mtu asiyekuwa Muislamu kuishi chini ya kivuli cha dola ambayo rejea yake ni Uislamu pamoja na kuwa dini yake haiti kwenye kusimamisha dola yake maalumu katika ardhi… wakati ambapo mnawalazimisha Waislamu kutii mifumo inayokwenda kinyume na dini yake na kukubali rejea ambazo zina kwenda kinyume na itikadi yake pindi anapoishi katika dola ya kisekula, pamoja na kuwa dini yake haikubaliani nayo.

Ya Pili: Uislamu kufanywa kuwa ni rejea ya dola haina maana kulazimisha Uislamu kwa wasio waislamu, na kikwazo hiki kimeibuka kutokana na taswira ya usekula kwa dini ambayo inaiona kuwa mipaka yake inaishia kwenye itikadi yake yeye mwenyewe ndani ya nafsi yake, wakati ambapo Uislamu hauishii hapo; Uislamu kulingana na Muislamu ni itikadi na sheria (yaani ni mfumo na kanuni) na ni rejea ya Ustaarabu, ama asiyekuwa Muislamu anaweza kuuchukua Uislamu kama ni ustaarabu na kuwa chini ya mfumo na kanuni zake, bila kuingia katika itikadi na ibada zake, haswa haswa kama mnavyozungumza kuhusu uwezekano wa kutekeleza Uliberali na Ujamaa katika jamii ambazo hazikuibukia katika mambo hayo na kwa wafuasi wa dini na mila nyingine.

Ya Tatu: Kusimama kwa dola ambayo rejea zake ni za Kiislamu haina maana kumeza haki za wachache au kuingilia katika hukumu maalumu za kidini kwao, Uislamu unadhamini haki za wachache, wala haikatazi wao kuhukumiana katika dini zao na katika mambo yao maalumu.

Maiko: Lakini sisi hivi sasa tunaishi katika zama zisizokuwa zile ambazo

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Uislamu uliibukia, ukatekeleza na kusimamisha dola yake, hata kama juhudi hizi zitafanikiwa tutahesabu kuwa ni hatua ya kurudi nyuma…ni hatua ya kukosa maendeleo; kwa hili nyie mnataka sisi tuhame fikra zetu na tusimamie mambo ambayo leo hii hayakubaliki wala hayana mantiki yoyote pamoja na maisha mapya.

Nyie kwa mfano bado mnashikilia kuharamisha riba, na hilo ni jambo muhimu katika uchumi hakuna nchi leo hii inaweza kuiacha.

Rashidi: Ewe rafiki yangu maneno yako kwa mfano huu na mifano mingine imejengeka katika misingi isiyokuwa ya kweli, leo hii taswira ya mfumo wa dola na utaratibu wa ulimwengu ambao tunaishi baada ya kulazimisha mfumo huu (riba) na kupuuzia athari zake hadi kwa kuwafanya wanadamu wafungamanishe mfumo wa uchumi na riba.

Ni kweli Uislamu umeharamisha riba, lakini sio sahihi kuwa riba ndio msingi wa uchumi.

Mabepari ndio waliolingania riba na ndio walimbikizaji ulimwenguni, na wanawadanganya walimwengu kuwa uchumi bila riba hauendi, ukweli ni kuwa hauendi katika ulimwengu wa mabepari, pamoja na hayo wana uchumi wakubwa katika ulimwengu wa Magharibi (mabepari) sasa hivi wanapinga mfumo wa riba na wanasema kuwa matokeo yaliyohitimishwa kwa vizazi vingi ni kuangukia katika matatizo ya kiuchumi na ya kifedha, na matatizo ya kijamii yanayoifuatia kwa sababu ya kuuweka uchumi mikononi mwa watu wachache tu, na kuwanyima watu wengi katika jamii, na ni haki yetu kuangalia matatizo ya madeni ya majengo na matatizo yaliyofuatia na balaa ulimwenguni, na kabla yake matatizo mengi, yaliyokuwa maarufu zaidi ni tatizo la: kuanguka kwa uchumi wa ulimwengu (Great Depression) katika miaka ya thelathini katika karne iliyopita ili tuweze kujua ukubwa wa tatizo hili.

Miongoni mwa miujiza ya mfumo wa Kiislamu ni kuharamisha riba na ulimbikizaji (nguzo mbili za mfumo wa ubepari) kabla ya kuibuka kwa rasilimali (mfumo) kwa miaka elifu moja. Rafiki yangu kwa hakika dola ya Kiislamu sio tu ni jambo la ulazima katika sheria ya Kiislamu, bali ni lazima vile vile kwa mwanadamu.

Safari ya Milele

www.path-2-happiness.com

Safari ya Milele

Maiko aliwasalimu rafiki zake pindi tu alipoingia katika chumba cha mazungumzo, Rajev alijibu maamkizi wakati ambapo Rashidi alisema;

Ni subirieni kidogo…. Na watayarishia onesho lenye kusisimua. Je, mmeona onesho la kuanguka kwa Piermario Morosini mchezaji wa timu ya Levono katika mchezo wake na timu ya Pescara katika ligi ya Italia….alikufa papo hapo kutokana na kusimama kwa moyo….ulikuwa ni mshtuko kwa watazamaji wakimuona anakata roho.

Maiko: Lakini la ajabu zaidi kuhusu tukio hilo: Ni tukio la kuanguka kwa mchezaji wa timu ya Bolton, Fabrice Ndala Muamba pindi timu yake ilipocheza na timu ya Tottenham katika kombe la F.A. Uingereza, mchezaji alianguka huku akipoteza fahamu huku moyo wake ukiwa umesimama, na watu wote walijua ameshakufa, katika hali isiyokuwa ya kawaida moyo wake ulirejea tena kufanya kazi baada ya kusimama kwa dakika sabini na nane na hili madaktari walilisema kuwa ilikuwa ni kifo cha dakika 78, kilichomfanya daktari wa timu Jonathan Tobin kuzungumza kwa kustaajabia hali hiyo kwa kusema: “Ni jambo ambalo mtu hawezi kuliamini, hatukuwa na matarajio ya kupona Muamba katika hali hii”, Muamba alikufa na akarejea tena katika maisha.

Rashidi: Mauti ni ukweli pekee ambao watu wote wanaukubali….lakini ni nini baada ya mauti? Je, ni mwisho, ama baada yake kuna mwanzo mwingine (siku ya mwisho) kama wanavyoamini watu wengi?

Rajev: Imani ya siku ya mwisho ni itikadi ya asili aliyoibeba mwanadamu tokea kuanza kwake kuishi ardhini, dalili nyingi na athari na kumbukumbu za kihistoria zimethibitisha kuwa itikadi hii ilikuwepo katika staarabu nyingi za zamani, Wamisri wa kale walijua hilo, kabila la Maya na Waroma na katika bonde la Ar-Rafidiyn na nyinginezo…ni itikadi ambazo hakuna dini yoyote ya mbinguni haikuacha kuiamini, hata dini zilizotungwa na wanadamu waliamini kama vile Brahma, Budha, Majusi, n.k.

Rashidi: Ulichosema ni sahihi, na itikadi hii imeita kuamini Mtume wa Uislamu, kama ambavyo mitume waliitangaza na kuonesha kwa watu, na imani hii ni sharti katika masharti ya mtu kuwa Muislamu katika zama na zama, kwani hakuna maana ya kumuamini Mwenyezi Mungu, vitabu vyake na Mitume yake bila ya itikadi hii.

Maiko: Hata hivyo mimi nimeona kuwa athari ya itikadi hii katika maisha ya watu yanatofautiana, kama ambavyo wachache miongoni mwao huichukua na kuiweka katika hisia na matendo yao.

Rashidi: Kweli kabisa, watu wote hilo wanalithibitisha katika kiwango cha itikadi ya nadharia, lakini wachache tu miongoni mwao ndio ambao wanaweka kwenye hisia zao itikadi ile ikiwa hai katika uhalisia….na ushahidi wa hilo: Tunapofikiria mlio wa filimbi ya hatari inayotokana na mashambulizi ya anga wakati wa vita…..ni katika hali ya kawaida ya tabia katika hali hiyo kutarajia barabara kuwa tupu kwa wapita njia na shughuli, kiasi cha kuwa asiyefanya hivyo itasemwa kuwa ni mpumbavu au mwendawazimu…. Ikiwa hilo ni kwa jambo dogo tu la duniani, itakuwaje hatari kubwa kuliko hiyo….hatari ambayo watu wanaamini kuwa lazima itatokea, na Mola wa ulimwengu huu ametahadharisha na kuitangaza kwa ndimi za Mitume wote, ilikuwa ni hali ya kimantiki kukubali kwao onyo hili kuwe ni kukubwa zaidi.

Maiko: Nadhani sababu katika hilo ni kuwa watu wanaona na wanasikia hatari inayopigwa na filimbi hiyo, hata kama hali hizo hawaja zijaribu basi watakuwa wameona katika hali zingine au katika nchi zingine na watakuwa wameona athari zake. Ama kuhusu siku ya mwisho ni jambo lililotenganishwa na ukuta wa kifo baina yetu na hiyo siku, na hilo halionekani kwa macho yetu leo na hili ndilo lillopelekea makundi ya yakini kati ya hali mbili.

Rashidi: Maneno yako ni sahihi, lakini kinachotakiwa ni kuwa mwanadamu anatakiwa afikie kwenye ukweli ambao atakinaishwa nao mwenyewe kwa akili yake na sio tu kwa hisia zake. Sababu kuu ya udhaifu wa yakini kwa watu wale ni kwa sababu hawatumii jicho la akili yao, kwani wanapoangalia jambo kwa makini na kutumia fikra zao wangediriki kuwa wanachokiona kwa macho yao haishindi yakini ya kile ambacho kiko mbali katika mtazamo wao.

Kisha kuna mambo kusubiri kuyaona au kuyajaribu ni maangamizi kwake; kwa sababu hayavumiliki ila tu kupita mara moja tu; ikiwa mtu akishindana na mtu mwingine akamwambia kuwa anaweza kujitupa kwenye jengo refu bila kuumia na kupatwa na lolote, na huyu mtu mwingine akamwambia, basi tujaribu hilo! Kwa hakika hilo litakuwa

www.path-2-happiness.com

jaribio la mwanzo na la mwisho la mtu huyu na utakuwa ndio mwisho wake, hivyo basi katika jaribio hili hatuwezi kuthibitisha usahihi wa madai hayo au makosa yake, lakini kuitumia akili na kuangalia yaliotangulia na lenye kufanana nayo yanatuwezesha kufikia kwenye matokeo yanayo tarajiwa ya uzoefu bila ya kuyaingia au bila ya kuyafanya.

Rajev: Hivyo basi, ni juu yetu ili tufikie yakini hii tuipe hoja imani hii kwa dalili za kiakili na mitazamo ya kisayansi.

Rashidi: Hamna neno katika hilo, lakini ninasema kuwa dalili kubwa katika hilo ni kuamini ukweli wa aliyetuambia hilo. Naye ni Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ndimi za Mitume wake, na huu ndio muktadha wa imani hii ya kumuamini Mtukuka, kwani yeye ndie anayejua kuliko sisi na mwenye kujali zaidi kuliko sisi kwa yale yenye kutufaa na kutunufaisha.

Ama ulichokitaka katika dalili za kiakili na vithibitisho vya kisayansi, ni vingi sana… miongoni mwavyo ni:-

Hoja ya Kwanza: Hoja ya kufufuliwa: Ikiwa tumekiri kuwa Mwenyezi Mungu ndie aliyetuumba mara ya kwanza, basi yule aliyetuumba mara ya kwanza kutokana na kuwa hatukuwa kitu hashindwi kutufufua tena baada ya mauti, bali uwezekano wa kutokea maisha mengine ni wenye nguvu (kinadharia) kuliko uwezekano wa maisha ya mwanzo.

Hoja ya Pili: Kutoweza kupatikana kwa vitu kutoka hali moja kwenda nyingine na kutoka katika mazingira fulani kwenda mengine, Qur'an imetupigia mifano ambayo tunaweza kuijaribu kwa watu wote, nayo ni moto kutoka kwenye mti mibichi (kijani), ambaye anaweza kutoa kitu kwenye kinyume chake, na kunyenyekea kwake maada na viumbe hashindwi kuhuisha mifupa ikiwa ni majivu.

Hoja ya Tatu: Kubadilika viumbe, mauti kisha uhai, kisha mauti kisha uhai, kutoka katika punje lisilo na uhai ndani yake kunatoka mmea wa kijani unastawi na kuzaa, kisha mmea huu kutoa mmea ulio hai ambao nao hutoa punje za mbegu zisizo hai ambazo hazioti, na kutoka kwa ndege hai hutoa yai mfu, kutoka katika yai hili hutoka ndege hai mwenye kutembea kwa mara nyingine. Hivyo basi uhai umejificha katika ambacho tunadhania hakina roho na maiti… vivyo hivyo mwanadamu na wanyama wote.

Hoja ya Nne: Kushuhudia wazi kufufuliwa katika maisha ya mwanadamu, mnyama na mimea, mwili wa mwanadamu wa kawaida una seli zipatazo 260,000,000,000,000,000 zinabadilika kila sekunde, zinapungua kwa haraka, na upungufu huu unazibwa na chakula; hivyo mwili wa mwanadamu hubadilika wenyewe kwa wenyewe kama vile mto upitao, vivyo hivyo mwili wetu huwa chini ya mabadiliko ya mara kwa mara, kiasi cha kufikia muda ambao haitobakia ndani yake seli yoyote ya zamani katika kiwiliwili chake….tendo hili hukariri kwa vijana na watoto kwa haraka, wakati ambapo huenda pole pole kwa wazee.. mabadiliko haya hutokea mara moja kila baada ya miaka kumi.

Katika hili tunajifunza kuwa miili yetu ya kimaada hubadilika mara kwa mara, ama mwanadamu kwa ndani habadiliki: Elimu yake, desturi zake, kumbukumbu zake, matarajio yake, fikra zake…. Vyote hubakia kama vilivyokuwa. Lau ingekuwa mwanadamu anakwisha na kubadilika (kama seli) basi kwa uchache mabadiliko yangekuwa ni makubwa zaidi….na hili linathibitisha kuwa maisha ya mwanadamu ni mengine na sio kiwiliwili peke yake, nayo ni yenye kubaki pamoja na kiwiliwili kubadilika mara kwa mara kwa kubadilika kwa seli zake.

Hoja ya Tano: Elimu leo hii inaashiria kuwa vyombo vya ulimwengu vinasajili matendo yote ya mwanadamu, katika malengo muhimu ya akhera ni: Kulipwa watu kwa matendo yao hapa duniani yakiwa ni kheri au yakiwa ya shari, kulingana na matendo ya mwanadamu yalivyosajiliwa na matendo hayo yanakusanya nia ya mtu, maneno yake na matendo…. na ushahidi wa kisayansi unathibitisha kwamba hayapotei bure; bali kuna uwezekano wa kuyajua na kuyarejea baada ya kwisha kwake.

Hivyo basi fikra au nia ambazo zinapita akilini mwetu na kuzisahau… tunayaona usingizini au tunayazungumza katika hali ya Historia au wendawazimu bila ya kujua, na hili linathibitisha kuwa akili au kinachohifadhi sio yale ambayo tunayahisia peke yake, bali kuna pande zingine katika hifadhi hii ambayo hatuihisi nazo zipo zikiwa zinajitegemea, na sayansi imethibitisha kuwa sisi hatuna uwezo wa kuzifuta.

Ama kauli kuwa sayansi ya leo hii imethibitisha kuwa sauti ambazo tunazisikia ni mawimbi katika hewa na imethibitika kuwa kipande cha mawimbi haya hubakia baada ya kutokea kwake kwa mara ya kwanza, na kuna uwezekano wa kuisikia tena kwa mara nyingine baada ya kupita karne na karne, hata kama wanazuoni hawakuweza kutekeleza kivitendo

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

hadi sasa, na hili linathibitisha kuwa kila anachozungumza mwanadamu kinarekodiwa.

Ama suala la kufanya kazi, utasadiki katika hali inayoshangaza uwezekano wa kutokea akhera, sayansi leo hii inathibitisha kuwa harakati zetu zote na matendo yetu yapo katika mwanga au kiza na yote yapo katika anga katika hali ya picha, na inawezekana wakati wowote kukusanya picha hizi, kwa hiyo miili isiyo na uhai inayotembea hutoa joto muda wote, na hivyo kwa upande wake huakisi mambo ya kiwiliwili na pande zake, na kuna chombo makini kimevumbuliwa chenye kuchukua picha ya mawimbi ya joto yanayotoka kwa kila kiumbe, lakini vitu hivi haviwezi kupiga picha mawimbi ya joto ila baada ya masaa machache ya tukio lenyewe.

Maiko: Kama tutakubaliana kwa hitimisho la kutokea siku ya mwisho, na tukajua nafasi yake katika Uislamu, sasa ni alama zipi muhimu za itikadi hii?

Rashidi: Vipengele vya itikadi hii katika Uislamu vinatofuatiana sana na yaliyokuja katika dini nyingine, hata hivyo tunaweza kufupisha kwa haya yafuatayo:-

1. Kwamba Mwenyezi Mungu atafuta ulimwengu huu, na vyote vilivyomo katika viumbe, katika siku inayofahamika kama siku ya kiama.
2. Kisha yeye Mtukuka atawafufua kwa mara nyingine, na atawakusanya mbele yake, na huko ndio kukusanywa na kufufuliwa.
3. Kisha atawaweka katika mahakama ya Kiungu kila mtu atakachokuwa amekipata kama vile kheri au shari katika maisha yao duniani, bila ya upungufu au nyongeza.
4. Mwenyezi Mungu anapima kila tendo la mtu katika matendo mema au maovu, ambae matendo yake mema yamezidi basi atasamehewa, na ambae makosa yake yatazidi basi ataadhibiwa.
5. Wale watakao samehewa wataingia peponi na wale watakaoadhibiwa wataingizwa motoni.

Rajev: Kweli, jambo hili ni zito mno.

Uislamu na Ugaidi

www.path-2-happiness.com

Uislamu na Ugaidi

Katika ahadi iliyoainishwa ya kuanza mazungumzo kwenye chumba cha mazungumzo walipoahidiana kukutana Maiko, Rashidi na Rajev–Maiko alianza kuzungumza baada ya kuwasalimu wenzake.

Maiko: Mimi naona mazungumzo ya Rashidi katika vikao vilivyopita ni maneno yaliyo kinyume na kinachofahamika kuhusu dini yake na kwa hakika tunahitaji kuchuja, Ustadh Rashidi amejitahidi kuonesha maeneo yenye kuvutia katika dini yake, lakini amepuuzia maeneo yenye kiza…. Sisi tunaona kwa kutumia macho yetu kuwa ugaidi ambao unatikisa ulimwengu leo ni ugaidi wa Kiislamu.

Rajev: Naafikiana nawe katika sehemu ya mazungumzo yako, lakini ugaidi ni tabia ambayo haifungamani na dini au taifa na hili ndilo ambalo nimelifahamu India, nchini mwangu, ambapo matukio ya matumizi ya nguvu ni ya watu mbali mbali na yana sababu nyingi, Je, ni sababu zipi zinapelekea kuwepo kwa hali hii ambayo tunaweza kuijadili.

Maiko: Hili ndilo nililotaka kueleza, mimi dhana yangu ni kuwa ugaidi upo ndani ya Uislamu wenyewe, na inajulikana wazi kuwa Uislamu umeenea kwa upanga…Je, utapinga hilo bwana Rashidi?

Rashidi: Bila shaka nitalipinga hilo na uhalisia vile vile unalipinga.

Maiko: Ni uhalisia upi unaokusudia?

Rashidi: Hakika za kidini na ukweli wa kihistoria lakini niache niseme kwanza: Inabidi tuziepushe akili zetu na propaganda ambazo kwazo vyombo vya habari na wenye maslahi hukamata akili zetu.

Rajev: Mimi nadhani tunaishi katika jamii huru, na haiwezekani tukafanyiwa imla na shinikizo la kutengeneza akili zetu.

Rashidi: Ni kweli hatushurutishwi na hatulazimishwi, na sisi tu huru kwenye uchaguzi wetu, lakini mwisho wa siku tunachagua tunachopewa na wenye kutawala vyombo vya habari, wanasiasa wenye maslahi wanavyotuelekeza, bado maneno ya wana siasa na wanafikra wa Magharibi yametawala kuhusu ugaidi na kuufungamanisha na Uislamu, na madai ya vita vya wana msalaba chini ya kinachoitwa (kupiga vita ugaidi), na madai kuwa operesheni hii ni ya kulinda ustaarabu wa Magharibi wenye kusifika na kusamehe na kufunguka kama walivyotaja.

Maiko: Nakuahidi kuwa tutabaki kama tulivyokuwa tupe ukweli vyovyote iwavyo chanzo chake na vyovyote iwavyo tabia yake.

Rashidi: Ikiwa Uislamu ni dini ya uadui katika tabia na mazingira yake na kuwa imeenea kwa upanga, na Ukristo ambao wa Magharibi wanadai kuwa unajinasibisha na dini ya upole, Je, rafiki yangu unajua ni mara ngapi Qur'an imetaja neno 'upanga', na mara ngapi imetajwa katika kitabu kitakatifu?

Maiko: Sijui haswa, lakini bila shaka kwenye Qur'an imetajwa zaidi kuliko kwenye kitabu kitakatifu (Biblia)?

Rashidi: Haya pokeeni habari hizi zitakushangazeni Qur'an Tukufu ina sura 114, ina aya 6,236 na maneno 77,439. Neno 'upanga' au visawe vyake havikutajwa hata mara moja, pamoja na kuwa neno hili lina visawe vinavyofikia 60 katika lugha ya kiarabu, wakati ambapo neno 'upanga' limetajwa mara 200 katika kitabu kitukufu (Biblia).

Maiko: Aaah:…kweli ni jambo la kushtua….Je, hili ndilo ulilokusudia kuwa ndio ukweli wa kidini?

Rashidi: Bali huu ni ukweli mmoja tu ambao sitourefusha ili nitoe fursa nitaje mwingine.

Maiko: Ni upi huo ukweli mwingine?

Rashidi: Ukweli huu ni muhimu sana, hapana budi utakuwa unafahamu baadhi yake ewe rafiki yangu Rajev; nao ni kuwa sehemu zenye Waislamu wengi duniani, na kilele cha sehemu hizi ni Asia Mashariki na kusini mwake hakujawahi kufika jeshi la kiislamu hata mara moja na mfano wake vile vile ni sehemu kubwa katika Afrika.

Ukweli huu wa kihistoria unathibitishwa na wanahistoria waadilifu kuwa haujathibitika kwao hali za kulazimishwa kufuata Uislamu katika historia ya Uislamu.

Maiko: Mbali na hayo uliyoyataja ya maneno ya baadhi ya Wanahistoria; ambao na mimi naweza kuleta maneno ya wanahistoria wengine wanaoona kinyume na hivyo; ni kipi kinachothibitisha madai haya?

Rashidi: Kuna zaidi ya dalili zenye kuthibitisha nilichosema:

Kwanza: Sehemu nyingi zilizofunguliwa na Waislamu kijeshi watu wake walibaki katika dini zao za kale chini ya utawala wa Waislamu, na wengine wamebaki katika dini zao hadi sasa, na hili ndilo lililotokea

www.path-2-happiness.com

huko Misri, Palestine, Lebanon, Ugiriki na India……kwa mkabala wa sura nyingine kinyume chake pindi Wakristo walio tawala kijeshi huko Andalus (Hispania) Quds, na Ufilipino… kulikuwa na mauaji yaliyoenea (ya halaiki) au kulazimishwa kuingia Ukristo au kuhama, hayo ndio malipo (hisa) ya waliotofautiana nao katika dini.

Pili: Pindi utawala wa kijeshi wa Kiislamu katika nchi ilizozifungua ulipoondoka na kutokuwepo kwa sura yoyote ya shinikizo kutoka kwa Waislamu au wengineo, hatujaona watu au mataifa haya yakiacha Uislamu, bali tumeona watu Waislamu wa Soviet Union hapo kabla wakihifadhi Uislamu wao kwa siri chini ya ukandamizaji wa Ukomunisti wakisubiria fursa ya kuondoka kwa utawala huu kandamizi ili warejee kwa nguvu katika Uislamu wao.

Tatu: Historia inataja visa vya mataifa ambayo yalishambulia nchi za Kiislamu na kushinda nguvu zake za kijeshi na kuteka sehemu zake kubwa zilibadilika na kuufuata Uislamu kama vile Tatari na Waturuki.

Maiko: Nitakubaliana nawe kuwa Uislamu haukusambaa kwa upanga, lakini tuachane na historia, tuzungume hali tuliyonayo hivi sasa. Je, hutokubaliana nami nilichokisema: Kwa hakika ugaidi unaousumbua ulimwengu hivi sasa ni ugaidi wa Kiislamu mia kwa mia?

Rashidi: Tuainishe kwanza: Ni nini maana ya ugaidi? Kisha tuangalie ulimwengu ili tuone ni nani anauongoza ugaidi katika zama hizi, nani anautengeneza?.

Rajev: Dola za ulimwengu wala taasisi zake za kimataifa hazijaafikiana/hazijakubaliana juu ya maana ya ugaidi, hata hivyo sisi tunaweza kuafikiana juu ya maana yake, “Kuwatisha watu waliokuwa katika hali ya amani kwa sura yoyote ile juu ya kuathiri utashi wao au kupata mapato ya kisiasa au ya kiuchumi kwa upande unaoshambuliwa.”

Rashidi: Bila ya shaka kutokuainisha makusudio haya katika baadhi ya nchi, ili ufahamu uwe kama mpira ambao unaweza kuuchezea, hata hivyo naongezea katika maana yako (taarifa): “Vyovyote awavyo huyu adui (anayeshambulia) ni mtu binafsi kundi au nchi.”

Maiko: Sina tatizo na nyongeza hiyo, na kulijenga hilo: Tukiangalia matukio yanayoendelea ulimwenguni tunaona ulipuaji wa kituo cha biashara huko New York miaka 2001 na yaliyofuatia kama vile ulipuaji wa treni Madrid, Bahi-Indonesia dhidi ya watalii wa nchi za Magharibi na matendo wayafanyayo Wapalestina dhidi ya Mayahudi yote hayo ni

matendo ya kigaidi yaliyofanywa na Waislamu.

Rashidi: Kidogo kidogo rafiki yangu, matendo wayafanyayo Wapalestina ni mapambano ya kujilinda dhidi ya waliowakalia kwa mabavu katika historia nyeusi ya ugaidi, je, inawezekana kufumbia macho ukaliaji ardhi ya taifa kamili kuwafukuza na kuwatisha kwa njia mbali mbali, miongoni mwazo ni:-

Mauaji ya Baldat As-Shaykh (al-Shaikh village) yaliyotokea tarehe 31/12/1947, ambapo waliuawa watu 600 wananchi wasio na hatia ndani ya nyumba zao.

Mauaji ya kijiji cha Deir Yassin, yaliyotokea 10/4/1984, ambapo zaidi ya nusu ya wakazi wa kijiji hicho waliuawa.

Mauaji ya Lydda yaliyotokea tarehe 11/7/1948 ambapo wananchi 426 waliokuwa wamekusanyika msikitini waliuawa, Mayahudi walivamia na wakaua waliomo ndani.

Mauaji ya Kafr Qasem yaliyotokea mwezi wa kumi 1965 amapo wananchi 94 waliuawa wakiwemo watoto na wanawake.

Mauaji ya Sabra na Shatila yalitokea tarehe18/9/1982 huko Lebanon na yalifanywa na jambazi la kivita, Ariel Sharon akishirikiana na jeshi la Kikristo la Lebanon ambapo mauaji yaliendelea kwa masaa 72 na kuuawa Wapalestina 3,500 na Mlebanoni mmoja wengi wao wakiwa ni wanawake, watoto na wazee, hawakuwa na kosa lolote zaidi ya kuwa walishambuliwa kwa kuwa ni Waislamu.

Mauaji ya msikiti wa Al-Ibrahimi yaliotokea tarehe 25/4/1994 yaliofanywa na mmoja wa askari wa jeshi la Israel akishirikiana na makundi mengine ya jeshi hili na masetla wa Kiyahudi, katika mauaji haya waliuawa watu 29 waliokuwa wakiswali msikitini na wengine 50 waliokuwa nje, na kujeruhiwa zaidi ya watu 350 waliokuwa wakiswali.

Lakini ili mtazamo wako uwe mpana, nitaongeza matukio mawili tena: Ulipuaji wa jengo la Federal la Oklahoma mwaka 1995 ambapo walikufa watu wapatao 168 na kujeruhiwa watu wengine 500, na mauaji ya Oslo na kisiwa cha Uto ya mwezi wa saba mwaka 2011 ambapo watu 92 walikufa na wengine 90 kujeruhiwa, matukio yaliyofanywa na Wakristo wenye siasa kali wenye kushikilia ugaidi na ubaguzi wa hali ya juu.

Kama ambavyo sisi ikiwa tunafuata uhusiano kati ya dini au ustaarabu fulani na ugaidi hatuwezi kusahau ukweli uliopo katika karne hii sasa:-

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Haijawahi kutokea nchi yoyote ya Kiislamu kuvamia nchi ya Ki-Magharibi (yoyote), lakini kinyume chake kabisa historia imeshuhudia kuwa ulimwengu wa kale na ulimwengu mpya umekuwa ni lengo la kushambuliwa na nchi za Magharibi.

Wahindi wa Kimarekani waliuwawa katika mauaji ya Kimbari na waliokuwa wakibeba bendera ya ustaarabu wa Kimagharibi; ili kupunguza idadi yao kutoka milioni 10 kufikia laki mbili (200,000) pamoja na kuwanyang'anya bara lao.

Watu wa Magharibi ndio ambao wamesababisha ulimwengu maafa ya vita viwili vikubwa ambayo vimeitwa (Vita vikuu viwili vya dunia), lakini ukweli wenyewe na haswa vya kwanza (vya Ulaya mbili) ambapo wahanga wake (vya kwanza) ni milioni ishirini na majeruhi na vilema mfano wa idadi hiyo, na vya pili wahanga wake walifikia milioni 55, na majeruhi milioni 53, na wengine milioni 3 hawajulikani walipokuwa, wengi katika wahanga hawa ni watoto katika koloni zao na miongoni mwa raia, kwani kilichokuwa ni katika tabia maarufu ya wapiganaji ni kuwalenga raia wasio na hatia ili kuvunja utashi wa adui.

Kama ambavyo (hata kama tumeafikiana kimsingi uharamu wa kuwafanyia uadui raia wasio na hatia) hatuwezi kupuuzia malengo ya waliofanya matukio haya kwa lengo la kuilinda na kuizuia Marekani na Magharibi na muendelezo wa uadui na ugaidi wa Waislamu, haswa Iraq na msaada wao wa mauaji ya Wazayuni kwa Wapalestina.

Rajev: Kwa hivyo basi, muhtasari wa kauli tunaoweza kutoka nalo ni kuwa: Ugaidi hauna dini wala ustaarabu.

Rashidi: Ninaweza kukubaliana nawe kuwa hauna dini, lakini kuna haja ya kuangalia muelekeo wa ustaarabu wa Kimagharibi ambao umesimama katika msingi wa magomvi na kutukuza nguvu na uhusiano wake na matumizi yao ya kiuadui; hivyo basi ustaarabu huu wa leo wa Kimagharibi msingi wake fikra yake umetegemea na kuathiriwa na urithi (staarabu mbili) wa Kiyunani na Kiroma, na ndani ya staarabu hizo ilikuwa ni maarufu kutoka kwao fikra kama: fundo la kuwa juu, kutukuza nguvu na ulazima wa mgogoro…fikra hizi zimerithiwa na ustaarabu wa kisasa na mamboleo, na mafundisho ya Kikristo haukuweza kuzuia matendo hayo mabaya yenye kutisha na ugaidi ulioenea Ulaya na ulimwenguni kote.

Maiko: Kwaheri tutaonana katika mjadala mwingine.

Mustakbali wa Dini Hii

www.path-2-happiness.com

Mustakbali wa Dini Hii

Rajev alichelewa (katika hali isiyokuwa kawaida yake) katika kikao na rafiki zake, na alitokezea katika Skrini ya Laptop, Maiko akaanza kuzungumza nae.

Halo! Rajev, umezoea kufika kwa wakati katika miadi yetu tunataraji kuchelewa kwako kusiwe ni kwa tatizo lililokusibu.

Rajev: Samahani rafiki zangu, hakuna neno, lakini nilishughulishwa kumalizia utafiti wangu ambao nilitaka kuwaonesha.

Maiko: Vizuri sana, kama ni hivyo mjadala utakuwa na faida kubwa, utafiti wako unahusu nini?

Rajev: Kwa hakika mjadala wetu wa mara kwa mara umenivutia sana na umenipa maarifa mengi kuhusu Uislamu, hivyo basi nikataka kufanya utafiti kuhusu kuchambua katika harakati ya kuenea kwa dini hii na kupanuka kwake ulimwenguni.

Maiko: Jambo hilo hilo limenivuta kufanya utafiti vile vile, lakini katika nyanja nyingine zinazohusika na kupanua utafiti wa nyanja ambazo tutaziangalia kwa undani zaidi na kutokana na vyanzo vyake vya asili…. hata hivyo nini ulichokipata katika utafiti wako? bwana Rashidi!! je upo nasi??!

Rashidi: Ndio, ndio, nipo nafuatilia pamoja nanyi.

Rajev: Nimekuta marejeo na elimu nyingi zinaashiria kuzidi kupanuka kwa Uislamu ulimwenguni, utafiti umegundua kuwa kuwepo kwa zaidi ya mila na desturi 4,200 ulimwenguni, na takwimu zinathibitisha kuwa dini ya Kiislamu ndio yenye kuenea zaidi kati ya itikadi zote ulimwenguni! Na kuwa leo hii inasambaa mabara yote uliwenguni kwa haraka, tutakapoangalia kiwango cha ukuaji wa Waislamu na kulinganisha na ukuaji wa wafuasi wa Ukristo mathalani, unapata takwimu ya Umoja wa Mataifa inayosema:Kiwango cha ukuaji cha Waislamu ulimwenguni ni asilimia 6.4% wakati ambao cha Wakisto haizidi asilimia moja 1%.

Utafiti wangu umeangalia Ulaya, nikakuta Uislamu kwa mfano: Ndio dini ya pili nchini Hispania, Ufaransa na Uingereza.

Huko Ujerumani Waislamu wanaongezeka, na kulingana na gazeti la Die Zeit la Ujerumani la kila siku ni kuwa: Uislamu husambaa Ujerumani na kuongezeka kila siku.

Utafiti uliofanywa na wizara ya ndani ya Ufaransa umethibitisha kuwa: Zaidi ya watu 3,600 wanasilimu kila mwaka kama ambavyo inaashiria kuwa kuna misikiti 2,300 na Waislamu milioni 7, na kuna matarajio kuwa ifikapo mwaka 2025. Waislamu watafikia robo ya wakazi wote wa Ufaransa, wakati ambapo utafiti huo huo unaashiria kuwa ifikapo mwaka 2050 kutakuwa na Waislamu asilimia 20% Ulaya, kadhalika kuna takwimu nyingine zinaona kuwa ifikapo mwaka 2040 Waislamu ndio watakaokuwa wengi Ulaya.

Takwimu zinasema kuwa theluthi ya wananchi wote wa Holland watakuwa ni Waislamu baada ya miaka kumi, na moja katika tafiti hizo zinathibitisha kuwa idadi ya Waislamu inaongezeka kwa kustaajabisha kwa raia wa Sweden, ambapo takwimu rasmi zinaashiria kuwa idadi ya Waislamu inaongezeka kila siku kiasi cha kufikia leo hii Waislamu 120 elfu.

Baada ya upanuzi wa misikiti ambacho ni kiashiria cha kusambaa kwa Waislamu, haswa wale walioshikamana na dini yao, tafiti hizo zinaonesha kuwepo kwa zaidi ya misikiti elfu 25 Ulaya pamoja na ongezeko la wenye kuswali katika misikiti hiyo miongoni mwa Waislamu.

Kwa mkabala tafiti zinathibitisha kupungua sana kwa wanaokwenda makanisani, utafiti uliofanywa na Dresdner Bank kuwa idadi ya wanaokwenda Makanisani huko Ujerumani imepungua katika miaka ya karibuni ambapo imetarajiwa kusimamisha misa za kidini katika makanisa 96 katika jumla ya makanisa 350 katika Essen Parish peke yake, na hivyo majengo ya kanisa kutumika katika malengo mengine, na hiyo ni kwa sababu ya kupungua wenye kwenda makanisani na kupungua kwa mapato ya kanisa.

Pengine kinachoonekana ni udhaifu mkubwa wa Wakristo kwenda makanisani mwao, kiasi cha hali hiyo kufikia katika kanisa moja katika nchi ya Ulaya lilifanya mashindano ya magari ili kuwavuta watu kwenye sala; kwa sababu ya uchache wa wenye kwenda kwenye makanisa.

Maiko: Hilo linaweza kufasiri tunachokiona katika zile hali ngumu za vyama vya mlengo wa kulia na baadhi ya wenye kasumba Ulaya kwa kuwabana Waislamu na kukebehi Uislamu Tuli zake na kuwafanyia uadui watu wake au nembo zao, bali kuwataka Waislamu wote waondoke

www.path-2-happiness.com

Ulaya, Je, ni nini sababu za kuenea huku…haujakusudia bwana Rashidi kinyume cha mazoea yako?!

Rashidi: Bila shaka mimi ni mwenye kufurahi kwa ninayosikia, kwa hiyo nimechagua kunyamaza ili nizidi kusikiliza….kwa mtazamo wangu kuna sababu ndani ya Uislamu wenyewe, na kwa sababu ya jamii yenyewe ya Magharibi, na sababu zingine za mazingira: Na vipengele vingine vyenye kuchangia kusambaa kwa Uislamu…. Lakini nitaashiria kuwa hilo sio geni kwa dini kongwe, mizizi yake imesambaa na kunyooka tokea kuumbwa kwa mwanadamu, tokea Adam (‘Alayhi salaam), wala mzizi huu wa kihistoria hadi hivi sasa haujakatika.

Maiko: Hata hivyo bwana Rashidi sisi tunajua kuwa Uislamu haujadhihiri isipokuwa miaka elfu moja na mia nne tu iliyopita, na kama unavyojua kuwa kuna dini zingine za mbinguni, kama vile Ukristo na Uyahudi au utapinga hilo?!

Rashidi: Kuna ufahamu katika jambo hili unapaswa kusahihishwa, nao ni kuwa dini ya Mwenyezi Mungu ni moja na sio nyingi, moja kwa sababu inatoka katika chanzo kimoja, nacho ni kutoka kwa Allah (Mungu Mmoja) aliyeumba viumbe vyote, lakini kuna baadhi za hali ambazo huchungwa na dini hii moja inapelekea uwepo wa sheria mahsusi kwa hali hizi au katika umma mbali mbali, kama ambavyo inaweza kutokea upotofu wa dini hii kutokana na matokeo au umbali wa (wakati) kutoka kwenye chanzo cha ujumbe wenyewe, hivyo basi ikabidi kuhuisha dini kwa kutuma Mtume mpya ambae atathibitisha misingi ya dini hii, hili ndilo lililoashiriwa na hadithi ya Mtume wa Uislamu: “Manabii ni ndugu, dini yao ni moja, lakini mama zao ni wengi.” Yaani nyakati zao na sheria zao ni nyingi na zinatofauatiana, ama kilele chake kilikuwa wakati wa Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) na Ujumbe huu wa Mtume huyu ulikusanya vipengele vyenye kuhifadhi usalama wa dini hii na kuto kupotea, ambao umeihuisha na kurejesha katika usafi wake. Hivyo basi dini hii haitokatika na unyoofu huu wa kihistoria utaendelea hadi kuisha kwa wanadamu, kwa kuzingatia kuwa ni dini ya mwisho aliyoichagua Mwenyezi Mungu kwa wanadamu, hivyo katika hali ya kawaida ni yeye kuwaridhia wao yanaoafikiana na maumbile yao na kawaida kupata kuenea huku kukiachwa yatafanyika kwa njia ya kawaida.

Rajev: Huu ni mtazamo mpya na wenye kunisisimua, kama ni hivyo turejee pale ilipokuwa ututajie sababu za kuenea kwa Uislamu.

Rashidi: Ndio; ama sababu za dhati za Uislamu tutafupisha kuwa sifa zake ndizo zinaifanya kuenea; nazo ni:-

Ni dini nyepesi katika jengo lake, yenye undani katika maana yake, wazi kwa mtazamo wake, imeenea katika mfumo wake, mafundisho yake ni mepesi, haihitaji uwezo mkubwa wa kiakili, haina talasimu, wala siri, wala ugumu wowote.

-Dini ya utu, huzungumza na maumbile ya mwanadamu na hutangamana nae katika mazingira yake, na kuitikia mahitajio yake, na kutibu kadhia zake, hujibu maswali yanayoelekezwa kwake na huunganisha katika jamii na kuthibitisha usawa uliotimia kati ya wanadamu kulingana na asili zao, juu ya tofauti walizonazo za rangi zao, ndimi zao, maarifa yao na viwango vyao vya kijamii.

Dini inayokwenda na mazingira, haiwi juu ya uhalisia wa mwanadamu wala haipotei, na kwa uhalisia huu ni dini inayokusanya baina ya dunia na akhera, wala haioni mgongano kati yake.

Dini inayoheshimu akili ya mwanadamu, na huithamini fikra ya mwanadamu na kuweka hoja za kiakili na njia za kimantiki juu ya kilele cha kufahamiana na kujadiliana katika mambo yanayofaa yenye faida.

Dini isiyopiga vita elimu na maendeleo, bali inaihamasisha, na hakika za kisayansi zilizothibitika walizofikia wanazuoni wa kisasa zinaafikiana na tafsiri ya mandiko ya Qur’an yaliyopokelewa katika nyanja zile kabla ya karne kumi na nne.

Dini inayokwenda pamoja na harakati za maendeleo, Uislamu umethibitishwa uwezo wake katika kuamiliana na mambo yenye kujitokeza na mabadliko ya kijamii ambayo yanajitokeza katika maisha kwa kutekeleza mabadiliko ya zama na mahala.

Dini yenye kumhakikishia mwanadamu uhuru wa kweli, ambao haufikiwi kwa ajili ya maana yake isipokuwa pindi mwanadamu anapompwekesha Mola wake kwa ibada ya kweli; kwa sababu ya hilo hawi mwanadamu ni mja kwa mwanadamu yeyote yule, au kwa kiumbe chochote, au mja wa kuyaabudu mazingira yake.

Dini iliyokuwepo na haitaacha kufunguka juu ya desturi zingine.

Maiko: Mimi nitakuambia sababu zilizojificha katika jamii ya Ki-magharibi.

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Jamii zetu za Magharibi zinaishi katika janga la kifikra toka mwanzo wa karne iliyopita na kabla yake, na tatizo hili limejitokeza katika migongano mingi iliyoishi nayo jamii ya Magharibi, haswa baina ya kanisa na sayansi (elimu), kisha kati ya madhehebu mbali mbali ya kifalsafa na baina ya tabaka mbali mbali katika jamii tofauti, na hayo yameacha mpasuko mkubwa na babaiko, kukosekana kwa utambulisho.

Kisha baada ya hapo faragha ya kiroho ambayo inatoka kwa mwananchi wa Magharibi….faragha inayokaba roho ya mwanadamu na kuondoa hadhi yake na kushuka thamani ya mwanadamu…wakati ambapo vitu na maada vinakuwa juu ya hadhi ya mwanadamu na kufunika thamani zote za mwanadamu, kiasi cha kwenda kama vile mashine au sehemu ya mashine kubwa.

Kipengele kingine muhimu kina wakilishwa na shaka wanayoishi nayo Wamagharibi wengi kuhusu dini yao, na wanachokiona kuhusu kuwepo kwa migongano katika itikadi zao, pamoja na kasumba zilizo wazi kwao, achilia mbali yale yanayofanywa na Kanisa kwa kuzingatia kuwa ndio njia safi (tohara) na kusamehewa madhambi kwa njia ya utawa, wengi wetu wanaona kuwa ni kwenda kinyume na tabia na maumbile ya mwanadamu na kugongana nae katika mambo mengi ya maisha.

Hatuwezi kusahau kumomonyoka kwa maadili na kuparanganyika kwa familia na jamii ambayo imezikumba jamii nyingi za Magharibi.

Rashidi: Tukitaka kuzungumzia vipengele vya uhalisia, tunachokiona ni propaganda za kuupaka matope Uislamu, na kuwatesa wafuasi wake, hili linatupa kikwazo cha mtu kutaka kujua juu ya dini hii.

Kama ambavyo juhudi za wanaoita kwa Allah (wanaoutangaza Uislamu) na kuusambaza Uislamu, miongoni mwazo ni mijadala baina ya wanazuoni wa dini ya Kiislamu na dini zingine…hupelekea watu wa Magharibi kuujua Uislamu.

Usisahau athari za Waislamu wachache waliopo katika nchi za Magharibi, ambapo kuna fursa ile kwa Wamagharibi kujua kuwa ukaribu wa Uislamu kwa kuwaona Waislamu, jambo ambalo linatayarisha kuujua Uislamu na kuona namna wanavyoishi Waislamu wenyewe kiuhalisia.

Yote hayo yananipa hisia za hali nzuri ijayo inayothibitisha kuwa mustakbali ni wa dini hii.

Rejea Muhimu:

www.path-2-happiness.com

Rejea Muhimu:

Qur'an tukufu

Vitabu vya Sunna

Dr. Ibrahim Khalil:

Kwa nini rafiki yangu amesilimu? Na rai ya Vatican kuhusu changamoto ya Qur'an

Dr. Ibrahim Muhammad Ibrahim:

Dini za wanadamu katika vyanzo vyake vitukufu na mtazamo wa Kiislamu

Abu Al-A'ala Al-Maududi:

Uislamu kukabiliana na changamoto za kileo/kisasa

Uislamu na Mambo leo

Al-Hijab

Kuhusu utekelezaji wa shari'ah katika zama hizi

Misingi ya Uislamu

Sisi na Utamaduni wa Kimagharibi

Mfumo wa maisha katika Uislamu

Abu 'Abdul Malik Walid bin Fahd Al-Wad'an:

Ujumbe kwa kila anayemuamini Yesu (Isa) amani iwe juu yake

Ahmad Deedat:

Dini inayokuwa haraka

Uchaguzi kati ya Uislamu na Ukristo

Suluhisho la Uislamu kuhusu Ubaguzi

Tofauti za kimsingi kati ya Uislamu na Ukristo

Mungu (Allah) katika Uyahudi, Ukristo na Uislamu

Kati ya Injili na Qur'an

Tuhuma ya Upanga

Kwanini Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ndie mtukufu zaidi?

Kitabu kitakatifu kinasema nini kuhusu Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam)?

Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ndiye mtukufu zaidi ulimwenguni

Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ni khalifa baada ya masihi

Mtazamo wa Ibada katika Uislamu

Je, Masiya ndie Mungu? Jibu la injili kuhusu hayo.

Dr. Ahmad 'AbduRahim As-Saayih:

Falsafa ya ustaarabu wa Kiislamu

Dr. Ismail Raji Al-Faruqi na Dr. Luis Limya Al-Faruqi:

Atlasi ya ustaarabu wa Kiislamu.

Dr. Ikram Lam'i:

Talaka katika Ukristo (Mtazamo wa Biblia)

Andrew Newton na wenzake:

Misingi ya Upagani katika Ukristo

Anwar Mahmuud Zanatiy:

Kamusi ya upotoshaji wa magharibi juu ya Uislamu

Bernad Louis:

Istanbul na Ustaarabu wa Dola ya Ukhalifa

Ja'ad Al-Karim Jaba'i:

Haki za wanadamu katika Fikra ya Kiarabu leo hii

Jamil bin Subaih:

Utekelezaji wa ukhalifa wa mwanadamu ardhini

Dr. Godfrey Conzelin:

Balaa lililoikumba ukristo na usekula ulaya (ushuhuda wa Ujerumani)

www.path-2-happiness.com

Dr. Hussein Mu'unis:

Ustarabu-Utafiti na misingi yake

Muhtasari wa katiba ya Umma wa Kiislamu

Khalid 'Abu Al-Futuuh:

Uislamu na uliberali-Ukweli wa muelekeo wa Marekani na uwezekano wa makutano ya kifikra (makala)

Matumizi ya wakati na kuiongoza nafsi (makala)

Ustaarabu na istilahi zake (makala)

Kwa nini tunaichukia Marekani? (makala)

Yaliyojitenga na changamoto zake (makala)

Dr. Dawud Darwesh Hals:

Haki za kitamaduni za mwanadamu kati ya sheria za kiislamu na mikataba ya kimataifa

Roger Garuddy:

Wachimba makaburi-Ustarabu unaochimba utu kaburi lake.

Zigrid Honka:

Sun rising in the west: athari ya ustaarabu wa kiarabu ulaya

Sami 'Amiriy:

Je, Qur'an imechukua kutoka katika vitabu vya mayahudi na manasara?

Su'd bin 'Abdul 'Aziz bin Muhammad Al-'Arifi:

Dalili za kiakili na za kunukuu juu misingi ya itikadi

Sayyid Qutb:

Uislamu na matatizo ya ustaarabu

Mustakbali wa dini hii

Taswira za Kiislamu na nguzo zake

Dini hii

Dr. Sayyid Muhammad Badawiy:

Akhlaq kati ya Falsafa na Elimu Jamii

Dr. 'Adil Swadiq:

Talaka sio suluhisho

Dr 'Adil 'Ali Shadi na Dr. 'AbduRazaq Ma'ash:

Haja ya mwanadamu ya Ujumbe wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam)

'Abass Al-'Aqaad:

Athari ya waarabu katika ustaarabu wa watu wa Ulaya

'Abdu Ad-Daim Kahiil:

Miujiza ya tiba ndani ya Qur'an na Sunna

Insaiklopidia ya miujiza ya nambari katika Qur'an tukufu

'Abdur-Rahman Hassan Habanakah:

Udhibiti wa maarifa na misingi kutoa hoja na mijadala

'Abdur-Rahman Al-Juzairy:

Dalili za yakini za kujibu ukosoaji wa wamishionari

Dr. 'Abdul'Aziz Swaqr:

Dini na Dola katika mazingira ya magharibi..utafiti kuhusu nafasi ya dini katika nchi yenye kulingania uzalendo

Dr. 'Abdul'Aziz bin 'Uthman At-Tuwaijry:

Haki za mwanadamu katika mafundisho ya Uislamu

Dr. 'Abdullah bin 'Abdul Muhsin At-Turkiy:

Haki za mwanadamu katika Uislamu

'Abullah Nasih 'Ulwaan:

Vielelezo vya Ustaarabu katika Uislamu na athari yake katika kunyanyuka kwa Ulaya

Dr. 'Abdul Muhsin bin Zain Al-Mutwairy:

Dalili za wazi kuhusu ukweli wa Utume wa mbora wa viumbe Swalla Llahu 'alayhi wasallam

www.path-2-happiness.com

‘Ali Ezzet Bigovich:

Uislamu kati ya mashariki na magharibi

Dr. ‘Ali Muhyyiddin Al-Qurra Daghi:

Sisi na wengine

‘Ali bin Nayf Ash-Shuhud:

Kipambanuzi katika kujibu kuhusu ustaarabu wa magharibi

Dr. ‘Imaduddin Khaliil:

Walivyosema kuhusu Uislamu

Dr. Fahd bin ‘Abdu Rahman bin Sulaiman Ar-Rumiy:

Sifa za Qur’an tukufu

Dr. Mazin Al-‘Armouty, Numeir ‘Abass Madh-har, Kayyid Hashim

Uislamu na Umagharibi na Haki za binadamu

Michael Hart:

Watukufu mia moja mbora wao ni Muhammad

Mujahid Mahmud Ahmad Nasir:

Mfumo wa Qur’an katika kusimamisha hoja na dalili

Muhammad bin Ibrahim Al-Hamd:

Uislamu ni njia ya furaha ya milele

Muhammad Abu Zahra:

Jamii ya mwanadamu katika kivuli cha Uislamu

Muhammad Abul Qasim Hajj Hamd:

Mjadala juu ya yasiyoonekana (Ghaib) na mwanadamu

Dr. Muhammad Bashariy:

Uhuru wa kidini katika sheria ya Kiislamu

Muhammad Taqiddin Hilaal Al-Maghribiy:

Dalili ndani ya Biblia kuwa Issa ni mja na sio Mungu

Muhammad Rashid Al-‘Uwaidy:

Wao wanaangalia inavyoporwa

Dr. Muhammad Az-Zuhaily:

Haki za binadamu kiini cha makusudio ya sheria

Dr. Muhammad Dwiyaa Rahman Al-Aadhwami:

Tafiti katika Uyahudi, Ukristo na dini za India

Muhammad bin Twahir At-Tanyar Al-Bairuti:

Itikadi za kipagani katika dini ya ukristo

Muhammad Twahir bin ‘Ashuur:

Muhtasari wa msingi wa mfumo wa kijamii katika Uislamu

Dr. Muhammad bin ‘Abdullah bin Swalih As-Suhaim:

Uislamu-Misingi yake

Dr. Muhammad ‘Ammarah:

Uislamu na haki za binadamu…mambo ya msingi na sio haki peke yake

Baina ya Kusamehewa madhambi na maendeleo..manabii katika Qur’an na kitabu kitakatifu (makala)

Muhammad Al-Ghazali:

Haki za mwanadamu

Muhammad Qutb:

Shubuhaat (utata) dhidi ya Uislamu

Muhammad Mutawalli Ash-Sha’arawiy:

Dalili za Kimaada za kuwepo Mungu

Muhammad Yasin:

Majibu ya wanazuoni wa Kiislamu kuhusu tuhuma za wayakinifu na mustashrikina

Kituo cha mabadilishano ya Utamaduni, kwa kushirikiana na

www.path-2-happiness.com

Unesco:

Athari ya Waarabu na Waislamu katika kunyanyuka kwa ulaya

Dr. Marwan Ibrahim Al-Qaisiy:

Insaiklopidia ya haki za mwanadamu katika Uislamu

Nasir bin Dakhilillah bin Falih As-Su'aydiy:

Hoja za kiakili na maana za kibalagha

Harun Yahya:

Hadaa ya maendeleo

Ufahamu wa haraka wa imani

Qur'an ni muujiza wa miujiza

Miujiza ya Qur'an

Hanz Henry. H. Shebder:

Roho ya Ustaarabu wa kiarabu

Dr. Hiba Rauf Ezet:

Matatizo ya maana ya haki za binadamu (makala)

Wahiddudin Khan:

Changamoto ya Qur'an

Kadhia kubwa

Dr. Yahya bin Muhammad Hassan Zamzami:

Haki za mwanadamu-maana na utekelezaji wake katika Qur'an tukufu

Yusri Muhammad Sa'id Mubyadh:

Siku ya mwisho katika dini za mbinguni na dini za kale

Dr.Ya'aqub bin 'AbdulWahab Al-Bahusein:

Njia za kutolea dalili na nguzo zake kwa watu wa mantiki na watu wa usuli

Faharasi ya Yaliyomo

www.path-2-happiness.com

Faharasi

Utangulizi	3
Kikombe cha Usahaulifu	8
Je, Mke Mmoja Anatosha?!	16
Waridi Lenye Kuvuja	22
Sitara ya Kimaadili	30
Mwanamke ni Malkia	38
Kuparaganyika Kwa Nyumba Yenye Matatizo	44
Mwanamke Baada ya Kuwa Huru	50
Upambanuzi wa Ustaarabu	56
Pamoja na Freud Ndani ya Mgahawa - Paris	62
Nafsi ya Mwanadamu Baina ya Mifumo Miwili	68
Haja Yetu ya Imani	74
Minara ya Njia	80
Mjue Mungu Wako	86
Nuru ya Mbinguni	92
(Haja ya Watu na Utume)	92
Sifa ya Dini ya Haki	100
Mwanadamu Mtukufu Zaidi	106
Ujumbe wa Mwisho	112
Bara la Amani	118
Sheria ya Mwenyezi Mungu	124
Hakika za Kistaarabu:	130
Jua la Waislamu Linaangaza Kwa Wanadamu	136
Mwanadamu Anapotengwa	142
Haki za Mwanadamu Katika Uislamu	148
Samahani Kidogo	154
Tafadhali Niruhusu	162
Tabia ya Qur'an	168
Dola ya Kiislamu	174
Safari ya Milele	180
Uislamu na Ugaidi	186
Mustakbali wa Dini Hii	192
Rejea Muhimu:	198
Faharasi ya Yaliyomo	205

www.path-2-happiness.com

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ni nani miongoni mwetu hatafuti furaha.? Hapana shaka kuwa kila mwanadamu anahaha kuitafuta, lakini ni wangapi katika sisi wanaofanikiwa katika kufikia hii furaha? Si hivyo bali ni wangapi miongoni mwetu ambao wanajua njia ya kuifikia? Bila shaka sababu za furaha ni nyingi, lakini kwa mtazamo wangu ni kuwa la muhimu zaidi katika sababu hizi ni mtu kuhakiki dhati yake, na mtu hawezi kuhakiki dhati yake ila kwa kuhakiki utu wake kwanza. Utu wake ambao unamtofautisha mtu na mnyama na viumbe wengine. Ama kwa hakika tafakuri kwa maswali makubwa kuhusu ulimwengu, mwanadamu na maisha, na kufikia kwenye majibu sahihi ya maswali haya humfikisha mwanadamu katika utulivu, bali kuridhika na furaha. Majadiliano haya huchangia katika kuweka miguu yetu katika njia ya mwanzo ya furaha, kwa kuondosha dhana na kufikia kwenye hakika, na kumfikisha mtu kwenye majibu kuhusu maswali yenye kushughulisha fikra za wengi wetu, ambapo maudhui mengi yamewekwa kuhusiana na pande za utu wa mwanadamu, ambayo yamewekwa katika hali ya mvuto wenye kunasibiana na wasomaji wengi.

بيانات الاتصال
المملكة العربية السعودية : ٠٠٩٦٦-٥٣٧١٢١٥٠٤
جمهورية مصر العربية : ٠٠٢٠١١٤٠٤٨١٦٠٦

www.path-2-happiness.com

Tovuti rafiki

أكاديمية البلدة الطيبة
Balda Tayiba Academy

Imam Academy
أكاديمية الأئمة والخطباء

أكاديمية شيخ الإسلام ابن تيمية

حواء
أكاديمية

الهدى اكيدمى
Alhuda academy

Al-Huda Academy

AIA
African Islamic Academy

AIA
African Islamic Academy

ইলম একাডেমি

أكاديمية الإمامين ابن باز-ابن عثيمين

KAP
KNOWLEDGE ACADEMY
PHILIPPINES

تدارس

جامعة ابن كثير الدولية
Ibn Kathir International University
of Humanities and Islamic Sciences